



TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA

# **ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI KWA AJILI YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020**





## YALIYOMO

SURA YA KWANZA .....	1
<b>UTANGULIZI .....</b>	<b>1</b>
SURA YA PILI .....	9
<b>MAPINDUZI YA UCHUMI KWA MAENDELEO YA WATU.....</b>	<b>9</b>
SURA YA TATU .....	124
<b>HUDUMA ZA JAMII .....</b>	<b>124</b>
SURA YA NNE .....	151
<b>SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU .....</b>	<b>151</b>
SURA YA TANO .....	155
<b>ULINZI NA USALAMA .....</b>	<b>155</b>
SURA YA SITA .....	161
<b>UTAWALA BORA, UTAWALA WA SHERIA NA MADARAKA YA WANANCHI.....</b>	<b>161</b>
SURA YA SABA .....	182
<b>MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA .....</b>	<b>182</b>
SURA YA NANE .....	187
<b>MAZINGATIO MAALUM YA ILANI KUHUSU ZANZIBAR .....</b>	<b>187</b>
SURA YA TISA .....	272
<b>MAENEO MENGINE YA KIPAUMBELE .....</b>	<b>272</b>
SURA YA KUMI .....	297
<b>CHAMA CHA MAPINDUZI .....</b>	<b>297</b>





## SURA YA KWANZA

### UTANGULIZI

TUMETEKELEA KWA KISINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA

1. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya uongozi wa vyama vya TANU na ASP na baadae CCM, imejengwa katika misingi ya ujamaa na kujitegemea inayozingatia utu, usawa na haki. Misingi hii imeimarishwa na siasa safi na uongozi bora wa CCM na imekuwa ndio nguzo ya kudumisha amani, umoja na mshikamano wa kitaifa. CCM itaendelea kuzisimamia Serikali zake kuhakikisha kuwa zinazingatia, kulinda na kudumisha misingi hii adhimu.
2. CCM itahakikisha kuwa Tanzania inaendelea kulinda Uhuru wake, kudumisha Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, na kuimarisha Muungano wetu wenye mfumo wa serikali mbili pamoja na tunu nyingine za Taifa ikiwemo falsafa ya Mwenge wa Uhuru ili kuendelea kujenga Taifa imara linalojitegemea kiuchumi na kisiasa, lenye ustawi wa watu wake na linaloenzi na kuthamini mila nzuri, desturi na utamaduni wetu.
3. CCM inaamini kwamba uzalendo kwa nchi ndio msingi wa maendeleo ya kweli ya Tanzania ambayo yataletwa na Watanzania wenyewe. Hivyo basi, CCM itaendelea kuhimiza wananchi kuwa wazalendo kwa nchi yetu kwa kufanya kazi kwa uadilifu, bidii na maarifa kama msingi imara wa maendeleo.
4. CCM inaamini pia kuwa kila mtu ana jukumu la kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kujiletea maendeleo yake na Taifa kwa ujumla. Imani hii ndiyo chimbuko la kauli mbiu za **Hapa Kazi Tu!** na **Kuacha Kufanya Kazi kwa Mazoea!** Aidha, CCM inatambua kuwa serikali inazoziongoza zina jukumu la msingi la kuhakikisha kuwa walio wanyonge katika jamii wanapata fursa ya kipekee ya kustawisha maisha yao na kuondokana na unyonge wao ili kupunguza tofauti za matabaka.
5. CCM inatambua kuwa nchi yetu ina watu wenye uwezo na rasilimali za kutosha kama vile ardhi, madini, gesi asilia, misitu, wanyama, malikale/mambo ya kale, bahari, maziwa na mito, pamoja na nafasi na fursa nzuri za kijiografia. Rasilimali na fursa hizi zikitumiwa vizuri zitakuwa chachu kubwa kwa maendeleo ya Taifa, kama ambavyo imethibitika katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020 na kwamba **tukiamua tunaweza**. Ni katika muktadha huu CCM inaamini kuwa **Tanzania ni nchi tajiri**.
6. Katika miaka mitano ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 -2020 chini ya uongozi wa **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na **Dkt. Ali Mohamed Shein**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, mafanikio makubwa yamepatikana katika nyanja na sekta zote za maendeleo kwa ustawi wa wananchi. Mafanikio haya ni pamoja na:-



- (a) Kuendelea kulinda na kuimarisha umoja, mshikamano, amani, utulivu, ulinzi na usalama;
- (b) Kuendelea kulinda, kuimarisha na kudumisha Uhuru, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na Muungano wa Tanzania;
- (c) Kuendelea kulinda na kuimarisha demokrasia ya vyama vingi, haki za binadamu, nchi isiyofungamana na dini yoyote, na kupambana na unyanyasaji na udhalilishaji wa aina zote;
- (d) Kuendelea kuwa nchi isiyofungamana na upande wowote ili kuweza kutetea na kulinda masilahi ya nchi yetu kwa kuzingatia misingi tunayoiamini;
- (e) Kuimarisha utumishi wa umma unaozingatia weledi, nidhamu, uadilifu, bidii na maarifa katika kazi;
- (f) Kuimarisha mifumo ya kisera, kitaasisi na kisheria, ikiwemo kutungwa kwa sheria inayotaka Serikali za mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya uwezeshaji wa wanawake (4%), vijana (4%) na watu wenye ulemavu (2%);
- (g) Kuimarishwa kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina kulikowezesha kusimamia na kuboresha utendaji wa mashirika ya umma yaliyoweza kuchangia jumla ya shilingi trilioni 1.052 kama gawio na michango kwa Serikali.
- (h) Kuhamishia Serikali Makao Makuu ya Nchi Dodoma;
- (i) Kudhibiti na kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa, uhujumu uchumi na ufiadini, na hivyo kuokoa fedha na rasilimali nyingine na kuzielekeza kwenye mipango ya maendeleo ya nchi;
- (j) Kudhibiti na kuimarisha mapambano dhidi ya uzalishaji, uagizaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya dawa za kulevya, utakatishaji wa fedha haramu na biashara ya kusafirisha binadamu;
- (k) Kujitoshesha kwa chakula na kuzalisha ziada kwa ajili ya masoko ya nje;
- (l) Kuimarisha uchumi wa viwanda ambapo idadi ya viwanda imeongezeka kutoka viwanda 52,633 mwaka 2015 hadi kufikia viwanda 61,110 mwaka 2019, ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.1. Kutokana na hatua hii, uzalishaji wa bidhaa na ajira umeendelea kuongezeka;
- (m) Kutekeleza miradi ya kimkakati yenye tija kubwa katika uchumi na ustawi wa jamii ikiwemo miradi ifuatayo: Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere; ujenzi wa reli ya kisasa (SGR); kufufuliwa kwa Shirika la Ndege la Taifa kwa kununua ndege mpya 11; kununua meli mbili mpya Zanzibar; na ujenzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume;



- (n) Kuimarisha mfumo wa udhibiti, usimamizi na umiliki wa madini na hivyo kuongeza mapato yatokanayo na mazao ya madini kutoka shilingi bilioni 168 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 517.57 mwaka 2020;
- (o) Kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kutoka wastani wa shilingi bilioni 850 kwa mwezi mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa shilingi trilioni 1.3 mwaka 2019. Kwa upande wa Zanzibar, mapato ya Serikali yameongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 428.5 mwaka 2015/2016 hadi kufikia shilingi bilioni 748.9 mwaka 2018/19. Mafanikio hayo yameongeza uwezo wa Serikali wa kutekeleza miradi ya maendeleo na kutoa huduma za jamii kwa wananchi;
- (p) Kuchukua hatua za kulinda mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na athari za mazingira ikiwa ni pamoja na kuondoa matumizi ya mifuko ya plastiki; na
- (q) Kuendelea kupiga hatua za maendeleo katika maeneo mbalimbali kama vile ujenzi wa miundombinu ya kisasa, kukua kwa kasi kwa uchumi na kuimarika kwa ustawi wa jamii. Tanzania ni miongoni mwa nchi kumi ambazo uchumi wake unakua kwa kasi barani Afrika na hivyo kuwa miongoni mwa nchi za uchumi wa kati mwaka 2020, miaka mitano (05) kabla ya lengo lake la kufikia ngazi hiyo ya uchumi mwaka 2025.
- (r) Matokeo ya mafanikio haya kwa maendeleo na ustawi wa wananchi ni pamoja na:-
- (i) *Kwa upande wa Tanzania Bara:*
- Wastani wa pato la mwananchi limekua kutoka shilingi 1,968,965 mwaka 2015 hadi shilingi 2,458,496 mwaka 2018, na Pato la Taifa limeongezeka kwa wastani wa asilimia 6.9 kwa mwaka;
  - Wastani wa umri wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 61 mwaka 2015 hadi miaka 65 mwaka 2020;
  - Kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme kutoka megawati (MW) 1,308 mwaka 2015 hadi megawati (MW) 1,602.32 mwaka 2020. Vilevile, usambazaji wa umeme vijijini umeongezeka kutoka asilimia 16.4 mwaka 2015 hadi asilimia 67.1 mwaka 2020;
  - Kuimarika kwa huduma ya umeme nchini na hivyo kuondoa mgao wa umeme uliokuwa kero na kikwazo kikubwa kwa shughuli za kiuchumi na kijamii;
  - Kutoa elimu bila malipo katika ngazi ya shule za msingi na sekondari na hivyo kuongeza udahili wa wanafunzi katika ngazi zote za elimu. Kwa mfano, idadi ya wanafunzi wa sekondari imeongezeka kutoka wanafunzi 1,648,359 mwaka 2015 hadi 2,185,037 mwaka 2019;
  - Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu nchini kutoka 65,064 mwaka 2015 hadi 87,813 mwaka 2019;
  - Kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaopata huduma ya



maji safi na salama vijijini kutoka asilimia 47 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 70.1 mwaka 2020. Kwa upande wa mijini, idadi ya wananchi wanaopata maji safi na salama imeongezeka kutoka asilimia 74 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 85 mwaka 2020. Kwa ujumla, idadi ya kaya zinazopata maji safi nchini kutoka vyanzo salama imeongezeka hadi kufikia asilimia 77 mwaka 2020;

- Kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya (zahanati, vituo vya afya na hospitali) kutoka 7,014 mwaka 2015 hadi 8,446 mwaka 2020;
- Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma za afya kutoka asilimia 42 ya mahitaji mwaka 2015 hadi asilimia 94.5 mwaka 2020;
- Kiwango cha umasikini wa mahitaji ya msingi kimepungua kufikia asilimia 26.4; na
- Kuboresha makazi na nyumba za wananchi, ambapo asilimia ya kaya zinazoishi katika nyumba zenye mapaa ya kisasa imeongezeka kutoka asilimia 68.0 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 84.1 kwa mwaka 2018/19.

(ii) *Kwa upande wa Zanzibar*

- Wastani wa pato la mwananchi limekua kutoka shilingi 1,666,000 mwaka 2015 hadi shilingi 2,549,000 mwaka 2019, na Pato la Taifa limeongezeka kwa wastani wa asilimia 6.8 kwa mwaka;
- Wastani wa umri wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 66.6 mwaka 2015 hadi miaka 68.4 mwaka 2020;
- Usambazaji wa huduma za umeme umeongezeka kutoka asilimia 70 mwaka 2015 hadi asilimia 90 mwaka 2020;
- Kuendelea kutoa elimu bure hadi ngazi ya sekondari, ikiwa ni utekelezaji wa sera ya msingi ya Mapinduzi ya 1964;
- Kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaopata maji safi na salama vijijini kutoka asilimia 60 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 72 mwaka 2020. Kwa upande wa mijini, idadi ya wananchi wanaopata maji safi na salama imeongezeka kutoka asilimia 80 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 87 mwaka 2020. Kwa ujumla, idadi ya kaya zinazopata maji kutoka vyanzo salama imeongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 83 mwaka 2020;
- Kuendelea kutoa huduma ya matibabu bure na kuongeza bajeti ya ndani ya ununuzi wa dawa muhimu kutoka shilingi bilioni 0.5 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 12.7 mwaka 2020 na hivyo kuongeza ugharamiaji huo kutoka asilimia 7 ya mahitaji hadi asilimia 97 ya mahitaji yote; na
- Kuimarisha na kupanua matumizi ya utafiti katika kufanya maamuzi sahihi ya sekta mbalimbali.

7. Ilani hii inalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kutokana na





utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015. Vilevile, maudhui ya Ilani hii yamezingatia Mwelekeo wa Sera za Chama Cha Mapinduzi wa 2020-2030, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020-2050. Aidha, Ilani hii imezingatia fursa na changamoto zinazotokana na mabadiliko mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiteknolojia yanayotokea nchini na duniani, pamoja na madhara ya janga la ugonjwa wa Corona.

8. CCM inatambua kwamba utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo utafikia kikomo chake katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii. Hivyo, Chama kitazisimamia Serikali zake kuandaa Dira mpya ya Taifa ya Maendeleo kuelekea mwaka 2050, na kuanza utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020 - 2050. Katika miaka mitano ijayo, lengo la CCM ni kuendelea kustawisha maisha ya kila Mtanzania, kutokomeza umasikini na kuhakikisha kuwa Taifa linafikia uchumi wa kati. Katika kufikia lengo hili vipaumbele vikuu vya serikali za CCM katika miaka mitano ijayo vitakuwa vifuatavyo:-

- (a) Kulinda na kuimarisha misingi ya utu, usawa, haki na uongozi bora ili kudumisha amani, umoja na mshikamano wa Taifa letu;
- (b) Kukuza uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishii na shindani uliojengwa katika msingi wa viwanda, huduma za kiuchumi na miundombinu wezeshi;
- (c) Kuleta mageuzi ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwa na uhakika wa chakula na kujitegemea kwa chakula wakati wote na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi;
- (d) Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu, maji, umeme na makazi vijijini na mijini;
- (e) Kuchochea matumizi ya utafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu kama nyenzo ya maendeleo ya haraka ya kijamii na kiuchumi; na
- (f) Kutengeneza ajira zisizopungua **8,000,000 (milioni nane)** katika sekta rasmi na isiyo rasmi kwa ajili ya vijana.

9. Mambo muhimu yatakayozingatiwa katika kutekeleza vipaumbele vikuu vya Ilani hii ni kama ifuatavyo:-

- A. *Kulinda na kuimarisha utu, usawa, haki na uongozi bora ili kudumisha amani, umoja na mshikamano wa Taifa letu:-*
  - (i) Kudumisha na kuimarisha umoja, udugu, mshikamano, amani, utulivu, ulinzi na usalama;
  - (ii) Kuimarisha Muungano wa Serikali mbili, kuenzi Uhuru wa nchi yetu na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar pamoja na kutumia tunu nyingine za kitaifa ikiwemo falsafa ya Mwenge wa Uhuru katika kujenga moyo wa uzalendo na uwajibikaji;



- (iii) Kuimarisha demokrasia, utawala bora na haki za binadamu na mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi, pamoja na udhalilishaji wa aina zote;
- (iv) Kuimarisha Serikali za Mitaa ili ziweze kutimiza wajibu wao kwa wananchi katika maeneo husika;
- (v) Kuchukua hatua madhubuti za kujenga mazingira wezeshi kwa asasi za kiraia, kidini na vyombo vya habari kustawi ili kuchangia katika maendeleo ya Taifa; na
- (vi) Kuimarisha huduma na kulinda haki kwa makundi maalum wakiwemo wanawake, vijana, wazee, watoto na watu wenye ulemavu.

*B. Kukuza uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani uliojengwa katika msingi wa viwanda, huduma za kiuchumi na miundombinu wezeshi:-*

- (i) Kujenga na kukuza uchumi shindani hususan kupitia sekta za viwanda na huduma za kiuchumi utakaowezesha ustawi wa wananchi wote;
- (ii) Kuimarisha miundombinu ya kimkakati ili kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kufanya shughuli zao kwa ufanisi na tija;
- (iii) Kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kukua na kustawi pamoja na kuvutia wawekezaji ili watoe mchango stahiki katika maendeleo ya nchi yetu;
- (iv) Kuboresha masilahi na mazingira ya kazi kwa wafanyakazi katika sekta zote;
- (v) Kuongeza faida ambazo nchi yetu inapata kutokana na maliasili zetu na utajiri wa nchi kwa kuimarisha usimamizi wa mikataba ya uzalishaji na kujenga uwezo wa ndani wa kuvuna na kuchakata/kusarifu rasilimali hizo;
- (vi) Kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira na uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;
- (vii) Kutenga maeneo maalum ya akiba ya ardhi na uwekezaji;
- (viii) Kuimarisha mawasiliano ya simu za mkononi nchini ili yaweze kurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa maendeleo ya wananchi; na



- (ix) Kuendeleza diplomasia ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ikiwa ni pamoja na kufanya lugha ya Kiswahili kutumika kikamilifu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Afrika (AU) na Umoja wa Mataifa (UN).
- C. *Kuleta mageuzi ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwa na uhakika wa chakula na kujitegemea kwa chakula wakati wote na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi:-*
- (i) Kuhakikisha uzalishaji unaongezeka katika mazao ya chakula, mifugo na uvuvi kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula na lishe bora;
- (ii) Kuongeza tija katika kilimo, ufugaji na uvuvi kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya uchumi, hasa katika sekta za viwanda na huduma;
- (iii) Kuimarisha ushirika ili kuunganisha nguvu za wazalishaji, hasa katika kupata pembejeo na kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi;
- (iv) Kuimarisha miundombinu na kuongeza maeneo ya umwagiliaji katika kilimo ili kupata mazao mengi zaidi wakati wote wa mwaka; na
- (v) Kukamilisha na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya shughuli za kijamii, uwekezaji na uzalishaji.
- D. *Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za Afya, Elimu, Maji, Umeme na Makazi vijijini na mijini:-*
- (i) Kuongeza kasi ya usambazaji majisafi na salama ili kutosheleza mahitaji kwa zaidi ya asilimia 85 vijijini na zaidi ya asilimia 95 kwa mijini, kwa upande wa Tanzania Bara, ifikapo mwaka 2025, na zaidi ya asilimia 95 kwa upande wa Zanzibar;
- (ii) Kuimarisha mfumo wa elimu ili uweze kuzalisha wataalam mahiri zaidi wenye uwezo katika sayansi, teknolojia, ufundi na nyanja nyingine ambao wanaweza kujiajiri na kuajirika mahali popote duniani;
- (iii) Kusambaza umeme kwenye mitaa na vijiji vyote ifikapo mwaka 2025;
- (iv) Kutoa huduma za afya kwa wote; na
- (v) Kuhamasisha na kuweka mazingira wezeshi ili wananchi katika maeneo yote nchini wawe na makazi bora (“Nyumba bora kwa wananchi wote inawezekana”).



- E. *Kuchochea matumizi ya utafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu kama nyenzo ya maendeleo ya haraka ya kijamii na kiuchumi:-*
- (i) Kuimarisha na kuhuisha taasisi za utafiti, sayansi, teknolojia na ufundi ili ziweze kubuni nyenzo za kuongeza tija katika sekta za uzalishaji na huduma;
  - (ii) Kuhakikisha kila shule ya sekondari nchini inakuwa na kompyuta na huduma za intaneti;
  - (iii) Kusomesha Watanzania nje ya nchi katika vyuo bora na maalum duniani kwenye masuala ya sayansi, tiba, teknolojia na maeneo mengine yenye umuhimu ili kupata maarifa bora na ya kisasa na ujuzi ili kuchochea maendeleo ya sayansi na teknolojia nchini; na
  - (iv) Kuchochea na kuendeleza ubunifu, uvumbuzi na ugunduzi nchini kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.
- F. *Kutengeneza ajira zisizopungua 8,000,000 (milioni nane) katika sekta rasmi na isiyo rasmi kwa ajili ya vijana:-*
- (i) Kuchochea ukuaji wa uchumi, hususan katika sekta ya viwanda vinavyotumia malighafi za kilimo, mifugo, uvuvi, madini, maliasili na sekta ya huduma za kiuchumi pamoja na utalii;
  - (ii) Kuwawezesha vijana kushiriki katika shughuli za ujasiriamali, ikiwemo kuwapatia mafunzo na kuwaunganisha na taasisi na asasi za utoaji mikopo yenye riba na masharti nafuu;
  - (iii) Kuwahamasisha na kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika utamaduni, michezo na sanaa kwa ajili ya afya bora na burudani na pia kuongeza fursa za ajira na kipato; na
  - (iv) Kuhakikisha kuwa miradi mikubwa ya kimkakati inaajiri vijana wengi zaidi wa Kitanzania.

10. CCM itahakikisha serikali zake zinatekeleza mambo yote yaliyoahidiwa katika Ilani hii kwa manufaa na ustawi wa Taifa letu. Utekelezaji wa Ilani hii utaongozwa na kauli mbiu ifuatayo: ***“Tumetekeleza kwa Kishindo; Tunasonga Mbele Pamoja”***

11. Ilani hii ni tamko na ahadi maalum ya nia inayodhihirisha uwezo wa CCM kuendelea kuongoza nchi, kuleta ustawi wa Watanzania wote na kuendelea kutatua changamoto zinazowakabili wananchi, hususan wanawake, vijana, watoto, wazee, pamoja na watu wenye ulemavu. Katika miaka mitano ijayo, CCM itahakikisha matarajio ya wananchi katika nyanja zote yanafikiwa. Chama Cha Mapinduzi kinawaomba Watanzania wote waendeleo kukiamini na kukichagua ili kiendeleo kuongoza nchi na kuleta maendeleo makubwa na ya haraka kwa faida ya wananchi wote.



## SURA YA PILI

### MAPINDUZI YA UCHUMI KWA MAENDELEO YA WATU

TUMETEKELEZA KWA MASHINDO; TUNAKONGA MBELE PAMOJA

12. Chama Cha Mapinduzi kinatambua umuhimu wa kujenga *uchumi wa kitaifa* ili kuhakikisha kwamba Watanzania ndio wanufaika wakuu wa uchumi na maliasili za nchi na ndiyo wenye kauli juu ya namna uchumi unavyoendeshwa. Kwa muktadha huo CCM itaelekeza Serikali kuendelea na juhudi za kuifanya Tanzania kuwa nchi inayojitegemea kiuchumi pamoja na kuimarisha mahusiano ya kiuchumi na nchi nyingine. Juhudi maalum zitaelekezwa kuhakikisha rasilimali za asili za nchi hii, hasa ardhi, madini, gesi asilia, mafuta, maji na misitu zinanufaisha wananchi na Taifa kikamilifu.
13. Katika miaka mitano ijayo, CCM itazisimamia Serikali zake ili ziendeze juhudi za kuleta mageuzi ya kiuchumi kwa kuendelea kujenga *Tanzania ya viwanda* na uchumi *fungamanishi, jumuishii na shindani* unaotumia sayansi na teknolojia za kisasa na ambao unahimili utandawazi na unaoweza kutumia kikamilifu fursa zake kwa kuuza zaidi bidhaa za viwandani na bidhaa nyingine nje ya nchi. CCM inatambua fika kwamba ili kutimiza azma ya kujenga uchumi shindani wa viwanda na huduma, ni lazima kila Mtanzania afanye kazi kwa bidii, kujituma, na kutumia maarifa, hekima na ubunifu.
14. CCM inatambua na kuthamini sana nafasi ya sekta binafsi katika kujenga uchumi wa kitaifa na ambao ni shindani uliojikita katika ujenzi wa Tanzania ya viwanda na katika kuleta mageuzi kwenye kilimo, ufugaji, uvuvi, utalii na sekta nyingine zote. CCM itaendelea kusimamia serikali zake kuhakikisha sekta binafsi inalindwa na kuendelezwa na kwamba haki ya kila mtu, kikundi, ushirika na kampuni ya kuendesha shughuli za uchumi na biashara kwa uhuru na kwa mujibu wa sheria zinalindwa wakati wote. CCM itaelekeza Serikali kuendelea kujenga mazingira ya kiuchumi na kibiashara ambayo yatakutia zaidi wawekezaji wa ndani na nje na ambayo yatakuwa tulivu na yanayotabirika. CCM inaamini kuwa mazingira mazuri yanayovutia uwekezaji na kukuza uchumi yanahitaji mambo matano makubwa yafuatayo:-
- Amani na usalama, utawala wa sheria na utulivu wa kisiasa;
  - Mwenendo tulivu wa uchumi mpana (*macroeconomic stability*);
  - Ubora wa miundombinu na huduma wezeshi kama vile uchukuzi, nishati na mawasiliano;
  - Urahisi, ufanisi na uhakika wa sheria, kanuni, taratibu na utendaji wa sekta ya umma katika kuwezesha shughuli za uchumi na biashara za sekta binafsi; na



- (e) Uwepo wa rasilimaliwatu ya kutosha yenye elimu, ujuzi na maarifa stahiki hususan katika nyanja za sayansi na teknolojia.

15. Pamoja na kwamba serikali za CCM zitaendelea kuitambua sekta binafsi kama injini ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu na kuwa italindwa na kukuzwa kwa juhudi zote, CCM itaendelea kuelekeza Serikali kujihusisha moja kwa moja kwenye shughuli za uchumi na biashara za kimkakati na zile ambazo sekta binafsi haijaweza kujihusisha nazo kwa ufanisi au haivutiwi kuwekeza.

16. CCM inatambua kwamba mageuzi ya kujenga uchumi wa viwanda ni lazima yaendane na mageuzi ya kuongeza tija kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi. Juhudi za kukuza tija kwa wakulima wadogo, wavuvi wadogo na wafugaji ni vigumu sana kufanikiwa bila ya kuimarisha ushirika katika uzalishaji na masoko. Ni changamoto kwa mkulima mmoja mmoja kumudu ununuzi wa pembejeo, huduma za ugani kuongeza thamani ya mazao na kufikia masoko yanayotoa bei nzuri ya kile kinachozalishwa. CCM inatambua kwamba kwa vile theluthi mbili ya nguvu kazi ya nchi ipo vijijini na inajihusisha na kilimo, ufugaji na uvuvi lakini nguvu kazi hii inapata theluthi moja tu ya pato la Taifa, ni wazi kwamba tija ni ndogo. Ili kuongeza tija vijijini na kuleta mageuzi ya kiuchumi kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi, CCM inatambua kwamba ni muhimu kuhakikisha vyama vya ushirika vinaendelezwa kwa kuongezwa kitalaamu na kidemokrasia. Vilevile, ni lazima vyama hivi vilinde masilahi ya wanachama wake kikamilifu na kujenga uwezo wa kukuza uzalishaji katika sekta za kilimo na viwanda.

### Hali ya Uchumi

17. Mafanikio yaliyopatikana katika kujenga uchumi imara na kupunguza utegemezi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015-2020) ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kuwezesha rasilimali za Taifa kutumika kimkakati na kikamilifu katika ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda na ustawi wa jamii kwa kuandaa na kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21;
- (b) Kukua kwa Pato la Taifa kwa wastani wa asilimia 6.9 katika kipindi cha mwaka 2016 - 2019;
- (c) Pato la wastani la kila mtu liliongezeka kutoka shilingi 1,968,965 (Dola za Kimarekani 992) mwaka 2015 hadi kufikia shilingi 2,458,496 (Dola za Kimarekani 1,086) mwaka 2018;
- (d) Viashiria kadhaa vinaonesha umasikini umepungua na ustawi wa watu umeimarika. Baadhi ya viashiria hivyo ni:-
- (i) Wastani wa miaka ya kuishi kwa Watanzania umeongezeka kutoka miaka 61 mwaka 2015 hadi takribani miaka 65 mwaka 2020;





- (ii) Usambazaji wa umeme vijijini umeongezeka kutoka asilimia 16.4 mwaka 2015 hadi asilimia 67.1 mwaka 2019; na
  - (iii) Umasikini wa mahitaji ya msingi umepungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 26.4 mwaka 2017/18. Aidha, kiwango cha umasikini wa chakula kimepungua kutoka asilimia 9.7 mwaka 2011/12 hadi asilimia 8.0 mwaka 2017/18.
- (e) Utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na za bajeti ambao umewezesha yafuatayo:-
- (i) Mfumuko wa bei umeendelea kubaki ndani ya wigo wa tarakimu moja kwa wastani wa asilimia 4.4 kati ya mwaka 2016 na mwaka 2019. Kiwango hicho ni cha chini zaidi katika kipindi cha miaka 40 iliyopita. Aidha, kiwango hiki kilivuka lengo la nchi la kipindi cha muda wa kati la asilimia 5.0, lengo la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) la asilimia 7.0 na la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki la asilimia 8.0;
  - (ii) Uwepo wa utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine duniani kwa takriban miaka minne mfululizo;
  - (iii) Kuimarisha mizania ya malipo ya nje kwa kuongeza uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi kutoka dola za Kimarekani bilioni 5.33 mwaka 2015 hadi bilioni 5.57 mwaka 2019;
  - (iv) Kuimarisha akiba ya fedha za kigeni ambapo hadi Aprili 2020, akiba hiyo ilifikia Dola za Kimarekani bilioni 5.3 kiasi ambacho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 6.2. Kiwango hiki kinavuka lengo la kuwa na akiba ya kutosha kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa muda usiopungua miezi 4;
  - (v) Kupungua kwa nakisi ya bajeti ya kutoka asilimia 3.5 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16 hadi asilimia 3.1 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19;
  - (vi) Kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ya kodi kutoka wastani wa shilingi bilioni 850 kwa mwezi mwaka 2015 na kufikia wastani wa shilingi trilioni 1.3 kwa mwezi mwaka 2019 na hivyo kuongeza uwezo wa Taifa kugharamia shughuli za maendeleo kwa ustawi wa Taifa;
  - (vii) Kuimarika kwa huduma za jamii, hususan uboreshaji wa utoaji huduma za afya, elimu bila malipo katika ngazi ya elimumsingi, ununuzi wa ndege na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya usafiri na usafirishaji kutokana na kuongezeka



kwa bajeti ya Serikali kutoka shilingi trilioni 25.7 mwaka 2015/16 hadi shilingi trilioni 33.1 mwaka 2019/20;

- (viii) Kupungua kwa utegemezi wa kibajeti kutokana na hatua za kuongeza makusanyo ya Serikali na hivyo kupunguza ruzuku ya washirika wa maendeleo kwenye bajeti ya Serikali kutoka asilimia 10.3 mwaka 2015/16 hadi asilimia 8 mwaka 2018/19;
- (ix) Kuhakikisha Deni la Taifa linabaki kuwa himilivu na mikopo inatumika kwa shughuli zenye tija; na
- (x) Kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji nchini kwa kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve Business Environment*) kwa kutatua changamoto zinazokabili uwekezaji na ufanyaji biashara.

**18. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya Mwaka 2020 - 2025, Chama kitaelekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kujenga uchumi wa kisasa, shirikishi na shindani, msingi wake mkuu ni viwanda utakaowezesha ustawi wa wananchi ambao wote kwa kuandaa na kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2021/22 - 2025/26 kwa kuzingatia yafuatayo:-
  - (i) Kuongeza tija, ufanisi na ubora wa bidhaa na huduma ili kuwa shindani katika soko la ndani na la nje na hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa;
  - (ii) Kuongeza uzalishaji na fursa za ajira;
  - (iii) Kuimarisha mazingira ya uchumi na biashara kwa kuendelea kufanya mageuzi kwenye sheria, kanuni, tozo na utendaji wa sekta ya Umma kulingana na mwongozo wa kuboresha mazingira ya biashara nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*);
  - (iv) Kuongeza kasi ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa kuendelea kujenga na kuimarisha miundombinu na huduma muhimu na wezeshi zikiwemo maji na nishati;
  - (v) Kuongeza mchango wa uchumi wa rasilimali za maji (*blue economy*) katika kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, kutengeneza fursa za ajira na kupunguza umasikini wa kipato;
  - (vi) Kuendeleza rasilimali za asili za Taifa ili ziweze kuchangia ipasavyo katika uchumi wa nchi na maendeleo ya watu wake;





- (vii) Kuimarisha zaidi Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kusimamia mashirika ya umma ipasavyo;
  - (viii) Kuimarisha mashirika ya umma ili yaweze kuendelea kutoa michango katika maendeleo ya Taifa;
  - (ix) Kuendeleza uchumi wa kidigitali (*digital economy*) ili uweze kuchochea maendeleo ya sekta za kiuchumi na kijamii nchini;
  - (x) Kuimarisha matumizi ya sayansi na teknolojia katika kuleta maendeleo; na
  - (xi) Kuimarisha utafiti, ubunifu na ujuzi kama kitovu na injini ya uchumi.
- (b) Kuweka sera madhubuti za uchumi jumla ili:-
- (i) Kukuza uchumi kwa wastani usiopungua asilimia 8 kwa mwaka;
  - (ii) Kutekeleza mikakati itakayoimarisha utulivu wa uchumi kwa kuwa na mfumko wa bei kwa kiwango kisichozidi wigo wa tarakimu moja;
  - (iii) Kupunguza utegemezi wa kibajeti kwa kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, ikiwemo kuibua vyanzo vipya vya mapato; kuongeza idadi ya walipakodi; kuboresha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara; na kukusanya maduhuli yote kwa kutumia mifumo ya kielektroniki;
  - (iv) Kuboresha mfumo wa uendeshaji wa taasisi za umma na usimamizi wa matumizi ya Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuondoa matumizi yasiyo na tija kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa;
  - (v) Kuongeza wigo wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia mfumo wa Ubia Baina ya Serikali na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership - PPP*);
  - (vi) Kuhakikisha kuwa Deni la Taifa linaendelea kuwa himilivu na mikopo inatumika katika miradi yenye tija;
  - (vii) Kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kutumia ipasavyo fursa za upatikaji wa rasilimali fedha katika mifuko ya kikanda na kimataifa inayoshughulika na masuala hayo;



- (viii) Kuimarisha sera, sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa mali na fedha za umma;
- (ix) Kuweka sera madhubuti za fedha (*monetary policies*) zitakazowezesha ukwasi stahiki katika uchumi; utulivu wa riba za soko la fedha; utulivu wa thamani ya sarafu yetu; na kupungua kwa gharama ya mikopo na kushusha riba;
- (x) Kukuza uuzaji wa bidhaa zilizoongezewa thamani nje ya nchi ili kuwezesha upatikanaji wa fedha za kigeni kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa za mtaji kwa ajili ya ujenzi wa miradi mikubwa bila kuteteresha urari wa malipo ya kawaida katika mizania ya malipo ya nje; na
- (xi) Kukuza sekta za huduma hususan utalii ili kutumia fursa zilizopo kikamilifu na kuongeza mchango wake katika uchumi wa Taifa.

### **Sekta ya Fedha**

19.

Kutokana na umuhimu wa sekta ya fedha katika kuchochea shughuli za kijamii na kiuchumi, katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020, Chama kiliendelea kuisimamia Serikali kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha huduma za fedha kwa wananchi. Hatua hizi zimeongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma za fedha nchini kutoka asilimia 58 mwaka 2013 hadi kufikia asilimia 65 mwaka 2017. Jitihada zilizofanyika ni pamoja na:-

- (a) Kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi ya kusimamia sekta ya fedha, iliyosaidia kurahisisha matumizi ya huduma za kifedha kwa wananchi kwa kutekeleza yafuatayo:-
  - (i) Kutungwa kwa Sheria ya Mifumo ya Malipo ya mwaka 2015 ambayo imewezesha taasisi za fedha na kampuni za simu kutoa huduma za fedha kupitia simu za viganjani. Hii imewezesha watumiaji kuongezeka kutoka 19,006,176 mwaka 2015 hadi watumiaji 23,964,458 mwaka 2020, huku miamala ikiongezeka na kufikia takriban wastani wa miamala 234,921,601 kwa mwezi kwa mwaka 2020 kutoka wastani wa miamala 115,674,176 kwa mwezi mwaka 2015;
  - (ii) Kuimarisha huduma za kifedha kwa wananchi kutokana na kutungwa kwa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017 na kanuni zake za mwaka 2019 pamoja na kuboresha usimamizi wa taasisi za kifedha na maadili ya watumishi wa taasisi hizo ili kumlinda mteja. Taasisi hizo ni pamoja na: taasisi zinazotoa huduma ndogo za fedha zisizopokea amana; wakopeshaji binafsi; mifuko na programu za Serikali zinazofanya biashara ya huduma ndogo za fedha; Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa (SACCOS) na vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii kama vile VICOBA na VISLA (*Village Savings and Loan Association*);



- (iii) Kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaopata huduma za kifedha kutokana na kutekelezwa kwa Mpango Mkakati wa Taifa wa Kwanza na wa Pili wa Huduma Jumuishi za Fedha;
  - (iv) Kuimarishwa kwa upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu, huduma za amana na mikopo kwa gharama nafuu, upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo ili waweze kuwekeza katika maeneo mbalimbali na kujikwamua kiuchumi kwa kuziimarisha na kuziongezea mitaji benki za maendeleo na biashara za Serikali; na
  - (v) Kuimarishwa kwa benki za maendeleo ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ambayo ni mahsusi kwa ajili ya kutoa mikopo ya kilimo kwa wakulima, ambapo benki hiyo imeendelea kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kufungua matawi Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya na Mwanza.
- (b) Kuimarishwa na kuendelezwa kwa mifuko mbalimbali na programu maalum za kusaidia wananchi wenye kipato cha chini na wenye mahitaji maalum ili waweze kuondokana na umasikini;
  - (c) Kuwezesha utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali wadogo kwa kuanzisha na kuendeleza mifuko inayotoa dhamana kwa benki na taasisi za fedha ikiwemo: Mfuko wa Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo; Mfuko wa Kudhamini Mikopo ya Mauzo Nje ya Nchi; Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa Wakulima Wadogo; Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa Wajasiriamali katika Sekta ya Kilimo; Mfuko wa Mikopo Midogo ya Nyumba; na Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati;
  - (d) Kuwezesha ongezeko la huduma za uwakala wa benki (*agent banking*) kutoka mawakala 3,299 mwaka 2015 hadi kufikia takriban 28,358 mwaka 2020; na
  - (e) Kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Kutoa Elimu ya Fedha kwa Umma wa Mwaka 2015 - 2019, elimu iliyotolewa imechangia yafuatayo:-
    - (i) Kuongezeka kwa mwamko wa wananchi kushiriki kwenye masoko ya mitaji ambapo, kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi mwaka 2020, jumla ya shilingi bilioni 586.53 zilipatikana kama mtaji kwa makampuni mbalimbali kutokana na kuuza hisa kwa umma. Makampuni hayo ni pamoja na Vodacom Tanzania, Benki ya - Yetu Microfinance, Benki ya Biashara ya Mwalimu, Benki ya MUCOBA, Kampuni ya Uwekezaji ya TCCIA; Kampuni ya NICOL, Benki ya Biashara ya DCB, Benki ya Biashara ya Akiba, na Benki ya Maendeleo;
    - (ii) Mafanikio katika Soko la Hatifungani ambapo jumla ya shilingi bilioni 176.00 zilikusanywa kutokana na mauzo ya



hatifungani kwa umma zilizotolewa na NMB, Benki ya Exim, Kampuni ya TMRC (*Tanzania Mortgage Refinance Company*) na Benki ya Biashara na Maendeleo ya Mashariki na Kusini mwa Afrika (TDB). Aidha, katika kipindi cha kuanzia 2015 hadi 2019 jumla ya hatifungani za shilingi trilioni 10.89 zilitolewa kwa umma na kuorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam;

- (iii) Kuimarika kwa Soko la Kukuza na Kuendeleza Ujasiriamali (*Enterprise Growth Market - EGM*) ambapo, hadi mwaka 2019, jumla ya shilingi bilioni 88.4 zilipatikana kwa njia ya kuuza hisa kwa umma na kuorodheshwa kwenye soko la hisa; na
- (iv) Kukua kwa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) ambapo, hadi mwaka 2020, kampuni 28 zilizoorodheshwa kwenye soko zilitoa gawio la shilingi trilioni 2.95 kwa wanahisa.

- (f) Kupambana na makosa ya kiuchumi ikiwemo utakatishaji wa fedha haramu, kama vile fedha zinazotokana na madawa ya kulevywa na utengenezaji na usambazaji wa fedha bandia.

20.

**Katika kipindi cha mwaka 2020 - 2025, Chama Cha Mapinduzi kitaelekeza Serikali kuzingatia yafuatayo katika kuimarisha sekta ya fedha:-**

- (a) Kusimamia misingi ya kiseria, kisheria na kanuni za usimamizi wa sekta ya fedha;
- (b) Kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa gharama nafuu kwa kupanua wigo wa matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kifedha ili kuongeza huduma jumuishi za fedha nchini, kuchochea uwekezaji wa ndani na kukidhi mahitaji halisi ya wananchi hususan wa kipato cha chini na waishio vijijini;
- (c) Kupunguza vikwazo vya ushirikishwaji wa Watanzania kwenye mfumo rasmi wa fedha, ikiwemo kuimarisha ulinzi wa watumiaji wa huduma za kifedha (*consumer protection*) kwa kukamilisha na kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha 2019/20 - 2029/30;
- (d) Kuboresha na kuimarisha huduma za kifedha zikiwemo benki, masoko ya mitaji, bima na huduma ndogondogo za kifedha na utendaji wa taasisi za sekta ya fedha na kodi ili ziendeele kutoa mchango mkubwa katika ukuzaji wa uchumi wa Taifa. Taasisi hizo ni pamoja na Benki kuu ya Tanzania (BoT), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA);
- (e) Kuweka mazingira wezeshi kwa sekta ya bima kukua zaidi, kuwanufaisha wananchi wengi na kuchangia katika uchumi kwa kiwango kikubwa zaidi;



- (f) Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya mashirika na taasisi zilizobinafsishwa ili kuhakikisha mikataba inatekelezwa ipasavyo;
- (g) Kuongeza ubunifu katika upatikanaji wa rasilimali fedha inayohitajika ili kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo kukuza na kuimairisha masoko ya mitaji;
- (h) Kuongeza udhibiti wa huduma za kifedha na mapambano dhidi ya fedha haramu ili kupambana na uhalifu na kujenga uhimilivu katika mfumo wa kifedha; na
- (i) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuimarisha mahusiano ya taasisi za kifedha za kikanda na kimataifa katika utekelezaji wa sera za fedha ili kuwezesha Watanzania kunufaika na fursa mbalimbali.

### **Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Uwekezaji**

21.

Chama Cha Mapinduzi kinatambua umuhimu wa sekta binafsi katika kuleta maendeleo kwa kuwa sekta hii ni moja ya nguzo muhimu za kujenga uchumi wa viwanda na maendeleo ya sekta nyinginezo za kuichumi na kijamii inaposhirikiana na Serikali katika uwekezaji. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015-2020), Chama kimeendelea kuchukua hatua za kuhakikisha Serikali inaishirikisha na kuiwezesha sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji, hususan katika miradi ambayo inaweza kuendeshwa kibiashara. Katika kipindi hicho, mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- (a) Kuimarisha uratibu na usimamizi wa masuala ya uwekezaji kwa kuanzisha Ofisi ya Waziri wa Nchi yenye dhamana ya uwekezaji katika Ofisi ya Waziri Mkuu;
- (b) Kuongezeka kwa usajili wa miradi ya uwekezaji ya ndani na ya kutoka nje ipatayo 1,307 kwa kipindi cha mwaka 2016 - 2019 yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 14.607. Miradi inakadiliwa kuzalisha ajira 183,503. Zaidi ya asilimia 50 ya miradi hiyo ilikuwa katika sekta ya uzalishaji viwandani;
- (c) Kuimarishwa kwa ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuwezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo kwa kuimarisha mfumo na muundo wa majadiliano kupitia Baraza la Taifa la Biashara na mabaraza ya biashara ya mikoa na wilaya, ambao uliwezesha mikutano ya mashauriano baina ya Serikali, wafanyabiashara na wawekezaji katika mikoa;
- (d) Kuongezeka kwa ushiriki wa wananchi katika miradi mikubwa ya kimkakati kwa kutekeleza Mwongozo wa Kitaifa wa Ushiriki wa Watanzania katika miradi hiyo;
- (e) Kuimarishwa kwa jitihada za kubaini na kunadi fursa za uwekezaji kwa ngazi za mikoa kwa kuandaa Miongozo ya Uwekezaji ya Mikoa



(*Regional Investment Guides*) ambapo hadi mwaka 2020, miongozo 13 ya mikoa ya Dodoma, Geita, Simiyu, Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Mwanza, Pwani, Morogoro, Ruvuma, Mtwara, Songwe na Lindi ilizinduliwa;

- (f) Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*) ambapo baadhi ya maboresho yaliyofanyika ni pamoja na:-
- (i) Kufutwa kwa jumla ya tozo kero 168, zikiwemo tozo 114 za sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi;
  - (ii) Kuongeza ufanisi katika ukaguzi na uidhinishaji wa bidhaa kwa kuhuisha majukumu ya Shirika la Viwango (TBS) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na hivyo kuondoa mwingiliano wa majukumu;
  - (iii) Kuimarika kwa biashara na nchi jirani kutokana na kuanzishwa kwa Kituo kimoja cha utoaji huduma bandarini kinachofanya kazi saa 24 na kuanzishwa kwa vituo vya utoaji wa huduma kwa pamoja vya mipakani (*one stop border posts*);
  - (iv) Kupunguza muda wa kupata cheti cha usajili wa sehemu za kazi kutoka siku 14 mwaka 2015 hadi siku moja mwaka 2020; na
  - (v) Kuimarisha mifumo ya utoaji huduma kwa njia ya kieletroniki kwa wizara na taasisi za umma.

22.

**Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuweka msisitizo katika kujenga sekta binafsi iliyo bora, inayoshirikiana na Serikali katika kutoa mchango wenye manufaa kwa Taifa. Vilevile, Chama kitasimamia Serikali ili kuhakikisha watendaji wanakuwa na mtazamo chanya juu ya sekta binafsi na kuhakikisha inashirikishwa kikamilifu katika uwekezaji, hususan katika viwanda kwa kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*) ili kuendelea kuvutia sekta binafsi kushiriki katika uwekezaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuiweka nchi katika nafasi nzuri kwenye mizania ya kimataifa ya wepesi wa kufanya biashara;
- (b) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kubaini na kusuluhisha changamoto mpya zitakazojitokeza ambazo hazipo kwenye Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*);





- (c) Kuweka utaratibu wa kuufanyia mapitio Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*) angalau kila baada ya miaka miwili na kutoa nafasi kwa Tanzania kujipima yenyewe na sio kutegemea mizania ya kimataifa pekee;
- (d) Kuweka mazingira wezeshi kwa kampuni za kitanzania kukua na kuimarika ili yaweze kuwa shindani zaidi katika miradi ya kimkakati;
- (e) Kuhamasisha sekta kutumia sayansi, teknolojia na ubunifu nchini (*science, technology and innovation - STI*) na kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kufanya uwekezaji kwenye taasisi za utafiti wa teknolojia za kisasa hasa *4<sup>th</sup> industrial revolution*;
- (f) Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kuendeleza uwekezaji na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kwa kushirikisha sekta binafsi;
- (g) Kuimarisha miundombinu wezeshi ya kiuchumi kama vile nishati ya umeme na miundombinu ya usafiri na usafirishaji;
- (h) Kuimarisha huduma za kiuchumi ikiwemo huduma za kifedha na kuwezesha upatikanaji wa mitaji;
- (i) Kuimarisha upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji kwa kuhimiza Mamlaka za Serikali kutenga maeneo ya uwekezaji, kulipa fidia na kuweka miundombinu ya msingi ili kufanikisha uwekezaji;
- (j) Kuondoa urasimu na dosari zinazosababisha ucheleweshaji wa utoaji wa mizigo bandarini na kuongezeka kwa gharama zisizokuwa za lazima kwa wawekezaji na wafanyabiashara;
- (k) Kutenga ardhi ya kutosha (Hazina ya Ardhi) kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje na kuiweka chini ya Kituo cha Uwekezaji (TIC) ili kurahisisha uwekezaji nchini;
- (l) Kupitia upya taratibu za utoaji vibali vya ujenzi ili kuhakikisha kwamba vibali hivyo vinatolewa ndani ya siku saba za kazi; na
- (m) Kuhamasisha sekta binafsi kuzingatia malengo ya Mkakati wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa (NACSAP III) na kuishirikisha katika tathmini ya utekelezaji wake na katika maandalizi ya mkakati utakaofuata.

### **Kupambana na Umasikini na Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi**

23. Umasikini ni moja ya maadui wa maendeleo ambao Chama kimeendelea kupambana nao kwa nguvu zote. Katika kipindi cha mwaka 2015-2020, Chama Cha Mapinduzi kiliendelea kusimamia Serikali kutekeleza sera na



mipango mbalimbali yenye lengo la kuinua ubora wa maisha, ustawi wa jamii, hifadhi ya jamii na kupunguza umasikini. Mikakati ya kupambana na umasikini iliyochukuliwa ni pamoja na kuhakikisha wananchi wanapata fursa za kuendesha maisha yao kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kuandaa na kutekeleza programu mbalimbali za kukabiliana na umasikini na ukosefu wa ajira hususan vijana na wanawake.

24. Hatua hizo zimewezesha umasikini wa mahitaji ya msingi kupungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 26.4 mwaka 2017/18. Aidha, kiwango cha maendeleo ya watu kimeimarika kutokana na kuboreshwa kwa huduma za jamii zikiwemo za afya, elimu na kipato cha mwananchi. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na:-

### ***Ujasiriamali***

- (a) Kuimarishwa kwa vyama vyenye mwelekeo wa ushirika ambapo vikundi vya vijana vilivyoandikishwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika skimu mbalimbali vimeongezeka kutoka vikundi 56,120 mwaka 2015 hadi 156,520 mwaka 2020 ambapo wanachama wameongezeka kutoka 32,140 mwaka 2015 hadi 560,600 mwaka 2020. Miongoni mwa skimu hizo ni pamoja na Wakulima Skimu, Boda Boda Skimu, Wavuvi Skimu, Madini Skimu, Mashambani Skimu, Mama Lishe Skimu na Toto Card;
- (b) Kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wajasiriamali 3,035 katika mikoa 26 yote ya Tanzania Bara ambapo shilingi bilioni 2.05 zimetolewa na Benki ya Posta Tanzania kama mikopo. Aidha, Halmashauri 185 zimetoa shilingi bilioni 93.3 katika Mfuko wa Kuwawezesha Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu na hivyo kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi vya wajasiriamali 32,553;
- (c) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo ambapo Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali (NEDF) uliopo chini ya SIDO hadi mwaka 2019 ulitoa mikopo kwa wananchi 90,862 yenye thamani ya shilingi bilioni 71.87 na kutengeneza ajira zipatazo 184,542 katika sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, madini na uzalishaji. Aidha, Mfuko wa Dhamana wa Mikopo kwa Wajasiriamali katika Sekta ya Kilimo (SIDO SME-CGS) umetoa udhamini wa mikopo 33 yenye thamani ya shilingi 1,048,000,000 kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Arusha, Kigoma, Mwanza, Singida, Mbeya, Iringa, Njombe, Tanga na Manyara;
- (d) Kuwezesha wajasiriamali wa misitu kushiriki katika shughuli za misitu kupitia Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) ambapo hadi kufikia mwaka 2019 mfuko ulikuwa umetoa ruzuku yenye thamani ya shilingi 6,215,743,987 kwa miradi 51.4. Kati ya miradi hiyo, 244 ni ya kuongeza kipato cha jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu,





miradi 235 ni ya uhifadhi, uendelezaji na usimamizi wa misitu na 35 ni ya utafiti katika misitu;

- (e) Kuongezeka kwa wananchi waliojiunga na vikundi vya kuweka na kukopa ambapo vikundi 449 vya kuweka na kukopa (SACCOS na VICOBA) vya wajasiriamali vyenye wanachama 11,643 wakiwemo wanawake 9,564 na wanaume 2,079 vilianzishwa katika mikoa ya Kilimanjaro, Njombe, Morogoro, Tabora, Katavi, Rukwa na Geita na SACCOS 130 za wanawake zilianzishwa katika mikoa 16 ya Mara, Mwanza, Tanga, Kigoma, Dodoma, Kagera, Shinyanga, Simiyu, Rukwa, Ruvuma, Mbeya, Lindi, Mtwara, Geita, Manyara na Dar es Salaam;
- (f) Kuhamasisha maendeleo ya ushirika katika sekta ya kilimo kwa kufufua na kuanzisha vyama vipya vipatavyo 1,560. Vyama hivyo ni vya mazao ya Michikichi (Vyama 12 Kigoma); Pamba (Simiyu, Geita, Mwanza, Singida, Shinyanga, Tabora, Mara, Kigoma na Dodoma vyama 1,469 vimefufuliwa); Miwa (Manyara, Kagera-Missenyi, Morogoro-Mtibwa); Chai (Mbeya vyama 8) vimeanzishwa, Kakao (Mbeya vyama vya Msingi 53 na chama kikuu 1 vimefufuliwa na vyama vya msingi 6 vimeanzishwa); Korosho (Lindi vyama vya msingi 2 vimeanzishwa); na Kahawa (Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Songwe, Kagera, Mara, vyama 6 vimefufuliwa);
- (g) Kuwawezesha wajasiriamali kukuza uzalishaji na masoko ya bidhaa zao ndani na nje ya nchi kwa kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali, masoko na usimamizi wa biashara kwa wazalishaji wa bidhaa za ngozi, viungo vya chakula na wafanyabiashara wa mazao ya nyuki pamoja na wafugaji wa nyuki. Mikoa iliyonufaika na mafunzo hayo ni Shinyanga, Geita, Tabora, Singida, Kagera, Kigoma, Dar es Salaam, Pwani na Mwanza. Zaidi ya wajasiriamali 500 wamenufaika na mafunzo hayo;
- (h) Mfuko wa Pembejeo wa Taifa hadi mwaka 2019 umefanikiwa kutoa mikopo ya shilingi 82,097,446,770 ambayo imesaidia kuongeza kipato na kupunguza umasikini. Mikopo hii ilitolewa katika miradi 3,589 ambapo wanaume walionufaika ni 2,871 na wanawake 718;
- (i) Kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kushiriki katika uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ambapo Mfuko wa Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (*PASS Trust*) ulifanikiwa kudhamini miradi 20,355 yenye thamani ya shilingi billioni 470.8 kwa walengwa 679,892 na kutengeneza ajira zipatazo 1,534,994. Wanufaika wa mfuko huu ni wajasiriamali wanaojishughulisha na miradi mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa kilimo; na
- (j) Kuanzishwa kwa Kanzidata ya watoa huduma katika sekta ndogo ya mafuta na gesi. Zaidi ya kampuni 400 zimesajiliwa na EWURA



ili kuwawezesha kutoa huduma na kuuza bidhaa katika miradi inayotekelezwa kwenye sekta ndogo ya mafuta na gesi.

### **Wafanyabiashara Wadogo**

- (a) Kutengwa kwa maeneo rasmi yenye ukubwa wa hekta 15,822.64 kwa ajili ya wajasiriamali wakiwemo mama lishe na wauza mbogamboga kufanyia biashara katika mikoa 19 ya Arusha, Iringa, Mara, Rukwa, Tanga, Shinyanga, Mwanza, Kilimanjaro, Singida, Morogoro, Manyara, Njombe, Kagera, Dar es Salaam, Dodoma, Lindi, Geita, Tabora na Ruvuma;
- (b) Kuwezesha wafanyabiashara wadogo kufanya biashara zao bila bughudha kwa kutoa vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo zaidi ya 1,527,323 katika mikoa yote Tanzania bara; na
- (c) Kuongezeka upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara wadogo wadogo ambapo Mfuko wa SELF (*Small Entrepreneur Loan Facility*) Microfinance umetoa mikopo yenye thamani ya zaidi ya shilingi billioni 26 kwa wajasiriamali na kutengeneza ajira zaidi ya 13,000 kwa wanufaika.

### **Kuwawezesha Vijana**

- (a) Kuongeza ujuzi katika stadi za kazi ambapo vijana 7,800 wa kada mbalimbali wamehamasishwa na kujiunga na programu za kujitolea. Aidha, wahitimu 5,975 wamewezesha kushiriki mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi, ambapo kati ya hao, vijana 1,827 wamepata ajira;
- (b) Kuwawezesha vijana 52,353 kumudu ushindani katika soko la ajira kwa kuwapatia mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kupitia programu ya kukuza ujuzi nchini. Aidha, vijana 28,941 wamepatwa mafunzo kwa njia ya uanagenzi katika fani za ufundi stadi wa ushonaji nguo, useremala, uashi, TEHAMA, uchongaji wa vipuri, ufundi magari, umeme, ufungaji wa mabomba, vyuma, terazo, vigae na ujuzi wa kutengeneza bidhaa za ngozi. Vilevile, vijana 14,432 wamepatwa mafunzo ya kurasimisha ujuzi uliopatikana kwa mfumo usio rasmi kwa fani za uashi, useremala, ufundi magari, upishi na uhudumu katika hoteli;
- (c) Vijana 8,980 wamepatwa mafunzo ya kilimo kwa njia ya teknolojia ya kitalu nyumba;
- (d) Kuongezeka kwa fursa za ajira kwa vijana kwa kuanzisha makampuni 217 ya vijana ambapo 76 yameunganishwa na PPRA kwa ajili ya kupata zabuni. Aidha, idadi ya vijana waliopatiwa mafunzo ya ujasiriamali na uanzishwaji wa makampuni imeongezeka kutoka vijana 5,250 mwaka 2015 hadi 13,500 mwaka 2020; na



- (e) Kuongezeka utoaji wa mikopo kwa vijana katika halmashauri zote nchini ambapo mitaji ya biashara imeongezeka kutoka shilingi bilioni 2.3 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 28.2 mwaka 2020.

**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF**

25. Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kusimamia Serikali kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kutekeleza Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III) katika kukabiliana na changamoto za umasikini kwa wananchi ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- (a) Miradi ya jamii 7,725 ya kutoa ajira za muda yenye thamani ya shilingi bilioni 83.3 imetekelezwa. Aidha, miradi 615 ya kuboresha miundombinu katika Sekta ya Afya, Elimu na Maji yenye thamani ya shilingi bilioni 24.6 imetekelezwa katika Halmashauri 67;
- (b) Jumla Shilingi Bilioni 931.6 zililipwa kama ruzuku kwa kaya masikini milioni 1.1 katika vijiji/mitaa 9,627 katika halmashauri 159 kati ya 185 zilizopo. Ruzuku hiyo iliwezesha kaya masikini kumudu mahitaji ya msingi na kuanzisha shughuli za kukuza uchumi wa kaya ikiwemo miradi ya kilimo, mifugo na biashara ndogo ndogo; na
- (c) Vikundi 15,349 vya kuweka akiba na kuwekeza vyenye wanachama 214,495 viliundwa kwenye halmashauri 44 na kuweza kuweka akiba ya shilingi Bilioni 2.5 na kukopeshana shilingi bilioni 1.6 ili kutekeleza miradi ya kukuza uchumi wa kaya na hivyo kupunguza umasikini katika kaya husika. Aidha, miradi 405 ya kuongeza kipato ilitekelezwa na vikundi hivyo.

26. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuchukua hatua za kuhakikisha wananchi wanaendelea kuwekewa mazingira mazuri ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo kwa kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kutoa msukumo katika kuhamasisha na kusimamia uanzishwaji na usajili wa vikundi vyenye mwelekeo wa ushirika na makampuni pamoja na kuwawezesha kupata mitaji kupitia mikopo yenye masharti nafuu;
- (b) Kufuatilia kwa karibu utoaji wa elimu ya ujasiriamali unaofanywa na wadau mbalimbali ili kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa inakidhi viwango;
- (c) Kuwezesha vijana, wanawake na makundi mengine ya wajasiriamali kujiajiri kwa kuwapatia mafunzo na stadi za ujasiriamali na usimamizi wa shughuli za kiuchumi na kuwezesha kurasimisha shughuli zao ifikapo mwaka 2025;



- (d) Kuimarisha mifuko na programu zinazolenga kuwezesha kiuchumi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili waweze kujiajiri na kutoa ajira kwa wengine;
- (e) Kuwa na programu maalum za kuwezesha vijana waliomaliza taasisi za elimu ya juu na kati kujiajiri na kuajirika. Programu hizo zinalinga kuweka mazingira ya vijana kupata mitaji, elimu ya ujasiriamali, ardhi na mazingira wezeshi kuweza kushiriki kikamilifu katika shughuli wanazokusudia kuzifanya;
- (f) Kuanzisha utaratibu wa kuwakopeshwa vifaa na mitaji kwa masharti nafuu wanafunzi wanaohitimu mafunzo ya ufundi;
- (g) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuhakikisha kuwa elimu ya ujasiriamali inayotolewa na wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi na Asasi za Kiraia ina ubora unaokidhi mahitaji ya vijana na walengwa wengine;
- (h) Kuanzisha kanzidata ya watoa huduma katika miradi mikubwa ya kimkakati na kutoa elimu kwa umma juu ya ushiriki wa wajasiriamali katika miradi hiyo. Kanzidata hii itawezesha kuunganisha sekta binafsi na wawekezaji au wakandarasi na hivyo kuwawezesha kupata masoko ya bidhaa zao na kufanya kazi kwa ubia na kampuni za nje ili kukuza ujuzi na kuhaulisha teknolojia;
- (i) Kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi shirikishi kwa kutoa fursa kwa wananchi wote kuinua hali ya maisha yao;
- (j) Kushirikiana na wadau kuanzisha vituo vya uendelezaji wajasiriamali (*enterprise development centres*) kwa lengo la kuwajengea uwezo na kuwawezesha wananchi kupata ithibati za kimataifa ili kupanua wigo wa fursa za ajira na biashara;
- (k) Kuanzisha vituo vya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi katika kila mkoa. Vituo hivyo vitatoa huduma za mikopo, mafunzo, urasimishaji wa shughuli za kiuchumi, upatikanaji wa taarifa mbalimbali zikiwemo za masoko na kutoa ithibati ya bidhaa zinazozalishwa;
- (l) Kuimarisha viwanda vilivyopo na kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vipya vya kuchakata mazao ya kilimo, mifugo na samaki na rasilimali nyingine za maji kwa kutumia taasisi za umma, sekta binafsi na vikundi vilivyosajiliwa na vyama vya ushirika;
- (m) Kujumuisha urasimishaji wa mali na biashara za wananchi hasa wanyonge katika ngazi za mamlaka za serikali za mitaa, hivyo kuongeza kasi ya kuwawezesha Wananchi wengi zaidi kuondokana na umasikini kwa kutumia mali zao kama dhamana ya kupata mikopo na mitaji kutoka kwenye vyombo vya fedha; na



- (n) Kuboresha kasi ya utekelezaji Awamu ya Tatu ya TASAF ili kuwafikia wananchi masikini katika vijiji/mitaa yote kwa kutekeleza miradi ya kutoa ajira za muda, kukuza uchumi wa kaya na kuendeleza rasilimali watu.

### **Uchumi wa Rasilimali za Maji (Blue Economy)**

**Chama Cha Mapinduzi kinatambua fursa zilizopo katika uchumi wa rasilimali za maji (*blue economy*), zikiwemo bahari, mito na maziwa pamoja na rasilimali zilizomo ndani yake. Katika kutumia fursa hizi, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaelekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kuimarisha miundombinu ya bandari na shughuli nyingine za lojistiki na uchukuzi ili Taifa letu liwe kitovu cha shughuli hizi;
- (b) Kuimarisha mifumo ya kitaasisi ya kuratibu na kusimamia maendeleo ya uchumi wa rasilimali za maji (*blue economy*);
- (c) Kufanya utafiti kwa lengo la kuendeleza uchumi wa rasilimali za maji; na
- (d) Kuandaa mkakati utakaowezesha Taifa kunufaika na uchumi wa rasilimali za maji.

### **Kutumia Fursa za Kijiografia za Nchi Yetu Kuchochea Maendeleo**

Tanzania ina fursa nyingi zinazotokana na nafasi yake kijiografia kwa kuwa imezungukwa na nchi sita ambazo zinategemea miundombinu yetu kwa kiasi kikubwa kwa usafiri na usafirishaji wa bidhaa. Mazingira hayo yameendelea kuchangia kukuza biashara na uchumi baina ya nchi yetu na nchi jirani. Hatua hii imewezesha miundombinu kutumika kwa faida, ajira na mapato ya fedha za kigeni kuongezeka.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), Chama Cha Mapinduzi kimeisimamia Serikali na kuweza kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo:-

- (a) Kuimarisha miundombinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na huduma za bandari, viwanja vya ndege, reli, meli, vivuko, gati na njia za usafirishaji umeme. Aidha, mtandao wa barabara kuu za lami pamoja na madaraja yanayounganisha nchi yetu na nchi jirani yameboreshwa na hivyo, kurahisisha usafiri na usafirishaji kwa mfano mizigo ambayo imesafirishwa kwenda nchi jirani kupitia bandari zetu imefikia tani 5,197,252 mwaka 2020;
- (b) Kuimarishwa kwa huduma za mawasiliano kwa wananchi ambapo Tanzania imekuwa kitovu cha mawasiliano katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kati kutokana na kuimarishwa kwa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Nchi za jirani zilizounganishwa na Mkongo huo ni



Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi na Zambia na pia Mikongo ya Baharini ya SEACOM na EASSy inayotuunganisha na mabara mengine;

- (c) Makubaliano ya kihistoria ya kikanda kati ya Tanzania na Uganda yamefanyika ambapo ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) litajengwa;
- (d) Kujenga vituo vya pamoja vya huduma mipakani vya Namanga, Mutukula, Rusumo, Tunduma/Nakonde ili kuchochea zaidi manufaa ya kijiografia ya nchi yetu; na
- (e) Kurejeshwa kwa huduma ya usafirishaji wa mizigo kwenye mabehewa (*Wagon Ferry*) kutoka Mwanza hadi Bandari ya *Port Bell*, Uganda. Utoaji wa huduma za meli hii ulikoma mwaka 2008 na kurejeshwa tena mwaka 2018.

30. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha Serikali inachukua hatua ili Taifa liendeleo kunufaika na fursa zake za kijiografia kwa kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kubuni na kukamilisha miradi mikubwa ya kimkakati ili Tanzania iweze kunufaika zaidi na fursa hiyo ya kijiografia;
- (b) Kuboresha na kuimarisha diplomasia ya kiuchumi kwa lengo la kudumisha uhusiano wenye tija kiuchumi na nchi zinazotuzunguka;
- (c) Kubuni mikakati itakayowezesha kuimarika kwa Jiji la Dar es Salaam kuwa kitovu cha biashara kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati;
- (d) Kubuni na kutekeleza mikakati itakayowezesha kuainisha maeneo yote ambayo yatakuwa na manufaa kiuchumi ili kuweza kuzitumia fursa hizo kwa ajili ya kukuza uchumi; na
- (e) Kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji na shughuli nyingine za lojistiki na uchukuzi ili Taifa letu liweze kutumia fursa za kijiografia ipasavyo.

### **Kuongeza Fursa za Ajira**

31. Uwepo wa fursa za ajira ni muhimu katika kukuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii, ambapo jamii hususan vijana hupewa nafasi ya kuchangia utalaam walionao katika kufanya kazi ili kuchangia katika kukuza maendeleo ya Taifa lao. Chama Cha Mapinduzi kinatambua umuhimu huo na katika miaka mitano iliyopita (2015-2020), kiliendelea kutekeleza mikakati thabiti ya kuongeza fursa za ajira nchini. Kutokana na utekelezaji uliofanyika, mafanikio makubwa yamepatikana yakiwemo:-

- (a) Kuongezeka kwa ajira kutokana na kukua kwa uchumi katika sekta mbalimbali za uzalishaji na utoaji huduma pamoja na kutekeleza mikakati na mipango mbalimbali ikiwemo Mpango wa Kuboresha





Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*);

- (b) Kulinda ajira za Watanzania na kuhakikisha kuwa ajira wanazopewa wageni ni zile tu ambazo Watanzania hawana ujuzi nazo. Vilevile, kuzingatia kuwa Watanzania wanafundishwa ujuzi ambao hawana ili kuzimudu kazi hizo pindi muda wa kibali utakapomalizika kwa kuendelea kusimamia Sheria Namba 1 ya mwaka 2015 ya Kuratibu Ajira za Wageni Nchini (*The Non-Citizens (Employment Regulation) Act No. 1 of 2015*);
- (c) Kukuza ujuzi katika sekta muhimu za kipaumbele ikiwemo kilimo, ujenzi, ukarimu, teknolojia ya habari na utalii kwa kuendelea kutoa mafunzo. Kupitia hatua hii, yafuatayo yamefanyika:-
- (i) Mafunzo ya kukuza ujuzi katika maeneo ya kazi kwa njia ya uanagenzi (*apprenticeship*) ambapo washiriki 28,941 wamepatiwa mafunzo hayo;
  - (ii) Mafunzo ya uzoefu kazini kwa wahitimu (*internship*), 5,975 wa vyuo nchini ambapo wahitimu waliopata mafunzo 1,827 wamepata ajira za moja kwa moja;
  - (iii) Mafunzo ya kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo (*Recognition of Prior Learning Skills-RPL*), yametolewa kwa vijana 14,432;
  - (iv) Mafunzo ya kilimo cha kisasa cha kutumia teknolojia ya vitalu nyumba (*greenhouse*) yametolewa kwa vijana 8,980 katika Halmashari 84 za mkoa 12 nchini;
  - (v) Vijana 14,890 walio katika sekta isiyo rasmi wamepewa mafunzo ya ujasiriamali na kurasimisha biashara;
  - (vi) Wakulima na wafanyabiashara 9,300 wamepewa mafunzo ya uongezaji thamani mazao ya mifugo, kilimo biashara na masoko; na
  - (vii) Vijana 13,500 wamepewa mafunzo ya ujasiriamali pamoja na ya namna ya uanzishwaji na uimarishaji wa makampuni ilikinganishwa na vijana 5,250 mwaka 2015.
- (d) Kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali ya kuongeza ajira hususan kwa vijana ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-
- (i) Takriban fursa za ajira 6,032,299 zimezalishwa katika sekta rasmi na isiyo rasmi. Kati ya fursa hizo, ajira 1,975,723 zimezalishwa katika sekta rasmi ya umma na binafsi ikiwemo miradi ya maendeleo ya Serikali ambayo imezalisha jumla ya



- ajira 1,074,958 ambapo kati yake miradi ya maendeleo ya Serikali ya kimkakati imezalisha ajira 163,729 katika kipindi hicho. Ajira 4,056,576 zilizalishwa katika sekta isiyo rasmi;
- (ii) Mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya shilingi bilioni 17.9 imetolewa kwa vikundi vya vijana 535 vyenye wanachama 3,745 ili kuwawezesha vijana hao kupata mitaji ya kuanzisha biashara. Aidha, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana unaochangiwa asilimia nne ya mapato ya ndani ya mamlaka za serikali za mitaa umetoa shilingi bilioni 14.7 kwa vikundi vya vijana 2,026 vyenye wanachama 20,260;
  - (iii) Vijana 67,243 wamepatiwa mafunzo katika maeneo ya: kukuza ujuzi na stadi za kazi katika ujenzi; kurasimisha ujuzi uliopatikana kwa mfumo usio rasmi; na ujasiriamali na kurasimisha biashara;
  - (iv) Wahitimu 5,975 wamepata mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi katika fani walizosomea na vijana 1,827 wamepata ajira kutokana na uzoefu walioupata;
  - (v) Halmashauri za wilaya 111 zimetenga maeneo yenye ukubwa wa ekari 217.8 na kuwawezesha vijana kufanya shughuli mbalimbali ikiwemo kilimo, ufugaji, biashara na viwanda;
  - (vi) Makampuni 217 ya vijana yameanzishwa ambapo kati ya makampuni hayo 76 yamethibitishwa na kupewa kibali cha kuomba zabuni za Serikali; na
  - (vii) Kupitia programu ya stadi za maisha kwa vijana walio nje ya shule, wawezeshaji wa kitaifa 78 wameandaliwa na kutoa elimu hiyo kwa vijana 12,500 kwa njia ya elimu rika.
- (e) Kuongezeka fursa za ajira kutokana na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ambapo:-
- (i) Mradi wa ujenzi wa reli kwa kiwango cha *Standard Gauge* hadi mwaka 2020 ulikuwa umetoa ajira 14,139 ambapo 11,756 ni kwa Watanzania na 2,383 kwa wageni;
  - (ii) Mradi wa Ubungo *Interchange* hadi mwaka 2019 ulikuwa umetoa ajira 502 ambapo ajira 449 zilikuwa za Watanzania na ajira 53 zilikuwa za wageni ambao walikuwa wameajiriwa kwenye nafasi zenye ujuzi wa juu tu;
  - (iii) Upanuzi wa Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Julius Nyerere kwa kujenga *Terminal III* hadi mwaka 2019 ulikuwa umetoa ajira 1,056 ambapo Watanzania walikuwa 997 na wageni walikuwa 59; na





- (iv) Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere hadi mwaka 2020 ulikuwa umetoa jumla ya ajira 3,412 ambapo Watanzania ni 2,783 na wageni 629.

32. TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMBA

**Katika miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza Serikali kuongeza fursa za ajira katika sekta rasmi na isiyo rasmi zisizopungua milioni saba (7,000,000) kwa kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-**

- (a) Kuchochea ukuaji wa uchumi, hususan katika sekta ya viwanda vinavyotumia malighafi za kilimo, mifugo, uvuvi, madini, maliasili na sekta ya huduma za kiuchumi ikiwa ni pamoja na utalii;
- (b) Kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*) ili shughuli za uchumi na biashara ziongezeke na kuzalisha ajira;
- (c) Kuhamasisha na kusimamia halmashauri zote nchini kuendelea kutenga, kurasimisha na kupima na kuweka miundombinu kwenye maeneo maalum kwa ajili ya uwekezaji na kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili waweze kujishughulisha na uzalishaji mali na biashara;
- (d) Kuwawezesha vijana kushiriki katika shughuli za ujasiriamali, ikiwemo kuwapatia mafunzo na kuwaunganisha na taasisi na asasi za utoaji mikopo yenye riba na masharti nafuu;
- (e) Kuweka mkakati wa makusudi wa kuwawezesha vijana wabunifu na makundi mbalimbali ya vijana na wanawake kuanzisha shughuli za uzalishaji mali na ujasiriamali ili waweze kujijiri na kuajiri wengine;
- (f) Kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyo vya elimu ya juu na kati ili kuhakikisha vijana wanaohitimu wanapata maarifa na ujuzi wa kazi utakaowawezesha kujijiri na kuajirika;
- (g) Kuimarisha mifumo na kuongeza kasi ya kurasimisha ujuzi ili nguvukazi ya Taifa itumike ipasavyo katika soko la ajira la ndani na nje;
- (h) Kuwahamasisha na kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika utamaduni, michezo na sanaa kwa ajili ya kuongeza fursa za ajira na kipato;
- (i) Kuhakikisha kuwa miradi mikubwa ya kimkakati inaajiri vijana wengi zaidi wa Kitanzania.
- (j) Kuimarisha mifumo ya taarifa za soko la ajira na mitaji ili kuwawezesha vijana kutumia fursa hizo;
- (k) Kutoa mafunzo ya kukuza ujuzi na stadi mbalimbali za kazi kwa nguvukazi ya Taifa katika sekta za kipaumbele;



- (l) Kuimarisha SACCOS na makampuni ya vijana katika halmashauri zote nchini ili yaweze kupata mikopo kutoka kwenye benki na taasisi nyingine za kifedha ili waweze kujiajiri na kutoa ajira wengine;
- (m) Kuwawezesha vijana wanaohitimu elimu ya juu na vyuo vya ufundi kuunda makampuni kwa lengo la kuwapatia mitaji na nyenzo kupitia taasisi za fedha na mifuko mingine ya uwezeshaji;
- (n) Kuhamasisha na kuweka mazingira yatakayowezesha vijana wajasiriamali wadogo kujiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii ili kunufaika na mafao yanayotolewa na mifuko hiyo;
- (o) Kuanzisha vituo maalum ili kuwawezesha vijana kupata sehemu ya kujifunza kwa vitendo shughuli mbalimbali za ujasiriamali na kupata taarifa mbalimbali za maendeleo;
- (p) Kushirikiana na sekta binafsi katika kuwawezesha vijana wanaohitimu vyuo vikuu na vyuo vya kati kufanya kazi kwa kujitolea katika asasi mbalimbali kwa lengo la kuwapatia uzoefu na maadili ya kazi ili waweze kuajirika au kujiajiri;
- (q) Kuweka mazingira wezeshi ya kisera na kisheria kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali na huduma ili vijana wengi waweze kujiajiri;
- (r) Kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha sekta ya misitu kuzalisha ajira nyingi zaidi kupitia mazao mbalimbali yatokanayo na maliasili hiyo kama ufugaji wa nyuki;
- (s) Kuhakikisha kwamba halmashauri zote nchini zinaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa mujibu wa sheria ili kuwezesha vijana na makundi mengine katika jamii zetu kupata mikopo isiyo na riba.

### **Vyama vya Ushirika**

33.

Chama Cha Mapinduzi kinaamini kuwa ushirika ni njia ya uhakika ya kuwezesha wanachama kuwa na uwezo mkubwa wa kutatua matatizo yao ya kiuchumi na kijamii kwa kutumia juhudi zao za pamoja katika kufikia malengo ambayo yasingefikiwa kwa juhudi za mtu mmoja mmoja. Katika kipindi cha miaka mitano (2015 - 2020), Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ilijielekeza katika kuviimarisha na kuviwezesha vyama vya ushirika kuwa na uwezo wa kujiendesha kwa kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi kwa kuweka mifumo madhubuti ya ukusanyaji, uchambuzi na uenezaji wa taarifa za masoko na kutoa elimu juu ya uongezaji thamani na kupata mafanikio yafuatayo:-

- (a) Kuimarisha ushiriki wa wananchi kwenye vyama vya ushirika kwa kuhamasisha na kutoa elimu ya ushirika kwa umma na Vyama vya Ushirika ambapo idadi ya vyama vya ushirika imeongezeka kutoka



7,991 mwaka 2015 hadi 11,626 mwaka 2020 sawa na asilimia 45.5. Aidha, idadi ya wanachama wa Vyama vya Ushirika iliongezeka kutoka milioni 2.4 mwaka 2015 hadi milioni 5.9 Mwaka 2020 sawa na asilimia 146 ya ongezeko la wanachama;

- (b) Kuongezeka kwa idadi ya wanachama na wananchi wanaonufaika na huduma za kifedha kupitia vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOs). SACCOs zimeongezeka kutoka 4,206 mwaka 2015 na kufikia 6,178 mwaka 2020. Aidha, idadi ya wananchi waliojiunga na kunufaika na huduma za SACCOs imeongezeka kutoka 676,202 mwaka 2015 hadi 2,447,332 mwaka 2020;
- (c) Kuongezeka kwa mikopo iliyotolewa na SACCOs kwa wanachama wake kutoka Shilingi bilioni 854.3 mwaka 2015 hadi Shilingi trilioni 1.5 mwaka 2020 na mitaji ya SACCOs kupitia akiba, amana na hisa Shilingi bilioni 428.8 mwaka 2015 na kufikia Shilingi bilioni 819.0 mwaka 2020;
- (d) Kuongezeka kwa thamani ya bidhaa zinazozalishwa na wanaushirika kutokana na kuhamasisha na kuhimiza vyama vya ushirika kuanzisha na kufufua viwanda. Jumla ya viwanda 75 vya kuchakata mafuta ya alizeti na michikichi, kutengeneza samani za majumbani, kuchakata pamba na mazao ya nafaka vimeanzishwa na kufufuliwa katika maeneo mbalimbali ya nchi. Idadi hiyo inafanya viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika vinavyofanya kazi kufikia viwanda 117 kwa mwaka 2020;
- (e) Kurejeshwa kwa mali za vyama vya ushirika zilizokuwa zimeuzwa kiholela na nyingine kuporwa zikiwemo nyumba za makazi, maghala, viwanda na viwanja. Baadhi ya mali zilizorejeshwa zilitoka katika Chama Kikuu cha Ushirika NCU (1984) Ltd (Mwanza), Chama Kikuu cha Ushirika SHIRECU Ltd (Shinyanga), Chama kikuu cha Ushirika KNCU (1984) Ltd (Kilimanjaro), Chama Kikuu cha Ushirika KCU (1990) Ltd (Kagera) na Mamlaka ya Mkongwe Tanzania;
- (f) Kuunganishwa kwa vyama vya ushirika wa mazao ya Kakao na Kahawa katika mfumo wa soko la moja kwa moja (*direct export*) na nchi za Uswizi, Afrika kusini, Japani na Uholanzi na kuuza mazao kwa bei shindani. Katika mwaka 2018/19 mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na gunia la kahawa la kilo 60 kuuzwa wastani wa Dola za Kimarekani 160.63 ikilinganishwa na bei ya mnada ya Dola za Kimarekani 84.97, na kilo moja ya kakao kuuzwa kwa bei ya juu ya Shilingi 5,011 ikilinganishwa na bei ya Shilingi 3,200 iliyokuwa msimu 2017/18; na
- (g) Kuunganishwa kwa vyama vya ushirika vya mazao ya Pamba na taasisi za fedha ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) na taasisi nyingine ili kuviwezesha kupata zana za kilimo ikiwemo matrekta. Hadi kufikia 2019 Vyama vya



Ushirika (AMCOS) 32 vilikopeshwa matrekta yenye jumla ya thamani ya Shilingi bilioni 1.5.

34.

**Katika kipindi cha miaka mitano (2020 - 2025), Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha dhana ya Ushirika wa hiari inajengwa na kusimamiwa na sheria ili kuwalinda na kuwanufaisha wanaushirika, hivyo kuchangia ipasavyo katika ustawi wao na Taifa kwa ujumla, ili kufikia azma hiyo, chama kitaelekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kuhakikisha kuwa vyama vikuu vya ushirika vinatekeleza majukumu na kuvihudumia vyama wanachama wake kwa kusimamia uzalishaji, upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani, masoko na kuajiri watendaji wenye sifa kwa kuzingatia ukubwa wa chama na miamala inayofanywa ili kuongeza ufanisi na usimamizi katika Vyama vya Ushirika;
- (b) Kuhakikisha vyama vya ushirika vinakuwa na uwezo wa kusimamia mifumo rasmi ya masoko ikiwemo stakabadhi za ghala kwa mazao yote hususan ya kimkakati na kuhamasisha mazao mengi kuingia kwenye Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;
- (c) Kuanzisha mfuko wa kuendeleza shughuli za ushirika (*cooperative seed fund*) kupitia vyama vya ushirika na kuunganisha na taasisi za fedha ili kuhudumia uzalishaji, uhifadhi na uchakataji wa mazao ya kilimo ili kujenga ushirika uliokamilika (*comprehensive cooperative*);
- (d) Kufufua na kuhamasisha vyama vya ushirika kumiliki viwanda ili kuongeza mnyororo wa thamani wa bidhaa zao kwa kufufua viwanda 262 ambavyo havifanyi kazi na kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vipya 33 kwa mfumo wa makampuni yatakayomilikiwa na Vyama vya Ushirika na kuendeshwa kibiashara kwa masilahi ya wanaushirika;
- (e) Kupanua wigo katika ushirika kwa kuhamasisha makundi maalum wakiwemo vijana, wanawake, mama lishe, bodaboda, watu wenye ulemavu, wazee n.k, kujiunga na kuanzisha vyama vya ushirika vinavyogusa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii;
- (f) Kuongeza mitaji katika vyama vya ushirika kwa kuanzisha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOs) kwenye Ushirika wa Mazao na Masoko (AMCOS) na aina nyingine za vyama vya ushirika (*Integrated Cooperatives*);
- (g) Kuimarisha elimu na mafunzo ya ushirika kwa wanachama, viongozi na watendaji kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ushirika kwa:-
  - (i) Kusimamia utekelezaji wa Mpango Maalum wa Elimu ya Ushirika unaoandaliwa na vyama vya ushirika; na



- (ii) Kuongeza idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika kutoka milioni 5.9 hadi milioni 14.5 mwaka 2025.
- (h) Kuimarisha vyama vya ushirika na kuwezesha wanachama kumiliki vyama vyao kwa kusimamia na kuhimiza uanzishwaji wa vyama imara vya msingi katika maeneo ambayo hakuna vyama vya ushirika kwa kuanzisha programu maalum ya kuwezesha umma kutambua umuhimu wa ushirika kama mbinu mojawapo ya kuondoa umasikini;
- (i) Kuboresha uongozi, kudhibiti wizi na ubadhirifu ndani ya vyama vya ushirika kwa kuhimiza uzingatiaji wa kanuni za maadili ndani ya vyama vya ushirika na kusisitiza matumizi ya mfumo wa TEHAMA ili kuimarisha usimamizi na upatikanaji wa takwimu sahihi; na
- (j) Kufanya mapitio ya kisheria na kitaasisi ya mfumo wa usimamizi, uratibu na ukaguzi wa ushirika katika ngazi zote ili kuuimarisha na kuwezesha kuhudumia vizuri zaidi ushirika katika sekta zote na kuchangia kwenye uchumi mpana.

### **Kilimo**

35. Kilimo cha kisasa ndio msingi katika kujenga uchumi na kina nafasi ya kimkakati katika kukuza ustawi wa Taifa. Mchango wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa ni wastani wa asilimia 28 na kinaajiri takriban asilimia 65 ya Watanzania. Katika kipindi cha mwaka 2015 - 2020, Chama Cha Mapinduzi kilielekeza Serikali kutilia mkazo utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Kuendeleza Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme-ASDP II*) ili kufikia malengo makuu ya kukifanya kilimo kuwa cha kisasa na cha kibiashara; chenye tija na ambacho mazao yake yatakuwa yameongezewa thamani. Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa Taifa linajitosheleza kwa chakula; kuimarisha uchumi; kuongeza kipato cha wakulima; kuwa kichocheo cha kukua kwa viwanda; na kuongeza ajira.
36. Katika kipindi hicho, Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kuhakikisha kuwa Taifa linajitosheleza kwa akiba ya chakula na kuwa na wastani wa utoshelevu wa asilimia 121.1 kati ya 2015 - 2020 ukifananisha na utoshelevu wa asilimia 114.6 kati ya mwaka 2010 - 2015; tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo imeongezeka; vipato vya wakulima kutokana na biashara ya mazao vimeboreshwa; na mapato yatokanayo na biashara ya mazao nje ya nchi yameongezeka kufikia tani 1,141,774 mwaka 2018/19 kutoka tani 796,512 mwaka 2015/16 ambalo ni ongezeko la asilimia 43.3. Mafanikio hayo yamepatikana kutokana na:-
- (a) Kuongezeka kwa upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo, ambapo:-
    - (i) Mbegu bora za mazao zimeongezeka kutoka tani 36,614 mwaka 2015 hadi kufikia tani 71,208 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 94.5. Aidha, uzalishaji wa mbegu bora ndani ya nchi umeongezeka kutoka tani 20,605 mwaka 2015 hadi kufikia tani 66,032 mwaka 2020;





- (ii) Upatikanaji wa mbolea nchini umeongezeka kutoka tani 302,450 mwaka 2015 hadi tani 586,604 mwaka 2020;
  - (iii) Uwekezaji katika kilimo umeongeza matumizi ya viatilifu; mfano, matumizi ya viudadu (*insecticides*) yameongezeka kutoka tani 343.5 mwaka 2015 na kufikia zaidi ya tani 6,300 mwaka 2020, na viuagugu (*herbicides*) toka tani 259 mwaka 2015 na kufikia zaidi ya tani 5,800 mwaka 2020; na
  - (iv) Idadi ya matrekta nchini imeongezeka kutoka matrekta 18,460 mwaka 2015 hadi kufikia 25,032 kwa mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 35.6.
- (b) Kuongeza uzalishaji wa miche bora ya mazao ya kimkakati ambapo uzalishaji wa miche bora ya chai umeongezeka kutoka miche 1,600,000 mwaka 2015 hadi miche 7,130,000 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 345.6; miche bora ya korosho 13,661,433 imezalishwa ambapo miche 12,252,197 imesambazwa kwa wakulima wa mikoa 17 inayolima zao hilo; na ndani ya miaka mitano jumla ya miche ya kahawa chotara 18,763,539 imezalishwa na kusambazwa kwa wakulima;
  - (c) Huduma za ugani zimeimarishwa ambapo wagani tarajiwa 7,530 walihitimu kwenye vyuo 14 vya mafunzo ya kilimo vya Serikali;
  - (d) Ujenzi wa Skimu za umwagiliaji 135 zikiwemo zile za Mforo (Mwanga), Hanga - Ngadinda (mji mdogo wa Madaba) na Skimu ya Igongwa iliyopo katika Halmashauri ya Misungwi umekamilika. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za Luiche (Kigoma Ujiji), Ibanda (Sengerema/Geita) na Gidahababieg (Hanang) umefanyika;
  - (e) Ukarabati wa jumla ya skimu 17 umekamilika na ukarabati unaendelea kwa skimu tano (5) za umwagiliaji ambazo ni Mbogo na Kigugu (Mvomero), Msolwa Ujamaa na Njage (Kilombero) na Mvumi (Kilosa) unaendelea ikiwa ni pamoja na ukarabati wa miundombinu ya barabara (*feeder roads*);
  - (f) Ukarabati wa ekari 2,000 za skimu kubwa ya Dakawa pamoja na barabara zake (*feeder roads*) na mafunzo ya uongezaji tija kufikia zaidi ya tani 7 kwa hekta umefikiwa ambayo ni kati ya tija za juu duniani;
  - (g) Ukarabati na ujenzi wa bwawa la Usoke (Urambo), bwawa la Itagata (Halmashauri ya Wilaya ya Itigi) na bwawa la Dongobesh (Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu) umekamilika;
  - (h) Kuongezaka kwa eneo la umwagiliaji kwa ekari 30,130 na hivyo kufikia ekari 1,187,630 (hekta 475,052) mwaka 2019;



- (i) Kukamilishwa utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP I) na kuanza kwa awamu ya pili (ASDP II) ambayo imewezeza wakulima na wafugaji kuanza kupata mafanikio katika mapinduzi ya sekta ya kilimo nchini;
- (j) Kuwaidhinishia ardhi wananchi wa vijiji 1,920 kati ya 1,975 vilivyokuwa ndani ya maeneo ya hifadhi ili kuwaongezea maeneo ya kilimo;
- (k) Uongezaji tija kwenye kilimo cha umwagiliaji, mfano, mpunga kutoka tani 1.8 hadi 2.0 kwa hekta kufikia tani 4.0 hadi 5.0 kwa hekta mwaka 2020 na vitunguu toka tani 13 hadi tani 26 kwa hekta;
- (l) Kuongeza ufanisi na kuimarisha uratibu wa shughuli za umwagiliaji kwa kuboresha muundo na kuipatia vitendea kazi Tume ya Taifa ya Umwagiliaji;
- (m) Kukamilika kwa ujenzi wa maghala mawili yenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 10,000 katika halmashauri za Wilaya za Songea na Mbozi. Aidha, ukarabati wa maghala 105 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 31,500 umekamilika;
- (n) Ujenzi wa maghala na vihenge vya kisasa vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 250,000 umekamilika katika Halmashauri za Wilaya za Babati (tani 40,000), Mpanda (tani 25,000), Sumbawanga (tani 40,000), Mbozi (tani 20,000), Songea (tani 50,000), Shinyanga (tani 35,000), Dodoma (tani 20,000) na Makambako (tani 30,000). Utekelezaji huo umefikia asilimia 57;
- (o) Kuongezeka kwa uwezo wa kuzalisha mbegu mpya zilizogunduliwa na kuidhinishwa kutoka aina 29 mwaka 2015 hadi aina 73 kufikia mwaka 2020;
- (p) Vyama vya ushirika 16 vya wabanguaji wadogo wa korosho vimeimarishwa katika mikoa ya Tanga, Ruvuma, Lindi, Mtwara na Pwani na kuweza kuuza korosho tani 291,329.51 katika nchi za India, China na Vietnam. Aidha, vyama 63 vinavyozalisha Ufuta na Kokoa vimeunganishwa na kuweza kuuza mazao yao kupitia mfumo wa Soko la Bidhaa (*Commodity Exchange*);
- (q) Kurahisisha uuzaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi hivyo kuwawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi kunufaika zaidi kwa kufuta na kupunguza viwango vya kodi, tozo, ada na ushuru zipatazo 114 zilizoonekana kuwa kero; na
- (r) Kuongezeka kwa matumizi ya zana za kilimo za kisasa kutoka asilimia 14 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 20 mwaka 2020 kwa eneo linalolimwa kutumia matrekta, na kutoka asilimia 24 mwaka



2015 kufikia asilimia 27 kwa eneo linalolimwa kwa kutumia maksai na kufanya eneo linalolimwa kwa mikono kushuka toka asilimia 62 mwaka 2015 mpaka asilimia 53 mwaka 2020.

37. TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMBA

**Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kusimamia mapinduzi ya kilimo ili kuhakikisha kinaendelea kuwa chenye tija na kinachotumia teknolojia ya kisasa. Aidha, Chama kitahakikisha kuwa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) inaendelea kutekelezwa na kutoa mchango mkubwa katika usalama wa chakula, pato la Taifa, maendeleo ya sekta ya viwanda na huduma kwa kutekeleza maeneo makuu manne (A mpaka D) yafuatayo:-**

- A. *Kusimamia kikamilifu hifadhi na matumizi endelevu ya maji, ardhi ya kilimo na mazingira sambamba na kuongeza miundombinu ya umwagiliaji itakayoendeshwa kiuchumi kwa kufanya yafuatayo;*
- (a) Kuongeza eneo lenye miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 561,383 mpaka kufikia hekta 1,200,000 ifikapo mwaka 2025;
    - (i) Kuongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 111,192 kwa kukamilisha ujenzi wa skimu za umwagiliaji 261 katika mikoa 25. Kati ya hizo skimu ndogo ni 179, skimu za kati 63 na skimu kubwa 19;
    - (ii) Kujenga skimu mpya za umwagiliaji 208 nchini, kati ya hizo skimu ndogo ni 123, skimu za kati 63 na skimu kubwa 22. Ujenzi huu unatarajia kuongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 136,928. Aidha, sekta binafsi itahamasishwa kushiriki kwenye ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji itakayoongeza eneo la umwagiliaji kwa eka 150,000;
    - (iii) Kujenga na kuimarisha mabwawa ya uvunaji wa maji ya mvua 88 katika skimu za umwagiliaji kwa ajili ya kilimo cha mpunga na mazao mengine katika mikoa 25 ili kuongeza maeneo ya kilimo cha umwagiliaji nyingi zaidi; na
    - (iv) Kujenga skimu ya umwagiliaji ya hekta 60,000 kwa kutumia fursa ya bwawa la Nyerere.
  - (b) Kuimarisha uendeshaji, usimamizi na matengenezo ya miundombinu ya umwagiliaji kwa uanzishaji na uendelezaji wa ushirika wa wanufaikaji wa umwagiliaji;
  - (c) Kuanzisha mfuko wa umwagiliaji wa Taifa kwa ajili ya kukusanya mapato kutoka katika miradi ya uwekezaji wa umma ili kuendeleza na kufanya upanuzi wa miradi mipya ya umwagiliaji nchini;





- (d) Kuendelezwa na kuendeshwa kwa miradi ya umwagiliaji ya umma kibiashara kwa kushirikisha wakulima na wanufaikaji ili kupata mitaji ya upanuzi wa kilimo cha umwagiliaji nchini;
- (e) Kujenga mabwawa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya umwagiliaji katika maeneo yanayopata mvua chache kama Kanda ya Kati, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kaskazini pamoja na maeneo yanayopata mafuriko ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuzuia mafuriko na kupanua kilimo cha umwagiliaji;
- (f) Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika kilimo cha kisasa cha kibiashara hususan ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na kuwashirikisha wakulima kwa kila mwaka;
- (g) Kuhamasisha na kuwezesha uanzishwaji wa mashamba ya wakulima wakubwa yatakayotumika kama kitovu cha teknolojia bora za uzalishaji kwa ajili ya kuwaendeleza wakulima wadogo kwa utaalamu na kwa kuwapatia uhakika wa masoko;
- (h) Kuanzisha mfumo wa kilimo cha kitalu (*block farms*) cha pamoja kwa mazao ya kimkakati na yenye mahitaji makubwa nchini ili kulinda ardhi ya kilimo na kurahisisha utoaji wa huduma za pembejeo na masoko;
- (i) Kuhamasisha na kutengeneza mfumo imara wa kilimo ili kuwahakikishia wakulima wadogo upatikanaji wa huduma bora za kilimo cha kisasa, masoko ya uhakika na bei nzuri ya mazao yao;
- (j) Kurejesha rutuba ya udongo ya hekta 300,000 kwenye mashamba yanayolimwa mahindi yaliyoathirika na tindikali katika mikoa ya Ruvuma, Iringa, Njombe, Rukwa, Songwe, Mbeya na Katavi kwa kutumia chokaa;
- (k) Kuhakikisha tunarasimisha ardhi ya wakulima wadogo kwa kuhakikisha wanapata hati ili kulinda usalama wa miliki ya ardhi yao;
- (l) Kuwezesha wakulima kutumia teknolojia na mbinu za kisasa za kilimo endelevu na chenye tija kwa njia ya kilimo mseto (*Agroforestry*) kwenye mazao ya parachichi, korosho, miembe, michungwa, michikichi, minazi na mazao mengine ya miti;
- (m) Kuendeleza matumizi ya teknolojia za kilimo hifadhi kutoka mikoa 11 inayotumia kilimo hifadhi hadi mikoa 25 ifikapo mwaka 2025; na



- (n) Kuwajengea uwezo wakulima wadogo kwa kuwapatia nyenzo na teknolojia za gharama nafuu (umwagiliaji wa matone, mbegu zinazohimili ukame na uvunaji maji mashambani) ili waweze kuhimili athari, kubaini na kutumia fursa za mabadiliko ya tabianchi katika halmashauri 185;

*B. Kuongeza uzalishaji, tija na faida katika shughuli za wakulima kwa kufanya yafuatayo;*

- (a) Kuendeleza na kuwezesha matumizi ya sayansi na teknolojia na ubunifu katika kilimo kwa kushirikisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MUCCOPS), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika ya Nelson Mandela (NM-AIST), Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO), Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC), Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO) na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kwa kufanya yafuatayo:-
- (i) Kuendeleza shughuli za ugunduzi na uzalishaji wa mbegu bora ambapo aina 40 za mbegu bora mpya zinazohimili ukame, magonjwa, na wadudu wa mazao ya nafaka, jamii ya mikunde, mafuta na mazao ya bustani;
- (ii) Kuongeza uzalishaji wa miche bora yenye ukinzani dhidi ya magonjwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa zilizo salama kwa afya ya Watanzania katika mazao ya kahawa, michikichi, migomba, mihogo, viazi, minazi, katani, mananasi na pareto;
- (iii) Kutumia teknolojia za kisasa ili kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo ukame, chumvi, tindikali ya udongo, wadudu na magonjwa kama virusi vinavyosababisha batobato kali na michirizi kahawia katika muhogo, ugonjwa wa mnyauko wa mahindi na migomba na viwavijeshi vamizi, sumu kuvu katika mazao ya nafaka, mafuta na mizizi; na
- (iv) Kutafiti, kuimarisha na kuendeleza teknolojia za zana za kilimo zikiwemo za kulimia, kupandia, kudhibiti magugu, kuvunia, kusindika na kuhifadhi.
- (b) Kujenga maabara moja na kuziimarisha maabara 10 za uzalishaji wa miche bora kwa afya ya Watanzania kwa njia ya chupa kwa ajili ya Michikichi (TARI Kihinga), Mkonge (TARI



Mlingano), Migomba (TARI Tengeru), Korosho, Muhogo na Ufuta (TARI Naliendele), Kahawa (TARI Maruku), Zabibu (TARI Makutopora), Pamba (TARI Ukiriguru), Minazi na Michikichi (TARI Mikocheni), Mpunga (TARI Ifakara) na Udongo (TARI Tanga);

- (c) Kuongeza usambaji wa pembejeo za kilimo kwa gharama nafuu ikiwa ni pamoja na mbegu bora, mbolea, viuatilifu na zana bora za kilimo kwa:-
- (i) Kuongeza upatikanaji wa mbolea kutoka tani 586,604 mwaka 2019/2020 hadi tani 800,000 mwaka 2020/2025;
  - (ii) Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vipya vya kuchanganya mbolea na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kuzalisha mbolea, chokaa kwa ajili ya kilimo na viuatilifu ifikapo 2025;
  - (iii) Kuimarisha ukaguzi wa mbolea, mbegu na viuatilifu kwa kuanzisha na kuimarisha ofisi za Kanda nchini ili kuhakikisha pembejeo zenye ubora zinapatikana kwa wakulima kwa wakati na kwa bei nafuu;
  - (iv) Kujenga maabara ya Kitaifa ya kudhibiti ubora wa mbolea;
  - (v) Kuongeza uzalishaji wa mbegu kutoka tani 71,000 hadi tani 140,000 na kupunguza bei ya mbegu na kutekeleza mikakati ya kuwafikishia wakulima kwa wakati ifikapo 2025;
  - (vi) Kuhamasisha kuwekeza katika uanzishaji wa mashamba makubwa ya kisasa ya mbegu ya umma na binafsi kwa kilimo cha umwagiliaji cha zaidi ya hekta 2,000 kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu wa uhakika ndani ya nchi;
  - (vii) Kuimarisha na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika viwanda vya kutengeneza mashine na zana za kilimo nchini ili kukuza matumizi ya teknolojia bora za zana za kilimo pamoja na kupunguza matumizi ya jembe la mkono kutoka asilimia 53 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 10 mwaka 2025;
  - (viii) Kuhamasisha sekta binafsi kuongeza utoaji wa huduma za kukodisha zana za kilimo kutoka vituo (*virtual centres*) 24 kufikia vituo 100 mwaka 2025;



- (ix) Kuimarisha usimamizi wa huduma za ugani kwa kutumia TEHAMA kwa kuanzisha kituo cha huduma kwa wakulima (*Call Centre*) na maafisa ugani kujengewa mfumo utakaohakikisha wanawafikia wakulima angalau 8 kwa siku; na
- (x) Kuanzisha na kuboresha Vituo vya Huduma za Kilimo vya Kata kufikia 1,000 kwa kuweka mifumo ya teknolojia za kisasa ili kuwawezesha wakulima kupata taarifa mbalimbali za kilimo na masoko kwa njia ya kielektroniki (redio na runinga).
- (d) Kuongeza uzalishaji na tija kwa mazao ya chakula ambayo ni pamoja na mahindi, mpunga, mtama, ndizi, mazao ya mizizi, na mazao jamii ya mikunde ili kuongeza kiwango cha utoshelevu wa chakula kutoka wastani wa kuwa na ziada ya asilimia 21 kufikia ziada ya asilimia 50 mwaka 2025. Baadhi ya malengo hayo ni:-
  - (i) Kuongeza tija ya wakulima wadogo kwenye uzalishaji wa mahindi kutoka tani 1.7 (magunia 17 ya kilo 100) kwa hekta hadi tani 3.0 (magunia 30 ya kilo 100) kwa hekta mwaka 2025;
  - (ii) Kuongeza tija ya wakulima wadogo kwenye uzalishaji wa mpunga kutoka tani 3 (magunia 30 ya kilo 100) kwa hekta hadi tani 5 (magunia 50 ya kilo 100) kwa hekta mwaka 2025;
  - (iii) Kuongeza tija ya wakulima wadogo kwenye uzalishaji wa maharage kutoka tani 1.1 (magunia 11 ya kilo 100) kwa hekta hadi tani 1.8 (magunia 18 ya kilo 100) kwa hekta mwaka 2025;
  - (iv) Kuongeza mchango wa sekta ya umwagiliaji katika kuzalisha chakula kutoka asilimia 26 ya sasa hadi asilimia 40 ya chakula chote kinachozalishwa nchini kufikia 2025; na
  - (v) Kuongeza tija kwa asilimia 30 katika mazao ya mtama, uwele, muhogo, viazi na ndizi.
- (e) Kuhamashisha kilimo cha mazao lishe (*nutritional-sensitive*) ili kupunguza udumavu kutoka asilimia 32 hadi asilimia 24 na kupunguza ukondefu ili kuendelea kuwa chini ya asilimia 5 kiwango ambacho kimewekwa na Shirika la Afya Duniani;
- (f) Kuongeza uzalishaji na tija kwa mazao ya asili ya biashara yanayojumuisha mazao ya pamba, kahawa, korosho, pareto, mkonge, tumbaku na chai kwa:-



- (i) Kuingia makubaliano ya kibiashara baina ya taasisi za umma na sekta binafsi zenye uzoefu wa mazao ya miti (korosho, kahawa, chai na mazao mengine ya miti) kuzalisha miche na kugawa kwa wakulima bila malipo kama motisha ya kulima mazao ya muda mrefu;
- (ii) Kuhamasisha halmashauri za wilaya zenye fursa za maeneo kuanzisha mashamba makubwa ya korosho (*Block Farms*) 10 yenye ukubwa wa ekari 20,000 kila moja;
- (iii) Kuongeza uzalishaji wa zao la korosho kutoka tani 300,000 hadi tani 700,000 ifikapo 2025;
- (iv) Kuongeza uzalishaji wa pamba kutoka tani 350,000 hadi kufika tani 1,000,000 ifikapo 2025;
- (v) Kuongeza uzalishaji wa kahawa kutoka tani 68,000 hadi kufikia tani 300,000 ifikapo 2025;
- (vi) Kuongeza uzalishaji wa majani ya chai kutoka tani 37,000 za sasa hadi tani 60,000 ikiwa ni pamoja na kuongeza tija ya mkulima mdogo wa chai kutoka kilo 1000 hadi 1500 kwa hekta na mkulima mkubwa kutoka kilo 2000 hadi 3000 kwa hekta ifikapo 2025;
- (vii) Kuongeza uzalishaji wa tumbaku kutoka tani 60,595 hadi tani 200,000 ifikapo 2025;
- (viii) Kuongeza uzalishaji pareto kutoka tani 2,400 hadi tani 3,200 ifikapo 2025;
- (ix) Kuongeza uzalishaji wa mkonge kutoka 38,506 hadi tani 80,000 ifikapo 2025; na
  - (x) Kuongeza uzalishaji kwa asilimia 50 wa mazao ya mbegu za mazao ya mafuta za karanga, ufuta, soya kwa ajili ya kukuza biashara na lishe.
- (g) Kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani kutoka tani 7,230,217 hadi tani 14,600,000 ifikapo 2025 kwa kufanya yafuatayo:-
  - (i) Kuimarisha utafiti wa mbegu na magonjwa kwa mazao ya bustani kupitia TARI - Tengeru kwa kuwekeza katika miundombinu ya uzalishaji na kujenga uwezo wa watafiti;



- (ii) Kutengeneza mfumo wa ithibati wa wazalishaji binafsi wa miche na mbegu za mazao ya bustani;
  - (iii) Kuhamashisha uwekezaji wa pamoja wa Serikali na sekta binafsi kwenye mashamba ya miti mizazi Lushoto (Jegetal na Malindi), Muheza (Songa na Zigi), Morogoro (LITI), Ifakara (KATRIN), Kasulu (Bugaga), Mbeya (Igurusi); na
  - (iv) Kuhamasisha uwekezaji wa mitaji ya sekta binafsi, wanawake na vijana na kuilinda ili kuongeza uzalishaji, uhifadhi, usindikaji na usafirishaji wa mazao ya bustani.
- (h) Kuongeza uzalishaji wa mazao yenye mahitaji ya matumizi makubwa ya ndani (miwa, mazao ya mafuta, na ngano) ili kupunguza uingizaji wa bidhaa zitokanazo na mazao hayo kutoka nchi za nje kwa kufanya yafuatayo:-
- (i) Kuongeza uzalishaji wa mafuta ya mawese kutoka tani 40,500 za mafuta za sasa hadi tani 100,000 mwaka 2025 kwa kusambaza miche bora kutoka 1,744,000 za sasa hadi miche 10,000,000 mwaka 2025;
  - (ii) Kuongeza uzalishaji wa alizeti kutoka tani 790,000 hadi kufikia tani 1,500,000 zitakazozalisha tani 300,000 za mafuta;
  - (iii) Kuongeza uzalishaji wa ngano kutoka tani 63,000 hadi kufikia tani 200,000 kwa kuongeza uzalishaji na tija na kuwawezesha wazalishaji wa ndani kuwa shindani; na
  - (iv) Kuongeza uzalishaji wa sukari kutoka tani 345,000 hadi tani 700,000 ifikapo 2025 kwa kuimarisha uzalishaji na uwekezaji wa ubia na ushirika wa wazalishaji wa miwa.

C. *Kuwezesha uwekezaji katika kilimo biashara kwa kufanya yafuatayo;*

- (a) Kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao kwa kujenga na kukarabati maghala yenye uwezo wa kuhifadhi tani 531,850 kama ifuatavyo:-
  - (i) Kujenga ghala 14 katika mikoa 10 ya Kigoma, Mtwara, Dodoma, Mwanza, Ruvuma, Tabora, Manyara, Geita, Simiyu na Morogoro zenye uwezo wa kuhifadhi tani 34,000;
  - (ii) Kujenga vihenge vya kisasa 13 vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 97,000 vitajengwa katika mikoa ya Dodoma na Mwanza;





- (iii) Kukarabati vihenge 18 vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 41,850 katika mikoa ya Arusha na Iringa;
  - (iv) Kukarabati jumla ya ghala 11 zenye uwezo wa kuhifadhi tani 59,000 katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa na Mwanza; na
  - (v) Kuhamasisha taasisi za Serikali na sekta binafsi kujenga ghala zenye uwezo wa kuhifadhi tani 300,000.
- (b) Kuwajengea uwezo na kuwapatia vifaa vijana 400 katika halmashauri za wilaya katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Manyara, Kigoma, Tabora, Ruvuma, Mtwara, Morogoro na Geita kwa ajili ya kutengeneza vihenge visivyoruhusu hewa (*metal silo*) vya kuhifadhi nafaka katika ngazi ya kaya na hivyo kuwaongezea vijana uwezo wa kiuchumi na kuongeza kipato cha wakulima kwa kupunguza upotevu;
  - (c) Kujenga maabara kuu ya kitaifa ya kilimo katika Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya ithibati, kusimamia ubora na kuimarisha biashara ya mazao ya kilimo kimataifa;
  - (d) Kuwezesha maabara za kilimo zilizopo nchini kukidhi viwango vya ubora wa kimataifa ili kupunguza gharama za kilimo biashara;
  - (e) Kujenga uwezo wa taasisi za ndani za Serikali na binafsi za ithibati (*local certification bodies*) ili kupunguza gharama za ithibati za mazao yanayosafirishwa nje hasa mazao ya bustani ambayo wawekezaji wakuu ni wanawake na vijana;
  - (f) Kuboresha mifumo ya uendeshaji biashara katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo kwa kuondoa vikwazo vya kibiashara vikiwemo kodi na tozo mbalimbali pamoja na utoaji vibali kwa wakati;
  - (g) Kutengeneza mfumo wa kusimamia na kuratibu hifadhi ya mazao ya kilimo ili kuwa na taarifa sahihi za kiasi cha mazao yaliyohifadhiwa;
  - (h) Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji na bima kwa wakulima wadogo na wawekezaji wa sekta ya kilimo kwa kushirikisha taasisi za fedha ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na benki nyingine katika kugharamia uzalishaji, uhifadhi, uchakataji na uuzaji wa mazao ya kilimo kwa kuweka mazingira wezeshi ya kisera, kisheria na kikodi;



- (i) Kuanzisha mfumo wa bima utakaounganisha Serikali, sekta binafsi na vyama vya ushirika katika kujenga bidhaa za huduma ya bima kwa wakulima zinazoendana na mahitaji na mazingira halisi ya mkulima;
- (j) Kurasimisha na kuwatambua wafanyabiashara wadogo wa mazao ya kilimo katika masoko ya msingi (*primary markets*) ili waweze kusimamiwa na kuhakikisha wakulima wadogo wanapata huduma na bei stahiki ya mazao yao;
- (k) Kushirikisha sekta binafsi katika ujenzi wa miundombinu ya kisasa ya masoko, ikiwa ni pamoja na kuweka mfumo wa masoko yenye uwazi na shirikishi ili kuleta ushindani, ufanisi na kutanua wigo wa kibiashara kwa kuwapatia wakulima fursa ya kuuza mazao yao ndani na nje ya nchi kupitia vyama vyao vya msingi vya ushirika;
- (l) Kuimarisha Kitengo cha Intelijensia ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Market Intelligence Unit*) kwa kuweka mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa sahihi za mwenendo wa masoko ya mazao ya kilimo kwa wadau;
- (m) Kuboresha mfumo wa masoko wa mazao ya kilimo kuwa na soko la awali (*primary market*) kwa wanunuzi wa ndani na viwanda na soko la upili (*secondary market*) kwa wauzaji wa nje kupitia stakabadhi za ghala na Soko la Bidhaa (TMX) mfumo wa malipo wa kielektroniki na mabenki ili kuleta ufanisi na kudhibiti udanganyifu na kuongeza pato la mkulima;
- (n) Kujenga kituo mahiri cha mafunzo kwa wakulima na usimamizi wa mazao baada ya kuvuna (*post harvest center of excellency*) kwa ajili ya kuwezesha masoko na kueneza teknolojia mbalimbali za usimamizi na uchakataji wa mazao kilimo baada ya kuvuna;
- (o) Kuongeza uzalishaji na mauzo ya nje ya mbogamboga kwa zaidi ya maradufu kwa kuchukua hatua zifuatazo:-
  - i. Kujenga vituo vya kuchakata na kuhifadhi mazao ya bustani (*industrial packs*) katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya na Songwe;
  - ii. Kujenga vituo vya kuchakata na kuhifadhi mazao katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Iringa, Kagera, Kigoma, Manyara, Mara, Mbeya, Tabora, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Singida, Shinyanga, Songwe, Tanga, na Katavi;



- iii. Kuimarisha huduma za vituo vya kukusanyia mazao (*collection centres*) zilizopo Mlali Wilaya ya Mvomero na Kiwangwa Bagamoyo; na
- iv. Kuimarisha majukwaa ya wadau wa mazao makuu ya bustani, viungo, matunda na mbogamboga;
- (p) Kufanya makubaliano ya kibiashara na nchi walaji na wanunuzi wa mazao yetu ili kupata soko la uhakika hasa kwa mazao ya kimkakati, mikunde, soya na karanga kabla ya kuzalisha;
- (q) Kuongeza matumizi ya ndani ya mazao ya kahawa, chai, mikunde, matunda na bidhaa za kilimo zinazozalishwa nchini katika soko la ndani na kikanda ili kuongeza mahitaji ya mazao ya wakulima;
- (r) Kwa kushirikiana na wizara yenye dhamana ya viwanda na biashara, kujenga na kuimarisha viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo yakiwemo mazao ya pamba, kahawa, chai, korosho, tumbaku, mkonge na pareto;
- (s) Kwa kushirikiana na wizara inayosimamia viwanda kuhamasisha ujenzi wa viwanda vidogo vya awali (*primary processing*) kuongeza thamani ya mazao (korosho, kahawa, chai, alizeti na mazao mengine) vijijini ili kutengeneza ajira na masoko pamoja na kuongeza muda wa kuhifadhi mazao na kuuza kwenye viwanda vya kati na vikubwa vya ndani kwa umaliziaji wa kuongeza thamani kwa viwango vya ubora wa kitaifa na kimataifa (*secondary processing for finished goods*);
- (t) Kuboresha miundombinu ya barabara mashambani na kupeleka miundombinu wezeshi ya umeme na maji vijijini ili kuwa na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao kwa kushirikiana na wizara za kisekta; na
- (u) Kuanzisha kiliko cha mimea dawa kitakachotoa malighafi kwa ajili ya kiwanda cha kuzalisha dawa zitokanazo na mimea dawa.

D. *Kuweka mfumo mpya wa usimamizi kitaasisi na uratibu wa shughuli za kilimo kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi na kuwezesha wakulima kuwa na sauti katika uendeshaji na biashara ya mazao yao:-*

- (a) Kupitia upya sheria zilizopo pamoja na miundo ya Bodi za mazao na Taasisi kufanya marekebisho ili kuakisi mahitaji ya usimamizi wa mazao ya kimkakati kwa nia ya kuwa na Taasisi



chache ili kuimarisha usimamizi na kuongeza ufanisi katika Sekta ya kilimo;

- (b) Kuanzisha mamlaka ya kusimamia afya ya mimea ambayo itakuwa ni mamlaka ya kisheria ya kuchukua hatua kwa wauzaji wa viuatilifu visivyo na ubora na viwango vinavyokubalika kitaalamu;
- (c) Kuweka mwongozo wa kisheria katika maeneo ya usimamizi wa ardhi, uendelezaji na uratibu wa mifumo ya kilimo; usimamizi na uratibu wa huduma za ugani; na matumizi ya zana bora za kilimo;
- (d) Kuanzisha taasisi ya kusimamia mazao ya bustani, nafaka na mazao mengine ili kusimamia mazao hayo na kuhakikisha yanatoa mchango zaidi katika usalama wa chakula na pato la mkulima;
- (e) Kuimarisha utaratibu na vigezo, mfumo wa usimamizi na usajili wa maghala ya uhifadhi wa nafaka na mazao kwa sekta ya umma na binafsi;
- (f) Kuendelea kutozuia mazao kuuzwa nje ya nchi ili kuongeza wigo wa masoko ya mazao kwa mkulima; bei nzuri kwa mkulima; kuongeza mauzo ya nje; mchango wa mauzo ya nje kwenye pato la Taifa;
- (g) Kuweka msukumo katika mabadiliko ya fikra na mazingira ya kibiashara kwa sekta ya kilimo kwa lengo la kubadili mtazamo wa uendeshaji kilimo kama shughuli ya kujikimu na badala yake iendeshwe kibiashara kwa faida ya nchi na wakulima; na
- (h) Kutengeneza, kuimarisha na kusimamia matumizi ya mifumo ya kanzidata ya wakulima, ardhi na wadau wa kilimo.

### **Ufugaji**

38. Sekta ya mifugo ni miongoni mwa sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi. Kutokana na umuhimu huo, ni dhahiri kuwa ipo haja ya kuendelea kuimarisha ufugaji wa kisasa na kuchakata/kusarifu bidhaa za mifugo kwa ajili ya mahitaji ya ndani, ikiwemo ya lishe bora, na usafirishaji nje. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020) Chama Cha Mapinduzi kilijielekeza katika kuhakikisha sekta ya ufugaji inaimarishwa ili kuwawezesha wananchi kunufaika na ukuaji wa sekta hiyo.
39. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho ni pamoja na kuimarika kwa sekta ya ufugaji kwa kuongeza uhamilishaji wa ng'ombe na uzalishaji wa mbegu bora za mifugo; kuongeza uzalishaji wa chanjo za mifugo ili kupunguza magonjwa yanayoenezwa na wadudu, maboresho ya sera, sheria na kanuni katika kuimarisha usimamizi wa sekta ya mifugo na kuongeza maeneo ya



malisho yaliyotengwa kwa ajili ya ufugaji. Mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA

- (a) Kuimarisha mashamba matano ya kuzalisha mifugo ya Sao Hill, Mabuki, Ngerengere, Kitulo na Nangaramo pamoja na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) ambapo mitamba 51,735 ilizalishwa katika mashamba ya Serikali, NARCO na Sekta Binafsi na kusambazwa kwa wafugaji;
- (b) Kuongeza maeneo ya ufugaji kutoka hekta milioni 1.4 mwaka 2015 hadi hekta milioni 5.0 mwaka 2020; ambapo hadi mwaka 2020 Vijiji 1,852 vimeandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kati ya Vijiji 12,545 vilivyopo nchini ambapo maeneo ya malisho hekta 2,788,901.17 yametengwa kwa ajili ya ufugaji katika Mikoa 22;
- (c) Kujenga na kukarabati mabwawa ya Nyakanga (Butiama) na Wami - Dakawa (Mvomero) na hivyo kufanya idadi ya mabwawa/malambo kufikia 1,482 mwaka 2020 kutoka 1,378 mwaka 2015 sawa na ongezeko la malambo 104;
- (d) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ufugaji kiasi cha shilingi bilioni 22;
- (e) Kuongeza idadi ya ng'ombe waliohamilishwa kutoka 105,000 mwaka 2015 hadi 514,700 mwaka 2020. Mitungi 71 ya kuhifadhi kimiminika cha naitrojeni (lita 35) na vifaa vingine vya uhamilishaji na usafiri vimenunuliwa. Aidha, uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita bilioni 2.1 mwaka 2015 hadi lita bilioni 2.7 mwaka 2020;
- (f) Kudhibiti magonjwa ya mifugo ambapo lita 21,373.06 za dawa za kuogeshea mifugo zilisambazwa katika Mikoa 25, Halmashauri 152 katika majosho 1,738 yanayofanya kazi. Aidha, majosho mapya 104 yamejengwa na 301 yamekarabatiwa;
- (g) Kuboresha huduma za chanjo za magonjwa ya mlipuko yanayoathiri afya ya mifugo na binadamu na kuwezesha biashara ya mifugo katika soko la kimataifa, ambapo wastani wa upatikanaji wa chanjo umeongezeka kwa baadhi ya magonjwa na kupungua kwa mengine kutokana na uwepo au kutokuwepo kwa tishio la ugonjwa husika nchini kama ifuatavyo;
  - (i) Wastani wa upatikanaji wa chanjo ya mdondo wa kuku umeongezeka kutoka wastani wa dozi milioni 55 mwaka 2015 hadi dozi milioni 121 mwaka 2020;
  - (ii) Wastani wa upatikanaji chanjo ya ugonjwa wa Kimeta umeongezeka kutoka wastani wa dozi 500 mwaka 2015 hadi dozi 1,846,600 mwaka 2020;



- (iii) Wastani wa upatikanaji chanjo ya ugonjwa wa kutupa mimba umeongezeka kufikia wastani wa dozi 3,825 mwaka 2020 tofauti na awali ambapo hakuna chanjo zilizotolewa;
- (iv) Wastani wa upatikanaji chanjo ya ugonjwa wa chambavu umeongezeka kutoka wastani wa dozi 500 mwaka 2015 hadi dozi 2,045,870 mwaka 2020;
- (v) Wastani wa upatikanaji chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa umeongezeka kutoka wastani wa dozi 122,550 mwaka 2015 hadi dozi 302,000 mwaka 2020; na
- (vi) Kujenga kiwanda chenye uwezo wa kuzalisha chanjo za mifugo aina 37 cha *Hester Bioscience* – Kibaha mkoa wa Pwani.
- (h) Kuongeza uzalishaji wa chanjo za mifugo katika kituo Kibaha (*Tanzania Vaccine Institute-TVI*) kutoka dozi 26,367,200 mwaka 2015 hadi dozi 185,867,275 mwaka 2020;
- (i) Kuongeza udahili wa wanafunzi katika vituo 8 vya Serikali (LITA) kutoka wanafunzi 1,800 mwaka 2015 hadi wanafunzi 3,634 mwaka 2020;
- (j) Kuongeza viwanda vya kusindika maziwa kutoka 82 mwaka 2015 hadi 99 mwaka 2020. Viwanda vya kusindika nyama nchini vimeongezeka kutoka 25 mwaka 2015 hadi viwanda 33 mwaka 2020. Aidha, kuna viwanda 9 vya ngozi ambavyo vimesaidia usindikaji wa ngozi wa hatua ya kati kufikia futi za mraba 124,420,000 kwa mwaka; na
- (k) Kuongeza usindikaji wa maziwa kutoka wastani wa lita 167,620 mwaka 2015 hadi kufikia lita 194,335 kwa siku mwaka 2020.

40.

**Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kitaelekeza Serikali kuendelea kuleta mabadiliko makubwa na ya kisayansi katika ufugaji kwa kuhimiza ufugaji wa kisasa wenye kuzingatia kinga, tiba na utafiti wa mifugo ili kuzalisha ajira nyingi zaidi hasa kwa vijana na kuinua mchango wa sekta katika Pato la Taifa na kuleta ustawi wa wananchi. Aidha, Serikali itatakiwa kushughulikia kwa nguvu zaidi migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Ili kufikia azma hiyo, CCM itaelekeza Serikali kujikita katika kuboresha maeneo ya kimatokeo kama ifuatavyo:-**

- (a) Kuendeleza na kuimarisha huduma za Ugani katika ngazi za Kata na Vijiji kwa kuhakikisha kuwa kila mfugaji anafikiwa na huduma za Ugani na kwa wakati. Yafuatayo yatatekelezwa:-
  - (i) Kuongeza idadi ya maafisa ugani kwa kuajiri na kuhakikisha kuwa kila kata na kijiji kinafikiwa na afisa ugani au mtoa huduma za ugani nchini;





- (ii) Kuimarisha usimamizi wa maafisa ugani, kuwawezesha na kuwapatia vitendea kazi vikiwemo vyombo vya usafiri na vifaa kazi vya uwandani ili kuwafikia walengwa;
- (iii) Kuanzisha mashamba darasa na mashamba ya mfano ya malisho katika vijiji, halmashauri za wilaya na miji nchini;
- (iv) Kuweka mkazo zaidi kwenye usambazaji wa teknolojia na kutoa mafunzo kwa wafugaji na wadau wote kwa njia ya machapisho, majarida, vipeperushi, vipindi vya redio na luninga;
- (v) Kuongeza udahili kwa mwaka katika vyuo vya mafunzo ya mifugo nchini kutoka 3,634 mwaka 2020 kwa mwaka hadi 9,760 kwa mwaka 2025 ikiwa ni jitihada za kutosheleza mahitaji ya rasilimaliwatu katika Sekta;
- (vi) Kubuni na kutekeleza mipango ya kutoa mafunzo rejea kwa wafugaji na maafisa ugani katika halmashauri zote nchini kwa kushirikiana na sekta binafsi;
- (vii) Kujenga mazingira wezeshi na kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha mashamba ya mifugo na jamii ya wafugaji wa asili kubadili namna ya kutekeleza shughuli zao za ufugaji na kuwa za kisasa;
- (viii) Kutenga, kupima na kumilikisha maeneo ya shughuli za ufugaji kwa wafugaji katika halmashauri zote nchini;
- (ix) Kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kwa kuboresha ranchi tano (Kongwa, Ruvu, Kalambo, Missenyi na West Kilimanjaro) ili kuongeza tija katika mnyororo wa thamani ya mazao ya mifugo. Aidha, sekta binafsi na wafugaji mmoja mmoja watahimizwa kuendelea kumiliki na kuboresha miundombinu katika ranchi zao ili kuwa na ranchi za kisasa ndani ya Serikali na pia kwa wafugaji binafsi;
- (x) Kuongeza na kuimarisha ujenzi wa machinjio ya kisasa katika maeneo yote nchini;
- (xi) Kuimarisha utambuzi na usajili wa mifugo nchini ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wafugaji na mifugo yao;
- (xii) Kuboresha maeneo ya wafugaji kwa kuyapatia huduma muhimu zikiwemo maji, afya na elimu kwa ajili kusaidia jamii hiyo kutulia sehemu moja na hivyo kuepuka kuhamahama kufuata huduma hizo; na
- (xiii) Kuhamasisha jamii ya wafugaji wa asili na watumiaji wengine wa ardhi ili kuepuka migogoro ya kijamii kwa ajili ya kuhakikisha



kuwa uchumi wa sekta ya ufugaji unafungamanishwa na uchumi wa sekta nyingine na kuchangia katika pato la Taifa.

- (b) Kuendeleza na kuibua tafiti mbalimbali zenye kujibu changamoto za Sekta ya Mifugo kwa kutekeleza yafuatayo:-
- (i) Kuibua na kufanya tafiti katika maeneo makuu ya vipaumbele vya maendeleo ya mifugo nchini. Aidha, tafiti 37 za muda mfupi na 26 za muda mrefu katika Agenda ya Kitaifa ya Utafiti wa Mifugo zitafanyika; na
  - (ii) Kuendeleza taasisi za kitafiti ili kufanya tafiti ambazo zitajikita kutoa suluhisho kwa changamoto katika sekta ya mifugo ili kuongeza ubora wa mazao ya mifugo ikiwa ni pamoja na wingi wa nyama na maziwa; na ubora wa ngozi.
- (c) Kuboresha afya ya mifugo nchini kwa kuimarisha kinga, chanjo na tiba kwa kufanya yafuatayo:-
- (i) Kuhakikisha kuwa mifugo yote nchini inapatiwa chanjo kwa kuzingatia mpango na ratiba ya chanjo;
  - (ii) Kutoa chanjo za ruzuku kwa magonjwa 13 ya kipaumbele ili kuimarisha afya ya mifugo na binadamu nchini kwa kushirikisha sekta binafsi;
  - (iii) Kuimarisha upatikanaji wa chanjo na dawa za mifugo nchini kwa kujenga viwanda vya kuzalisha chanjo na dawa ili kutosheleza mahitaji;
  - (iv) Kuhakikisha kuwa kila halmashauri nchini inakuwa na mfumo baridi (*cold chain*) kwa ajili ya kutunza chanjo za mifugo;
  - (v) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa chanjo na kudhibiti kuenea kwa vimelea vya magonjwa kwa mifugo ili kuwa na mifugo yenye afya bora;
  - (vi) Kuimarisha afya ya mifugo ili pamoja na mambo mengine kupunguza kiwango cha athari ya magonjwa yahamayo kutoka nchi moja kwenda nyingine (*trans-boundary diseases*) na kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu (*zoonotic diseases*);
  - (vii) Kuimarisha huduma za tiba ya mifugo nchini kwa kuhakikisha kuwa kila Wilaya ina daktari wa mifugo (*Veterinarian*) na kila kata ina daktari msaidizi wa mifugo (*Paraveterinarian*) na kuwapatia vitendea kazi ikiwemo usafiri na vifaa vya msingi vya matibabu ya wanyama kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia magonjwa na huduma za tiba ya mifugo;



- (viii) Kuboresha huduma za mifugo kwa kuhakikisha kuwa Mikoa 18 ambayo haina vituo vya uchunguzi wa magonjwa kati ya 26 nchini ina vituo vya kisasa vya uchunguzi wa magonjwa, kuanzisha maabara na kliniki ya mifugo kila wilaya na kukarabati vituo vya uchunguzi wa magonjwa vilivyopo katika kanda 8 yenye uchakavu wa majengo na miundombinu mingine na kuvipatia vituo vyote 26 watalaam wa kutosha kulingana na mahitaji na vitendea kazi vya kisasa ikiwemo usafiri kwa ajili ya kuwezesha usimamizi na ufuatiliaji wa magonjwa nchini;
  - (ix) Kuhakikisha kuwa maeneo yote yenye majosho katika vijiji yanatambuliwa, yanapimwa na kupatiwa hatimiliki; na
  - (x) Kuhakikisha kuwa kila kijiji chenye mifugo kina joshho linalofanya kazi kwa kuzingatia ratiba ya uogeshaji, pamoja na kutoa dawa za ruzuku ya kuanzia kwa ajili ya kuogeshea mifugo kwa kuzingatia bei elekezi inayotolewa na Serikali itakayotozwa na kamati za uogeshaji wa Mifugo katika Halmashauri, makusanyo hayo yatatumika kwa ajili ya kununua dawa ili kuwa na huduma endelevu.
- (d) Kuongeza uzalishaji wa mazao yatokanayo na mifugo yakiwemo ya: maziwa kutoka lita bilioni 2.7 hadi wastani wa lita bilioni 4.5, nyama nyekundu kutoka tani 690,629 hadi tani 790, 000, nyama nyeupe kutoka tani 82,500 hadi tani 150,000, mayai kutoka bilioni 3.6 hadi bilioni 5 na ngozi kutoka tani 16 hadi tani 25 kwa mwaka, kwa kufanya yafuatayo:-
- (i) Kuimarisha vituo vya kuzalisha mbegu bora na kuhakikisha zinawafikia wafugaji kwa bei nafuu ya ruzuku na kwa wakati;
  - (ii) Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vya kusindika mazao ya mifugo nchini ili kuongeza thamani ya mazao;
  - (iii) Kuendeleza masoko ya mifugo ili kutosheleza mahitaji na kuongeza thamani ya mifugo;
  - (iv) Kuhamasisha ufugaji wa kuku na kuanzisha Kituo cha Umahiri cha Ufugaji wa Kuku katika mashamba ya serikali kwa ajili mafunzo na usambazaji wa mbegu bora kwa wafugaji;
  - (v) Kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika uzalishaji wa mbegu bora za mifugo; na
  - (vi) Kuhakikisha kuwa malighafi baki (pembe, manyoya, mifupa na kwato) baada ya kuchinja mifugo zinaingizwa kwenye mnyororo wa thamani ili kutengenza bidhaa nyingine.



- (e) Kuimarisha huduma za maji, malisho na vyakula vya mifugo kwa kutekeleza yafuatayo:-
- (i) Kubainisha na kutenga maeneo ya ufugaji kwa kuyatambua, kuyapima, kuyasajili na kuyamilikisha ili kuongeza maeneo yaliyotengwa kutoka Hekta 2,788,901.17 hadi Hekta 6,000,000;
  - (ii) Kuongeza malambo na mabwawa ya maji ya mifugo kutoka 1,384 hadi 1,842 na visima 103 hadi 225 ili kurahisisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo;
  - (iii) Kuongeza uzalishaji wa vyakula vya mifugo viwandani kutoka tani 900,000 mwaka 2020 hadi tani milioni 8.0 mwaka 2025;
  - (iv) Kuhamasisha matumizi ya zana bora katika kuzalisha, kuchakata na kuhifadhi malisho ya mifugo na kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala itokanayo na samadi (*biogas*); na
  - (v) Kuwahamasisha wafugaji kujiunga katika vikundi au vyama vya ushirika na kuwaunganisha na Taasisi za fedha kwa ajili ya kupatiwa mikopo.

### Uvuvi

41. Tanzania ina fursa maalum ya kuendeleza uchumi wake kupitia rasilimali zilizo katika bahari, maziwa, mito na mabwawa kama vile uvuvi na ufugaji wa samaki na mazao mengine. Katika kipindi cha mwaka 2015 - 2020, Chama Cha Mapinduzi kilielekeza Serikali kuhakikisha shughuli za uvuvi nchini zinaboreshwa, vitendo vya uvuvi haramu vinadhibitiwa ili kuwezesha upatikanaji wa samaki wenye ukubwa unaokubalika na kuongezeka kwa viwanda vya kuchakata samaki na hivyo kuongeza mauzo ya bidhaa za samaki nje ya nchi.
42. Katika kipindi hicho, Chama Cha Mapinduzi kimehakikisha mialo inaboreshwa na kuwa ya kisasa kwa ajili ya kupokelea samaki katika maziwa ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya masoko ya samaki nchini. Maboresho ya sera, sheria na kanuni katika kuimarisha usimamizi wa sekta ya uvuvi yamefanyika na ulinzi wa rasilimali katika maziwa na bahari umeongezwa na hivyo kuongeza usalama kwenye mazalia ya samaki. Mafanikio katika sekta ya uvuvi yametokana na:-
- (a) Vyama vya ushirika vya msingi vya wavuvi 113 kusajiliwa ikilinganishwa na vyama 67 vilivyokuwepo mwaka 2015;
  - (b) Kuboreshwa kwa mialo 13 ya kupokelea samaki na kuwa ya kisasa katika ukanda wa Ziwa Victoria (6), Ziwa Tanganyika (4) na ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi (3);
  - (c) Sekta binafsi kuhamasishwa kujenga viwanda vipya vya kuchakata samaki katika ukanda wa Bahari ya Hindi na maziwa makuu na hivyo kuchangia kuongezeka kwa thamani ya mazao ya uvuvi. Hadi sasa



kuna viwanda vikubwa 12 vya kuchakata samaki (8 Ziwa Victoria, 4 Ukanda wa Pwani). Vilevile, kuna viwanda 4 vya kati vinavyochakata mazao ya uvuvi kwa ajili ya masoko ya Kikanda na nchi nyingine za Canada, Asia na Marekani. Aidha, kuna viwanda vidogo vidogo 34 vya kupokelea samaki hai na maghala rasmi 52 kwa ajili ya mazao ya uvuvi yaliyokaushwa;

- (d) Kuondolewa kwa kodi katika zana na malighafi za uvuvi zikiwemo injini za kupachika, nyuzi za kushonea nyavu (*twines*) na vifungashio. Aidha, sekta binafsi imehamasishwa kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya kutengeneza zana za uvuvi hapa nchini ili kuwezesha wavuvi kupata zana za uvuvi kwa bei nafuu ambapo hadi sasa kuna viwanda 5 vya kutengeneza nyavu za uvuvi;
- (e) Kupambana na uvuvi haramu ili uwe endelevu na wenye tija. Katika kutekeleza azma hiyo yafuatayo yamefanyika:-
  - (i) Kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake na Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Na.1 ya mwaka 1998 (na marekebisho yake ya mwaka 2007); na
  - (ii) Kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kuanzisha Kanda Kuu tatu (3) katika ukanda wa Ziwa Victoria, Tanganyika na Pwani. Aidha, zimeanzishwa kanda nne ndogo za Ukerewe, Sengerema, Nyumba ya Mungu na Mtera; na
  - (iii) Kudhibiti matumizi ya zana haramu zikiwemo nyavu za makila 806, 883, makokoro 17,382, nyavu za timba 50,328, nyavu za dagaa 9,926, Kamba za makokoro zenye urefu wa mita 2,462,161, takriban vilipuzi 600 na mabomu 100 vilikamatwa. Hivyo, jitihada hizo zimewezesha kupungua kwa uvuvi haramu kwa zaidi ya asilimia 75 kwa maji baridi na kupungua kwa uvuvi wa milipuko katika ukanda wa mwambao wa bahari kwa asilimia 99.
- (f) Kuongezeka kwa wafugaji bora wa samaki kutoka wavuvi 2,000 mwaka 2015 hadi wavuvi 7,974 mwaka 2020; kuimarika kwa matumizi ya zana endelevu za uvuvi; na kupungua kwa uvuvi haramu kwa kutoa mafunzo ya usimamizi, uhifadhi na uvunaji wa rasilimali za uvuvi kwa njia endelevu katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mbeya, Kilimanjaro na Songwe;
- (g) Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) imeendelea kuimarishwa kwa kujenga madarasa, kumbi za kufundishia katika Kampasi za Mbegani-Bagamoyo (Pwani), Nyegezi (Mwanza), Mikindani (Mtwara), Kibirizi (Kigoma) na Gabimori-Rorya (Mara);



- (h) Wananchi wameendelea kuhamasishwa kuwekeza katika ukuzaji viumbe maji, hususan ufugaji wa samaki kwa kutoa elimu, ambapo hadi sasa kuna wakuzaji viumbe maji 26,474 waliozalisha samaki tani 16,228 mwaka 2020 ikilinganishwa na wakuzaji viumbe maji 16,284 waliozalisha tani 10,000 mwaka 2015;
- (i) Kuhamasisha na kuwezesha wananchi kuwekeza katika zao la Mwani kwa kutoa elimu ya kilimo na kuongeza thamani ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 552.8 mwaka 2015 hadi tani 1,449 mwaka 2020. Jumla ya wananchi 292 wamepatiwa elimu ya utengenezaji wa sabuni na *shampoo*; na
- (j) Kuhamasisha ufugaji wa samaki katika maeneo yenye ukame nchini kutoka mabwawa 153 mwaka 2015 hadi 445 mwaka 2020 yamechimbwa katika mikoa ya Dodoma (90), Singida (105), Shinyanga (103), Simiyu (68) na Tabora (79) pamoja na vizimba 7 katika bwawa la Mwamapuli Tabora.

43. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha Sekta ya uvuvi inaimarika kwa kuongeza matumizi ya sayansi na teknolojia ya uvuvi endelevu ili iweze kuhimili ushindani na kuifanya nchi kujitosheleza kwa mahitaji ya samaki na kuachana na uagizaji kutoka nje. Pia, kuwezesha mauzo ya bidhaa za uvuvi nje ya nchi ili kuchangia zaidi katika ukuaji wa uchumi wa Taifa, kuzalisha ajira nyingi zaidi kwa vijana na kuboresha maisha ya wavuvi na wananchi kwa ujumla. Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuzihimiza serikali zake kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kujenga bandari ya uvuvi katika ukanda wa Pwani ambayo itawezesha meli zinazovua kutia nanga kwa lengo la kuhaulisha na kuuza samaki, kutoa takwimu sahihi na huduma nyingine. Katika hatua hii inatarajiwa kuzalisha takriban ajira 30,000 na kuongeza pato kwa jamii;
- (b) Kuweka mazingira bora katika uvuvi wa bahari kuu kwa kutoa vivutio kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, kwa kutekeleza kikamilifu Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu ya mwaka 2020;
- (c) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuwaelimisha wavuvi juu ya matumizi ya zana bora na kushirikiana na wananchi katika mapambano dhidi ya uvuvi haramu ili kuwa na uvuvi endelevu na wenye tija kwa vizazi vya sasa na vijavyo;
- (d) Kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kujenga mialo tisa katika maeneo ya Ziwa Victoria (3), Ziwa Tanganyika (4) na Ziwa Nyasa (2). Vilevile, kuimarisha masoko ya samaki ya Feri (Dar es Salaam), Kirumba (Mwanza), Kipumbwi (Pangani), Sahare (Tanga) ili kuongeza





thamani na ubora wa samaki pamoja na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi;

- (e) Kuimarisha teknolojia rahisi za uzalishaji, uhifadhi na uchakataji wa samaki kwa kujenga: mitambo ya kuzalisha barafu, mitambo ya kukausha samaki hususan dagaa na vyumba vya baridi vya kuhifadhi samaki katika maeneo ya uvuvi ili kuimarisha mnyororo wa thamani;
- (f) Kuanzisha maeneo mapya sita ya hifadhi katika maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa pamoja na kuimarisha hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu 18 ili kuhakikisha kuwa mazalia na makulia ya samaki yaliyoharibika yanarejeshwa katika hali yake ya awali;
- (g) Kurejesha mazalia na makulia ya samaki yaliyoharibika kutokana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira kwa kuweka matumbawe bandia na kupanda mikoko katika bahari ili kuongeza wingi wa samaki;
- (h) Kuhamasisha uanzishaji na kuimarisha vikundi na vyama vya ushirika vya msingi vya wavuvi wadogo wadogo kwa lengo la kuwapatia mitaji, ujuzi na vifaa pamoja na zana za uvuvi katika maeneo ya mwambao wa Bahari ya Hindi, maziwa, mabwawa na mito ili kuongeza uzalishaji, ajira na kipato;
- (i) Kuhamasisha sekta binafsi na vyama vya ushirika kutekeleza mpango wa kununua meli tano (5) za uvuvi zenye uwezo wa kuvua samaki bahari kuu ambapo ajira zaidi ya 15,000 kwa mwaka zitapatikana;
- (j) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuwezesha viwanda vilivyopo kuwa shindani na kuhamasisha mashirika ya umma na sekta binafsi kuwekeza katika uanzishaji wa viwanda saba vipya vya kusindika na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi;
- (k) Kuimarisha vituo vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji vya Kingolwira (Morogoro), Ruhila (Ruvuma), Mwamapuli (Tabora) na Nyengedi (Lindi) ili viweze kuzalisha vifaranga vya samaki 3,000,000 na kutoa huduma za ugani kwa wananchi 5,000 kwa mwaka;
- (l) Kuanzisha vituo vipya vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji katika Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa na mwambao wa Pwani ili kuongeza wigo wa kutoa huduma za ugani na kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji vifaranga na ukuzaji viumbe maji kibiashara ili kuongeza uzalishaji wa samaki kutoka tani 16,000 hadi 50,000 kwa mwaka na kupanua wigo wa ajira kwa vijana;
- (m) Kuwawezesha wakulima wa Mwani, hususan vikundi vya akina mama na vijana wa mwambao wa Pwani katika kuongeza uzalishaji kutoka tani 1,400 hadi tani 5,000 kwa mwaka;



- (n) Kupitia upya tozo katika maeneo mbalimbali ili kuwapunguzia wavuvi kero na kuvutia wawekezaji;
- (o) Kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa vifaa bora vya uvuvi, kuzuia uzalishaji na uagizaji wa zana haramu za uvuvi na kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji wa vyakula vya samaki;
- (p) Kuimarisha usimamizi wa maafisa ugani, kuwawezesha na kuwapatia vitendea kazi vikiwemo vyombo vya usafiri na vifaa kazi vya uwandani ili kuwafikia walengwa; na
- (q) Kuanzisha mashamba darasa ya ukuzaji viumbe maji katika halmashauri za wilaya ili kusogeza huduma za ugani na utoaji wa mafunzo kwa vitendo kwa wananchi katika maeneo hayo.

### Viwanda

44.

Chama Cha Mapinduzi kinatambua kuwa sekta ya viwanda ni nguzo muhimu katika kukuza uchumi wa nchi, kukuza pato la mwananchi, kupunguza umasikini na kuongeza uwezo wa Taifa kujitegemea. Katika Kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), Serikali iliweka nguvu kubwa katika kufanikisha utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda sambamba na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2015/16 - 2020/21) uliolenga kuendeleza uchumi wa viwanda hasa ujenzi wa viwanda mama (*basic industries*) na kuimarisha viwanda vilivyopo.

45.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kutokana na hatua hizo ni kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani, kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje, kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na kuchangia kwenye mizania ya biashara ya nchi yetu, hususan katika masoko ya kikanda. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na:-

- (a) Kuongezeka kwa thamani ya bidhaa za mazao ambayo malighafi zake zinazalishwa kwa wingi hapa nchini ambapo viwanda 25 vya usindikaji wa mazao ya mifugo vimejengwa. Vikiwemo viwanda vya 17 vya maziwa na nane vya nyama. Hivyo, kuwawezesha sekta ya usindikaji wa mazao ya mifugo kuwa na jumla ya viwanda 145 vinavyojumuisha 33 vya nyama, 99 vya maziwa na 13 vya kusindika ngozi;
- (b) Kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara na kutambuliwa kwa sekta binafsi kama nguzo muhimu katika ujenzi wa uchumi wa viwanda ambapo kumeongeza kasi ya ujenzi wa viwanda nchini. Juhudi hizo zimechangia ongezeko la viwanda vipya 8,477 kati ya mwaka 2015 hadi 2019 na kufanya idadi ya viwanda kufikia 61,110. Kati ya viwanda hivyo vipya 201 ni vikubwa, 460 vya kati, 3,406 vidogo na 4,410 vidogo sana. Viwanda hivi vinatumia kwa kiasi kikubwa malighafi za ndani na kuajiri wananchi wengi (*labour intensive*) na kuwaongeza kipato;



- (c) Kuongezeka kwa ajira za viwandani kutoka ajira 254,786 mwaka 2015 hadi kufikia ajira 482,601 mwaka 2020. Ongezeko hilo limetokana na ajira mpya viwandani kufuatia uwekezaji mkubwa katika upanuzi na uanzishaji wa viwanda vipya nchini;
- (d) Kujitosheleza katika baadhi ya mahitaji ya ndani kwa uzalishaji wa bidhaa za ujenzi (saruji, marumaru, nondo na bati) na chuma. Viwanda saba vya saruji vimejengwa na hivyo kufikisha idadi ya viwanda 10 ambapo kwa sasa uzalishaji halisi ni tani milioni 7.4 kwa mwaka ikilinganishwa na mahitaji halisi ya tani milioni 4.8 na hivyo kuwa na ziada ya tani milioni 2.6 ambayo huuzwa nje. Kwa upande wa uzalishaji wa bidhaa za chuma, viwanda vikubwa vitatu vimejengwa na hivyo kuwezesha idadi ya viwanda vya chuma nchini kufikia 25 vinavyozalisha tani 240,336 kwa mwaka. Aidha, viwanda vikubwa viwili vya utengenezaji wa marumaru vimejengwa vinavyozalisha mita za mraba 32.4;
- (e) Kuimarika kwa upatikanaji wa mitaji ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo kupitia vyanzo mbalimbali vya mitaji vinavyoratibiwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo-SIDO na Mfuko wa Maendeleo ya Ujasiriamali (NEDF). Vilevile, utoaji elimu ya ujasiriamali na upatikanaji wa masoko kwa wamiliki wa viwanda umefanyika na hivyo kuongeza uwezo wa uongezaji wa thamani kwa bidhaa wilayani (bidhaa moja kwa kila Wilaya). Aidha, wananchi wamesogezewa huduma na kuhamasishwa kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa viwanda ambapo ofisi nne za SIDO katika mikoa mipya ya Simiyu, Katavi na Geita zimejengwa. Pia, majengo ya viwanda (*industrial shades*) 12 yamejengwa katika mitaa ya viwanda ya SIDO iliyopo mikoa ya Dodoma (3), Manyara (3), Kagera (1), Mtwara (1) na Geita (4) ambapo jumla ya viwanda 29 vimeanzishwa katika majengo hayo; na
- (f) Kuimarishwa kwa taasisi mbalimbali zinazochochea ujenzi wa uchumi wa viwanda na uhamasishaji wa uwekezaji ikiwemo Mamlaka ya Ukanda Maalum ya Uwekezaji (EPZA).

46. **Kwa kutambua umuhimu wa sekta ya viwanda, Chama Cha Mapinduzi kitaelekeza Serikali kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kubuni mikakati zaidi ili kujenga uchumi wa viwanda jumuishi, fungamanishi, shindani na vinavyotumia malighafi za ndani, teknolojia ya kisasa na vinavyokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Katika Kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama kitaisimamia Serikali kuhakikisha inatekeleza kwa kushirikiana na sekta binafsi kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kujenga ukanda na kongani za viwanda kila mkoa kulingana mazao na maliasili zinazopatikana katika kila mkoa na fursa za kijiografia kwa mkoa husika;



- (b) Kuimarisha mazingira ya ujenzi wa viwanda vya kimkakati kwa kufanya mapitio na maboresho ya sera na mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*);
- (c) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuwezesha ujenzi wa viwanda ambavyo sehemu kubwa ya malighafi yake itatoka ndani, hususan kilimo, uvuvi, mifugo, maliasili na madini. Aidha, viwanda hivyo ni pamoja na vinavyotumia teknolojia itakayotoa ajira kwa watu wengi (*labour intensive*). Lengo ni kuongeza ajira zitokanazo na uzalishaji wa bidhaa viwandani kutoka 306,180 mwaka 2020 hadi 500,000 mwaka 2025;
- (d) Kubuni na kutekeleza mkakati wa kuanzisha viwanda vya kimkakati kwa lengo la kujitosheleza kwa mahitaji ya msingi;
- (e) Kuchukua hatua za makusudi kuwezesha ustawi wa viwanda vya ndani ili kuwa shindani;
- (f) Kuendeleza na kujenga viwanda mama ikiwemo viwanda vya Chuma (miradi ya Mchuchuma na Liganga), Madawa na Kemikali (Magadi Soda Engaruka) ambavyo vitaweza kuleta faida nyingi kwa Taifa letu ikiwa ni pamoja na ajira, uongezaji thamani malighafi za ndani, uanzishwaji viwanda vingine, na kupanua shughuli katika sekta za ujenzi na miundombinu;
- (g) Kuandaa mikakati ya upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo, vya kati na vikubwa;
- (h) Kuendeleza miundombinu ya msingi ya ujenzi wa viwanda. Hii ni pamoja na kuendelea kujenga kanda na kongano (*clusters*) za viwanda zenye miundombinu wezeshi ya ujenzi wa viwanda, katika maeneo ya kimkakati kulingana na upatikanaji wa malighafi katika maeneo hayo, mfano ngozi, bidhaa za ngozi na uongezaji thamani madini;
- (i) Kufungamanisha ujenzi wa kanda maalum za viwanda na biashara na miundombinu ya kimkakati iliyopo na itakayojengwa ikiwemo Reli ya Kisasa (SGR), Reli ya Kati, TAZARA, bandari kavu na upanuzi wa barabara;
- (j) Kuweka utaratibu wa kuendelea kufuatilia viwanda vilivyobinafsishwa ili kuhakikisha vinafanya kazi kwa malengo yaliyokusudiwa na hivyo kuongeza ajira na uzalishaji wa bidhaa nchini;
- (k) Kuimarisha taasisi za utafiti kwa lengo la kubuni teknolojia rahisi, zenye gharama nafuu kwa ajili ya kusaidia uongezaji thamani kwenye malighafi zinazopatikana nchini ikiwemo katika sekta ya kilimo, uvuvi, mifugo, maliasili na madini. Hatua hiyo itahusisha



kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo maeneo ya vijijini ili kutumia fursa ya Mpango wa Kusambaza Umeme Vijijini-REA;

- (l) Kutenga na kuendeleza maeneo maalum ya uwekezaji (EPZ/SEZ) na kuyawekea miundombinu muhimu kama barabara, maji na umeme kwa ajili ya viwanda; na
- (m) Kufanya tathmini ya mifumo ya utoaji huduma za kuanzisha na kuendeleza viwanda ili kuchukua hatua za kupunguza urasimu na kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi na wawekezaji wengine.

### Biashara

47. Chama Cha Mapinduzi kinatambua kuwa biashara ni kichocheo cha maendeleo ya viwanda na sekta nyingine za kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), Chama kimeendelea kuisimamia Serikali na kuhakikisha sekta ya biashara inaendelea kuimarika na kutoa fursa za masoko kwa mazao na bidhaa na kuwaunganisha wananchi na masoko yenye upendeleo wa ushuru wa forodha kikanda na kimataifa.

48. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kuboreshwa kwa mazingira ya ufanyaji biashara nchini na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa katika masoko ya kikanda na kimataifa. Mafanikio mengine yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma kwenye masoko ya kikanda yanayotoa fursa za upendeleo maalum (*preferential market access*) ambapo kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoka mwaka 2015 hadi mwaka 2018 Tanzania imekuwa na urari chanya wa mauzo ya bidhaa kwa wastani wa Dola za Kimarekani milioni 288.04. Bidhaa zilizouzwa zaidi ni pamoja na madini ya Tanzanite, Chai, Kahawa, Sigara, Dawa na Vifaa Tiba;
- (b) Kuimarisha mahusiano ya kibiashara na nchi za nje ikiwemo nchi za Ulaya mfano Uswisi ambapo mauzo ya Tanzania yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 153.93 mwaka 2015 hadi 257.17 mwaka 2018 na nchi za Asia kwa mfano India ambapo mauzo yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 20.55 mwaka 2015 hadi milioni 42.42 mwaka 2018. Bidhaa zilizouzwa zaidi ni kahawa, pamba, chai, viungo, samaki na bidhaa za baharini, mavazi, bidhaa za mikono (*handcrafts*), bidhaa za mazao ya kilimo (*Agro-processing*), tumbaku, ngozi, maua, mapambo, madini na vito vya thamani;
- (c) Kuendeleza uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini kwa kuandaa na kutekeleza Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*) ambao umewezesha kufutwa kwa jumla ya tozo kero 168 kati ya hizo, tozo 114 ni za sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi. Vilevile, tozo 54 za TBS, OSHA na iliyokuwa TFDA nazo zilifutwa hali ambayo imechochea urasimishaji wa biashara mbalimbali;





- (d) Kuanza kutumika kwa soko la bidhaa (*commodity exchange*) na kupungua kwa upotevu wa mazao baada ya uzalishaji (*post harvest loss*) na kuanzishwa kwa mfumo wenye uwazi na rahisi kwa wanunuzi kwa kujenga maghala katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo maghala matano (5) katika maeneo ya Mvumi *Scheme* - Kilosa, Msola Ujamaa *Scheme* na Njage *Scheme* Wilaya ya Kilombero na *Scheme* za Mbogo Komtonga na Kigugu Wilaya ya Mvomero. Vilevile, sekta binafsi imehamasishwa kujenga na kumiliki maghala yakiwemo ya Pawaga, Iringa Vijijini, Dakawa, Kilolo na Ifwagi. Juhudi hizo zimesaidia kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa kutokana na kukamilisha kwa mfumo wa mauzo kwa njia ya kielektroniki kwa Soko la Bidhaa Tanzania ambapo tani 519.89 zimeuzwa kwa mfumo huo;
- (e) Kuongezeka kwa uwazi na ushindani sanjari na kuimarisha bei za mazao na kuwanufaisha wakulima kwa kushirikisha wadau mbalimbali ikiwemo vyama vya ushirika katika kuweka mifumo madhubuti ya uzalishaji na upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kilimo;
- (f) Kuongezeka kwa wigo wa kibiashara na masoko kati ya Tanzania na nchi jirani kutokana na fursa ya nchi yetu kijiografia (*strategic geographical location*). Katika kutumia fursa hiyo, vituo nane (8) vya biashara mpakani vimeanzishwa ambavyo ni: Holili/Taveta (Tanzania na Kenya); Sirari/Isebania (Tanzania na Kenya); Namanga/Namanga (Tanzania na Kenya); Kabanga/Kobero (Tanzania na Burundi); Rusumo/Rusumo (Tanzania na Rwanda); Mtukula/Mtukula (Tanzania na Uganda); Horohoro/Lungalunga (Tanzania na Kenya); na Kituo cha Tunduma/Nakonde (Tanzania na Zambia); na
- (g) Kurahisishwa kwa utaratibu wa usajili na utoaji leseni kwa kuanzisha mfumo wa usajili wa majina ya biashara, makampuni, alama za biashara na huduma, hataza (*Copy right*), leseni za viwanda na leseni za biashara kwa njia ya mtandao (*online registration*) kupitia anuani ya [www.brela.go.tz](http://www.brela.go.tz). Vilevile, kutoa leseni zote za biashara kwa njia ya mtandao kupitia Dirisha la Taifa la Biashara (*National Business Portal - NBP*).

**49. Chama Cha Mapinduzi kinatambua kuwa biashara ni chanzo cha mapato na hivyo kitaendelea kuelekeza Serikali kuimarisha biashara za ndani na nje ya nchi. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama kitahakikisha mchango wa sekta ya biashara kwenye Pato la Taifa unaendelea kuimarika na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi na wananchi kwa ujumla kwa kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuweka mazingira wezeshi ya biashara na kuhakikisha kwamba zinapatikana fursa nafuu za kibiashara ili kuchochea ujenzi wa viwanda na uzalishaji wa bidhaa zenye ubora wa kimataifa na zinazohimili ushindani;





- (b) Kufanya mapitio na maboresho ya sera na mikakati mbalimbali itakayoimarisha mazingira ya ufanyaji biashara na kukuza biashara ndani na nje ya nchi;
- (c) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kurahisisha mazingira ya ufanyaji biashara nchini kwa kuimarisha utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*) ikiwemo kuhakikisha taratibu bora za udhibiti na utoaji wa leseni za biashara; kuondoa mwingiliano wa majukumu kwa taasisi za usimamizi na udhibiti wa biashara; kuhimiza matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma za usajili na uendeshaji wa biashara; kupunguza idadi na viwango vya tozo, ada na kodi na kuweka mfumo imara wa ufuatiliaji na tathmini;
- (d) Kuratibu ujenzi wa masoko ya kimkakati katika maeneo ya mipakani ili kuwapa wakulima, wajasiriamali wadogo hususan wanawake na vijana fursa ya kuuza mazao yao nje ya nchi. Vilevile, wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara wataunganishwa kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi kupitia mifumo maalum;
- (e) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kutoa elimu na kuondoa vikwazo vya utaratibu wa stakabadhi ya mazao ghalani ikiwa ni pamoja na kuhamasisha sekta binafsi kujenga miundombinu ya maghala bora ya kuhifadha mazao mbalimbali, hususan vijijini;
- (f) Kubuni na kuendeleza mikakati ya uhamasishaji wa Watanzania kupenda kutumia bidhaa zinazozalishwa katika viwanda vya ndani;
- (g) Kuimarisha majadiliano ya biashara ya kikanda na kimataifa ili kuongeza fursa mbalimbali za ufanyaji biashara kwa bidhaa zinazozalishwa nchini ikiwa ni pamoja na kumahasisha sekta binafsi kuchangamkia fursa hizo;
- (h) Kuweka mikakati madhubuti ya kuimarisha biashara ya mtandao (*e-commerce*) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi; na
- (i) Kuandaa na kutekeleza mikakati ya upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuimarisha na kukuza biashara ndani na nje ya nchi.

### **Miundombinu (Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano)**

50.

Chama Cha Mapinduzi kinatambua umuhimu wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara, uchukuzi na mawasiliano kwa lengo la kuwezesha ujenzi wa uchumi imara unaojitegemea. Manufaa ya sekta hii ni pamoja na kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuwawezesha usafiri na usafirishaji wa bidhaa; na kuongezeka kwa matumizi ya fursa za kijiografia na mapato ya nchi.



51. Katika kipindi cha miaka mitano kilichopita (2015 - 2020), sekta ya miundombinu ililenga kuboresha miundombinu mbalimbali hususan reli, barabara, viwanja vya ndege na vivuko ambapo maboresho makubwa yamefanyika katika maeneo hayo na kuwezesha wananchi kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi. Katika kufikia azma hiyo maeneo mbalimbali yalitekelezwa na mafanikio mbalimbali kupatikana kama ifuatavyo:-

### **Ujenzi**

- (a) Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) umeimarishwa kwa kufanya yafuatayo:-
- (i) Kuongeza vyanzo vipya viwili (2) vya mapato vya Mfuko ambavyo ni tozo ya matumizi ya hifadhi ya barabara (*road reserve usage fees*) na tozo za maegesho ya magari (*parking fees*) ambapo mapato yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 722.7 mwaka 2015/16 hadi shilingi bilioni 784.8 kwa mwaka 2018/19;
  - (ii) Kuboresha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za barabara kwa kuhakikisha thamani na ubora wa kazi unaendana na fedha zilizotumika (*value for money*) kwa kununua na kuzipatia halmashauri vifaa vya kupima ubora wa kazi za matengenezo ya barabara (*dynamic cone penetrometer*); na
  - (iii) Kuboresha usimamizi wa barabara za vijijini na mijini kwa kuanzisha Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ili kusimamia ujenzi na matengenezo ya barabara za Wilaya.
- (b) Kutekelezwa kwa masuala ya kisera kwa kuchukua hatua zifuatazo:-
- (i) Kuunganisha makao makuu ya mikoa ambayo bado hayajaunganishwa kwa kiwango cha lami na kujenga barabara kuu zote zinazounganisha Tanzania na nchi jirani. Mikoa iliyounganishwa ni pamoja na iliyopo katika ushoroba wa Kusini ambayo ni Mtwara, Lindi na Ruvuma kwa kukamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Tunduru - Nakapanya - Mangaka - Mtambaswala, Namtumbo - Kilimasera - Matemanga - Tunduru pamoja na mikoa ya Dodoma, Manyara na Arusha kwa kukamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Dodoma - Mayamaya - Mela - Bonga - Babati - Arusha;
  - (ii) Kushirikisha kikamilifu vikundi vya wananchi katika kazi za matengenezo madogo madogo ya barabara ambapo vikundi vya wananchi, hususan waliopo kwenye maeneo ya miradi vimeendelea kushiriki kikamilifu katika kazi za matengenezo madogo madogo ya barabara kupitia mpango wa nguvukazi (*labour based*) ambapo asilimia 20 ya fedha za Mfuko wa



Barabara zimekuwa zikitengwa na kutumika katika mikoa yote;

- (iii) Kuwezesha makandarasi wazalendo kushiriki katika kazi kubwa za ujenzi wa barabara kwa kuwapatia dhamana kupitia mfuko wa kuwasaidia makandarasi wa ndani wadogo na wa kati (madaraja ya 4 - 7 makandarasi wa kawaida na madaraja ya 2-3 makandarasi wa kazi maalum) ili kuwajengea uwezo wa kutumia fursa za kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za sekta ya ujenzi;
- (iv) Kukuza ushindani wa makandarasi wa ndani kwa kutoa mafunzo mbalimbali yenye lengo la kuwajengea ujuzi kupitia Mpango wa Mafunzo Mahsusi kwa Makandarasi (*Sustainable Structured Training Programme – SSTP*) ambapo idadi ya makandarasi waliofaidika na mpango huo imeongezeka kutoka 4,021 mwaka 2015 hadi 5,037 mwaka 2019; na
- (v) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuwajengea uwezo makandarasi wazawa, kimtaji na menejimenti ya uendeshaji wa kampuni kwa kuwashirikisha kikamilifu katika ujenzi wa miradi mikubwa ya barabara na madaraja ambapo jumla ya kampuni nane (8) zilipatiwa miradi tisa (9) kati ya miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara na viwanja vya ndege.

### **Barabara**

52. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 – 2020), Chama Cha Mapinduzi kiliisimamia Serikali katika uendelezaji wa barabara nchini na kuweza kuongeza mtandao wa barabara za kiwango cha lami, hususan zile zinazounganisha mikoa na wilaya kwa lengo la kuimarisha usafiri na usafirishaji. Katika kufikia azma hiyo, ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 2,023.34 zilikamilika pamoja na madaraja 10. Ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 748.17 na madaraja saba unaendelea.
53. Uimarishaji wa usafiri na usafirishaji umewezeshwa pia kwa kukamilisha ukarabati wa barabara zenye urefu wa kilomita 404.7. Katika kupunguza foleni katika miji na majiji, barabara zenye urefu wa kilomita 97.3 zimejengwa. Upembuzi yakinifu wa barabara zenye urefu wa kilomita 5,974.2 na daraja moja umekamilika. Upembuzi yakinifu unaendelea kwa barabara zenye urefu wa kilomita 3,342.6 kwa lengo la kuwezesha shughuli za ujenzi na ukarabati kuanza.
54. Mchanganuo wa miundombinu mbalimbali iliyofanyiwa kazi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020) ni kama ifuatavyo:-

#### **(a) Miundombinu ya Barabara**

- (i) *Barabara ambazo ujenzi umekamilika (Kilomita 2,023.34)*
  - Sumbawanga – Matai – Kasanga (km 56);



- Magole – Turiani (km 45.2);
- Bariadi - Lamadi (km 13);
- Mbeya – Lwanjilo (km 17);
- Bagamoyo - Makofia - Msata (km 7);
- Kisarawe - Maneromango (km 10.2);
- Nyamuswa – Bunda – Kisorya;
  - Sehemu ya Bulamba – Kisorya (km 24);
- Babati – Dodoma (km 195.5);
- Sumbawanga - Kanyani – Nyakanazi;
  - Sehemu ya Sumbawanga – Kizi – Kibaoni (km 151.6);
  - Sehemu ya Sitalike – Mpanda (km 36.9);
  - Sehemu ya Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 27);
  - Sehemu ya Kidahwe – Kasulu (km 50); na
  - Sehemu ya Kibondo – Nyakanazi (km 26).
- Nzega – Tabora (Puge) (km 20.5);
- Manyoni - Itigi – Tabora;
  - Sehemu ya Manyoni – Itingi – Chaya (km 89.35);
  - Sehemu ya Chaya – Nyahua (km 41); na
  - Sehemu ya Nyahua – Tabora (km 85).
- Mangaka – Mtambaswala (km 65);
- Makutano – Nata – Mugumu;
  - Sehemu ya Makutano – Nata (Sanzate) (km 22);
- Kyaka – Bugene (km 28);
- Tunduru – Namtumbo (km 194);
- Tunduru – Mangaka ( km 137);
- Mwigumbi – Maswa – Bariadi;
  - Sehemu ya Mwigumbi – Maswa (km 50.3);
  - Sehemu ya Maswa – Bariadi (km 18);
- Tabora – Urambo (km 8.8);
- Uyovu – Bwanga – Biharamulo (km 112);
- Kisesa – Usagara (km 17);
- Katumba – Mbambo – Tukuyu;
  - Sehemu ya Busokelo – Mbambo (km 10);
- Kidahwe - Kasulu (Kanyani) (km 50);
- Kikusya – Ipinda – Matema Beach ( km 39.5);
- Barabara ya KIA- Mererani ( km 26);
- Mwanga – Kikweni – Lomwe (km 3.2);
- Kaliua – Kazilambwa (km 42);
- Dodoma University Road (km 12);
- Njombe – Ndulamo - Makete;
  - Sehemu ya Njombe – Moronga (km 31);
  - Sehemu ya Moronga – Makete (km 15.85);
- Tabora – Ipole – Koga – Mpanda;
  - Sehemu ya Tabora – Sikonge (Usesula) (km 30);
  - Sehemu ya Usesula – Komanga (km 35.5 );
  - Sehemu ya Komanga – Kasinde (km 27.74);
  - Sehemu ya Kasinde – Mpanda (km 34);
- Sanya Juu – Kamwanga;



- Sehemu ya Sanya Juu – Alerai (km 32.2);
  - Mbinga – Mbamba bay (km 34);
  - Mtwara – Newala – Masasi;
    - Sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 28);
  - Mbande – Kongwa Jct. – Mpwapwa (km 13);
  - Itoni – Ludewa – Manda;
    - Sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 12).
- (ii) *Barabara zinazoendelea na ujenzi (km 748.17)*
- Dumila – Kilosa;
    - Sehemu ya Ludewa – Kilosa (km 18);
  - Maswa - Bariadi (km 31.7);
  - Bulamba – Kisorya (km 27);
  - Sumbawanga - Kanyani – Nyakanazi;
    - Sehemu ya Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 8);
    - Sehemu ya Kibondo – Nyakanazi (km 24);
  - Manyoni – Itigi – Tabora;
    - Sehemu ya Chaya – Nyahua (km 44.4);
  - Makutano – Nata – Mugumu;
    - Sehemu ya Makutano – Nata (Sanzate) km 28;
  - Urambo – Kaliua (km 28);
  - Katumba – Mbambo – Tukuyu;
    - Sehemu ya Bujesi – Mbambo (km 7);
    - Sehemu ya Tukuyu – Mbambo (km 10);
  - Mwangi – Kikweni – Lomwe (km 4.26);
  - Njombe – Ndulamo – Makete;
    - Sehemu ya Njombe – Moronga (km 22.9);
    - Sehemu ya Moronga – Makete (km 37.65);
  - Tabora – Ipole – Koga – Mpanda;
    - Sehemu ya Usesula – Komanga (km 79.5);
    - Sehemu ya Komanga – Kasinde (km 92.26);
    - Sehemu ya Kasinde – Mpanda (km 84);
  - Mbinga - Mbamba Bay (km 32);
  - Mtwara - Newala – Masasi;
    - Sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 22);
  - Mbande - Kongwa Jct - Mpwapwa (km 6.5);
  - Itoni – Ludewa – Manda;
    - Sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 38);
  - Musoma – Makojo – Busokelo (km 5);
  - Mpemba – Isongole (km 49);
  - Mto wa Mbu – Loloiondo;
    - Sehemu ya Wasso (Loliondo) – Sale Junction (km 49).
- (iii) *Barabara zilizokarabatiwa na kukamilika (km 404.7)*
- Mafinga – Igawa (km 137.9);
  - Ushirombo – Lusahunga (km 110);
  - Segera – Same – Himo;
  - Sehemu ya Mkumbara – Same (km 96);



- Arusha – Moshi – Himo – Holili;
    - Sehemu ya Arusha (Sakina) – Tengeru (km 14.1);
  - Arusha Bypass (km 42.4);
  - Kawawa Jct - Mwenge (km 4.3).
- (iv) *Barabara ambazo upembuzi yakinifu na usanifu wa Kina umekamilika (km 5,974.2)*
- Singida – Sepuka – Ndago – Kizaga (km 89);
  - Natta – fort Ikoma (km 30);
  - Sanya Juu – Boma Ng’ombe (km 25);
  - Matai – Kasesya (km 50);
  - Rujewa – Madibila – Mafinga (km 151);
  - Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200);
  - Makongolosi – Rungwa – Mkiwa (km 412);
  - Kibaha – Mapinga (km 23);
  - Geita – Bukoli – Kahama (km 107);
  - Ipole – Rungwa (km 172);
  - Njombe (Kibena) – Lupembe – Madeke (Mfuji);
  - Morogoro/Njombe Border (km 125);
  - Tabora – Mambali – Bukene – Itobo – Kahama (km 149);
  - Lupilo – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo – Kitanda (km 296);
  - Ifakara – Mahenge (km 67);
  - Kibondo – Mabamba (km 35);
  - Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Matala – Oldean Junction (km 328);
  - Mugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105);
  - Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 74);
  - Makofia – Mlandizi – Vikumbulu (km 148);
  - Handeni – Kiberashi – Kondoa – Singida (km 460);
  - Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magohe – Bunju (km 34);
  - Kisarawe – Mlandizi (km 52);
  - Kiboroloni – Tsuduni – Kidia (km 10.8);
  - TPC – Mabogini – Kahe (km 11.4);
  - Nyamirembe Port – Katoke (km 50);
  - Iringa – Ruaha National Park (104);
  - Njombe (Ramadhani) – Iyayi (km 74);
  - Mziha – Handeni (km 68);
  - Kilosa – Mikumi (72.8);
  - Makambako – Songea (km 295);
  - Lusahunga – Rusumo (km 92);
  - Nyakasanza – Kobero (km 60);
  - Mlandizi – Chalinze (km 53);
  - Mbeya – Tunduma (km 104);
  - Mbeya – Igawa (km 116);
  - Arusha – Kibaya – Kongwa (km 430);
  - Bugene – Kasulo (BENACO) (km 124);
  - Mwanangwa – Misasi – Salawe – Kahama (km 149);





- Magu – Bukwimba – Ngudu – Jojiro (km 64);
- Tarime – Mugumu (km 87);
- Amani – Muheza (km 34);
- Murushaka – Nkwenda – Murongo (km 125);
- Morogoro (Bigwa) – Mvuha (km 78);
- Kamanga - Sengerema (km 35);
- Upanuzi wa (Tegeta) – Bagamoyo (km 57);
- Kibada – Kimbiji (km 29.2);
- Kongwa – Mbuyuni NARCO JCT – Kibaya – Orkemet (km 340);
- Madaba – Mundindi (Liganga) – Mkiu (km 46);
- Kitahi – Lituhi (km 93);
- Madaba – Mavanga – Ludewa (40).

(v) *Barabara ambazo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaendelea (km 3,342.6)*

- Kibaoni - Majimoto - Inyonga (km 162);
- Mpanda - Ugala - Kaliua - Ulyankulu - Kahama (km 428);
- Murushaka - Murongo (km 125);
- Kilindoni - Ras Mkumbi (km 55);
- Morogoro - Dodoma (km 263);
- Mwanza - Mwanza/Shinyanga (km 102);
- Kibaoni - Majimoto - Kasansa - Muze - Kilyamatundu (km 200);
- Nyehunge - Sengerema (km 68);
- Mvuha - Kisasi (km 73);
- Bigwa - Kisasi (km 151);
- Geita - Nzera - Nkome (km 54);
- Murugarama - Rulenge - Nyakahura (km 85);
- Karatu - Mbulu - Haydom - Singida (km 190);
- Bariadi-Kisesa-Mwandoya-Ngoboko-Mwanhuzi-Sibiti-Mkalama-Iguguno (km 289);
- Mika - Utegi - Shirati (km 44);
- Chimala - Matamba - Kitulo (km 51);
- Upanuzi wa Kitonga Escarpment (km 10);
- Mbulu - Magugu (Mbuyu wa Mjerumani) (km 63);
- Mafinga - Mgololo (km 77.6);
- Babati (Dareda) – Dongobesh (km 60);
- Liwale - Nachingwea - Ruangwa (185);
- Kongwa Ranch - Kiteto - Simanjiro - KIA (km 483);
- Likuyufusi - Mkenda (km 124).

(vi) *Madaraja yaliyokamilika kujengwa*

- Kilombero (Magufuli) na barabara unganishi (km 9.3);
- Nyerere (Kigamboni) na barabara unganishi (km 10);
- Kavuu (Katavi);
- Sibiti (Singida);
- Lukuledi II (Lindi);



- Ruvu Chini (Pwani);
- Magara (Manyara);
- Momba (Rukwa);
- Mlalakuwa (Dar es Salaam);
- Mara (Mara).

(vii) *Madaraja yanayoendelea kujengwa*

- Kigongo - Busisi (Mwanza);
- Ruhuhu (Ruvuma);
- Salender (Daraja jipya) (DSM);
- Daraja Jipya la Wami Chini (Pwani);
- Pangani (Tanga);
- Kitengule (Kagera);
- Msingi (Singida);
- Daraja la Gerezani (Dar es Salaam).

(viii) *Daraja ambalo usanifu wake umekamilika*

- Daraja la Simiyu (Mwanza).

(ix) *Daraja ambalo usanifu wake unaendelea*

- Mzingi (DSM).

**(b) Kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam**

(i) Katika kutekeleza azma ya kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye jumla ya kilomita 68.3 umekamilika. Vilevile, ujenzi wa Barabara ya Juu ya Mfugale (*Mfugale flyover*) umekamilika na ujenzi wa *Interchange* ya Ubungo unaendelea. Barabara zilizokamilika ni:-

- Mbezi - Malamba Mawili Kinyerezi - Banana (km 14);
- Tangi Bovu - Goba (km 5.2);
- Kimara Baruti - Msewe - Changanyikeni (km 2.0);
- Kimara Kilungule - *External* Mandela Road (km 8.8);
- Kigogo *Round About* - Bonde la Msimbazi - Twiga/Msimbazi Junction (km 0.5);
- Tabata Dampo - Kigogo (km 1.6);
- Kibamba - Mlonganzila (km 4.0);
- Ardhi - Makongo - Goba (Sehemu ya Goba - Makongo km 4.0);
  - Tegeta Kibaoni - Wazo Hill - Goba - Mbezi/Morogoro Rd;
    - Sehemu ya Goba - Madale (km 5.0); na
    - Sehemu ya Goba - Mbezi/ Morogoro Rd (km 7.0).

(ii) Miradi mingine ya Barabara (km 52.1) za kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam inayoendelea na kuwa katika hatua mbalimbali ni:-

- Tegeta Kibaoni - Wazo Hill - Goba - Mbezi/Morogoro Rd;
  - Sehemu ya Madale - Wazo Hill (km 4.2);



- Banana – Kitunda – Kivule – Msongola;
  - Sehemu ya Kitunda – Kivule (km 3.2);
- Upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha kuwa njia nane (8 lanes), (km 19.2) na madaraja matatu ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji;
- Ardhi – Makongo – Goba (km 5.0); na
- Upanuzi wa barabara ya Morocco – Mwenge (km 4.3).

**(c) Miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya pili na ya tatu**

Utekelezaji wa Mradi wa Awamu ya Pili wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (*BRT Phase II*) ambao unahusisha barabara za Nyerere na Kilwa (km 19.3) umeanza na unaendelea. Aidha, maandalizi ya utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Miundombinu ya Mabasi Yaendayo haraka (*BRT Phase III*) ambao unahusisha barabara za Nyerere, Uhuru, Bibi Titi Mohamed na Azikiwe (km 23.6) mapitio ya usanifu na nyaraka za zabuni yanaendelea;

**(d) Kupunguza msongamano wa magari katika majiji na miji mingine**

- (i) Katika kutekeleza azma ya kupunguza msongamano wa magari katika majiji ya Mwanza, Dodoma, Mbeya, Arusha na Tanga pamoja na miji ya Iringa na Babati jumla ya kilomita 100.8 za barabara zilipangwa kujengwa. Barabara zilizopangwa kujengwa na utekelezaji wake ni:-
- Barabara ya Usagara - Kisesa (km 17) (Mwanza): Ujenzi umekamilika;
  - Upanuzi wa barabara ya Mwanza - Mwanza Airport (km 12): Ujenzi umekamilika;
  - Uyole - Songwe (km 40) (Mbeya): Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea;
  - Iringa Bypass (km 7): Usanifu wa kina umekamilika. Ujenzi umeanza;
  - Upanuzi wa barabara ya Arusha Mjini - Kisongo (km 8.8): Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika;
  - Babati Bypass (km 12): Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaendelea;
  - Utofu - Majani Mapana - Duga Mwembeni (km 4) (Tanga): Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika.

**(e) Kuimarisha usafiri wa majini katika mito, maziwa na bahari ili kufanya barabara kuwa na kiunganishi cha uhakika**

- Ujenzi wa vivuko vitatu vya Kigongo – Busisi (Mwanza), Pangani – Bweni (Tanga) na Magogoni – Kigamboni (DSM) ulikamilika;
- Ujenzi wa vivuko vipya vinne unaendelea ambapo vivuko hivyo vitakapokamilika vitatoa huduma katika maeneo



- ya Nkome – Chato – Muharamba (Geita), Kayenze – Bezi (Mwanza), Bugolora – Ukara (Mwanza) na Nyamisati – Mafia (Pwani);
- Ununuzi wa boti tano za uokozi kwa ajili ya Ilugwa, Nafuba na Gana katika Kisiwa cha Ukerewe, boti moja kwa ajili ya kivuko cha Magogoni pamoja na boti moja kwa ajili ya kivuko cha Lindi – Kitunda ulikamilika;
- Upanuzi wa jengo la abiria wa kivuko cha Magogoni kwa kwa upande wa Kigamboni kwa awamu ya awamu umekamilika;
- Ujenzi wa maegesho ya kivuko cha Kayenze – Bezi umekamilika;
- Ujenzi wa maegesho ya Nyamisati – Mafia na Kikove – Malinyi unaendelea.

**(f) Nyumba na Majengo ya Serikali**

- (i) *Kujenga nyumba za watumishi wa umma na majengo ya Serikali yenye kuzingatia mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu*  
Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilikamilisha ujenzi wa majengo ya Serikali na nyumba 103 zinazojumuisha Ofisi pamoja na nyumba za Makazi ya Viongozi na Watumishi wa Umma.
- (ii) *Kuboresha karakana 6 za kutengeneza samani za ofisi na nyumba za Serikali ili kupunguza gharama za uagizaji wa samani kutoka nje ya nchi*  
Upembuzi yakinifu kwa ajili ya kukarabati na kuendeleza Karakana za Samani katika Mikoa sita ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Tabora, Mbeya na Arusha umekamilika. Ukarabati umeanza kufanyika kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza itahusisha Mikoa ya Dodoma, Mwanza na Arusha. Awamu ya pili itahusisha Mikoa iliyobaki ya Dar es Salaam, Mbeya na Tabora.
- (iii) *Kuendelea na mradi wa ujenzi wa nyumba 10,000 kwa ajili ya watumishi wa umma ambapo asilimia 50 zitajengwa katika maeneo ya vijijini*  
Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) iliendelea na ujenzi wa nyumba 10,000 za Watumishi wa Umma kwa kujenga jumla ya nyumba **1,265** katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Kati ya nyumba hizo, ujenzi wa nyumba **527** kwa ajili ya kuwapangisha na kuwakopesha watumishi wa Umma umekamilika. Aidha, nyumba **738** zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. TBA pia inaendelea na ujenzi wa makazi ya Watumishi wa Umma, eneo la Bunju 'B' jijini Dar es Salaam unaohusisha nyumba **851**. Mradi huu umekamilika katika awamu ya kwanza na ya pili ambapo nyumba 219 zimekamilika na kuanza kuuzwa kwa watumishi wa umma. Utekelezaji katika awamu ya tatu unaendelea na utakapokamilika utakuwa umetoa makazi kwa watumishi wa umma wapatao 632.



- (iv) *Kujenga nyumba za watumishi wa umma na majengo ya Serikali kupitia Watumishi Housing*  
Watumishi Housing wamejenga nyumba za makazi za kuuza kwa Watumishi na watu wengineo. Jumla ya nyumba 893 zimejengwa katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Dodoma (Kisasa Relini – 39, Kisasa Hiltop - 70), Dar es Salaam (Bunju B – 65, Gezaule Kigamboni – 329). Nyumba za maghorofa (apartments) 88 eneo la Magomeni Usalama (Dar es Salaam), Mwanza (Kisasa – 59) na Morogoro (Mkundi – 50). Pia, Watumishi Housing wamejenga majengo ya taasisi mbalimbali kama vile ujenzi wa nyumba za walimu 186 katika mikoa 17 Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Ujenzi wa nyumba saba za polisi – Nyang’wale, Geita; na Ujenzi wa Jengo la Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) katika mji wa kiserikali Mtumba – Dodoma

**Katika miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaelekeza Serikali kuendeleza shughuli za ujenzi wa miundombinu mbalimbali ili kuifanya sekta ya ujenzi ifikie malengo yake ya kuwezesha wananchi kuendelea na uzalishaji kwa ajili ya kuongeza kipato chao. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali itatekeleza yafuatayo:-**

**(a) Kuimarisha Mfuko wa Barabara**

Ili kufikia azma ya Serikali, Mfuko wa Barabara unalenga kutekeleza masuala yafuatayo:-

- (i) Kuimarisha uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya Mfuko kwa kutumia mifumo ya kielektroniki. Hii ni pamoja na kuboresha mfumo wa ukusanyaji mapato unaotumiwa na TARURA na TANROADS;
- (ii) Kufanya tafiti zenye lengo la kuibua na kuongeza vyanzo vya mapato ya Mfuko pamoja na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji kwenye vyanzo vilivyopo;
- (iii) Kuimarisha uwezo wa kitaalam, kimfumo na kitaasisi wa TARURA wa kutekeleza shughuli za matengenezo ya barabara;
- (iv) Kufanya tafiti juu ya matumizi ya teknolojia ya matengenezo ya barabara ya gharama nafuu pamoja na teknolojia ya ujenzi bora wa barabara;
- (v) Kuimarisha ufuatiliaji wa matumizi na shughuli za matengenezo ya barabara ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha inapatikana; na
- (vi) Kufanya marejeo ya mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara kati ya TANROADS na TARURA.



**(b) Masuala ya kisera**

- (i) Kuunganisha makao makuu ya mikoa na wilaya zilizobakia nchini kwa barabara za lami na barabara zinazounganisha Tanzania na nchi jirani;
- (ii) Kushirikisha kikamilifu vikundi vya wanavijiji/wananchi (*community works units*) pamoja na Makandarasi wadogo katika kazi za matengenezo madogo ya barabara kama vile kufyeka nyasi, kuzibua mifereji/mitaro ya barabara na kufanya usafi wa barabara;
- (iii) Kuendelea kuwajengea uwezo makandarasi wazalendo ikiwemo kuwapatia kazi nyingi zaidi za fedha za Mfuko wa Barabara na kuwawezesha kupata mikopo ili kushiriki kikamilifu kwenye kazi kubwa za ujenzi wa barabara, madaraja na majengo;
- (iv) Kuendelea kuweka taa za barabarani katika maingilio ya majiji na miji nchini ili kuimarisha usalama;
- (v) Kuboresha na kuimariasha miundombinu kwenye maeneo yanayoathiriwa mara kwa mara na mafuriko ikiwemo eneo la Jangwani, Jijini Dar es Salaam;
- (vi) Kuimarisha mfumo shirikishi wa ulinzi wa miundombinu kwa kurekebisha sheria ya kulinda miundombinu ya barabara, kutoa elimu na kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika ulinzi wa miundombinu hiyo;
- (vii) Kuanzisha na kuimarisha taasisi za umma ili ziweze kushiriki katika ujenzi wa majengo na miundombinu ya kimkakati;
- (viii) Kuanzisha kanzidata ya wataalam wote wa sekta kwa ajili ya kutunza kumbukumbu na taarifa zao ili zitumike katika kuendeleza sekta ya ujenzi; na
- (ix) Kuwekeza katika matumizi ya teknolojia stahiki za utekelezaji wa shughuli za ujenzi ili kupunguza gharama za vifaa vya ujenzi (*building materials*) na kuongeza ubora wa kazi.

**(c) Barabara**

Kukamilisha ujenzi na ukarabati wa barabara unaoendelea kwa kiwango cha lami katika barabara kuu na barabara za Mikoa kama ifuatavyo:-

- (i) *Kukamilisha ujenzi (km 1,716.75)*
  - Sumbawanga - Kanyani – Nyakanazi;
    - Sehemu ya Kibaoni – Sitalike (km 71.1)
    - Sehemu ya Vikonge – Uvinza (km 159)
    - Sehemu ya Kasulu – Kabingo (km 184)





- Sehemu ya Nduta Junction – Kibondo Mjini (km 26)
  - Tabora - Ipole - Koga - Mpanda (km 202 kati ya km 359);
  - Mto wa Mbu - Loliondo: Sehemu ya Sale Junction – Mto wa Mbu (km 164);
  - Itoni - Ludewa - Manda (km 185 kati ya km 211);
  - Makurunge - Saadani - Pangani – Tanga (km 178);
  - Magole – Turiani – Handeni: Sehemu ya Turiani – Mziha - Handeni (km 128);
  - Nyamuswa – Bunda – Bulamba – Kisorya – Nansio: Sehemu ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 56.4);
  - Njombe – Makete: Sehemu ya Moronga – Makete (km 37.65);
  - Musoma - Makojo - Busekela (km 92);
  - Katumba - Mbambo – Tukuyu (km 53 kati ya km 80);
  - Mbinga - Mbamba bay (km 25 kati ya km 66);
  - Rudewa – Kilosa (km 14 kati ya km 28);
  - Kisarawe - Maneromango (km 44 kati km 54);
  - Mpemba – Isongole (Tanzania/Malawi) (km 15 kati ya km 49);
  - Kibosho Shine - Kwa Raphael - International School (km 30.5 km kati ya 43);
  - Pugu - Kifuru - Mbezi Mwisho - Mpiji Magoe - Bunju (km 22 kati ya km 34);
  - Kirua - Nduoni - Marangu Mtoni (km 16.5 kati ya km 31.5);
  - Mwanga - Kikweni - Lomwe (km 9.3 kati ya km 22.5);
  - Kawawa Jct - Mwenge (km 4.3).
- (ii) *Kuanza ujenzi mpya (km 6,006.04) na ukarabati wa barabara kwa kiwango cha lami:-*
- Upanuzi wa Barabara ya Kibaha – Chalinze kuwa njia nane (km 75)
  - Handeni - Kiberashi - Kondoa – Singida: Sehemu ya Handeni – Kiberashi (km 50);
  - Arusha – Kibaya – Kongwa (km 430);
  - Makongolosi – Rungwa – Mkiwa (km 412);
  - Nyoni – Maguu (km 25);
  - Kongwa – Mbuyuni NARCO Junction – Kibaya – Orkesmet (km 340);
  - Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Matala – Oldeani Junction (km 328);
  - Mtwara pachani – Lingusenguse – Tunduru (km 300);
  - Lupilo – Malinyi – Kilosa Kwa Mpepo – londo – Kitanda (km 296);
  - Itoni – Ludewa – Manda);
  - Sehemu ya Itoni – Lusitu (km 50);



- Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ileje (km 90.7);
- Sehemu ya Mawengi – Manda (km 110) ;
- Mtwara – Newala – Masasi (km 160);
- Makete – Kitulo – Isyonje (km 97.6);
- Ipole – Rungwa (km 172);
- Lujewa – Madibila – Mafinga (km 15);
- Tabora – Mambali – Bukene – Itobo – kahama (km 149);
- Mwanangwa – Misasi – Salawe – Kahama (km 149);
- Makofia – Mlandizi – Vikumburu (km 148);
- Mugakorongo – Rwambaizi – Murongo (km 125);
- Njombe (Kibena ) – Lupembe – Madeke (Mfuji) – Morogoro / Njombe Border (km 125);
- Bugene – Kasulo (Benaco) (km 124);
- Mbamba Bay - Liuli – Lituhi (km 112.5);
- Geita – Bukoli – Kahama (km 107);
- Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105);
- Iringa – Ruaha National Park (km 104);
- Kitahi – Lituhi (km 93);
- Singida - Sepuka – Ndago – Kizaga (km 89);
- Tarime – Mugumu (km 87);
- Morogoro (Bigwa) – Mvuha (km 78);
- Sanya Juu – Kamwanga: Sehemu ya Alerai – Kamwanga (km 42.8) ;
- Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 74);
- Njombe (Ramadhani) – Iyayi (km 74);
- Kilosa – Mikumi (km 72.8);
- Ifakara – Mahenge (km 67);
- Magu – Bukwimba – Ngudu – Jojiro (km 64);
- Kahama – Nyamilangano – Uyogo (km 54);
- Kisarawe – Mlandizi (km 52);
- Nyamirembe Port – Katoke (km 50);
- Nanganga- Ruangwa – Nachingwea (km 100);
- Mbande – Kongwa Junction – Mpwapwa: Sehemu ya Kongwa – Mpwapwa (km 30);
- Matai – Kasesya (km 50);
- Madaba – Mundindi (Liganga) – Mkiu (km 46);
- Makutano – Natta – Mugumu (75);
  - Sehemu ya Sanzate – Natta (km 40);
  - Sehemu ya Natta – Mugumu (km 35);
- Madaba – Mavanga – Ludewa (km 40);
- Kamanga – Sengerema (km 35);
- Kibondo – Mabamba (km 35);
- Amani – Muheza (km 34);
- Natta – Fort Ikoma (km 30);
- Sehemu ya Boma Ng’ombe – Sanya Juu (km 25);
- Kibaha – Mapinga (km 23);
- TPC – Mabogini – Kahe (km 11.4);
- Kiboroloni – Tsudini – Kidia (km 10.8);;



- Iponjola – Kiwira Port (km 6);
  - Mganza – Kasenda (km 4.2);
  - Kuanza ujenzi wa Kituo cha ushuru wa Forodha ‘One Stop Border Post (OSBP) cha mpakani mwa Tanzania/Burundi
  - Kasulu – Manyovu (km 45);
  - Nachingwea – Masasi (km 45);
  - Mlowo – Kamsamba - Utambalila – Chetete (km 145.14);
  - Fuga Station – Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere (km 41)
  - Kukarabati barabara za kuunganisha na Reli ya SGR
  - Kukarabati barabara zilizoathiriwa sana na mvua
  - Chazuru – Melela (km 64);
  - London – Kiwira Coal Mines (km 7).
- (iii)** *Kuanza ukarabati (km 1,465.5) kwa barabara zifuatazo*
- Makambako – Songea (km 295);
  - Segera – same – himo: Sehemu ya Same – Himo (km 66);
  - Morogoro – Dodoma (km 263);
  - Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200);
  - Arusha – Moshi – Holili: Sehemu ya Tengeru – Moshi – Himo – Holili (km 83.5);
  - Mbeya – Tunduma (km 110);
  - Mbeya - Igawa (km 116);
  - Mwanza – Mwanza/Shinyanga Border (km 102);
  - Lusahunga – Rusumo (km 92);
  - Nyakasanza – Kobero (km 60);
  - Mlandizi – Chalinze (km 53);
  - Ibanda – Itungi Port (km 25).
- (iv)** *Kukamilisha/Kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina (km 7,542.75) barabara zifuatazo:-*
- Kongwa Ranch - Kiteto - Simanjiro - KIA (km 483);
  - Mpanda - Ugala - Kaliua - Ulyankulu - Kahama (km 428);
  - Mto wa Mbu - Longido - Karatu - Ngorongoro (km 300);;
  - Bariadi-Kisesa-Mwandoya-Ngoboko-Mwanhuzi-Sibiti-Mkalama-Iguguno (km 289);
  - Ruangwa – Nanjilinji – Kiranjeranje (km 120);
  - Ngongo – Mandawa – Chukuani (km 85);
  - Morogoro - Dodoma (km 263);
  - Kilwa - Liwale (km 258);
  - Babati - Orkesumet - Kibaya (km 225);
  - Kibaoni - Majimoto - Kasansa - Muze - Kilyamatundu (km 200);
  - Karatu - Mbulu - Haydom - Singida (km 190) ;
  - Liwale - Nachingwea - Ruangwa (185);
  - Inyonga – Ilunda – Kishelo – Kitunda (162.8);



- Kibaoni - Majimoto - Inyonga (km 162);
- Njombe (Kibena) – Lupembe – Madeke (Mfuji) – Morogoro/Njombe Border (km 125);
- Murushaka – Murongo (km 125);
- Likuyufusi – Mkenda (km 124) ;
- Kagwila – Ikola – Kalema (km 112);
- Mwanza - Mwanza/Shinyanga (km 102);
- Murugarama - Rulenge - Nyakahura (km 85);
- Mafinga - Mgololo (km 77.6);
- Mvuha – Kisasi (km 73);
- Nyehunge – Sengerema (km 68);
- Sanya Juu – Longido (km 65);
- Mbulu - Magugu (Mbuyu wa Mjerumani) (km 63);
- Babati (Dareda) – Dongobesh (km 60);
- Upanuzi wa (Tegeta) - Bagamoyo (km 57);
- Kilindoni – Ras Mkumbi – Mafia (km 55);
- Igowole - Kasanga - Nyigo (km 54.5);
- Geita - Nzera - Nkome (km 54);
- Muhutwe - Kamachumu - Muleba (km 53);
- Chimala - Matamba - Kitulo (km 51);
- Mika - Utegi - Shirati (km 44) ;
- Nyololo - Igowole - Mtwango (km 40.4) ;
- Nangombo – Chiwindi (km 40);
- Kibada - Kimbiji (km 29.2);
- Uru – Mamboleo – Materuni (km 10.2);
- Upanuzi wa Kitonga Escarpment (km 10);
- Miyombo - Lumuma – Kidete (km 71.2);
- Bungu – Nyamisati (km 43);;
- Holili – Tarakea (km 53);
- Buhongwa – Kayenze – Nyanguge – Airport (km 46.13).
- Iringa – Pawaga (km 76)
- Ifakara – Mlimba – Njombe (km 220)
- Ubena – Ngerengere – Mvuha (km 100)
- Gairo – Nongwe (km 54)
- Utete – Nyamwage (km 37)
- Orkesumet – Mererani – (km 119),
- Katesh - Haydom (km 70);
- Busega – Shigala – Ngasamo – Dutwa- Bariadi (km 47)
- Kyaka 2 – Katoro – Ibwera - Kanazi – Kyetema (km 60.65)
- Magoti – Makonge - Maruku – Kanyangereko (km 19)
- Mandela – Mkange – Saadani (km 62.6)
- Mbalizi – Chang’ombe – Mkwajuni – Patamele – Makongorosi (km 118);
- Ruanda – Nyimbili – Hasamba – Izyila – Itumba (km 79.7);
- Ibungu – Kafwafwa – Kyimo (km 66);
- Mkalamo – Kwamsisi – Mkata (km 70)



- Mombo – Mzeri – Muheza (km 42)
- Mabokweni – Maramba – Bombo Mtoni – Umba hadi Same (278km)
- Puge – Ndala – Ziba – Chona (km 83)
- Mambali – Bukumbi - Ishilimulwa – Shitage– Kahama (105km)
- Solwa – Old Shinyanga (km 65)
- Bubiki – Shinyanga (km 35)
- Upanuzi wa Usagara – Sengerema (km 56)
- Kibiti – Mloka – Matemele jct (km 162)
- Dodoma – Mvumi Hospital (33km)
- Ihumwa– Hombolo (24km)
- Fulo – Nyambiti – Mallya (km 73)
- Ulemo – Kinampanda – Gumanga – Mkalama (km 44)
- Ngoma – Sengerema (km 30.46)
- Mwandiga- Chankele – Mwamgongo – Kagunga (60km)
- Kagongwa – Bukooba (Kahama) - (km 11.31)
- Mbalizi – Shigamba ( 52km)
- Mbalizi –Chang’ombe – Galula (48 km).

**(d) Madaraja**

*(i) Kukamilisha ujenzi wa madaraja saba (7)*

- Salender (Daraja Jipya) (Dar es Salaam)
- Daraja Jipya la Wami (Pwani)
- Daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza)
- Daraja la Kitengule (Kagera)
- Daraja la Msingi (Singida)
- Daraja la Malagarasi katika barabara ya Kabingo – Kasulu – Manyovu (Kigoma)
- Daraja la Gerezani (Dar es Salaam)

*(ii) Kuanza ujenzi/ukarabati wa madaraja 14 yafuatayo:-*

- Kirumi (Mara)
- Pangani (Tanga)
- Wami Chini (Pwani)
- Simiyu (Mwanza)
- Mzinga (DSM)
- Malagarasi Juu katika Barabara ya Buhigwe – Kitanga – Kumsenga (Kigoma)
- Mkenda (Ruvuma)
- Mtera Dam (Iringa)
- Mitomoni (Ruvuma)
- Ugalla (Katavi)
- Bujonde (100m) - Mbeya
- Sanza (Singida)
- Upanuzi wa daraja la Ipyana (Mbeya)



- Kalebe (Kagera)
- (iii) *Kuanza/Kukamilisha usanifu wa madaraja 4 yafuatayo:-*
  - Malagarasi Chini (Kigoma)
  - Mkundi (Morogoro)
  - Godegode (Dodoma)
  - Mirumba (Katavi)

**(e) Kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam kwa kufanya yafuatayo:-**

- (i) *Kuanza/Kukamilisha ujenzi wa barabara za juu (Flyovers) kwenye makutano ya barabara katika maeneo yafuatayo:-*
  - Chang'ombe
  - Uhasibu
  - KAMATA
  - Morocco
  - Mwenge
  - Magomeni
  - Tabata
  - Fire
  - Makutano ya Ally Hassan Mwinyi na *United Nation*
  - Makutano ya Ally Hassan Mwinyi na Kinondoni.
- (ii) *Kukamilisha Ujenzi wa barabara (km 42.7)*
  - Upanuzi wa Kimara - Kibaha (km 19.2) na Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji
  - Tegeta Kibaoni - Wazo Hill - Goba - Mbezi/Morogoro Road: Sehemu ya Madale – Wazo Hill (km 4)
  - Banana - Kitunda - Kivule – Msongola (km 11.5)
  - Kibamba – Mloganzila: Sehemu ya Mloganzila – Mloganzila Citizen (km 8)
- (iii) *Kuanza ujenzi wa barabara (km 40.1)*
  - Upanuzi wa barabara ya Dar es Salaam Port -TAZARA - Uwanja wa Ndege (JNIA) (km 14);
  - Upanuzi wa Mwai Kibaki (Morocco - Kawe Round About) na Garden Road (km 9.1);
  - Ardhi - Makongo – Goba: sehemu ya Ardhi - Makongo (km 5);
  - Upanuzi wa barabara ya Uwanja wa Ndege (JNIA) - Pugu (km 8);
  - Upanuzi wa barabara ya Mbagala - Kongowe – Mwandege (km 4).
- (iv) *Kuanza/Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka (km 104.4):-*
  - Awamu ya II: Barabara ya Kilwa na Kawawa (km 19.3);
  - Awamu ya III: Barabara za Nyerere, Uhuru, Bibi Titi Mohamed na Azikiwe (Km 23.6);





- Awamu ya IV: Barabara ya Maktaba, Nyerere, Ali Hassan Mwinyi, Sam Nujoma na Mwenge – Tegeta (km 25.9);
- Awamu ya V: Barabara ya Mandela na Segerea – Tabata – Kigogo Round about (26.5);
- Awamu ya VI: Morrocco – Mwai Kibaki – Old Bagamoyo (km 9.1).

**(f) Kuanza/kukamilisha Miradi ya Kupunguza Msongamano katika Majiji na Miji Mingine yenye Jumla ya km 397 kama ifuatavyo:-**

- Kukamilisha Dodoma City Outer Ring Roads (km 110.2);
- Kukamilisha usanifu na Kuanza ujenzi Uyole - Songwe (km 40 Mbeya);
- Kuanza ujenzi wa Dodoma City Inner Ring Roads (km 15);
- Kukamilisha usanifu na kuanza ujenzi wa Babati Bypass (km 12);
- Upanuzi wa Barabara ya Arusha Mjini - Kisongo (km 8.8);
- Kuanza ujenzi wa Iringa Bypass (km 7);
- Kuanza usanifu na ujenzi wa Utofu - Majani Mapana - Duga Mwembeni (km 4) (Tanga);
- Upanuzi wa Barabara ya Dodoma – Dar es Salaam (km 50); Dodoma – Iringa (km 50); Dodoma – Singida (km 50); na Dodoma – Babati (km 50); na
- Barabara za juu (Fly overs) katika makutano ya Mijini kupunguza msongamano katika Jiji la Mwanza.

**(g) Mizani ya Kupima Magari**

Ili kulinda barabara zisiharibike mapema Serikali itaimarisha udhibiti wa uzito wa magari na kupunguza muda wa upimaji kwa kufanya yafuatayo:-

- (i) Kufunga mizani ya kisasa (*Electronic load cell*) ambayo itakuwa inatoa taarifa ya mwenendo mzima wa hali ya mizani wakati gari linapimwa ili kupata vipimo sahihi katika mizani; na
- (ii) Kufunga mfumo wa kielektroniki ambao utawezesha magari kupimwa kwenye mizani bila kuwa na operator (*human intervotion*).

**(h) Nyumba na Majengo ya Serikali**

Ili kukabiliana na changamoto ya mahitaji ya nyumba na majengo, Serikali kupitia TBA itatekeleza masuala yafuatayo:

- (i) Kuandaa na kutekeleza mipango ya kujenga na kukarabati nyumba na majengo ya Serikali kwa gharama nafuu na kwa kuzingatia mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu;



- (ii) Kujenga nyumba zenye uwezo wa kuchukua familia nyingi (*apartments*) kwenye viwanja vya nyumba zilizorejeshwa kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI;
- (iii) Kuiongezea TBA mtaji ili nyumba nyingi za kupangishwa watumishi wa umma ziweze kujengwa katika maeneo mbalimbali (*housing programme*);
- (iv) Kuendeleza ujenzi wa majengo yatakayotumika kama ofisi kwa taasisi za Serikali ili kuipunguzia gharama kubwa ya kodi ya pango katika soko;
- (v) Kuendeleza mradi wa nyumba 10,000 kwa ajili ya viongozi wa Serikali na watumishi wa umma;
- (vi) Kuendeleza kazi za usanifu na kuimarisha usimamizi wa majengo ya Serikali ikiwemo awamu ya pili ya mradi wa ujenzi wa majengo ya Serikali katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba, Dodoma; na
- (vii) Kuimarisha utekelezaji wa mikakati ya kuboresha karakana za kutengeneza samani za ofisi na nyumba za Serikali ili kupunguza gharama za uagizaji wa samani kutoka nje ya nchi.

*Watumishi Housing itaendelea kubuni na kutekeleza miradi ya kuwanufaisha Watumishi wa umma, wanachama wa mifuko ya jamii na wafanyakazi wengine kwa kujenga nyumba bora na zenye gharama nafuu. Miradi inayotarajiwa kutekelezwa katika kipindi kijacho ni :-*

- (i) Ujenzi wa nyumba za makazi eneo la Njedengwa - Kisasa Hiltop, Dodoma utakaokuwa na awamu mbili. Kumalizia awamu ya kwanza inayohusisha ujenzi wa nyumba 70 kati ya nyumba 174 na kuanza Awamu ya pili itakayokuwa na nyumba 104;
- (ii) Ujenzi wa nyumba za maghorofa (Apartments) - Dar es Salaam utakaohusisha ujenzi wa nyumba 150 eneo la Victoria jijini;
- (iii) Ujenzi wa jengo la biashara eneo la Gezaulole, Kigamboni, katika mradi wa nyumba za makazi za Gezaulole;
- (iv) Ujenzi wa nyumba za maghorofa (apartments) 124 za maghorofa katika mradi wa Kisasa Relini, Dodoma;
- (v) Ujenzi wa jengo la ofisi - Medeli Dodoma; na
- (vi) Kutekeleza mradi wa uuzaji wa viwanja vya makazi na biashara eneo la USA River Arusha



56.

**Uboreshaji wa Barabara za Vijijini na Mijini**

Chama Cha Mapinduzi kupitia Serikali yake kimeendelea kuhakikisha kuwa miundombinu ya barabara za mijini na vijijini inaboreshwa kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya miji ya kimkakati nane, Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam, Mradi wa kuendeleza miji 18 na Mfuko wa Barabara. Utekelezaji wa miradi hii umefanikiwa kwa kuanzisha Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) ambao unahudumia mtandao wa barabara za mamlaka za serikali za mitaa wenye urefu wa takribani kilomita 108,946 za vijijini na mijini. Kuimarika kwa miundombinu ya barabara za mijini na vijijini kunachangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi na kuondoa umasikini kwa kuimarisha usafiri na usafirishaji wa abiria na bidhaa. Katika kufikia mafanikio hayo, Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita 2015 - 2020 kimeisimamia Serikali kuboresha barabara za mijini na vijijini kama ifuatavyo:-

**(a) Ujenzi wa Barabara**

- (i) Kuimarisha barabara 42 za Miji ya Kimkakati zenye urefu wa kilomita 242 za kiwango cha lami katika Majiji matano ya Mbeya, Tanga, Mwanza, Arusha na Dodoma pamoja na Halmashauri tatu za Manispaa za Mtwara, Kigoma/Ujiji na Ilemela;
- (ii) Kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam kwa kujenga barabara zenye urefu wa kilomita 140 kwa kiwango cha lami katika Manispaa za Kinondoni, Ilala na Temeke;
- (iii) Kuimarisha barabara zenye urefu wa kilomita 175 kwa kiwango cha lami katika halmashauri za miji na manispaa 18, zikiwemo halmashauri za Manispaa za Morogoro, Tabora, Moshi, Sumbawanga, Shinyanga, Songea, Singida, Musoma, Iringa, Bukoba, Lindi na Mpanda na halmashauri za Miji ya Babati, Kibaha, Korogwe, Njombe, Geita na Bariadi;
- (iv) Kuwezesha halmashauri mbalimbali nchini kujenga barabara zenye urefu wa kilomita 490 kwa kiwango cha lami kupita Mfuko wa Barabara na mradi uliogharamiwa na Jumuiya ya Ulaya (EU) na Mradi wa Kuondoa Vikwazo vya Upitikaji (IRAT) ambazo zimerahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo na kupunguza usumbufu utokanao na changamoto za usafiri kwa wananchi;
- (v) Kuimarisha fursa za ufikishaji mazao sokoni kwa kuimarisha barabara za vijijini kwa kiwango cha changarawe zenye urefu wa kilomita 1,115 katika halmashauri mbalimbali nchini;
- (vi) Kupunguza gharama za ujenzi wa barabara katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Mwanza na Kigoma kwa kutumia malighafi za maeneo husika (mfano mawe) katika ujenzi wa barabara na madaraja; na

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA



- (vii) Kuanza utoaji wa huduma za Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) kwa kutumia miundombinu ya awamu ya kwanza ya BRT inayohusisha barabara za Kimara, Kivukoni, Magomeni, Morocco na Fire - Kariakoo zenye urefu wa jumla ya kilomita 20.29.

**(b) Ujenzi wa Madaraja na Makalvati**

- (i) Kuimarisha viungo vya barabara kwa kujenga madaraja makubwa 32, madaraja madogo 13 na vivuko 6 katika halmashauri mbalimbali nchini ili kurahisisha usafiri na usafirishaji wa mizigo ya wananchi;
- (ii) Kuzuia uharibifu wa barabara kwa kujenga makalvati 167 na mifereji yenye urefu wa kilomita 87.4 katika majiji 5 na Miji 3 ya kimkakati pamoja na miji 18 nchi;
- (iii) Kuimarisha utaalum wa upimaji na tathmini ya vifaa vya ujenzi ili kuwezesha kuwa na ujenzi wenye kuzingatia viwango stahiki kwa kujenga maabara tatu katika manispaa za Kinondoni, Temeke na Ilala;
- (iv) Kutoa mchango wa sekta ya barabara katika kuwezesha upatikanaji wa huduma za jamii kwa ujenzi wa vituo tisa vya maji safi na ujenzi wa zahanati ya Buza; na
- (v) Kuimarisha usalama wa watumiaji wa barabara kwa kuweka taa za umeme wa jua katika majiji sita ya Dodoma, Mbeya, Mwanza, Tanga, Dar es Salaam na Arusha, manispaa tatu za Kigoma/Ujiji, Ilemela na Mtwara na halmashauri 18 za Morogoro, Tabora, Moshi, Sumbawanga, Shinyanga, Songea, Singida, Musoma, Iringa, Bukoba, Lindi na Mpanda na halmashauri za miji ya Babati, Kibaha, Korogwe, Njombe, Geita na Bariadi.

57.

**Kwa kutambua umuhimu wa kuendelea kuboresha miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi katika kuwezesha shughuli za kiuchumi na kijamii mijini na Vijijini, Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kitahakikisha miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi inaboreshwa kwa lengo la kufungua fursa za kiuchumi na kijamii katika maeneo ya mijini na vijijini. Ili kufikia lengo hilo, Chama kitaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kuimarisha Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) kwa kuongeza bajeti ili kukidhi mahitaji ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za vijijini na mijini;
- (b) Kuongeza mtandao wa barabara unaohudumiwa na TARURA kutoka kilometa 108,946 za sasa hadi kufikia kilometa 143,881 katika



Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwezesha maeneo mengi ya vijijini kufikika kwa urahisi;

- (c) Kuongeza kiwango cha barabara za changarawe kutoka kilometa 24,493; hadi kilometa 35,000 ifikapo mwaka 2025;
- (d) Kuongeza urefu wa barabara za mijini na vijijini zilizojengwa kwa kiwango cha barabara za lami kutoka kilometa 2,025 hadi kilometa 3,100 ifikapo mwaka 2025;
- (e) Kuimarisha utoaji wa huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Kwanza katika Jiji la Dar es Salaam;
- (f) Kuanza utoaji wa huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Jiji la Dar es Salaam Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne katika maeneo yafuatayo:-
- (i) Barabara za Kilwa (Mbagala Terminal - Kariakoo - Terminal), Gerezani (Mtaa wa Bandari - Mtaa wa Sokoni), Chang'ombe/Kawawa (Mgulani JKT - Magomeni);
- (ii) Barabara za Nyerere (Gongo la Mboto - Posta ya Zamani kupitia Mitaa ya Nkrumah, Bibi Titi, Maktaba na Azikiwe, Uhuru (Buguruni - Kariakoo Terminal kupitia Mtaa wa Shaurimoyo na Lindi, Shaurimoyo kuanzia Nyerere - Lindi; na
- (iii) Barabara za Ali Hassan Mwinyi/Bagamoyo - Tegeta Nyuki, Sam Nujoma (Mwenge – Ubungo).
- (g) Kuweka utaratibu utakaozitaka halmashauri kutenga fedha kutoka katika mapato ya ndani kwa ajili ya kazi za ujenzi wa miundombinu ya barabara za vijijini na mijini;
- (h) Kufanya tafiti za matumizi za teknolojia sahihi katika ujenzi wa barabara za mijini na vijijini ili kujenga barabara kwa teknolojia sahihi na gharama nafuu; na
- (i) Kutumia vikundi vya jamii katika matengenezo ya barabara na madaraja ili kutoa ajira kwa wananchi, kuongeza umiliki wa miradi na kupunguza gharama.
- (j) **Kuimarisha Vivuko Nchini**
- (i) Kukamilisha panunuzi/ujenzi wa kivuko cha Rugezi – Kisorya (Mwanza) pamoja na kuanza ujenzi wa vivuko vipya nane ambavyo ni:
- Ijinga – Kahangala (Mwanza)
  - Musoma – Kinesi (Mara)
  - Nyamisati – Mafia (Pwani) kivuko cha nyongeza
  - Msangamkuu – Msemo (Mtwara)



- Nyakalilo – Kome (Mwanza)
  - Bwiro – Bukondo (Ukerewe)
  - Irugwa - Murutanga (Ukerewe)
  - Kakuru – Ghana (Ukerewe).
- (ii) Ununuzi wa boti kati ya Ilugwa – Ukara (Mwanza);
- (iii) Kukamilisha ujenzi wa maegesho ya Kikove (Mlimba – Malinyi); na
- (iv) Kuendelea na upanuzi wa maegesho ya Magogoni – Kigamboni (Upande wa Kigamboni), ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi na uzio) kwa ajili ya vivuko 10 kikiwemo kivuko cha Msangamkuu – Msemu, kutekeleza mradi wa ujenzi wa maegesho ya Rugezi – Kisorya (Mwanza), Kome na Nyakalilo (Mwanza), Utete (Pwani), Chato - Nkome (Geita), Iramba na Majita (Mwanza), Ilugwa (Ukerewe – Mwanza), Ijinga na Kahangala (Magu - Mwanza) na Kyanyabasa – Buganguzi (Kagera).

### Uchukuzi

58.

Chama Cha Mapinduzi kinatambua kuwa uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi ni hitaji la msingi katika kuchochea na kuwezesha maendeleo ya sekta za kiuchumi na kijamii. Kwa kutambua umuhimu huo, Chama katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020) kiliielekeza Serikali kuimarisha na kuboresha miundombinu na huduma za reli, bandari, viwanja vya ndege; kununua ndege, meli za abiria na mizigo; na kuboresha utabiri wa hali ya hewa. Lengo ni kuchochea ukuaji wa uchumi na kurahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo. Aidha, katika uendelezaji wa miundombinu, Sekta ya Uchukuzi iliendelea kutoa kipaumbele katika kuwezesha maendeleo ya viwanda nchini ili kuiwezesha Tanzania kufikia uchumi wa kati kwa kushirikisha wadau na sekta binafsi. Katika kipindi hicho, mikakati mbalimbali ilitekelezwa na kuleta mafanikio makubwa kama ifuatavyo:-

- (a) Kuboresha na kuimarisha utendaji wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Shirika la Ndege la Taifa (ATC) ili yaweze kutoa mchango stahiki katika usafiri na usafirishaji nchini na nchi jirani;
- (b) Kuanzisha Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) kwa ajili ya kutoa huduma za uwakala wa meli na kusimamia ulinzi na usalama wa usafiri na mazingira wa majini;
- (c) Maboresho ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na Huduma za Bandari nchini:-

*Miradi iliyokamilika katika kipindi cha mwaka 2015 - 2020*

- (i) Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam;
- Ujenzi wa Jengolaghorofa 35 kwa ajili ya kuwaweka pamoja wadau wanaotoa huduma za kibandari katika bandari ya Dar es Salaam (Bandari Tower);





- Uboreshaji wa gati namba 1 - 3;
  - Ujenzi wa gati la kushusha magari (RoRo);
  - Ujenzi wa Bandari ya Nyamisati ili kuboresha usafirishaji wa kwenda na kutoka Mafia;
  - Ukarabati wa Barabara za kuingia bandarini kupitia Geti Namba 4; 5 na 8;
  - Ukarabati wa Gati la kuhudumia mizigo ya Mwambao;
  - Ukarabati wa Mnara wa Kuongozea ndege (control tower);
  - Uwekaji wa mfumo wa ulinzi wa kisasa (intergrated port security) na ufungaji wa mashine za kukagua mizigo (scanners); na
  - Ununuzi wa Mitambo ya kuhudumia mizigo bandarini.
- (ii) Uboreshaji wa Bandari ya Tanga
- Ujenzi wa barabara ya kuingilia geti namba 2;
  - Ujenzi wa gati la Pangani;
  - Ukarabati wa maghala na gati namba 1 na 2; na
  - Ununuzi wa mitambo.
- (iii) Uboreshaji wa Bandari ya Mtwara
- Ujenzi wa uzio bandari ya Mtwara;
  - Ujenzi wa sakafu ngumu katika eneo la mita za mraba 600;
  - Ukarabati wa ghala la mizigo katika bandari ya Kilwa; na
  - Ujenzi wa gati la Lindi.
- (iv) Bandari za Ziwa Victoria
- Ujenzi wa gati la Lushamba;
  - Ujenzi wa gati la Ntama;
  - Ujenzi wa mitaro - Bandari ya Mwanza Kusini;
  - Ujenzi wa gati la majahazi Mwigobero;
  - Ujenzi wa gati la Nyamirembe awamu ya Kwanza;
  - Ujenzi wa gati la Magarini;
  - Ukarabati wa majengo na ofisi za bandari za ziwa Victoria; na
  - Ununuzi wa vifaa vya kuhudumia mizigo na meli.
- (v) Bandari za ziwa Tanganyika
- Ujenzi wa gati la Kagunga; na
  - Ujenzi wa barabara ya kuingia bandari ya Kipili.
- (vi) Bandari za ziwa Nyasa
- Ujenzi wa tishari 2 (self-propelled cargo barges) zenye uwezo wa kubeba tani za shehena 1,000 kila moja;
  - Ujenzi wa meli ya abiria 350 na tani 200 za mizigo; na
  - Ujenzi wa sakafu ngumu bandari ya Kiwira na Itungi.



*Miradi ya Bandari inayoendelea:*

- (i) Bandari ya Dar es Salaam
  - Uboreshaji wa gati namba 4 – 7;
  - Uboreshaji wa yadi ya shehena ya magari;
  - Ujenzi wa bandari kavu eneo la Kwala-Ruvu (Vigwaza); na
  - Ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mizigo.
- (ii) Bandari ya Tanga
  - Kupanua na kuchimba lango la kuingilia na eneo la kugeuzia meli (entrance channel and turning basin);
  - Ukarabati wa Zahanati;
  - Ujenzi wa nyumba moja ya wafanyakazi kwenye bandari Tanga; na
  - Ujenzi wa uzio katika eneo la Chongoleani.
- (iii) Bandari ya Mtwara:
  - Ujenzi wa awamu ya kwanza ya gati la mita 300 la kuhudumia; Shehena mchanganyiko (multi-purpose terminal);
  - Ujenzi wa kituo cha mafuta;
  - Ukarabati wa gati la Kilwa; na
  - Ujenzi kinu cha kuhifadhia korosho bandarini.
- (iv) Bandari za ziwa Victoria
  - Ujenzi wa ghala la mizigo, sehemu ya abiria na majengo mengine katika bandari ya Kyamkwikwi na Mwigobero;
  - Ujenzi wa bandari ya Kasenda iliyopo kijiji cha Mganza wilayani Chato;
  - Ujenzi wa nyumba moja ya wafanyakazi katika bandari Mwanza; na
  - Kuboresha gati la Chato.
- (v) Bandari za Ziwa Tanganyika
  - Ujenzi wa bandari ya Karema;
  - Ujenzi wa barabara - bandari ya Kagunga;
  - Ujenzi wa gati za Kibirizi, Ujiji na Ofisi ya Mkuu wa Bandari-Kigoma;
  - Uboreshaji na upanuzi wa bandari ya Kasanga;
  - Ujenzi wa miundombinu na gati la bandari ya Kabwe; na
  - Ujenzi wa miundombinu na gati la bandari ya Lagosa.
- (vi) Bandari za ziwa Nyasa
  - Ujenzi wa nyumba ya meneja wa bandari;
  - Ujenzi wa gati la Ndumbi; na
  - Ujenzi wa uzio wa bandari ya Itungi.



- (d) Huduma za Usafiri katika Maziwa na Bahari chini ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)
- (i) Miradi iliyokamilika katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020
- Ukarabati wa meli za MV. Clarias na ML. Wimbi katika Ziwa Victoria, MT. Sangara katika Ziwa Tanganyika;
  - Ukarabati wa meli za MV. Victoria na MV. Butiama;
  - Mradi wa Ujenzi wa Chelezo cha kujengea na kukarabati meli katika Bandari ya Mwanza.
- (ii) Miradi inayoendelea kwa sasa
- Mradi wa Ujenzi wa meli mpya MV. Mwanza Hapa Kazi tu katika Ziwa Victoria yenye Uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo.
- (e) Miundombinu na Huduma za Reli ya Kati
- (i) Miradi iliyokamilika katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020
- Ununuzi wa vichwa 11 vipya vya treni (aina ya 90xx);
  - Ukarabati wa mabehewa 347 ya mizigo na mabehewa 20 ya abiria;
  - Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa reli ya kisasa (*Standard Gauge Railway – SGR*) kutoka Mtwara hadi Mbambabay (km 1,000);
  - Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa SGR kutoka Tanga – Arusha hadi Musoma (km 1,108);
  - Usanifu wa kina wa ujenzi wa reli ya SGR kutoka Kaliua - Mpanda na Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa SGR kutoka Mpanda hadi Karema (km 360);
  - Usanifu wa awali wa SGR kutoka Tabora hadi Kigoma (km 411);
  - Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa SGR kutoka Uvinza hadi Musongati (km 156);
  - Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa SGR kutoka Isaka hadi Kigali (km 356);
  - Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa reli ya mjini Dar es Salaam kwa SGR;
  - Ukarabati wa reli ya Tanga hadi Moshi (km 359) na kurejesha huduma ya kati ya Dar es Salaam – Tanga na Tanga – Moshi – Arusha;
  - Kurejesha huduma ya kusafirisha shehena za mizigo kwa njia ya reli kutoka bandari ya Dar es Salaam kwenda Uganda;
  - Kukamilika kwa ujenzi wa SGR kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kwa asilimia 72.3;
  - Kukamilika kwa ujenzi wa SGR kutoka Morogoro hadi Makutupora kwa asilimia 30;
  - Ukarabati wa miundombinu ya reli iliyopo kutoka



Dar es Salaam-Kilosa (km 283) umekamilika kwa asilimia 58.86 na sehemu ya Kilosa-Isaka (km 687) umekamilika kwa asilimia 61.06.

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA

- (ii) Miradi ya reli inayoendelea
- Ujenzi wa SGR kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (Km 300);
  - Ujenzi wa SGR kutoka Morogoro hadi Makutupora (Km 422);
  - Ukarabati wa njia ya Reli ya Kati (*Metre Gauge Railway – MGR*) kutoka Dar es Salaam – Isaka (Km 970) na uboreshaji wa bandari kavu ya Isaka na Yadi ya Mizigo ya Ilala;
  - Ujenzi wa njia ya reli kwenda bandari kavu ya Kwala, Ruvu;
  - Ukarabati wa njia ya MGR kutoka Moshi – Arusha (Km 80) na kurejesha huduma;
  - Ununuzi wa vichwa 3 na mabehewa 44 vya treni;
  - Ukarabati wa vichwa 7 vya kugeuzia treni (*Shunting Engines*);
  - Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli katika Jiji la Dodoma;
  - Maandalizi ya ujenzi wa reli ya Mtwara – Mbambabay na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa Ubia kati ya Sekta Binafsi na Umma (PPP).

(f) Miundombinu na Huduma za Reli ya TAZARA

- (i) Miradi iliyokamilika katika kipindi cha mwaka 2015 – 2020
- Kununua vichwa vipya 4 vya treni ya njia kuu, vichwa vipya 4 vya treni ya sogeza, mabehewa mapya 18 ya abiria, mashine mbili za uokoaji pamoja na mitambo na vifaa vya usalama;
  - Ukarabati wa mabehewa ya mizigo 400;
  - Uboreshaji wa kituo cha reli cha Fuga/Kisaki ili kusafirisha mizigo na mitambo ya ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere na kukarabati nyumba 8 za watumishi, kuchimba kisima cha maji, kukarabati jengo la stesheni na ujenzi wa njia ya reli namba tatu.
- (ii) Miradi inayoendelea sasa
- Ununuzi wa mitambo na vipuri vya injini (Traction Motors 42) kwa ajili ya ukarabati wa injini 7; na
  - Ununuzi wa mitambo ya uzalishaji wa kokoto na mataruma ya zege katika mgodi wa kokoto ulioko Kongolo – Mbeya.



- (g) Udhibiti wa Usafiri wa Anga
- (i) Miradi iliyokamilika katika kipindi cha mwaka 2015 – 2020
- Ununuzi na ufungaji wa Rada 4 za kuongozea ndege za kiraia kwa ajili ya kudhibiti anga lote la Tanzania na zimefungwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA), Mwanza, Kilimanjaro na Songwe;
  - Kuboresha mitambo ya mawasiliano kwa njia ya radio baina ya Waongoza ndege na Marubani (VHF Radios/ Area Cover Relays) iliyoopo Mnyusi, Tanga;
  - Kununua Mtambo (Simulator) wa kufundishia wanafunzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga;
  - Utengenezaji wa mfumo wa ramani za kutua ndege katika viwanja vya Zanzibar na Mwanza; na
  - Kukarabati Mnara wa kuongozea ndege katika kiwanja cha Pemba.
- (ii) Miradi inayoendelea sasa
- Kununua na kisimika vifaa vya mawasiliano ya sauti kati ya Marubani na waongozaji ndege uwanja JNIA;
  - Kununua na kusimika vifaa vya mawasiliano katika jengo jipya la kuongozea ndege kituo cha Mwanza;
  - Ukamilishaji wa ujenzi wa uzio katika eneo la ujenzi wa Chuo cha usafiri wa anga;
  - Kufanya utafiti na hatua za awali za wa ununuzi na usimikaji wa mtambo wa kuongozea ndege kwa njia ya satelaiti upande wa magharibi mwa nchi; na
  - Mradi wa kufunga mfumo wa kuongoza ndege kutua salama (Instrument Landing System) katika Kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume – Zanzibar.
- (h) Viwanja vya Ndege
- (i) Miradi iliyotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2015 – 2020
- Jengo jipya la tatu la abiria (TB III) lenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka, JNIA;
  - Ukarabati Jengo la kuhudumia abiria 1,200,000 kwa mwaka, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kilimanjaro (KIA);
  - Ukarabati na upanuzi wa eneo la kuegesha ndege na njia ya ndege (*taxi way*) katika Kiwanja cha KIA;
  - Ununuzi wa magari mapya matatu ya zimamoto yenye uwezo mkubwa wa kubeba lita za maji 10,000;
  - Kufunga mifumo ya kamera za kufuatilia mienendo ya usalama kwa viwanja vya ndege vya JNIA, Arusha, Mwanza, Dodoma Iringa na Songwe;
  - Uandaaji wa programu za usalama katika viwanja vya ndege vya JNIA, Mwanza, Songwe, Bukoba, Shinyanga,



- Musoma, Tanga, Arusha, Iringa, Dodoma, Songea, Kigoma, Lake Manyara, Mafia na Tabora;
- Kukamilisha utayarishaji wa mpango kabambe wa uendelezaji wa sekta ya usafiri wa anga kwa nchi nzima;
- Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa viwanja 11 vya ndege vya Iringa, Njombe, Songea, Lindi, Kilwa Masoko, Tanga, Moshi, Lake Manyara, Singida, Musoma na Simiyu;
- Kufunga mfumo mpya wa kuhudumia abiria (CUPPS) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere;
- Ukarabati na upanuzi wa jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege Dodoma;
- Ununuzi na ufungaji wa vivuko vipya vitano vya abiria (aerobridges) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (TB II);
- Ununuzi wa mashine 16 za ukaguzi wa abiria na mizigo (X-Ray mashines) kwa Viwanja vya ndege vya JNIA (5), Kigoma(1), Iringa(1), Songea(1), Bukoba(1), Mafia(1), Arusha(1), Mwanza(1), Songwe(1), Mtwara(1), na Dodoma(2) na milango kumi na mbili (12) ya ukaguzi wa abiria kwa viwanja vya ndege vya Mafia(1), Iringa(1), JNIA (5), Arusha(1), Dodoma(1), Kigoma(1), Songea(1) na Kahama (1);
- Ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Mwanza na ujenzi wa jengo la kuongozea ndege na jengo la mizigo;
- Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa Ujenzi wa Kiwanja Kipya cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato.
- Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa viwanja vya ndege vya Moshi, Iringa, Musoma, Lake Manyara, Tanga, Songea, Lindi, Kilwa Masoko, Singida na Kiwanja Kipya cha Ndege cha mkoa wa Simiyu;
- Upanuzi na ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba kwa kiwango cha lami kwenye barabara ya kuruka na kutua ndege; barabara ya kiungo na maegesho ya magari pamoja na Jengo la abiria;
- Ukarabati wa kipande cha meta 250 kwa kiwango cha lami katika Kiwanja cha Ndege Iringa kwa ajili ya kuwezesha safari za ndege za ATCL aina ya Bombardier Q 400;
- Ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma;
- Ununuzi wa gari la zimamoto kwa ajili ya Kiwanja cha Ndege Geita;
- Ufungaji wa mifumo ya kuongozea ndege (AGL) katika viwanja vya Ndege vya Dodoma, Tabora na Mwanza;
- Upembuzi yakinifu wa Jengo la Pili la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere.





- (ii) Miradi inayoendelea sasa
- Ujenzi/ukarabati wa viwanja vya ndege vya Shinyanga na Sumbawanga.
  - Ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Songea na Mtwara;
  - Ununuzi wa magari matatu ya zimamoto katika viwanja vya ndege vya Mwanza na Mtwara;
  - Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Geita;
  - Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha katika maegesho ya ndege na maegesho ya magari;
  - Ujenzi wa barabara mpya ya magari ya kuingia kiwanja cha ndege cha Arusha;
  - Uwekaji wa mifumo wa maegesho ya magari katika viwanja vya Ndege vya JNIA na Arusha;
  - Ukarabati wa maegesho ya magari katika kiwanja cha Ndege JNIA-TBI;
  - Kusimika mifumo ya kamera za kufuatilia mienendo ya kwa viwanja vya ndege vya Mtwara na Lake Manyara;
  - Ununuzi wa mashine nane za ukaguzi wa mizigo (X-Ray Machines) kwa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza (2), Geita (2), Kahama (2), Kilwa Masoko (1), Nachingwea (1).
- (i) Huduma za Usafiri wa Anga
- (i) Miradi iliyokamilika katika kipindi cha mwaka 2015 – 2020
- Ufufuaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania kwa kununua ndege 11 ambapo ndege nane zimewasili na zinaendelea kutoa huduma. Ndege nyingine tatu zitawasili katika mwaka 2020/21;
  - Mafunzo kwa marubani wazawa 63, wahandisi 88 na wahudumu wa ndani ya ndege 125;
  - Kupanua huduma za usafiri wa anga kutoka vituo vinne mwaka 2015 hadi vituo 13 mwaka 2020 vya ndani ya nchi na vituo saba vya nje ya nchi; na
  - Kuongeza umiliki wa soko la ndani la usafiri wa anga kutoka asilimia 2.5 mwaka 2015 hadi asilimia 72 mwaka 2020.
- (ii) Miradi inayoendelea sasa
- Ununuzi wa ndege moja aina ya Dash 8 Q400 inatarajia kuwasili kabla ya Juni, 2020 na ndege nyingine mbili aina ya A220 – 300 zinazotarajiwa kuwasili Juni, 2021;
  - Kufanya matengenezo ya ndege ndogo aina ya Dash 8 Q300;
  - Maandalizi ya safari za Guangzoug (China) na Lububashi, Nairobi, Kigali na Uingereza katika robo ya nne ya Mwaka wa Fedha, 2019/2020;
  - Kukarabati karakana za JNIA na KIMAFa ili kufanya matengenezo madogo na makubwa nchini; na



- Kujenga uwezo wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kuanza kutoa Mafunzo ya Wataalam wa Usafiri wa Anga.
- (j) Huduma za Hali ya Hewa
- (i) Miradi iliyokamilika katika kipindi cha mwaka 2015 – 2020:
  - Ununuzi wa Rada tatu za hali ya hewa kwa ajili ya kufungwa Mikoa ya Mtwara, Mbeya na Kigoma; na
  - Ukarabati wa vituo saba vya hali ya hewa vilivyopo Zanzibar, Mtwara, Kilwa Masoko, KIA, JNIA, Handeni na Morogoro.
- (ii) Miradi inayoendelea sasa:
  - Kukamilisha miundombinu ya Rada tatu za hali ya hewa na ufungaji wake katika Mikoa ya Mtwara, Mbeya na Kigoma; na
  - Kununua vifaa vya hali ya hewa.

**59. Katika miaka mitano ijayo, Chama kitaelekeza Serikali kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya kimkakati. Miundombinu hiyo inajumuisha ya reli, viwaja vya ndege na bandari. Pia kuboresha huduma za usafiri wa anga, baharini na kwenye maziwa kwa kununua vyombo vipya vya usafiri na kukarabati vyombo vilivyopo ili kuimarisha huduma. Ili kufikia azma hiyo, katika kipindi hicho miradi itayotekelezwa katika maeneo mbalimbali ni kama ifuatavyo:-**

- (a) Kuboresha na kuimarisha utendaji wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Shirika la Ndege la Taifa (ATC) ili yaweze kutoa mchango stahiki katika usafiri na usafirishaji nchini na nchi jirani. Vilevile, Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) litaimarishwa kwa ajili ya kutoa huduma za uwakala wa meli na kusimamia ulinzi na usalama wa usafiri na mazingira wa majini;
- (b) Maboresho ya Huduma za Bandari
  - (i) Miradi itakayotekelezwa chini ya Bandari ya Dar es Salaam
    - Ujenzi wa matanki ya kuhifadhi Mafuta;
    - Ujenzi wa gati namba 12-15 kwa ajili ya makasha;
    - Usimikaji wa mikanda ya kushusha mzigo wa kichele;
    - Ujenzi wa (*central workshop*);
    - Kujenga ofisi jijini Dodoma;
    - Ujenzi wa gati katika bandari ya Bagamoyo;
    - Kuboresha miundombinu katika Chuo cha Bandari;
    - Kupanua na kuchimba lango la kuingilia na eneo la kugeuzia meli (*entrance channel and turning basin*);
    - Ujenzi wa barabara ya Bandari, Mivinjeni na daraja la Bandari;



- Ujenzi wa bandari kavu ya Ihumwa, Dodoma; na
  - Ununuzi wa mitambo.
- (ii) Bandari ya Tanga
- Ujenzi wa matanki ya kuhifadhia mafuta ghafi;
  - Kuweka sakafu ngumu katika maeneo yaliyobaki;
  - Kununua maeneo karibu na bandari;
  - Awamu ya pili ya uboreshaji wa bandari ya Tanga; na
  - Ununuzi wa mitambo.
- (iii) Bandari ya Mtwara
- Ujenzi wa uzio katika maeneo tofauti ya bandari;
  - Ujenzi wa Barabara inayounganisha gati jipya na maeneo mengine bandarini;
  - Ukarabati wa ghala bandari ya Lindi;
  - Kununua maeneo karibu na bandari kwa ajili ya upanuzi wa bandari ya Mtwara;
  - Ukarabati wa bandari ya majahazi ya Shangani; na
  - Ununuzi wa mitambo.
- (iv) Bandari za Ziwa Victoria
- Ujenzi wa gati la Nyamirembe–Chato awamu ya pili ziwa Victoria;
  - Ukarabati wa barabara za kuingia bandari ya Mwanza South;
  - Ukarabati wa *link span* bandari ya Musoma;
  - Kujenga kizuizi cha upepo cha bandari ya Bukoba; na
  - Ununuzi wa mitambo.
- (v) Bandari za Ziwa Tanganyika
- Kuimarisha bandari ya Kalema;
  - Ujenzi wa bandari kavu ya Katosho;
  - Ujenzi wa gati bandari ya Kirando;
  - Ujenzi wa sakafu ngumu bandari ya Kipili; na
  - Ununuzi wa mitambo.
- (vi) Bandari za Ziwa Nyasa
- Ujenzi wa zahanati katika bandari ya Kyela;
  - Ujenzi wa jengo la abiria eneo la Matema;
  - Ujenzi wa gati na eneo la kushukia abiria bandari ya Ndumbi; na
  - Ununuzi wa mitambo.
- (c) Huduma za Usafiri katika Maziwa na Bahari
- Ujenzi wa meli ya ya kutoa huduma katika Bahari ya Hindi kati ya Mtwara (Tanzania) na Visiwa vya Comoro;
  - Ujenzi wa meli mpya ya kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Tanganyika;



- Ujenzi wa meli mpya ya kubeba mabehewa (wagon ferry) katika Ziwa Victoria;
  - Ujenzi wa meli kubwa ya kutoa huduma katika Ziwa Tanganyika kati ya Kalema (Tanzania) na Karemii (DRC);
  - Ujenzi wa meli ya kubeba mafuta (tanker) katika Ziwa Tanganyika;
  - Kukamilisha ujenzi wa meli mpya MV. Mwanza Hapa Kazi tu katika Ziwa Victoria yenye Uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo;
  - Ujenzi wa boti tano za Uokozi (Ziwa Victoria 2, Tanganyika 2 na Ziwa Nyasa 1);
  - Ukarabati mkubwa wa meli za MV. Umoja, MV. Serengeti, MT. Ukerewe na MT. Nyangumi katika Ziwa Victoria, MV. Liemba, MT. Sangara na Boti ya *Sea Warriors* katika Ziwa Tanganyika.
- (d) Miradi ya Reli
- Ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* kutoka Makutupora – Tabora; (km 294), Tabora – Isaka (km 130), Isaka – Mwanza (km 250);
  - Ujenzi wa reli ya Tabora-Kigoma (km 411);
  - Ujenzi wa reli ya Kaliua- Mpanda – Karema (km 360);
  - Ujenzi wa reli ya Uvinza – Musongati (km 156);
  - Ujenzi wa reli ya Isaka – Kigali (Km 356);
  - Ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha – Musoma (km 1,253);
  - Ujenzi wa reli ya Mtwara - Songea - Mbamba-bay na Matawi; Liganga na Mchuchuma (km 1,000);
  - Ujenzi wa njia za reli za treni ya mjini Dar es Salaam;
  - Ununuzi wa vichwa 39 vya treni vya njia kuu, vichwa 18 vya sogeza, mabehewa 800 ya mizigo na mabehewa 37 ya abiria;
  - Kuunda upya vichwa 31 vya njia kuu, vichwa 20 vya sogeza, kukarabati mabehewa ya mizigo 690 na mabehewa 60 ya abiria; na
  - Kukarabati njia ya reli kati ya Kilosa – Kidatu.
- (e) Kuanza ujenzi wa reli ya jiji la Dodoma
- (f) Miundombinu ya Reli ya TAZARA
- Uboreshaji wa kiwanda cha kokoto – Kongoro, Mbeya;
  - Ukarabati wa injini saba za njia kuu;
  - Ukarabati wa mabehewa 21 ya treni ya abiria ya Udzungwa na treni ya mjini.
- (g) Usafiri wa Anga
- Ununuzi wa mfumo wa usambazaji taarifa za ndege kimtandao (AXIM - Aeronautical Information Exchange Modal);
  - Kujenga uzio katika wa mtambo wa kuongozea ndege unaotumia mawasiliano ya redio (Non-Directional Beacon – NDB) katika kituo cha Songwe;



- Kuandaa Mfumo wa kubaini njia za ndege kwa ajili ya kuingia na kutoka viwanjani (DAR-FIR Airspace Restructuring) kwa viwanja vya Songwe, Tabora, Iringa, Chato, Dodoma, Zanzibar, Kigoma, Bukoba na Mpanda.

(h) Viwanja vya Ndege

- Upanuzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Kigoma, Shinyanga, Sumbawanga, Tabora, Mwanza na Songwe;
- Ujenzi kwa kiwango cha lami wa Viwanja vya Ndege vya Iringa, Moshi, Lake Manyara, Tanga, Musoma, Lindi, Kilwamasoko, Njombe, Singida na Simiyu;
- Ujenzi wa uzio wa usalama kwa viwanja vya ndege vya Mwanza, Dodoma, Arusha, Geita, Shinyanga, Sumbawanga, Moshi, Iringa, Tanga, Msalato, Lake Manyara, na Tabora;
- Kuweka Mifumo ya Kuhudumia Abiria (CUPPS) katika viwanja vya ndege vya Mwanza, Bukoba, Arusha, Songwe na Dodoma;
- Kuimarisha ulinzi na usalama wa viwanja vya ndege kwa kununua mashine za ukaguzi wa mizigo na abiria katika viwanja vya ndege vya Tabora (1), Kigoma (1), Shinyanga (1) Sumbawanga (1), Tanga (1), Lake Manyara (1), Iringa (1), na Msalato (6);
- Kuweka mifumo ya taa za kuongozea ndege kwa viwanja vya ndege vya Iringa, Bukoba, Msalato, Tanga, Lake Manyara na Kigoma ili kuviwezesha kutumika saa 24 kwa siku;
- Ukarabati wa majengo ya abiria (I na II) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere;
- Ujenzi wa jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza (Awamu ya Pili);
- Ujenzi wa jengo la abiria pamoja na miundombinu yake katika Kiwanja cha Ndege cha Arusha; na
- Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika viwanja vya Manyara na Morogoro.

(i) Huduma za Usafiri wa Anga

- Kununua ndege ya mizigo kwa kuzingatia mahitaji ya kibiashara na ukuaji wa shughuli za uchumi;
- Kununua ndege kubwa mbili za masafa marefu ili kuongeza miruko ya masafa marefu;
- Kuongeza ndege mbili za masafa ya kati ili kuongeza fursa za kibiashara;
- Kujenga uwezo ATCL kuhudumia ndege, abiria na mizigo uwanjani;
- Kuendelea kujenga uwezo wa ATCL katika karakana, rasilimali watu, vifaa na mitambo katika kufanya matengenezo madogo na makubwa ya ndege;
- Kuboresha mazingira ya usafirishaji wa bidhaa zinazoharibika haraka (perishable goods); na
- Kukiwezesha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (National Institute of Transport – NIT) kutoa elimu kwa wataalam wa kada ya usafiri wa anga.



- (j) Hali ya Hewa
- Kununua rada mbili za hali ya hewa zitakazofungwa katika Mikoa ya Dodoma na Kilimanjaro;
  - Kununua vifaa vya kisasa vya hali ya hewa vikiwemo vitambuzi vya radi (Lighting Detectors);
  - Ujenzi wa kituo kikuu cha utabiri wa hali ya hewa; na
  - Mradi wa kuboresha miundombinu ya Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa.

### **Mawasiliano**

Chama Cha Mapinduzi kinatambua umuhimu wa sekta ya mawasiliano katika kuwezesha sekta nyingine kukua na kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya nchi. Katika miaka mitano iliyopita (2015 – 2020), Serikali iliendelea kuboresha sekta hiyo kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kuweka mazingira bora ya ushindani kwenye sekta ya mawasiliano ili wananchi wengi waweze kumudu gharama za mawasiliano. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali katika kipindi hicho ilipata mafanikio yafuatayo:-

- (a) Kufufua Shirika la Simu la Taifa (TTCL) kwa kuliwezesha kimtaji na kimenejimenti;
- (b) Kuimarisha mawasiliano kwa kuwezesha huduma za intaneti kupatikana katika ofisi za halmashauri 119, vituo vya posta 71, vituo vya polisi 129, hospitali za wilaya 95, na Mahakama 27 kwa kufikisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika maeneo hayo ambapo huduma ya intaneti ilitolewa bure kwa miaka mitatu katika shule 435 za sekondari;
- (c) Kuimarisha huduma za mawasiliano katika halmashauri za wilaya kwa kuziunganisha halmashauri hizo na Mkongo wa Taifa. Halmashauri zilizounganishwa na mawasiliano hayo ni pamoja na Mbulu, Monduli, Sikonge, Kaliua, Hanang, Wanging'ombe, Kiteto, Uvinza, Simanjiro, Urambo, Ngorongoro, Bukombe, Mbogwe, Mlele, Buhigwe, Siha, Mbeya, Morogoro, Buchosa, Nyang'wale, Kalambo na Nsimbo;
- (d) Kuwezesha huduma za mawasiliano kupatikana kwa asilimia 94 nchini, kutokana na Serikali kutoa ruzuku kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote katika kata 703 zenye vijiji 2,501 vilivyokuwa na changamoto ya kufikiwa na huduma ya mawasiliano;
- (e) Kupunguza gharama na kuimarisha ubora wa huduma za mawasiliano kwa wananchi kwa kujenga mkongo wa Taifa wa mawasiliano wenye urefu kilomita 7,560. Mkongo huo umepunguza gharama za uwekezaji wa miundombinu kwa watoa huduma za mawasiliano. Vilevile, mkongo huo umeunganishwa na mikongo ya mataifa jirani ya Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia na Malawi na hivyo kuongeza mapato kwa Taifa;





- (f) Kuwekwa kwa mazingira bora ya ushindani ili wananchi waweze kumudu gharama za mawasiliano na kupata huduma zenye viwango bora kwa kusimamia na kuweka bei elekezi ya huduma za mawasiliano ya mwingiliano (*Interconnection*) ambayo inatakiwa izingatiwe na watoa huduma wote wa mawasiliano kati ya mtandao mmoja na mwingine;
- (g) Kuimarika kwa usalama wa matumizi ya *data* na kuendelea kupungua kwa gharama za matumizi ya mtandao kwa kujenga kituo cha *data* cha Taifa chenye viwango vya juu;
- (h) Kuimarisha ubora, upatikanaji na usalama wa huduma za mawasiliano kwa kuongeza umiliki wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) kufikia asilimia 100. Hatua hiyo, umechangia kuongeza mapato na kutoa gawio kwa Serikali;
- (i) Kuwekwa kwa mazingira wezeshi ya ushindani kwa kampuni binafsi kutoa huduma bora kwa gharama nafuu, ikiwemo gharama za *data* ambazo ni ndogo nchini ikilinganishwa na gharama zinazotowwa katika nchi nyingine za Kusini mwa Afrika;
- (j) Kudhibitiwa kwa uhalifu wa kimtandao kwa kutekeleza Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 na Mkakati wake pamoja na Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015;
- (k) Kuimarika kwa matumizi ya TEHAMA katika jamii ambapo matumizi ya intaneti yameongezeka kutoka watumiaji milioni 9.0 sawa na asilimia 4.8 mwaka 2015 hadi watumiaji milioni 23.1 takribani asilimia 23.1 mwaka 2020;
- (l) Kurahisisha huduma mbalimbali kwa wananchi zikiwemo za malipo na kuboresha usalama wa miamala ya fedha kutokana na kuunganishwa kwa mifumo ya malipo kwa njia ya kielektroniki; na
- (m) Kuimarisha viwango vya ubora wa mawasiliano na kuboresha uhabiti wa matumizi ya mawasiliano kwa kupunguza vitendo vya ulaghai kupitia mawasiliano na kuongeza chanzo kipya cha mapato kwa kuweka Mfumo wa Kuratibu na Kusimamia Mawasiliano (TTMS).

**61. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, sekta ya mawasiliano itajikita zaidi katika kuimarisha ubora wa mawasiliano nchini na kuhakikisha wigo wa mawasiliano unaongezeka na kuwafikia wananchi wote. Katika kufikia lengo hilo, Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha Serikali yake inatekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuimarisha uwezo wa kimenejimenti na kimtaji wa kampuni ya TTCL ili iweze kupanua shughuli nchini na kuwa shindani iweze kuongoza soko la mawasiliano nchini;
- (b) Kuongeza faragha na usiri wa taarifa za wananchi katika mawasiliano kwa kukamilisha kutunga sheria ya kuimarisha ulinzi wa taarifa na takwimu;



- (c) Kuimarisha mfumo wa TEHAMA wa kudhibiti usalama na mapato katika mawasiliano;
- (d) Kuongeza mchango wa sekta ya mawasiliano kwenye Pato la Taifa kwa kuongeza matumizi ya TEHAMA;
- (e) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuweka mazingira bora ya ushindani na udhibiti katika sekta ya mawasiliano ili wananchi wengi zaidi wamudu gharama za mawasiliano;
- (f) Kuongeza wigo na matumizi ya mawasiliano ya kasi (*broadband*) kutoka asilimia 45 mwaka 2020 hadi asilimia 80 mwaka 2025;
- (g) Kuongeza watumiaji wa intaneti kutoka asilimia 43 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 80 mwaka 2025;
- (h) Kuanzisha huduma za mawasiliano za intaneti ya kasi (*broadband*) katika maeneo ya umma (*public places*) ikiwamo maeneo ya hospitali, taasisi za elimu na vituo vya usafiri hadi kufikia asilimia 40 mwaka 2025;
- (i) Kuunganisha taasisi za Serikali na miundombinu ya mtandao wa kasi (*broadband infrastructure*) kufikia asilimia 70;
- (j) Kuboresha huduma za mawasiliano ya simu za viganjani ili kupatikana maeneo yote;
- (k) Kuweka mazingira wezeshi ya kuanzisha viwanda vya uzalishaji wa vifaa vya TEHAMA vyenye uwezo wa kutoa ajira kwa wananchi walio wengi na kuzalisha vifaa vinavyotumika ndani na nje ya nchi, na kujenga kiwanda cha kuchakata taka za kielektoniki ili kudhibiti uharibifu wa mazingira;
- (l) Kuhamasisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kutoa huduma, biashara na uzalishaji ili kuongeza uwazi, ufanisi, na kuboresha maisha ya wananchi kichumii na kijamii;
- (m) Kuhakikisha anuani za makazi zinawekwa nchini ili kurahisisha upatikanaji, utoaji na ufikishishaji wa huduma mbalimbali;
- (n) Kuimarisha mtambo wa kusimamia mawasiliano wa TTMS ili kuhakikisha upatikanaji wa mapato stahiki kwa malipo ya kodi, kuboresha mawasiliano na udhibiti wa matumizi ya mawasiliano; na
- (o) Kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa maudhui stahiki kupitia mitandao yanayokidhi mahitaji ya wananchi kiutamaduni, kijamii na kuwezesha kujiendeleza kiuchumi.



## 62. Nishati

Chama Cha Mapinduzi kinatambua suala la nishati kuwa ni la kimkakati na muhimu kwa maendeleo ya nchi. Ni kwa kutambua hili sekta ya nishati imekuwa moja ya vipaumbele vya sera za CCM. Katika miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), CCM ilielekeza Serikali kuchukua hatua madhubuti katika kuendelea kuimarisha sekta ya nishati, ikiwemo kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali na kuimarisha huduma ya umeme kwa wananchi. Mafanikio makubwa yamepatikana katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, yakiwemo:-

### **Umeme**

- (a) Kuongeza uwezo wa kuzalisha umeme nchini, kutoka megawati (MW) 1,308 mwaka 2015 hadi MW 1,602.32 mwaka 2020. Ongezeko hili limefanya nchi kujitosheleza kwa mahitaji ya umeme na kuzalisha umeme wa zaida kwa MW 445, ukilinganisha na mahitaji ya sasa ya MW 1,120.12;
- (b) Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa umeme kwa ujumla (*overall electricity access level*) Tanzania Bara kutoka asilimia 36 mwaka 2015 na kufikia asilimia 70.3 mwaka 2020. Mafanikio haya yamepatikana kwa kutekeleza na kukamilisha miradi ifuatayo:-
  - (i) Ujenzi wa mradi wa Kinyerezi I (MW 150) ambapo mitambo yote imewashwa na umeme kuunganishwa katika gridi ya Taifa;
  - (ii) Ujenzi wa mradi wa Kinyerezi II (MW 240) ambapo mitambo yote sita (6) yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 248 imewashwa na kuingizwa kwenye gridi ya Taifa;
  - (iii) Kuongezeka kwa mtandao wa njia za kusafirisha umeme kutoka kilomita 4,796.17 mwaka 2015 hadi kufikia kilomita 6,142.27 mwaka 2020 kutokana na kukamilika kwa miradi ya:
    - Njia ya kusafirisha umeme wa msongo mkubwa wa kV 400 (*Backbone - Phase I*) yenye umbali wa kilomita 670 kutoka Iringa kupitia Dodoma - Singida hadi Shinyanga;
    - Kusafirishia umeme wa msongo kV 220 kutoka Makambako hadi Songea ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vituo vitatu vya kupozea umeme vya Makambako, Madaba na Songea. Jumla ya vijiji 122 na wateja 16,281 wameunganishiwa umeme; na
    - Kusafirisha umeme wa msongo wa kV 132 kutoka Mtwara hadi Maumbika pamoja na ujenzi wa vituo vya kupozea umeme.



- (c) Kutekelezwa kwa Mpango Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini (REA I, REA II na REA III) ambapo jumla ya vijiji 8,587 kati ya vijiji 12,319 vya Tanzania Bara vimefikiwa na umeme ambayo ni sawa na asilimia 70;
- (d) Kupunguza gharama za kuunganisha umeme vijijini ambapo gharama za kuunganisha umeme vijijini zimepungua kutoka wastani wa shilingi 454,000 hadi shilingi 27,000;
- (e) Kuongezeka kwa kasi ya usambazaji wa umeme vijijini kwa kutumia vifaa vilivyotengenezwa nchini vikiwemo transfoma, nyaya, nguzo na mita;
- (f) Kuimarika kwa Shirika la Umeme la Taifa nchini (TANESCO) kwa kuweza kujiendesha kwa faida na kuanza kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kiasi cha Shilingi bilioni 1.44 kwa mwaka 2019;
- (g) Kusitisha ukodishaji wa mitambo ya dharura ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta mazito yaliyokuwa ya gharama kubwa na hivyo kuwezesha kuokoa takriban shilingi bilioni 138 zilizokuwa zikitumika kununua mafuta kila mwaka;
- (h) Kuunganisha katika Gridi ya Taifa mikoa na maeneo ambayo hayakuwahi kutumia umeme wa gridi ikiwemo Mikoa ya Lindi, Mtwara, Njombe na Ruvuma pamoja na Wilaya za Biharamulo, Ngara na Muleba katika Mkoa wa Kagera;
- (i) Kuanza na kuendelea na ujenzi wa mradi wa Kinyerezi I - *Extension* (MW 185) ambao umekamilika kwa asilimia 84 ikiwa ni pamoja na ujenzi wa misingi ya mitambo, njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 220 kutoka eneo la Kinyerezi I hadi Kinyerezi II na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi I;
- (j) Kuanza na kuendelea na ujenzi wa mradi wa Julius Nyerere Hydro Power Project-JNHPP (MW 2,115) ambao unaendelea kutekelezwa kwa kuanza ujenzi wa bwawa (*main dam*) na njia za kupitisha maji (*tunnels*);
- (k) Kuendelea na ujenzi wa mradi wa Rusumo (MW 80) ambapo uchimbaji wa eneo la kuweka mitambo (*power house*) umekamilika; ujenzi wa nyumba tano za wafanyakazi umekamilika; na kuanza kuchimba handaki la kupitisha maji. Mradi huo unatekelezwa kwa pamoja kati ya nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi kwa uwiano sawa;
- (l) Kuanza na kuendelea na ujenzi mradi wa kusafirisha umeme wa msongo mkubwa wa kV 400 wa Awamu ya Pili (*Backbone - Phase II*) ambao unahusisha upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga vyenye uwezo wa kV 400/220/33;



- (m) Kuanza na kuendelea na ujenzi wa miradi ya kuunganisha Gridi ya Taifa na nchi jirani ikiwemo njia ya kusafirisha umeme kV 400 kutoka Singida - Arusha - Namanga itakayounganisha nchi za Tanzania na Kenya; na njia ya kusafirisha umeme kV 400 kutoka Iringa - Mbeya - Tunduma itakayounganisha nchi ya Tanzania na Zambia;
- (n) Kuanza na kuendelea na ujenzi wa miradi ya njia ya kusafirisha umeme kV 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi, njia ya kusafirisha umeme kV 220 kutoka Geita hadi Nyakanazi na njia ya kusafirisha umeme kV 220 kutoka Bulyanhulu hadi Geita;
- (o) Kuendelea na miradi ya kusambaza umeme vijijini na mijini inayotekelezwa na REA na TANESCO pamoja na kuendelea kuwaunganishia nishati ya umeme wananchi; na
- (p) Kukamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme kV 400 kutoka mradi wa Julius Nyerere HP hadi Chalinze, njia ya kusafirisha umeme kV 400 (North East) kutoka Kinyerezi - Chalinze - Segera - Tanga, na njia ya kusafirisha umeme kV 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma.

#### **Mafuta na Gesi Asilia**

- (a) Kuimarishwa kwa usimamizi wa sekta ya mafuta na gesi na kuwezesha ongezeko la gesi asilia iliyogunduliwa kutoka futi za ujazo trilioni 55.27 mwaka 2015 na kufikia futi za ujazo trilioni 57.54 mwaka 2019;
- (b) Kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi asilia kutoka wastani wa futi za ujazo bilioni 37 kwa mwaka 2015 hadi futi za ujazo bilioni 46 kwa mwaka 2019 katika visima vya Mnazi Bay na Songo Songo;
- (c) Kuongezeka kwa matumizi ya gesi asilia katika uzalishaji viwandani ambako kumepunguza matumizi ya mafuta ya kuzalisha umeme pamoja na gharama za uzalishaji;
- (d) Kuongezeka kwa matumizi ya gesi asilia ambapo wateja wa majumbani waliofikiwa na miundombinu ya usambazaji gesi asilia katika mikoa ya Dar es Salaam na Mtwara wamefikia zaidi ya 1,000 mwaka 2019 kutoka 70 mwaka 2015. Aidha, viwanda 48 vimeunganishwa mwaka 2019 ikilinganishwa na viwanda 42 mwaka 2015 na magari zaidi ya 300 yamefungwa mfumo wa matumizi ya gesi asilia ikilinganishwa na magari 60 mwaka 2015;
- (e) Kuongezeka kwa matumizi ya gesi ya mitungi (LPG) nchini kutoka tani 70,061 mwaka 2015 hadi tani 113,575 mwaka 2019 kulikochangia kupungua kwa matumizi ya mkaa na kuni ambazo ni chanzo cha uharibifu wa mazingira na matatizo ya kiafya kwa watumiaji;
- (f) Kuwekwa kwa mfumo bora wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (*Petroleum Bulk System*) ambao umewezesha: uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta zenye ubora; nchi kuwa na akiba ya mafuta



ya aina zote yanayotosheleza kwa wastani wa zaidi ya siku 35 ilinganishwa na siku 15 zinazotakiwa; na kupunguza gharama na kuongeza ubora wa bidhaa za mafuta nchini;

- (g) Kukamilishwa kwa Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia (*Natural Gas Utilization Master Plan - NGUMP*) 2016 pamoja na Mpango wa Kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia Nchini (*Domestic Natural Gas Promotion Plan - DNGPP*) ambayo inawezesha matumizi endelevu ya gesi asilia;
- (h) Kuongezeka kwa mchango wa gesi asilia katika kuzalisha umeme kutoka asilimia 36 mwaka 2016 hadi asilimia 57 mwaka 2019;
- (i) Kuimarisha udhibiti wa shughuli za mkondo wa juu kwa kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Masuala ya Petroli (*Petroleum Upstream Regulatory Authority - PURA*) ili kukagua mikataba na kuchambua masuala ya kiuchumi katika kuingia mikataba ya utafutaji na ugawanaji mapato yatokanayo na shughuli za mafuta na gesi asilia. Mamlaka hii imeweza kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 10.08 kwa kufanya kaguzi za gharama zilizoripotiwa na kampuni za kimataifa za mafuta;
- (j) Kuboresha na kuimarisha utendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)
- (k) Kuimarishwa kwa upatikanaji wa mafuta nchini na kuimarishwa kwa mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (*bulk procurement system*) kwa kuanzisha Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (*Petroleum Bulk Procurement Agency - PBPA*);
- (l) Kuongezeka kwa uwezo wa nchi kupakua mafuta kutoka tani 165,000 mwaka 2015 hadi tani 255,000 mwaka 2020 kwa kuimarisha bandari za Tanga na Mtwara. Aidha, uwezo wa kuhifadhi mafuta umeimarika kutoka lita milioni 900 mwaka 2015 hadi kufikia lita bilioni 1.3;
- (m) Kupunguza muda wa kushusha mafuta katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara kutoka kati ya siku 30 na 60 hadi kati ya siku 3 na 8;
- (n) Kudhibitiwa kwa vitendo vya uchakachuaiji (uchafuzi) wa mafuta na hivyo kupungua kwa uchakachuaiji kutoka asilimia 10.14 mwaka 2015 hadi asilimia nne mwaka 2020; na
- (o) Kuboresha kanuni za ujenzi wa vituo vya mafuta katika miji midogo na vijijini ili kuongeza upatikanaji wa bidhaa za mafuta kwa wananchi wa vijijini bila kuhatarisha afya, usalama na mazingira. Aidha, vigezo vya utoaji leseni vimerahisishwa na hivyo kuvutia wawekezaji kujenga vituo vyenye ubora katika maeneo mbalimbali ya vijijini.





63. **Katika miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kinakusudia kuimarisha zaidi sekta ya nishati kwa kuhakikisha kuwa nchi inazalisha umeme wa kutosha ili kukidhi mahitaji ya uchumi wa viwanda na soko la nje. Katika kufikia azma hii, CCM itaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-**

**Umeme**

- (a) Kukamilisha ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere (*Julius Nyerere Hydro Power Project-JNHPP*) unaotarajia kuzalisha MW 2,115;
- (b) Kukamilisha usambazaji umeme katika vijiji vyote na maeneo ya pembezoni mwa miji (miji-vijiji - *Peri Urban areas*) ya Tanzania Bara kupitia Mpango wa Umeme Vijijini pamoja na kuandaa na kutekeleza Mpango Kabambe wa Umeme Vijijini (*Rural Energy Master Plan*);
- (c) Kukamilisha ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa Kinyerezi I – Extension (MW 185) na mradi wa umeme wa maji wa Rusumo (MW 80);
- (d) Kukamilisha utekelezaji wa awamu ya pili (*Phase II*) wa mradi wa *Backbone* ambao unahusisha upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga vyenye uwezo wa kV 400/220/33;
- (e) Kukamilisha ujenzi wa miradi ya kuunganisha Gridi ya Taifa na nchi jirani ikiwemo njia ya kusafirisha umeme kV 400 kutoka Singida - Arusha - Namanga itakayounganisha nchi za Tanzania na Kenya; na njia ya kusafirisha umeme kV 400 kutoka Iringa - Mbeya - Tunduma itakayounganisha nchi ya Tanzania na Zambia;
- (f) Kukamilisha ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme kV 400 kutoka Julius Nyerere HP hadi Chalinze, njia ya kusafirisha umeme kV 400 (*North East*) kutoka Kinyerezi - Chalinze - Segera - Tanga, na njia ya kusafirisha umeme kV 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma;
- (g) Kukamilisha ujenzi wa miradi ya njia ya kusafirisha umeme kV 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi, njia ya kusafirisha umeme kV 220 kutoka Geita hadi Nyakanazi na njia ya kusafirisha umeme kV 220 kutoka Bulyanhulu hadi Geita;
- (h) Kuongeza uwezo wa uzalishaji umeme wa kutosha na wa gharama nafuu kwa kutumia vyanzo mbalimbali ikiwemo maji, gesi asilia, makaa ya mawe na nishati jadidifu (jotoardhi, upepo, jua na tungamotaka). Baadhi ya miradi itakayopewa kipaumbele ni pamoja na miradi ya umeme wa maji (Ruhudji MW 358, Rumakali MW 222, Kikonge MW 300, Kakono MW 87 na Malagarasi MW 45) na gesi asilia (Mtware MW 300, Somanga Fungu MW 330, Kinyerezi III MW 600 na Kinyerezi IV MW 300);



- (i) Kuimarisha taratibu na mikataba ya kuuziana umeme na nchi jirani na za kikanda ili kuongeza kiwango cha upatikanaji umeme nchini kunapokuwa na upungufu au kuuza umeme panapokuwa na ziada;
- (j) Kuimarisha Shirika la Umeme nchini (TANESCO) kwa kutumia vyanzo vyenye gharama nafuu katika kuzalisha umeme na kuunganisha mikoa yote katika gridi ya Taifa;
- (k) Kuendeleza juhudi za kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kama chanzo cha nishati kwa kuimarisha na kuhamasisha matumizi ya vyanzo mbadala kwa kushirikisha sekta binafsi wakiwemo wabunifu wadogo katika kubuni na kutekeleza miradi ya nishati;
- (l) Kuendelea kuhamasisha matumizi bora ya nishati ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo na uelewa kwa wananchi na taasisi kuhusu matumizi bora ya nishati ili kuokoa nishati nyingi inayopotea;
- (m) Kuongeza uwezo wa uzalishaji umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya nishati jadidifu (renewable energy) ikiwemo miradi ya umemejua, jotoardhi na upepo MW 1,100; na
- (n) Kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kuendeleza shughuli mbalimbali za umeme na nishati Jadidifu.

#### ***Mafuta na Gesi Asilia***

- (a) Kuboresha na kuimarisha utendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na kuanzisha Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Mafuta (PURA), ili yaweze kutoa mchango stahiki katika kutafuta, kuendeleza na kudhibiti sekta za mafuta na gesi;
- (b) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuvutia wawekezaji katika utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika maeneo ya nchi kavu, mabonde ya ufa, na maeneo ya kina kirefu cha bahari ili kuongeza kiasi cha rasilimali;
- (c) Kutekeleza Mpango wa Matumizi ya Gesi Asilia (NGUMP) kwa kujenga miundombinu na kuhamasisha matumizi ya gesi asilia viwandani, majumbani, kwenye taasisi na kwenye magari ili kupunguza uharibifu wa mazingira;
- (d) Kuimarisha hali ya upatikanaji wa mafuta nchini ikiwemo kuhamasisha wawekezaji wa ndani kujenga vituo vya mafuta katika miji midogo na vijijini ili kuongeza upatikanaji wa bidhaa hiyo;
- (e) Kuendeleza utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati ambayo ipo katika hatua za mwisho za makubaliano ikiwemo mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) na Mradi wa Kusindika Gesi Asilia (LNG) Mkoani Lindi ambayo itaongeza ajira kwa Watanzania na mapato kwa nchi;



- (f) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuhamasisha matumizi ya gesi ya mitungi (LPG) nchini kwa ajili ya kupikia ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa ambayo ina madhara kiafya na kimazingira;
- (g) Kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya ushirikiano na nchi jirani ikiwemo miradi ya kusafirisha mafuta na gesi asilia ili kuongeza ajira, mapato na usalama wa upatikanaji wa mafuta na gesi nchini ili kuimarisha ushirikiano na nchi jirani; na
- (h) Kuendeleza kwa kasi zaidi utekelezaji wa mpango wa kuwa na mindombinu ya mafuta ya akiba na kimkakati (*Strategic Petroleum Reserve - SPR*) ili kuongeza uhakika wa upatikanaji wa mafuta nchini.

### Madini

Sekta ya madini ni sekta muhimu kutokana na kuchangia kwake katika mapato ya Serikali na kutoa ajira kwa Watanzania, hususan katika ngazi ya wananchi wa kawaida. Katika miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ilisimamia mageuzi makubwa na ya kimkakati ikiwemo maboresho ya sheria na mifumo mbalimbali katika kuhakikisha sekta ya madini inaimarika kwa kiasi kikubwa na kuongeza mchango wake katika pato la Taifa. Hii imejidhihirisha kwa kuongezeka kwa umiliki na ushiriki wa wananchi katika uchimbaji na uchakataji ambapo ajira na mauzo nje yameongezeka. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho ni pamoja na:-

- (a) Kuimarisha mifumo ya kisera na kisheria ili kuwezesha wananchi na Taifa kwa ujumla kunufaika na utajiri wa madini na rasilimali zao;
- (b) Kuongezeka kwa mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa kutoka asilimia 3.4 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 5.1 mwaka 2018;
- (c) Kuimarisha mazingira ya uwekezaji, usimamizi na uboreshaji wa mifumo ya ukusanyaji mapato ambapo ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi umeongezeka kutoka shilingi bilioni 168 mwaka 2015 hadi kufikia shilingi bilioni 346 mwaka 2019;
- (d) Kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa kuwatengea na kuwapimia maeneo maalum ya uchimbaji na kuwapatia leseni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa teknolojia rahisi na rafiki katika uchimbaji na uchenjuaji wa madini;
- (e) Kuongeza ufanisi wa sekta ya madini kwa kuanzishwa Tume ya Madini mwaka 2017. Tume hiyo, pamoja na manufaa mengine imesaidia kuweka mifumo mbalimbali ya usimamizi, ukaguzi na udhibiti katika sekta hiyo;
- (f) Kuboreshwa kwa mazingira ya biashara ya madini kwa kuanzishwa kwa masoko 28 na vituo vidogo 25 vya uuzaji madini katika maeneo yenye madini nchini;



- (g) Kuimarisha usimamizi wa makaa ya mawe na madini ya gesi kwa kuzuia uingizaji wa makaa ya mawe kutoka nje. Hatua hiyo imechangia kuongezeka uzalishaji wa madini hayo kwa ajili ya viwanda vya ndani vya saruji na watumiaji wengine;
- (h) Kuboreshwa kwa miundombinu muhimu katika maeneo ya migodi na uchimbaji kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo ujenzi wa ukuta unaozunguka migodi ya Mirerani na kuimarisha udhibiti wa madini ya Tanzanite;
- (i) Kuboresha mfumo wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini kwa kuanzisha *Online Mining Cadastre Transactional Portal (OMCTP)*;
- (j) Kuimarisha udhibiti, usimamizi, utunzaji, usafirishaji na matumizi ya baruti katika shughuli za migodi kwa kuweka mfumo wa utoaji wa vibali ili kuhakikisha watumiaji wa baruti wanatambuliwa pamoja na kutoa elimu kuhusu matumizi bora na salama;
- (k) Kuliimarisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ili liweze kujiendesha kibiashara na kutoa mchango ipasavyo katika Pato la Taifa kwa kufanya yafuatayo:-
- (i) Kuhuisha Hati ya Uanzishwaji wa Shirika mwaka 2015 (*Amendment of Establishment Order*) ili kuendana na majukumu mapya ya Shirika;
  - (ii) Kuwezesha kwa shirika kwa kupatiwa leseni ya uchimbaji wa makaa ya mawe Kabulo huko Songwe, leseni 20 za uchimbaji kokoto katika maeneo ya Ubena Zomozi na Chigongwe-Dodoma, "*Rare Earth Element*" katika eneo la Sengeri-Songwe na *Phospate* katika eneo la Mvomero;
  - (iii) Kuliwezesha shirika kwa kulipatia vitendea kazi vifuatavyo: mashine ya uchorongaji (*RC Drill Rig*) "*software*" za uchimbaji na utafutaji wa madini. Aidha, kampuni tanzu ya Shirika la STAMIGOLD imeimarishwa; na
  - (iv) Kuanza ujenzi wa kiwanda cha kisasa cha usafishaji dhahabu (*refinery*) jijini Mwanza.
- (l) Kuimarishwa huduma zinazotolewa na Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) ikiwa ni taasisi maalum ya Serikali itakayofanya tafiti za kijiosayansi na kutoa mwelekeo wa uwepo wa madini nchini kwa kufanya yafuatayo:-
- (i) Kuboresha ukusanyaji, tathmini, uhifadhi wa kumbukumbu na uhakiki wa uhalisia wa wingi wa mashapo kwa kuanzisha Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania kupitia marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 yaliyofanyika mwaka 2017; na



- (ii) Kuboresha maabara ya GST na kuiwezesha kupata ithibati ya kimataifa ya uchunguzi wa sampuli za dhahabu kwa njia ya tanuru kutoka shirika la *Southern African Development Community Accreditation Services (SADCAS)*.
- (m) Kuimarisha uongezaji thamani madini kwa kutoa jumla ya leseni 221 za uchenjuaji; nne za uyeyushaji (*Smelting*) na nne za usafishaji (*Refining*) madini. Pia kuandaa na kuchapisha Mwongozo wa Uhakiki wa Uongezaji Thamani Madini au Miamba (*Value Addition*) nchini wa mwaka 2019 (GN No.60);
- (n) Kupunguza uhaba mkubwa wa wataalam wa uongezaji thamani nchini kwa kuzalisha wataalam wenye weledi katika fani za utambuaji wa madini ya vito (*gemology*), ukataji na ung'arishaji (*lapidary*) wa madini ya vito na utengenezaji wa bidhaa za usonara (*Jewellery making and Manufacturing*) katika ngazi za Astashahada na Stashahada katika Kituo cha TGC;
- (o) Kutekeleza mikakati mbalimbali ya kudhibiti utoro shaji wa madini kwa:-
  - (i) Kufuta baadhi ya kodi zenye kero katika biashara ya madini kwa wachimbaji wadogo zikiwemo kodi za: zuio (*Withholding Tax - 5%*) na kodi ya ongezeko la thamani (*Value Added Tax - 18%*);
  - (ii) Kuanzisha madawati maalum ya ukaguzi wa madini katika viwanja vya ndege, bandarini na mipakani;
  - (iii) Kutoa msamaha wa ushuru wa forodha kwa vifaa vya ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito ili kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; na
  - (iv) Kuhuisha kanuni za kusimamia eneo la Mererani (*The Mining Mererani Controlled Area (2019)*) na shughuli zote zinazoendelea kwenye migodi hiyo.
- (p) Kuongeza uzalishaji wa madini kwa kutenga maeneo ya uchimbaji madini kwa kufanya yafuatayo:-
  - (i) Kutenga maeneo 11 yenye jumla ya ukubwa wa hekta 38,567 kwa ajili ya wachimbaji madini wadogo;
  - (ii) Kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa njia mbalimbali ikiwemo mafunzo, teknolojia na maarifa ya kisasa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uchimbaji. Wachimbaji wadogo wapatao 10,338 walinufaika na mafunzo hayo; na



- (iii) Kujenga vituo vya mfano vya ujenzi wa migodi na uchenjuaji madini (*Demonstration Centres*) vya Lwamgasa-Geita, Kantente-Bukombe, Itumbi-Chunya; na vituo vya umahiri (*Centres of Excellence*) vya Mpanda, Songea, Chunya, Handeni, Bariadi, Bukoba na Musoma kwa ajili ya kuwapatia mafunzo wachimbaji wadogo.
- (q) Kuimarisha ukaguzi wa migodi katika masuala ya usalama, utunzaji wa mazingira na afya ambapo migodi 2,634, leseni 98 za utafutaji na mitambo 798 ya uchenjuaji madini pamoja na mabwawa ya kuhifadha takasumu (*Tailings Storage Facility*) vilikaguliwa. Aidha, migodi 11 imewasilisha mipango yao ya ufungaji migodi;
- (r) Kuanzisha kituo cha pamoja cha kutolea huduma (*one stop centre*) ndani ya ukuta wa Mirerani;
- (s) Tanzania kufanikiwa kukidhi matakwa na vigezo vya utoaji wa cheti cha uhalisia wa madini (*Certificate of Origin*) kinachotambuliwa kimataifa kupitia *International Conference on Great Lakes Region (ICGLR)*;
- (t) Kuboreshwa kwa usimamizi, udhibiti na umiliki wa rasilimali za madini ili ziweze kunufaisha mwananchi kwa ujumla kwa kutunga sheria ya kulinda maliasili na rasilimali za Taifa “The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017”; na
- (u) Kuongezeka kwa uwazi na uwajibikaji katika biashara ya madini na gesi kwa kutoa ripoti za uwazi na uwajibikaji (*transparency and accountability*) kwa makampuni ya madini na gesi kwenye sekta ya uziduaji (*Extractive Sector*) kwa miaka ya 2015/16 na 2016/17 kupitia *TEITI*.

65. **Katika miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuisimamia serikali kuhakikisha mapinduzi makubwa yaliyofanyika katika sekta ya madini yanaendelezwa, hususan katika kuwawezesha wananchi kuwa sehemu ya umiliki wa rasilimali hiyo. Aidha, CCM itahakikisha sekta ya madini inachangia zaidi katika Pato la Taifa na kupunguza umasikini nchini. Ili kufikia malengo hayo, Serikali itakayoundwa na Chama Cha Mapinduzi itatekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuimarisha udhibiti na usimamizi wa uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini ili uweze kufaidisha Taifa na wawekezaji kwa usawa, pia kuweka mazingira yatakayohamasisha uwekezaji katika sekta ya madini bila ya kuathiri ustawi na matarajio ya nchi kutokana na uwekezaji huo;
- (b) Kubuni na kuimarisha utekelezaji wa mipango ya kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija kwa kuwatengea maeneo au kuwapatia leseni kwenye maeneo ambayo





yana taarifa za msingi za kijiolojia, kutoa huduma za utafiti kwa gharama nafuu, kuwaendeleza kutoka uchimbaji mdogo kwenda wa kati na hatimaye uchimbaji mkubwa, na kuwapa mafunzo yanayohitajika kuhusu uchimbaji na biashara ya madini;

- (c) Kuimarisha Tume ya Madini ili iweze kuendelea kusimamia shughuli za madini, kukusanya takwimu za madini na kufuatilia maduhuli yatokanayo na madini kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali;
- (d) Kuimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa masoko kwenye maeneo mbalimbali kunakofanyika shughuli za madini ndani ya nchi kulingana na uhitaji na pia kuhimiza kuwepo kwa mikakati itakayovutia upatikanaji wa huduma saidizi mbalimbali;
- (e) Kutekeleza mikakati itakayowezesha kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchini;
- (f) Kufungua na kusimamia migodi ya uchimbaji mkubwa na kuweka msisitizo katika uchimbaji wa madini ya kinywe (*graphite*) na madini mengine;
- (g) Kuendeleza mikakati ya kuimarisha soko la Tanzanite na vito vingine hapa nchini ili kuongeza manufaa yatokanayo na madini hayo na madini mengine ya vito;
- (h) Kuanzisha na kuimarisha soko la dhahabu la Kalema;
- (i) Kuimarisha Taasisi zinazohusika na masuala ya madini kwa kuziwezesha kwa rasilimali na vitendea kazi;
- (j) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya madini kwa kufanya tafiti za madini mkakati, madini ya viwanda na madini ya metali;
- (k) Kuendeleza mipango ya kufanya tafiti za jiosayansi kwa lengo la kutatua changamoto katika nyanja za madini, kilimo, maji, majanga ya asili ya jiolojia na kutoa elimu kwa wananchi;
- (l) Kuimarisha kaguzi katika masuala ya afya, usalama na utunzaji wa mazingira dhidi ya uharibifu unaoweza kuepukika katika shughuli za utafiti, uchimbaji na uchenjuaji wa madini;
- (m) Kuhakikisha migodi yote mikubwa inaajiri, inanunua huduma na bidhaa kutoka hapa nchini kwa kiwango cha kuridhisha kwa kadiri ya upatikanaji wake na kutoa huduma za kijamii katika maeneo husika;



- (n) Kuimarisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ili liweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo;
- (o) Kuwezesha ujenzi wa miundombinu muhimu kupitia mamlaka zenye dhamana katika maeneo ambayo yanauwezekano wa kuanzishwa kwa migodi mikubwa mipya;
- (p) Kuainisha na kutambua madini ya kimkakati na kuhamasisha na kufanikisha uwekezaji wa kimkakati katika madini hayo ili taifa liweze kunufaika; na
- (q) Kujenga imani kwa biashara ya madini nchini kwenye uwanja wa kimataifa kwa kutekeleza wajibu wa nchi yetu kama wanachama wa EITI.

### Utalii

66.

Sekta ya utalii ina umuhimu katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi kwa ujumla katika nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania. Katika miaka mitano iliyopita Chama Cha Mapinduzi kupitia Serikali yake iliendelea kuimarisha utalii nchini kwa kusimamia ipasavyo mikakati ya kukuza vivutio mbalimbali vya utalii vikiwemo hifadhi za wanyama, maporomoko ya maji, milima, misitu ya mazingira asilia, utamaduni, fukwe na malikale. Kupitia uendelezaji wa vivutio hivyo, Serikali imeweza kupata mafanikio mbalimbali yakiwemo:-

- (a) Kuongeza idadi ya watalii kutoka 1,137,182 mwaka 2015 hadi kufikia 1,510,151 mwaka 2019 kutokana na kuitangaza sekta ya utalii kikanda na kimataifa. Ongezeko hilo la watalii limechangia kupanda kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii kutoka Dola za Kimarekani milioni 1,901.95 mwaka 2015 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 2,612.99 mwaka 2019;
- (b) Kuanzishwa kwa chaneli mahsusi ya televisheni (*Tanzania Safari Channel ya TBC*) inayotangaza utalii wa Tanzania nchini na nje ya nchi yetu;
- (c) Kuboresha makusanyo yatokanayo na sekta ya maliasili na utalii kwa kudhibiti upotevu wa mapato kwa kuanzisha mfumo funganishi wa kieletroniki wa “MNRT-Portal”;
- (d) Kuendelea kuboresha vituo vya utalii vyenye kumbukumbu za malikale kwa kuanzisha onesho la kudumu kuhusu chimbuko na maendeleo ya binadamu katika Bonde la Olduvai, Arusha pamoja na kutangaza mji wa Mikindani ulioko Mtwara na kuufanya kuwa kumbukumbu ya kihistoria na Urithi wa Utamaduni wa Taifa;
- (e) Kuongeza wigo wa mazao ya utalii kwa kuendeleza utalii wa meli, mikutano, fukwe, utamaduni, malikale, ikolojia na jiolojia. Aidha,



hatua hiyo imeenda sambamba na uongezaji wa shughuli za utalii katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo safari za puto (*balloon safaris*), safari za usiku (*night game drive*), Utalii wa kutembea kwa miguu (*walking safaris*), Kutembea kwa miguu kwa kutumia daraja la kamba (*canopy walk*), kutembea katika hifadhi za misitu ya asili (*natural forest reserves*) na utalii wa kitamaduni (*cultural tours*) ikiwa ni nyongeza kwenye utalii maarufu wa wanyamapori;

- (f) Kuimarisha miundombinu ya utalii ikiwemo kujenga na kukarabati barabara zilizopo ndani ya maeneo ya vivutio vya utalii, madaraja, njia za miguu, viwanja vya ndege na kununua boti za usafiri; na
- (g) Kuboresha Kanuni ya Utalii ya Usafirishaji Watalii “*The Tourism Agents*” (*Registration and Licensing Regulations 2015 & 2017*) iliyoongeza wigo wa Watanzania kushiriki katika biashara za utalii. Katika kutekeleza azma hii, Serikali imepunguza ada ya leseni ya biashara za utalii kwa wakala wa kusafirisha watalii yenye idadi ya magari chini ya manne kutoka Dola za Kimarekani 2,000 hadi 500. Kutokana na marekebisho hayo, kampuni za Kitanzania zimeongezeka kutoka idadi ya awali ya 643 mwaka 2015 hadi kufikia kampuni 1,687 mwaka 2020.

**67. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali chini ya Chama Cha Mapinduzi itaweka mkazo katika kupanua wigo wa bidhaa/mazao ya utalii ili sekta hiyo iendelee kuchangia zaidi katika pato la Taifa. Katika kutekeleza lengo hilo, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi itatekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuongeza na kukuza wigo wa bidhaa/mazao ya utalii ili kufikia watalii 5,000,000 kwa mwaka kufikia mwaka 2025 na kuongeza mapato kutoka Dola za Kimarekani bilioni 2.6 mwaka 2020 hadi Dola za Kimarekani bilioni 6.0 mwaka 2025 kwa kufanya yafuatayo:-
  - (i) Kukuza na kuimarisha utalii na uwindaji wa wanyamapori ili kuongeza mchango wa sekta katika uchumi wa Taifa;
  - (ii) Kukuza utalii wa mikutano kwa kujenga ukumbi mkubwa wa mikutano wa kisasa utakaojumuisha hoteli zenye hadhi ya kimataifa jijini Dar es Salaam;
  - (iii) Kuendeleza utalii wa fukwe kwa kutenga maeneo mahsusi ya fukwe, kuyasimamia na kuyaendeleza kimkakati;
  - (iv) Kujenga miundombinu ya kimkakati ya kuwezesha meli za kitalii kuzuru nchini; na
  - (v) Kutekeleza mikakati mingine ya kuongeza wigo wa utalii



ikiwemo ya kuendeleza maeneo ya kihistoria na malikale, utalii wa jiolojia, ikolojia, ufugaji nyuki pamoja na utalii wa kilimo ikiwemo maua na viungo.

- (b) Kubuni na kuboresha vipindi vya utangazaji wa vivutio vya utalii kupitia chaneli mahsusi ya televisheni (*Tanzania Safari Channel ya TBC*) inayotangaza utalii wa Tanzania nchini na nje ya nchi yetu. Pia, kuimarisha Bodi ya Utalii ili iweze kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kwenye masoko ya kimkakati;
- (c) Kufanya mapitio ya sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali kwa ajili ya kusimamia sekta ya utalii nchini ikiwemo kuhamasisha na kusimamia utalii endelevu na wenye kuzingatia masilahi ya nchi (*sustainable and responsible tourism*) ili kufanya vivutio kuwa endelevu na kuweka viwango vya utoaji huduma;
- (d) Kushirikisha sekta binafsi kuandaa wataalam wa ukarimu na kuwatambua wataalam wenye ujuzi na weledi unaohitajika katika utoaji wa huduma za utalii ili kukuza sekta ya utalii na kuongeza ajira kwa wananchi na Pato la Taifa kwa ujumla;
- (e) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi na umma zishiriki kikamilifu katika uwekezaji wa utalii, hususan katika sekta ndogo ya malazi kwenye maeneo ya hifadhi, kumbi za mikutano na huduma nyingine za kimkakati; na
- (f) Kuhamasisha jamii ili iweze kujua umuhimu wa utalii kuanzia ngazi ya chini ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa mitaala inayojumuisha utalii katika shule na vyuo kimkakati.

### **Maliasili**

68.

Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kusimamia Serikali katika kuhakikisha kuwa sekta ya maliasili inazidi kuimarika ili kuendelea kutunza maliasili za nchi na kuyafanya mazao yatokanayo na maliasili, hususan wanyamapori, misitu na nyuki kuchangia kikamilifu katika ukuaji wa uchumi; kuwaongezea wananchi kipato na fursa za ajira. Hatua hizo zimewezesha sekta ya maliasili kuongeza Pato la Taifa na fursa za ajira kwa wananchi na mafanikio mengine kama ifuatavyo:-

- (a) Kuimarisha uhifadhi, ulinzi na kuendeleza utalii kwa kuanzisha na kupandisha hadhi maeneo ya wanyamapori yaliyohifadhiwa ambayo yamewezesha Hifadhi za Taifa kuongezeka kutoka 16 mwaka 2015 hadi 22 mwaka 2020;
- (b) Kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za wanyamapori, misitu na nyuki kwa lengo la kupunguza ujangili kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuanzisha Kikosikazi cha Taifa cha Kupambana na Ujangili na kubadili mfumo wa usimamizi kutoka ule wa kiraia kwenda wa Jeshi Usu;



- (c) Kuimairisha ushiriki wa jamii katika usimamizi na manufaa ya rasilimali za misitu na nyuki kwa kutekeleza programu zinazosaidia kuzalisha ajira na kipato pamoja na uhifadhi wa mazingira;
- (d) Kuimarisha usimamizi wa rasilimali za wanyamapori, misitu na nyuki kwa kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS). Mamlaka hizi pamoja na manufaa mengine, zimeimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali hizo, hususan kwenye mashamba ya miti, hifadhi za misitu, mapori ya akiba, mapori tengefu, ardhioevu na maeneo ya wazi;
- (e) Kuwekeza katika mifumo ya TEHAMA katika ulinzi na usimamizi wa wanyamapori, mathalan matumizi ya *rola*, ndege zisizo na rubani na *GPS Collar* katika kufuatilia mienendo ya wanyamapori adimu na waliopo hatarini kutoweka;
- (f) Kuimarisha mahusiano kati ya maeneo ya hifadhi na wananchi kwa kufanya ulinzi wa wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa kufanya doria na kutoa elimu ya kujikinga ili kuendelea kuifanya sekta ya maliasili iendelee kuwa endelevu na inayojali haki na masilahi ya wananchi. Hatua hii imeleta amani na kupunguza migogoro kati ya wananchi hao na Serikali;
- (g) Kuwezesha wanavijiji 9,000 katika mikoa ya Iringa, Njombe, Morogoro na Ruvuma kupanda na kutunza jumla ya miti milioni 26 katika mashamba binafsi yenye ukubwa wa hekta 12,000 kupitia Programu ya Panda Miti Kibiashara. Aidha, jumla ya ajira 136,975 zilizalishwa kupitia Programu ya Panda Miti Kibiashara, mashamba binafsi na ya Serikali;
- (h) Kuendeleza utatuzi wa migogoro iliyopo baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa, kwa kuhakiki mipaka na kuweka vigingi. Katika hatua hiyo jumla ya vigingi 30,120 viliwekwa katika hifadhi za misitu, mapori ya akiba na hifadhi za Taifa;
- (i) Kuendeleza utekelezaji wa mikakati ya kuwanufaisha wananchi wanaoishi jirani na misitu kupitia miradi ya ufugaji nyuki ambapo kupitia uwezesaji uliofanyika, mwaka 2019 vikundi vya ufugaji nyuki 470 na watu binafsi 57 wamewezeshwa kupata mizinga ipatayo 17,833 ikilinganishwa na mizinga 11,730 mwaka 2015. Aidha, ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya nyuki, elimu pia imetolewa kwa wafugaji nyuki 2,097, vikundi 62 na mafundi seremala 10;
- (j) Kuanzishwa mashamba mapya matano yenye ukubwa wa hekta 185,456 kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, ambapo jumla ya hekta 34,977 zimepandwa miti. Hatua hii imeongeza idadi ya mashamba ya Serikali kutoka 18 mwaka 2015 hadi 23 Desemba, 2019. Aidha, Serikali imepandisha hifadhi za misitu ya asili tano



kuwa Misitu ya Hifadhi za Mazingira Asilia na kuzipa daraja au hadhi ya juu kabisa ya uhifadhi inayotambuliwa na Shirika Muungano wa Kimataifa wa Kuhifadhi wa Asili na Mali za Asili (IUCN) na hivyo kuwa na jumla ya hifadhi za misitu ya mazingira asilia 17. Pia, Wizara imewezesha uanzishaji wa hifadhi za nyuki mpya mbili na kufikia jumla ya hifadhi 37 hadi mwaka 2019;

- (k) Kuendeleza uboreshaji wa sekta ya nyuki kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kujenga viwanda viwili vya kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki katika wilaya za Manyoni na Mufindi; na
- (l) Kuendeleza uhifadhi wa mazingira kwa kupanda takriban miti milioni 40 ikiwemo miti 2,960,000 iliyopandwa katika jiji la Dodoma kupitia Kampeni ya Dodoma ya Kijani.

69.

**Katika miaka mitano ijayo, Serikali kupitia Chama Cha Mapinduzi kinalenga kuendelea kuimarisha usimamizi, ulinzi na uhifadhi maliasili kwa faida ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho. Katika kutekeleza azma hiyo, Chama Cha Mapinduzi kitaelekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kufanya mapitio ya sera, sheria, kanuni na miongozo na mikakati kwa ajili ya kusimamia rasilimali za wanyamapori, misitu na nyuki nchini;
- (b) Kujenga uwezo wa wadau katika kusimamia rasilimali za wanyamapori, misitu na nyuki ili kuongeza mchango wa sekta katika Pato la Taifa;
- (c) Kutekeleza mikakati ya kudhibiti ujangili wa wanyamapori, misitu na mazingira ya nyuki, kuimarisha ulinzi dhidi ya wanyamapori ili kulinda maisha ya wananchi na mali zao na kutatua migogoro baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa;
- (d) Kuhamasisha wananchi kuanzisha ranchi, mashamba na bustani za wanyamapori ili kuimarisha ushiriki wa wananchi katika uhifadhi na kujipatia kipato;
- (e) Kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia uwekezaji katika sekta ya wanyamapori, misitu na nyuki pamoja na kuimarisha mifumo ya kitaasisi kwa ajili ya kusimamia sekta ya maliasili. Aidha, pamoja na hatua nyingine Serikali itaanzisha mamlaka ya misitu na nyuki na taasisi ya utafiti wa nyuki ili kuboresha na kuongeza uzalishaji wa mazao ya nyuki nchini;
- (f) Kuanzisha na kuendeleza viwanda vya mazao ya misitu na nyuki vinavyochakata mazao hayo kwa ufanisi na tija ili kuepusha upotevu mwingi wa malighafi na kuwezesha kutumia mabaki yake kuzalisha bidhaa nyingine;

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASOGA MBELE PAMOJA





- (g) Kuendeleza programu mbalimbali za upandaji miti na ufugaji nyuki ili kutunza mazingira na kuongeza kipato kwa wananchi na Taifa; na
- (h) Kujenga na kuboresha miundombinu ya utalii katika hifadhi za misitu ili kuwezesha shughuli za utalii kufanyika kwa ufanisi zaidi.

### **Malikale na Kumbukumbu za Taifa**

Katika miaka mitano iliyopita (2015-2020), Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kusimamia Serikali katika kuchukua hatua za kulinda na kuhifadhi maeneo ya malikale kama urithi wa utamaduni na kumbukumbu za kihistoria za Taifa kwa maendeleo endelevu ya kizazi cha sasa na kijacho. Maeneo haya ya kihistoria yanatoa mchango mkubwa katika kukuza utalii wa ndani na Kimataifa. Aidha, maeneo ya malikale yameendelea kujenga uzalendo wa kitaifa wa wananchi kwa kuwawezesha kutambua na kuenzi historia ya Taifa letu. Mafanikio yaliyopatikana katika eneo hili ni pamoja na:-

- (a) Kuboresha na kuanzisha Makumbusho ya Zamadamu ya Olduvai-Ngorongoro, Rashid Mfaume Kawawa mjini Songea, Mji wa Kihistoria wa Mikindani na Makumbusho ya Mkoa wa Iringa. Aidha, nyumba ya kumbukizi ya makazi ya Mwl. Nyerere iliyopo Magomeni Dar es Salaam imekarabatiwa;
- (b) Maeneo ya malikale katika mji wa Kihistoria wa Mikindani na eneo la Zamadamu la Laetoli-Ngorongoro yametangazwa kuwa maeneo ya Kihistoria na Kumbukumbu ya Urithi wa Utamaduni wa Taifa;
- (c) Kukarabati miundombinu ya vituo saba vya Malikale katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Lindi na Tanga. Vilevile, ukarabati wa majengo tisa ya kihistoria umefanyika katika mikoa hiyo;
- (d) Kuanzisha na kusimamia Tamasha la Kimondo ambalo hufanyika sambamba na siku ya Vimondo Duniani kila mwaka na Tamasha la Urithi Wetu. Pamoja na manufaa mengine, matamasha haya yamesaidia kupanua wigo wa mazao ya utalii nchini; na
- (e) Katika kuboresha usimamizi na uendelezaji wa maeneo ya malikale yaliyopo jirani na hifadhi za misitu na wanyamapori, vituo 18 vya Mambo ya Kale vimekasimishwa kwa taasisi za Wizara ili kuviendeleza na kuvitangaza kama vivutio vya utalii jirani na maeneo ya hifadhi hizo.

70. UMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA

**71. Katika miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaelekeza Serikali kuhakikisha kuwa inasimamia na kulinda malikale, kumbukumbu na nyaraka za Taifa ili ziweze kuendelezwa. Katika kufikia lengo hilo, Serikali itatekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kufanya mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali kwa ajili ya kusimamia rasilimali za malikale nchini;



- (b) Kuboresha usimamizi, matumizi na uhifadhi wa maeneo ya malikale/mambo ya kale ili kuyahifadhi na kuyaendeleza kama urithi wa nchi na kutunza historia asili (*Natural History*) kwa kutungwa sheria na kuwekwa mikakati mahsusi ikiwemo kujenga Makumbusho ya Taifa ya Historia Asili;
- (c) Kuimarisha uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka katika teknolojia ya kisasa kwa kuingiza nyaraka katika mfumo ya kidijitali wa kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka (Digital Records and Archives Management and Preservation Systems) ili kurahisisha upatikanaji na kulinda nakala halisi;
- (d) Kuboresha usimamizi na matumizi ya maeneo ya malikale ili kuyahifadhi na kuyaendeleza kama urithi wa nchi ikiwemo kujenga kituo cha kumbukizi ya Dainosaria;
- (e) Kuimarisha miundombinu wezeshi ya utalii ikiwemo vituo vya taarifa, makumbusho na huduma kwa wateja katika maeneo ya Malikale;
- (f) Kuhamasisha na kujenga uwezo wa halmashauri za miji, manispaa na majiji kutambua na kuhifadhi maeneo ya malikale ambayo ni tunu za Taifa na vivutio vya utalii;
- (g) Kuhifadhi maeneo muhimu ya kihistoria nchini yakiwemo ya Mwl. Nyerere na wapigania uhuru ambayo ni urithi wa utamaduni wa Taifa, vivutio vya utalii na kwa ajili ya utafiti;
- (h) Kuhamasisha kufanyika kwa matamasha ya kitamaduni na kuyatumia kutangaza na kukuza utalii wa malikale na utamaduni;
- (i) Kujenga na kuimarisha miundombinu ya Makumbusho ya Taifa na makumbusho nyingine zilizopo nchini; na
- (j) Kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia uwekezaji katika sekta ya malikale pamoja na kuimarisha mifumo ya kitaasisi kwa ajili ya kusimamia sekta hiyo. Aidha, pamoja na hatua nyingine Serikali italipa mamlaka Shirika la Makumbusho ya Taifa ili kutekeleza majukumu ya kiutendaji ya Idara ya Mambo ya Kale.

### **Ardhi**

72. Ardhi imeendelea kuwa miongoni mwa rasilimali za msingi katika ujenzi wa uchumi tokea Taifa letu lipate uhuru. Ardhi, imekuwa muhimu katika kuziwezesha sekta nyingine kuzalisha kikamilifu hususan sekta za uzalishaji kama vile kilimo, mifugo, uvuvi ikiwa ni pamoja na maeneo ya ardhi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda.
73. Chama Cha Mapinduzi kwa kutambua umuhimu wa sekta ya ardhi, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020) kilichukua hatua za kuhahikisha sekta hii inaboreshwa katika maeneo ya utawala wa ardhi; mipango ya matumizi bora ya ardhi; maendeleo ya makazi; mipango miji



na vijiji; na upimaji na ramani. Kutokana na hatua hizo, yamepatikana mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na urasimishaji wa maeneo ya makazi kwa wananchi na kuchangia kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi na ujenzi wa makazi usio rasmi ambapo wananchi wamewezeshwa kuwa na nyumba bora. Mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

**Usimamizi wa Ardhi**

- (a) Kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kwa kusanifu na kutengeneza Mfumo Uganishi wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Ardhi (ILMIS). Mfumo huu umewekwa kwenye halmashauri tano za mkoa wa Dar es Salaam katika awamu ya kwanza. Jumla ya kumbukumbu za majalada yenye taarifa 728,370 za usajili wa hati; upimaji na umilikishaji wa ardhi yamebadilishwa kutoka mfumo wa analogia na kuwa kidijitali. Vilevile, miamala 254,944 na viwanja 239,317 viliingizwa kwenye mfumo wa ILMIS ambapo hakimiliki za ardhi 3,868 zilitolewa kwa njia ya kielektroniki. Uanzishwaji wa mfumo wa ILMIS umehusisha pia ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu za Ardhi kilichopo jijini Dar es Salaam ambacho kitatumika kuhifadhi kumbukumbu zote za ardhi kwa njia ya kielektroniki kwa nchi nzima;
- (b) Kumilikisha ardhi wananchi na kusajili hatimiliki na nyaraka nyingine za kisheria 403,54;
- (c) Kutoa hatimilki za kimila 863,474 kwa wananchi katika Halmashauri mbalimbali nchini na hivyo kuwezesha wananchi kutumia ardhi kama dhamana ya kupata mikopo ya kuendesha shughuli mbalimbali. Hatimilki za kimila 1,382 zilitumika kama dhamana kupata mikopo kwenye taasisi za fedha yenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya kuanzisha shughuli mbalimbali za kiuchumi;
- (d) Masjala za ardhi za vijiji 385 zimejengwa na kukarabatiwa;
- (e) Kupitia Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi, halmashauri 24 nchini ziliwezeshwa kwa kupatiwa vifaa na fedha kwa ajili ya kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi. Viwanja 40,241 vimepimwa kupitia program hii. Pia, jumla ya vyeti vya ardhi vya vijiji 2,513 vilitolewa;
- (f) Kuimarisha upangaji, upimaji, umilikishaji, usajili wa hati za hakimiliki za ardhi na nyaraka kwa kufanya maboresho ya muundo wa usimamizi wa ardhi katika ngazi ya mikoa na halmashauri;
- (g) Utatuzi wa migogoro ya ardhi na kuimarisha hifadhi za wanyamapori kwa kuhalalisha vijiji 920 kati ya 975 vilivyokuwemo ndani ya hifadhi. Aidha, migogoro ipatayo 10,120 imetatuliwa kiutawala na migogoro 112,243 imetatuliwa kupitia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya;
- (h) Kuwekwa kwa mazingira wezeshi kwa ajili ya uwekezaji, hususan viwanda kwa kutenga ekari 446 za ardhi katika mkoa wa Dar es



Salaam (Pemba mnazi). Aidha, ekari 224,439.4 za ardhi zimetengwa katika halmashauri mbalimbali kwa ajili ya uwekezaji; na

- (i) Kupunguzwa kwa ardhi isiyoendelezwa kwa kubatilisha mashamba 45 yenye jumla ya ekari 121,032.243. Kati ya hizo, ardhi yenye ukubwa wa ekari 12,488.49 imetengwa kwa ajili ya uwekezaji na sehemu ya ardhi kugawanywa kwa wananchi kwa matumizi mbalimbali.

***Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi***

- (a) Kuwajengea uwezo watendaji wa halmashauri 83 na wa halmashauri za vijiji 647 kuhusu kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi;
- (b) Kuboreshwa kwa matumizi bora ya ardhi kwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 647 katika halmashauri za wilaya 83; na
- (c) Kuboresha matumizi bora ya ardhi kwa kukamilisha mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya saba za Kilombero, Ulanga, Muheza, Morogoro, Serengeti, Malinyi na Mkinga.

***Mipango Miji na Vijiji***

- (a) Kuwezesha ujenzi wa miji ya kisasa na kupunguza makazi yasiyo rasmi kwa kuandaa Mipango Kabambe 22 ya majiji ya Dodoma, Arusha, Mwanza na Dar es Salaam; Manispaa ya Musoma, Iringa, Mtwara/Mikindani, Singida, Tabora, Shinyanga, Kigoma/Ujiji, Lindi, Morogoro, Songea, Sumbawanga na Bukoba pamoja na miji ya Korogwe, Kibaha, Bariadi, Babati, Geita na Tunduma; na
- (b) Kuhuishwa kwa Programu ya Taifa ya Kurasimishaji na Kuzuia Ukuaji wa Makazi yasiyo rasmi ambapo jumla ya viwanja 764,158 katika maeneo ya urasimishaji vilipangwa katika Halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, vipande vya ardhi 134,239 vilitambuliwa na leseni za makazi 868 zilitolewa kwa wananchi katika jiji la Dar es Salaam.

***Upimaji na Ramani***

- (a) Kuimarisha uwezo wa upimaji wa ardhi ya mipakani kwa kununua picha za *satellite* kwa ajili ya kutengeneza ramani ya msingi ya mpaka kati ya Tanzania na Msumbiji. Vilevile, picha za anga kwa ajili ya kutayarisha ramani za msingi kwenye eneo la mpaka kati ya Tanzania na Kenya lenye kilomita za mraba 760 zimepigwa na kukamilika.
- (b) Kuimarishwa kwa mpaka wa Tanzania na Kenya kutoka katika kijiji cha Kirongwe Wilaya ya Rorya hadi kijiji cha Naan Wilaya ya Ngorongoro ambapo jumla ya kilomita 172 zimewekewa alama. Aidha, mpaka wa Tanzania na Burundi kutoka katika kijiji cha Kasange Wilaya ya Ngara hadi kijiji cha Mrusagamba Wilaya ya Ngara wenye jumla ya kilomita 135.85 umewekewa alama;
- (c) Kuboresha makazi na matumizi bora ya ardhi kwa kupima viwanja 972,538 na mashamba 5,765 katika halmashauri mbalimbali nchini yakiwemo maeneo ya urasimishaji; na



- (d) Kuimarishwa kwa mpaka wa Tanzania na Uganda kwa kuweka alama nane za msingi na kuimarishwa kwa mpaka kati ya Tanzania na Zambia ambapo jumla ya kilomita 11 zimewekewa alama.

74. TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMBA

**Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuchukua hatua za kuendeleza rasilimali ardhi kwa kutambua kuwa hiyo ni rasilimali muhimu katika uhai na ustawi wa binadamu na Taifa. Chama kitahakikisha Serikali inaweka mikakati madhubuti ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii na ustawi wa watu wote kwa kuzingatia sera, sheria, miongozo na taratibu za uendelezaji wake. Katika kipindi hicho, Chama kitaelekeza Serikali kuendelea kutekeleza yafuatayo:-**

#### **Usimamizi wa Ardhi**

- (a) Kuhakikisha kuwa ardhi yote ambayo ndio rasilimali kuu inapangwa, kupimwa, kuwatambua watumiaji na kuwapa hatimiliki ili waweze kuzitumia kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kuongeza mchango wa rasilimali ardhi katika pato la Taifa;
- (b) Kuweka Mfumo Unganishi Kielektroniki wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi katika mikoa yote na halmashauri zote nchini;
- (c) Kumilikisha na kusajili vipande vya ardhi 2,500,000 mijini na kutoa hatimiliki za kimila 2,600,000 vijijini;
- (d) Kutenga ardhi ya kutosha (Hazina ya Ardhi) kwa ajili ya uwekezaji na kuimilikisha kwa Kituo cha Uwekezaji (TIC) ili kurahisisha uwekezaji nchini;
- (e) Kuimarisha Mfuko wa Fidia ya Ardhi ili uweze kufidia ardhi itakayotwaliwa kwa matumizi ya umma na uwekezaji nchini;
- (f) Kusimamia na kuratibu uendelezaji wa ardhi na makazi nchini ikiwa ni pamoja na kuanzisha miradi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi;
- (g) Kurasimisha ardhi zinazomilikiwa kimila na makazi yasiyo rasmi mijini ili kuwawezesha wamiliki wa ardhi kunufaika na kuchangia katika maendeleo;
- (h) Kufanya mapitio na kuhuisha sera, sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi na utawala wa ardhi kwa kushirikisha wananchi kikamilifu ili kuwawezesha kumiliki uchumi; na
- (i) Kuimarisha usimamizi wa utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini kwa kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuhamishia mabaraza ya ardhi kwenye utaratibu wa mahakama.



### **Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi**

- (a) Kupanga matumizi bora ya ardhi katika shoroba tatu (corridor development plans) ambazo ni ushoroba wa SGR, Bomba la Mafuta (EACOP) na ushoroba wa reli ya TAZARA ikiwemo eneo la mto Rufiji katika mradi wa uzalishaji wa umeme wa Mwalimu Nyerere;
- (b) Kupanga matumizi bora ya ardhi katika wilaya 54 zenye miradi ya kinkakati pamoja na vijiji 4,131 vilivyopo katika maeneo ya mipakani na nchi jirani;
- (c) Kuandaa mipango ya kina ya matumizi ya ardhi ili kutekeleza usimamizi wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya kilimo, makazi na malisho katika vijiji 874 vilivyopo katika nyanda zenye hali ya jangwa, nusu jangwa na kanda za malisho; na
- (d) Kutengeneza mfumo unganishi wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za mipango ya matumizi ya ardhi na vyeti vya vijiji.

### **Mipango Miji na Vijiji**

- (a) Kusimamia na kuratibu uandaaji na ukamilishaji wa Mipango Kabambe (*master plans*) ya miji mbalimbali nchini;
- (b) Kusimamia na kuratibu uandaaji wa mipango kina 10,000 ya uendelezaji wa miji na makazi nchini na kuandaa mipango kina 25 ya uendelezaji wa visiwa na fukwe;
- (c) Kuboresha maeneo hatarishi ikiwemo bonde la mto Msimbazi jijini Dar es Salaam ili kudhibiti mafuriko, kuhifadhi mazingira na kuyafanya kuwa vivutio kwa watalii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali;
- (d) Kuimarisha utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kurasimisha Makazi yasiyo rasmi katika mikoa 26 nchini ikiwa ni pamoja na kuwezesha ujenzi wa miji ya kisasa na kupunguza makazi yasiyo rasmi kwa kuandaa Mipango Kabambe 6 ya miji ya Mpanda, Njombe, Mererani, Chato, Ifakara na Kahama; na
- (e) Kusimamia na kuratibu upangaji upya maeneo yaliyochakaa (*re-development*) katika miji mbalimbali nchini.

### **Nyumba na Makazi**

75.

Chama Cha Mapinduzi kinatambua kuwa nyumba ni rasilimali ya msingi na hitaji muhimu kwa maisha ya binadamu. Katika kusimamia hilo, kwa kipindi cha mwaka (2015 - 2020), Chama kimeisimamia Serikali kutoa huduma stahiki ya makazi bora na kupata mafanikio yafuatayo:-

- (a) Kuendeleza uwezesaji wa watumishi kwa kuwapatia mikopo ya nyumba watumishi wa Serikali yenye thamani ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba;





- (b) Kuboreshwa kwa mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-
- (i) Kuongezeka kwa benki za kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kutoka tatu mwaka 2015 na kufikia 32 mwaka 2020;
  - (ii) Kushuka kwa kiwango cha riba ya mikopo ya ujenzi wa nyumba kutoka asilimia 21-23 mwaka 2015 kufikia asilimia 13-18 mwaka 2020;
  - (iii) Kuwezesha kutolewa kwa mikopo midogo midogo ya ujenzi wa nyumba kwa taasisi ndogo za fedha kiasi cha shilingi bilioni 17.91 kwa wananchi 1,474;
  - (iv) Kupungua kwa riba ya mikopo midogo midogo ya ujenzi wa nyumba kutoka asilimia 10 mwaka 2015 hadi asilimia 6 mwaka 2020;
  - (v) Kuongezwa kwa muda wa kurejesha mikopo midogo midogo kutoka miaka mitano mwaka 2015 hadi 10 mwaka 2020; na
  - (vi) Serikali kupitia mabenki ya biashara iliwezesha mikopo ya nyumba yenye thamani ya shilingi bilioni 421.07 kwa wananchi 4,996.
- (c) Shirika la Nyumba la Taifa, lilitekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba kama ifuatavyo:-
- (i) Kukamilisha miradi 52 kati ya 94 ambapo nyumba 1,185 kwa ajili ya wananchi wa kipato cha chini na nyumba 6,146 za makazi na biashara kwa ajili ya watu wa kipato cha kati zilijengwa;
  - (ii) Kukamilisha awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi wa nyumba katika eneo la Iyumbu jijini Dodoma ambapo nyumba 151 zimejengwa;
  - (iii) Kukamilisha miradi ya ujenzi wa Ofisi na nyumba mbalimbali za Taasisi za Umma ikiwemo mji wa Serikali Mtumba;
  - (iv) Kutoa mafunzo ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa vikundi 390 vya ujenzi kutoka katika halmashauri mbalimbali nchini na kuvipatia mashine za kufyatulia matofali ya kufungamana; na
  - (v) Kukamilika kwa mipango kabambe iliyoko katika eneo la Iyumbu jijini Dodoma; *Safari City* na Usa River jijini Arusha; na *Salama Creek* Kigamboni jijini Dar es Salaam na kuidhinishwa na mamlaka za upangaji husika.



76. **Kwa kutambua umuhimu wa nyumba, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuelekeza Serikali kujenga mazingira ya kuwawezesha wananchi nchini kujenga nyumba bora na za gharama nafuu vijijini na mijini. Katika miaka mitano ijayo Chama kitaelekeza Serikali kuendelea kuboresha sekta ya nyumba na makazi kwa kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kuandaa sera mpya ya nyumba na maendeleo ya makazi na kubuni mikakati mbalimbali ya kuwawezesha wananchi mijini na vijijini kujenga nyumba bora na za gharama nafuu kwa kushirikiana na wadau wote;
- (b) Kushirikiana na mamlaka za upangaji, kuandaa mfumo wa kisasa wa usimamizi wa uendelezaji wa miji ikiwemo upatikanaji na utoaji vibali vya ujenzi wa nyumba nchini;
- (c) Kuhakikisha maeneo yaliyopimwa kwa ajili ya makazi na biashara yanawekewa miundombinu ya kisasa ikiwemo barabara, maji, umeme na mawasiliano;
- (d) Kutambua na kuanzisha kanzidata ya nyumba zote nchini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha taratibu za mahusiano kati ya wapangaji na wamiliki wa nyumba na majengo;
- (e) Kukamilisha taratibu za kuanzisha chombo cha usimamizi na uendelezaji wa sekta ya milki ambacho pamoja na majukumu mengine, kitaratibu kodi za pango la nyumba za makazi na biashara, ufanyaji biashara zihusuzo ardhi na milki, uuzaji wake na ulipaji kodi, usajili wa madalali na uwekaji kumbukumbu zote za milki za makazi na biashara;
- (f) Kuandaa mwongozo wa mipango na ujenzi wa nyumba vijijini;
- (g) Kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa gharama nafuu kwa ajili ya ujenzi kwa kushirikiana na wadau wote wakiwemo Shirika la Nyumba la Taifa na Wakala wa Majengo Tanzania pamoja na sekta binafsi;
- (h) Kuhamasisha na kuweka mazingira wezeshi ya kuhakikisha wananchi katika maeneo yote nchini wanakuwa na nyumba bora. **“Nyumba bora kwa kila Mtanzania inawezekana”**; na
- (i) Kuendelea kuboresha na kuimarisha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ili litekeleze miradi kwa tija na kujenga nyumba, majengo ya Serikali na majengo ya biashara kwa gharama nafuu katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo:-
  - (i) Kuendelea na ujenzi wa nyumba 1,000 za gharama nafuu jijini Dodoma kwa ajili ya kuuza au kupangisha kwa wananchi na watumishi wa serikali;

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA



- (ii) Kukamilisha ujenzi wa nyumba za majengo makubwa ikiwemo *Morocco Square*, Kawe 711, *Golden Premier Residence* na Mradi wa Kiwanja Na. 300 *Regent Estate* katika jiji la Dar es Salaam;
- (iii) Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba 149 katika eneo la *Iyumbu* na nyumba 100 katika eneo la *Chamwino* jijini Dodoma;
- (iv) Kuendelea na miradi ya Vitovu vya Miji (*Satellite Cities*). katika maeneo ambayo yanamilikiwa ya *Luguruni* (ekari 156.53), *Uvumba*, *Kigamboni* (ekari 202) na *Kawe* (ekari 267.71) katika jiji la Dar es Salaam na *Burka/Matevesi* (ekari 579.2) na eneo la *Usa River* (ekari 296) katika jiji la Arusha; na
- (v) Kukamilisha mipango kabambe ya *Kawe*, *Luguruni* na *Kunduchi Rifle Range* iliyoko jijini Dar es Salaam.



## SURA YA TATU

### HUDUMA ZA JAMII

TUMETEKELEZA KIM KISHINDO; TUNAKONGA MBELE AMOJA

#### Utangulizi

77.

Sera ya msingi ya CCM kuhusu huduma za jamii ni kuhakikisha kuwa kila mwananchi anakuwa na fursa ya kupata huduma za jamii bora na za kutosha bila kikwazo. Kupitia Ilani yake ya Mwaka 2015, serikali ya CCM ilitekeleza sera, mikakati na mipango mbalimbali katika kufikia azma hii. Sura hii inatoa muhtasari wa mipango iliyotekelezwa, mafanikio yaliyopatikana na mipango itakayotekelezwa katika Ilani ya Mwaka 2020-2025 ili kuendelea kuimarisha na kupanua huduma za jamii nchini, ikiwemo elimu, afya, maji na ustawi wa jamii.

#### Elimu

78.

CCM inatambua kuwa rasilimaliwatu ndiyo nyenzo muhimu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Aidha, CCM inaamini kuwa elimu bora ndiyo nyenzo muhimu ya kujenga, kulea na kuendeleza rasilimaliwatu ili ziweze kuchangia kikamilifu katika ujenzi wa Taifa na maendeleo ya jamii kwa ujumla. Katika kuendelea kuimarisha elimu nchini, na kama sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2015, hatua mbalimbali zilichukuliwa. Hatua hizi ni pamoja na kutoa elimu bila malipo hadi ngazi ya sekondari, kuimarisha mazingira ya kufundisha na kujifunza, na kuajiri walimu zaidi katika ngazi zote za elimu. Vilevile, Sekta binafsi na asasi za kiraia zikiwemo taasisi za dini zimetoa mchango muhimu katika kupanua fursa za upatikanaji wa elimu, ukuzaji wa maarifa na ujuzi nchini.

79.

Katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 mafanikio makubwa yamepatikana katika sekta ya elimu kama ifuatavyo:-

#### *Elimumsingi*

- (a) Kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi wa Elimu ya Awali kutoka 1,069,823 mwaka 2015 hadi kufikia 1,429,169 mwaka 2020. Pia, idadi ya shule za msingi zenye madarasa ya Elimu ya Awali imeongezeka kutoka madarasa 16,889 mwaka 2015 hadi kufikia madarasa 17,771 mwaka 2020. Vilevile, maboresho yamefanyika kwenye mitaala, muhtasari, vitabu vya kiada vya wanafunzi na miongozo ya walimu;
- (b) Kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kuwajengea uwezo walimu 121,410, wanaofundisha Elimu ya Awali na darasa la I hadi la IV kuhusu mbinu za kufundishia na kujifunzia stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu;
- (c) Kuboresha uratibu na usimamiaji wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa kuwapatia mafunzo Waratibu Elimu Kata na Walimu Wakuu 13,350 katika elimumsingi;



- (d) Kuongezeka kwa uandikishaji katika elimumsingi kutoka wanafunzi 8,298,282 mwaka 2015 hadi kufikia wanafunzi 10,605,430 mwaka 2020;
- (e) Kuboresha fursa za upatikanaji wa elimu ambapo idadi ya madarasa imeongezeka kutoka 115,665 mwaka 2015 hadi kufikia 136,292 mwaka 2020 na kuongeza idadi ya shule za msingi kutoka 16,899 mwaka 2015 hadi 17,804 mwaka 2020;
- (f) Kuongezeka kwa uwiano wa kitabu cha kiada kwa mwanafunzi wa Darasa I-VI kufikia wastani 1:2 ambapo Serikali imekuwa ikigharamia uchapishaji na usambazaji wa vitabu;
- (g) Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaomaliza shule ya msingi kutoka asilimia 67 mwaka 2015 hadi asilimia 81 mwaka 2020 ambapo ufaulu wao umeongezeka kutoka asilimia 57 mwaka 2015 hadi asilimia 82 kwa mwaka 2020. Vilevile, idadi ya wanafunzi wanaoendelea na kidato cha kwanza imeongezeka kutoka asilimia 56 mwaka 2015 hadi asilimia 86 mwaka 2019;
- (h) Kuongeza uandikishaji wa wanafunzi katika Elimu ya Sekondari (Kidato cha I - IV) kutoka 1,648,359 kwa mwaka 2015 hadi kufikia 2,185,037 mwaka 2019 na (Kidato cha V - VI) kutoka 126,024 kwa mwaka 2015 hadi kufikia 153,420 mwaka 2019;
- (i) Kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya sekondari kwa: kuongeza idadi ya shule za sekondari kutoka 4,708 mwaka 2015 hadi kufikia shule 5,330 mwaka 2020. Aidha, mazingira ya kujifunzia na kufundishia yameimarishwa katika shule kongwe 89 zilizopo. Vilevile, shule 1,696 zimezipatiwa vifaa vya maabara vya masomo ya sayansi kati ya hizo, shule 1,625 ni za wananchi (Maarufu kama Shule za Kata) na 71 ni shule kongwe;
- (j) Kuongeza ufaulu wa mtihani wa kidato cha nne kutoka asilimia 68 mwaka 2015 hadi asilimia 82 kwa mwaka 2019. Vilevile, jumla ya wanafunzi 74,478 wa kidato cha nne walijiunga na kidato cha tano mwaka 2019, ikilinganishwa na wanafunzi 66,090 waliojiunga na kidato cha tano mwaka 2015;
- (k) Kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, kwa kununua na kusambaza vifaa vya nukta nundu (*braille*), kiwezesha kuongea (*speech trainer*), kipima sauti (*audio meter*) na fimbo nyeupe (*white cane*) kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Aidha, jumla ya walimu 60,007 wanaofundisha darasa la awali, na wanaofundisha darasa I hadi la IV, wamepatiwa mafunzo ili kuongeza umahiri katika kufundisha watoto wenye mahitaji maalum na watoto nje ya mfumo rasmi (MEMKWA);



- (l) Kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa taarifa za wanafunzi na shule kwa ujumla. Vilevile, kuongeza vitendea kazi vya mifumo ya ufuatiliaji wa utoaji elimu kwa kununua magari 84 ambapo 54 ni kwa ajili ya uthibiti ubora wa shule, 26 kwa ajili ya usimamizi wa elimu katika sektretarieti za mikoa na 4 kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini katika ngazi ya wizara. Aidha, ofisi 100 za Wathibiti Ubora katika ngazi mbalimbali za mamlaka za serikali za mitaa zimejengwa na kuwekewa vitendea kazi;
- (m) Kuimarisha elimu ya ufundi katika ngazi ya elimu ya sekondari ambapo, shule saba za ufundi za Sekondari ambazo ni Ifunda, Iyunga, Tanga, Mtwara, Moshi, Musoma na Bwiru Wavulana zimefanyiwa ukarabati mkubwa;
- (n) Kuimarisha kujifunza na kufundisha kwa njia ya TEHAMA kwa kutoa mafunzo kwa walimu 3,800 wa shule za msingi na sekondari;
- (o) Kuongeza idadi ya wanafunzi tarajali wa ualimu wanaodahiliwa kutoka 19,825 mwaka 2015 hadi 22,197 mwaka 2019;
- (p) Kuimarisha kujifunza na kufundisha kwa njia ya TEHAMA katika elimumsingi kwa kutoa mafunzo kwa walimu wote tarajali wa vyuo vya ualimu vya Serikali. Aidha, walimu 3,800 wa shule za msingi na sekondari wamepatiwa mafunzo ya kufundisha kwa njia ya TEHAMA ili kuwajengea uwezo wa kufundisha. Vilevile, vyuo vya ualimu 35 vya Serikali vimenunulia kompyuta 1,550; na
- (q) Kukarabati miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ikiwemo mabweni na mabwalo katika vyuo 18 vya ualimu ambavyo ni: Morogoro, Mpwapwa, Butimba, Kasulu, Songea, Tukuyu, Marangu, Kleruu, Korogwe, Tabora, Tandala, Nachingwea, Tarime, Kinampanda, Mandaka, Patandi, Mpuguso na Ilonga. Aidha, vyuo viwili vya Murutunguru na Kabanga vinajengwa upya na viko katika hatua mbalimbali za kukamilishwa.

***Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi***

- (a) Kuongezeka kwa udahili katika vyuo vya ufundi kutoka wanafunzi 96,694 mwaka 2015 hadi kufikia wanafunzi 151,969 mwaka 2020;
- (b) Vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi kutoka vyuo 672 mwaka 2015 hadi 712 mwaka 2020. Ongezeko hilo limewezesha udahili wa wanafunzi kutoka 117,067 mwaka 2015 hadi 226,767 mwaka 2020. Ili kurahisisha mafunzo kwa njia za TEHAMA, vyuo 27 kati vyuo 32 vya VETA vimeunganishwa katika mkongo wa Taifa;
- (c) Kutoa elimu ya ufundi na stadi za ujasiriamali kwa majaribio iliyogharimiwa na Serikali ambapo vijana wengi zaidi walipata fursa za kujijiri na kuajiri wengine;





- (d) Kujenga na kukarabati vyuo 10 vya VETA ambavyo ni: Ileje, Urambo, Nkasi, Newala, Muleba, Itilima, Babati, Kilindi, Ngorongoro na Kasulu. Aidha, ukarabati na uwekaji wa vifaa vya kisasa katika vyuo vya VETA vya Kihonda, Manyara, Pwani na Lindi umefanyika ili kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji; na
- (e) Kukarabati vyuo vyote 54 vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) na kuvipatia vifaa vya kufundishia. Aidha, udahili wa wanafunzi katika vyuo hivyo umeongezeka kutoka 6,693 mwaka 2015 hadi 9,736 mwaka 2020.

**Elimu ya Juu**

- (a) Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu nchini kutoka 65,064 mwaka 2015 hadi 87,813 mwaka 2020; Vilevile, wigo wa utoaji wa mikopo ya Elimu ya Juu umeongezeka kutoka idadi ya wanafunzi 98,300 waliopata mikopo mwaka 2014/15 hadi kufikia 130,883 mwaka 2020, na jumla ya fedha iliyotumika kwa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 ni shilingi trilioni 2.20;
- (b) Kutoa ufadhili kwa masomo ya udaktari kwa ngazi za Umahiri na Uzamivu ndani na nje ya nchi ambapo jumla ya wanafunzi 168 wamefadhiliwa na Serikali kusoma ndani ya nchi na madaktari 476 wamepata ufadhili wa masomo ya udaktari nje ya nchi;
- (c) Kujenga maktaba ya kisasa inayochukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
- (d) Kujenga mabweni mapya 24 katika vyuo vikuu, ambapo kwenye Chuo Kikuu cha Mzumbe ni mabweni manne yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 1,024 na mabweni 20 ya Dkt. John Pombe Magufuli ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 3,840. Aidha, ukarabati wa Bweni Na. 2 na Na. 5, yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 788, pamoja na karakana katika ndaki ya uhandisi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam vimefanyiwa ukarabati mkubwa kwa lengo la kupunguza adha kwa wanafunzi kupanga nje ya chuo na kuboresha mafunzo;
- (e) Kujenga majengo na kufanya ukarabati miundombinu ya kufundishia ya Taasisi za Sayansi za Bahari-Buyu Zanzibar ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kujenga maabara mtambuka yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,400 kwa wakati mmoja na kukarabati karakana ya Uhandisi Kilimo, Kujenga maabara za kemia, biolojia na jengo la mihadhara katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200 kwa wakati mmoja;
- (f) Kuboresha makazi ya wanachuo kwa kuvipatia Vyuo na Taasisi za Elimu ya Juu nyumba za Serikali zilizoko Kigamboni na Kijichi, jijini Dar es Salaam; na



- (g) Kukamilisha ukarabati wa ghorofa la kwanza na la pili la jengo la utawala katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam ambalo lina ofisi za Wahadhiri 63.

80. TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMBA

**Chama Cha Mapinduzi kinatambua umuhimu Sekta ya Elimu na mchango wake katika ajenda ya maendeleo kwa kuandaa mtaji watu wenye uwezo wa kutumia fursa za rasilimali zilizopo kujiletea maendeleo na kuchangia katika jitihada za nchi kufikia uchumi wa kati uliojikita katika misingi ya viwanda. Chama katika miaka mitano ijayo, kinalenga kuimarisha ubora wa elimu katika ngazi zote kwa kuzingatia falsafa ya kujitegemea yenye kuendana na mazingira ya nchi yetu, hususan elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Ili kutimiza azma hiyo, Chama kitaelekeza Serikali kutekeleza afua zifuatazo:-**

- (a) Kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu pamoja na kuhifadhi na kuendeleza mazingira ya shule hizo;
- (b) Kushirikiana na sekta binafsi, asasi za kiraia zikiwemo taasisi za dini katika kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu na ujuzi; na
- (c) Kuimarisha idara na taasisi za udhibiti ubora ikiwemo NACTE, TCU na Idara ya Udhibiti Ubora ili kuhakikisha kwamba kiwango cha ubora wa elimu itolewayo nchini kinazingatiwa na kuimarika; na
- (d) Kuimarisha misingi ya elimu ya kujitegemea katika ngazi zote za elimu.

***Elimumsingi hadi Kidato cha Sita***

- (a) Kuendeleza mpango wa kutoa elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari ili kuwawezesha vijana wenye sifa kuanza na kuendelea na masomo bila kikwazo;
- (b) Kuhakikisha kuwa kila shule ya msingi inatoa elimu ya awali kwa ufanisi katika mazingira na miundombinu iliyoboreshwa;
- (c) Kuimarisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum;
- (d) Kuimarisha ufundishaji wa masomo ya sayansi yakiwemo Hisabati, Fizikia, Kemia na Baiolojia na kuongeza upatikanaji wa walimu wa kufundisha masomo hayo;
- (e) Kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji wa masomo ya stadi za kazi na lugha ikiwemo lugha za alama katika elimu ya msingi;
- (f) Kuimarisha masomo ya maadili, uzalendo wa kitaifa na uraia kwa shule zote nchini;



- (g) Kuhakikisha mfumo mzima wa elimu unajengwa kwa umadhubuti na kuzingatia utamaduni, mila na desturi za kitanzania;
- (h) Kuimarisha ufundishaji wa masuala yote mtambuka katika ngazi zote za elimu, ikijumuisha UKIMWI/VVU, mabadiliko ya hali ya hewa, utunzaji wa mazingira, masuala ya jinsia n.k;
- (i) Kuimarisha shule zote za michepuo ikijumuisha Elimu ya Ufundi, Kilimo na Biashara kwa kuzipatia vifaa vya kisasa;
- (j) Kuongeza nafasi za wanafunzi wanaosoma masomo ya Sayansi na Hisabati katika shule za Sekondari hususan watoto wa kike;
- (k) Kuboresha mbinu na mikakati ya utoaji wa elimu ya watu wazima nchini ili iweze kuchangia katika ujenzi wa Taifa;
- (l) Kuboresha mbinu na mikakati ya utoaji wa elimu nje ya mfumo rasmi (MEMKWA) ili kuwawezesha waliokosa fursa au kupoteza sifa za kusoma katika mfumo rasmi kuweza kutimiza ndoto zao za kielimu na kuchangia ipasavyo katika ujenzi wa Taifa;
- (m) Kuongeza fursa za utoaji wa elimu ya ualimu katika ngazi ya stashahada hususan walimu wa sayansi, lugha na ufundi ili kuzalisha walimu wa kutosha kulingana na mahitaji;
- (n) Kuimarisha ubora wa walimu wa shule za msingi kwa kuanzisha Stashahada ya Ualimu wa shule za msingi;
- (o) Kuendelea kuboresha elimu ya michezo katika vyuo vya ualimu;
- (p) Kuhuisha mitaala ya elimumsingi na sekondari kidato cha tano na sita ili kuendana na mahitaji ya kujenga ujuzi, maarifa ya kujitegemea na weledi utakaowawezesha wahitimu kumudu na kufanya kazi mbalimbali za kuajiriwa na kujiajiri; na
- (q) Kuimarisha matumizi ya TEHEMA katika kuimarisha kujifunza na kufundisha katika vyuo vya ualimu.

***Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi***

- (a) Kuimarisha utoaji wa elimu ya mafunzo ya ufundi kwa kuwajengea uwezo wakufunzi/wahadhiri na kuvipatia vyuo vifaa vya kisasa ili kuzalisha wataalam wenye kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi;
- (b) Kuhuisha mitaala na kuanzisha programu kulingana na mahitaji ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ambayo yanaendana Mapinduzi ya Nne ya Viwanda;



- (c) Kuongeza udahili wa wanafunzi wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi;
- (d) Kuimarisha udahili wa wanafunzi wa stashahada za ufundi kwa lengo la kuimarisha uwiano wa idadi za wahandisi, mafundi na mafundi mchundo ili kuongeza ufanisi katika sekta za ujenzi na uzalishaji viwandani;
- (e) Kuweka mazingira wezeshi kwa kujenga na kukarabati vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuongeza idadi ya wahitimu;
- (f) Kuanzisha utaratibu wa kuwakopeshwa vifaa na mitaji kwa masharti nafuu wanafunzi wanaohitimu mafunzo ya ufundi;
- (g) Kujenga vyuo viwili vya elimu ya mafunzo ya ufundi vya ngazi ya kati (*polytechnics*) ili kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya ufundi; na
- (h) Kuboresha utekelezaji wa utambuzi na urasimishaji wa ujuzi unaopatikana nje ya mfumo rasmi wa utoaji elimu.

#### ***Elimu ya Juu***

- (a) Kuongeza rasilimaliwatu katika taasisi za elimu ya juu, ikijumuisha wahadhiri, wakutubi, wataalam wa maabara na karakana ili kukidhi mahitaji ya viwango na ubora wa elimu;
- (b) Kuboresha na kuongeza miundombinu na vifaa vya kujifunza, kufundisha na kutafiti ili kuongeza uwezo wa Taifa wa kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi;
- (c) Kuhuisha mitaala na kuanzisha programu kulingana na mahitaji ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili wahitimu wawe na stadi stahiki za kumudu kufanya kazi mbalimbali za kuajiriwa na kujiajiri na hasa kwa kuzingatia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda;
- (d) Kuimarisha mafunzo ya lugha kwa kutoa programu maalum ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za kigeni kwa ajili ya kuzalisha wataalam na wakalimani wa Kiswahili wenye viwango vya kimataifa;
- (e) Kuainisha na kutambua maeneo ya umahiri (*centres of excellence*) katika vyuo na taasisi za elimu ya juu za Serikali na kuziwezesha kutoa mchango stahiki katika maendeleo ya Taifa;
- (f) Kuongeza udahili katika Elimu ya Juu kwa makundi yote yakiwemo wanafunzi kutoka nje ya nchi;



- (g) Kuimarisha mfumo wa malezi kwa wanafunzi vyuoni kwa kuwapa stadi za maisha na huduma za ushauri nasaha ili kupata wahitimu wenye maadili; na
- (h) Kuimarisha na kuboresha mfumo wa ugharamiaji wa elimu ya juu, ikiwemo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, ili kuhakikisha wanafunzi wengi zaidi wenye uhitaji na sifa stahiki wanapata fursa ya kujiunga na elimu ya juu.

### **Afya**

81. CCM inatambua kuwa huduma za afya ni muhimu katika kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya bora ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za maendeleo ya nchi. Kutokana na umuhimu huo, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), Serikali imefanikiwa kuimarisha afya na ustawi wa Watanzania katika maeneo mbalimbali kwa kuhakikisha kuwa huduma bora za afya zinapatikana nchini kote na kwa makundi yote ikiwemo kuendelea kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto bure. Pamoja na mikakati mingine, hatua hii imefikiwa pia kwa kuimarisha mazingira ya sekta binafsi kushiriki katika utoaji wa huduma za afya kwa wananchi. Mafanikio yaliyopatikana katika maeneo mbalimbali kwa kipindi hicho ni pamoja na:-

#### ***Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Kutolea Huduma ya Afya***

- (a) Idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka 7,014 mwaka 2015 hadi 8,783 mwaka 2020, ambapo:-
  - (i) Zahanati zimeongezeka kutoka 6,044 mwaka 2015 hadi 7,242 mwaka 2020;
  - (ii) Vituo vya afya vimeongezeka kutoka 718 mwaka 2015 hadi kufikia 1,205 mwaka 2020;
  - (iii) Hospitali za halmashauri zimeongezeka kutoka 77 mwaka 2015 hadi 148 mwaka 2020. Idadi hiyo inajumuisha hospitali mpya za halmashauri 71 zilizojengwa. Aidha, Serikali imeendelea kuboresha utoaji huduma kwa kuweka dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na wataalam wenye ujuzi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya; na
  - (iv) Kuanza kwa ujenzi wa Hospitali ya Uhuru inayojengwa Chamwino mkoani Dodoma kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma za afya.
- (b) Hospitali 23 za rufaa za mikoa zimekarabatiwa katika vyumba vya upasuaji, wodi za kulaza wagonjwa, jengo la wagonjwa wa nje (OPD) na wodi za wazazi na watoto na kuwekewa vifaa vya kisasa vya upasuaji na maabara; Hospitali hizo ni pamoja na Mount Meru, Dodoma, Temeke, Ilala, Mwananyamala, Iringa, Kagera, Mawenzi,



Sokoine, Ligula, Bombo, Manyara, Mara, Maweni, Mbeya, Sekou Toure, Shinyanga, Singida, Songea, Sumbawanga, Tabora, Temeke na Tumbi Kibaha;

- (c) Kujengwa kwa Hospitali za Rufaa katika mikoa mitano mipya ya Njombe, Geita, Simiyu, Songwe na Katavi kwa lengo la kusogeza huduma za rufaa karibu na wananchi;
- (d) Ujenzi, ukarabati na upanuzi umefanyika katika vyuo vya mafunzo ya afya 13. Aidha, hospitali za rufaa 10 zinazotumika kutoa mafunzo zilifanyiwa ukarabati wa miundombinu ya kutolea mafunzo ikiwemo ukarabati wa mabweni, ofisi pamoja na ununuzi wa samani;
- (e) Kuunganishwa kwa vyuo 37 vilivyopo katika maeneo ya karibu na kuwa vyuo tisa na hivyo idadi ya vyuo vya Serikali kupungua kutoka 77 hadi 43 kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi wa utoaji mafunzo ya afya;
- (f) Kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali ya Mloganzila na kuanza kutoa matibabu ya ubingwa bobezi kwa wagonjwa ikiwemo huduma za upasuaji mkubwa ikiwa ni pamoja na upasuaji wa ubongo, kuweka vifaa vya usikivu na upandikizaji wa uloto (*Borne Marrow Transplant*);
- (g) Kuendelea na ukarabati wa Hospitali ya Muhimbili na Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) ili ziweze kutumika kama Hub zitakazounganishwa na Hospitali nyingine nchini;
- (h) Kuimarisha na kuboresha mifumo ya utoaji huduma kwa kufanya ununuzi wa mtambo wa upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu (*Angio Suite*) na kuutumia katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili pamoja na ununuzi wa PET Scan Machine kwa Taasisi ya Saratani Ocean Road;
- (i) Kuboresha huduma katika hospitali ya rufaa ya kanda ya nyanda za juu kusini - Mbeya kwa; kuboresha na kukamilisha ujenzi wa jengo la mapokezi, katika kitengo cha wazazi Meta, jengo la huduma za afya ya uzazi na mtoto (RCH) linapanuliwa kwa kuongeza vyumba vinne, wodi ya watoto, jengo la *Radiology, Infusion Production*; jengo la daraja la kwanza (*Grade I*), jengo la huduma za dharura na ukarabati wa jengo la huduma za uzazi na mtoto;
- (j) Kuboresha huduma katika hospitali ya rufaa ya kanda ya ziwa Bugando kwa: kujenga na kukarabati majengo ya kliniki ya wagonjwa wa nje, jengo la kutolea tiba ya saratani na kliniki ya wanachama wa bima ya afya;
- (k) Kuboresha huduma katika hospitali ya rufaa ya kanda ya kaskazini KCMC kwa: kukamilisha ujenzi wa jengo la kliniki kwa ajili ya wagonjwa wa saratani, jengo la tiba ya saratani kwa njia ya dawa (*chemotherapy*), na kuboresha jengo la huduma za dharura, jengo la





dawa na jengo la maabara. Aidha, huduma za kibingwa zimeboreshwa kama vile huduma za: Kusafisha figo; Wagonjwa walioungua moto; Tiba ya saratani; na Huduma za wagonjwa mahututi (ICU); na

- (l) Kuboresha huduma katika Hospitali ya Kanda ya Kusini - Mtwara kwa kuendelea na ujenzi kwa awamu ya pili, kukamilisha jengo la wagonjwa wa nje (OPD) na majengo mengine ya kutolea huduma.

***Mazingira Bora ya Sekta Binafsi ya Huduma za Afya***

- (a) Serikali imeendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya nchini, ambapo:-
- (i) Zahanati binafsi zimeongezeka kutoka 1,402 mwaka 2015 hadi kufikia 2,106 mwaka 2020;
  - (ii) Vituo vya afya binafsi zimeongezeka kutoka 231 mwaka 2015 hadi kufikia 323 mwaka 2020; na
  - (iii) Hospitali binafsi zimeongezeka kutoka 109 mwaka 2015 hadi kufikia 173 mwaka 2020.

***Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba***

- (a) Kuboresha huduma katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando kwa kufanya ununuzi wa vifaa tiba ikiwa ni pamoja na mashine ya tiba ya mionzi inayoitwa *brachy therapy*, mtambo wa kusafisha damu (*renal dialysis*), *CT-Scan* na mtambo wa kuzalisha maji tiba;
- (b) Kuboresha huduma katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini - KCMC kwa: kununua mashine za kisasa za uchunguzi wa magonjwa ikiwa ni pamoja na vifaa vya *MRI*, *CT-Scan* yenye ukubwa wa *Slice* 128;
- (c) Kusambazwa kwa vyandarua 47,382,746 vyenye dawa kwa wananchi bila malipo katika mikoa yote nchini mara mbili zaidi ya lengo la kugawa vyandarua 22,360,386 ifikapo mwaka 2020. Hii imewezesha maambukizi kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kupungua kutoka asilimia 14 mwaka 2015 hadi asilimia saba mwaka 2020;
- (d) Kusambazwa kwa jumla ya lita 586,420 za viuadudu vya kuangamiza viluwiluwi vya mazalia ya mbu katika halmashauri zote nchini. Aidha, lita 60,000 za viuadudu, pampu za kunyunyizia zipatazo 1,000 na vifaa vingine muhimu vimenunuliwa na kusambazwa katika halmashauri za mikoa mitano yenye kiwango kikubwa cha maambukizi ya malaria (Kagera, Geita, Mwanza, Kigoma na Mara). Vilevile, nyumba 501,587 zimepuliziwa dawa (*Indoor Residual Spray*) katika halmashauri 16 za mikoa hiyo;



- (e) Kununuliwa kwa jumla ya dozi za ALU 58,427,970 na vitepe vya vitendanishi vya Malaria (mRDT) 79,171,425 na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma ya afya kulikowezesha upimaji na matibabu sahihi ya Malaria na kupunguza idadi ya vifo vinavyotokana na ugonjwa huo;
- (f) Kununuliwa kwa mashine mpya za tiba ya mionzi za LIN-AC na CT simulator katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road na kuwezesha jumla ya wagonjwa 1,082 kupata huduma za kupima CT-Scan kufikia mwaka 2020;
- (g) Kukamilika kwa ujenzi wa maghala ya kisasa ya kuhifadha dawa katika mikoa ya Tanga, Tabora, Mtwara na Dar es Salaam;
- (h) Kuongezeka kwa bajeti ya dawa kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015 hadi kufikia bilioni 270 mwaka 2020. Hii imewezesha upatikanaji wa dawa muhimu kuongezeka kutoka asilimia 42 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 94.5 mwaka 2020;
- (i) Kuongezeka kwa idadi ya Washitiri ambapo Mshitiri mmoja mmoja amesajiliwa kila mkoa na hivyo kufanya jumla ya Washitiri kufikia 26 nchi nzima; ili kuondokana ukosefu wa dawa, vifaa, vifaa tiba kwenye vituo vya kutolea huduma za afya;
- (j) Kuongezeka kwa huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU kwa wananchi bila malipo mijini na vijijini ambapo idadi walionufaika imeongezeka kutoka 10,577,881 mwaka 2017 hadi kufikia watu 11,008,001 mwaka 2020. Aidha, vituo vya kutolea huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU vimeongezeka kutoka vituo 5,555 mwaka 2015 hadi vituo 6,596 mwaka 2020; na
- (k) Uanzishwaji wa huduma za uchunguzi kupitia X - ray, Ultra Sound zimeanza kutolewa kwenye vituo vya afya 125.
- Watumishi wa Kada ya Afya**
- (a) Kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa sekta ya afya kwa kuhakikisha kuwa kila kituo cha afya au zahanati inayojengwa inakuwa na nyumba za watumishi ambapo hadi mwaka 2020, jumla ya nyumba 784 zimejengwa;
- (b) Kuongezeka kwa watumishi wa sekta ya afya kutoka 86,152 mwaka 2015 hadi kufikia 100,631 mwaka 2020 ambapo watumishi 18,094 sawa na asilimia 18 ni wa sekta binafsi;
- (c) Kuimarika kwa udahili kwa wanafunzi katika vyuo mbalimbali vya afya nchini ambapo jumla ya wanafunzi 25,077 mwaka 2020 wamedahiliwa ikiwa ni zaidi ya lengo la kudahili wanafunzi 15,000. Kati ya hao maafisa tabibu waliodahiliwa walikuwa 6,670, wauguzi 1,241 na wataalam wengine 17,166; na



- (d) Kujenga uwezo wa kitaalam katika sekta ya afya kwa kuwezesha jumla ya watumishi 923 kupata mafunzo ndani na nje ya nchi katika ngazi ya shahada na shahada ya Uzamili katika kipindi cha 2015 hadi 2020. Aidha, jumla ya wataalam wa kigeni 241 kutoka mataifa mbalimbali washirika wa Tanzania walipata ajira katika taasisi mbalimbali za sekta ya afya hapa nchini katika kipindi hicho.

### **Matibabu ya Kibingwa**

82.

Huduma za kibingwa zimeboreshwa ili kuwawezesha wananchi wengi kupata huduma hizo nchini na kuokoa fedha zilizokuwa zinatumiwa kugharamia huduma hizo nje ya nchi. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

- (a) Kuimarishwa kwa matibabu ya ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa:-
- (i) Kuanzisha huduma ya kupandikiza Figo, ambapo wagonjwa 51 wamepandikizwa Figo hadi kufikia mwaka 2020;
  - (ii) Kuanzisha huduma ya kupandikiza vifaa vya usikivu kwa watoto, ambapo watoto 30 wameshapata huduma hiyo hadi kufikia mwaka 2020; na
  - (iii) Kuanza kwa huduma ya radiolojia, ambapo watu 133 walipatiwa huduma hiyo hadi kufikia mwaka 2020.
- (b) Kuimarika kwa huduma ya matibabu ya kibingwa katika Taasisi ya Mifupa (MOI):-
- (i) Katika kipindi cha miaka mitano wagonjwa 6,899 wamefanyiwa upasuaji (ikiwemo kubadilisha nyonga 188, goti 167, upasuaji wa goti kwa kutumia matundu 107, upasuaji wa mfupa wa kiuno 75, upasuaji wa uti wa mgongo 337, Femur 511, ubongo 239); na
  - (ii) Kukamilika kwa miundombinu ya chumba maalum (*high dependancy unit - HDU*) pamoja na kuweka vitanda vipya vya kisasa 16 na *monitor* zake, ujenzi wa chumba maalum cha kisasa kwa ajili ya kufanya matibabu ya ubongo kupitia mishipa ya damu na ujenzi wa chumba cha tiba maalum kwa njia ya mtandao na kutoa matibabu ya kifafa kwa njia ya upasuaji (*epilepsy*);
- (c) Kuimarishwa kwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kwa:-
- (i) Kuanzisha na kuboresha huduma za upasuaji kwa tundu dogo kwa wagonjwa 2,742 (*catheterization laboratory, stents, percutaneous intervention, device closure, pacemaker*); na
  - (ii) Kuongezeka kwa wagonjwa waliofanyiwa upasuaji wa



kufungua kifua (*open heart surgery*) kutoka 290 mwaka 2015 hadi 987 mwaka 2020.

- (d) Kuimarika kwa matibabu ya kibingwa katika Hospitali ya Benjamin Mkapa - Dodoma kwa kuanzisha na kuboresha huduma ya upandikizaji wa Figo, ambapo hadi kufikia mwaka 2020 jumla ya wagonjwa saba wamepata huduma hiyo;
- (e) Kujengwa kwa majengo ya huduma za dharuara (EMD) katika hospitali za rufaa za mikoa ya Tabora (Kitete), Rukwa, Mara, Mbeya, Iringa, Kilimanjaro (Mawenzi), Ruvuma na Tanga (Bombo); na
- (f) Kuunganishwa kwa hospitali nne za rufaa (Amana, Mbeya, Muhimbili na Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*) kwenye mfumo wa Tiba Mtandao (*Telemedicine*) kwenye eneo la magonjwa ya Saratani (*Oncology*) na uchunguzi wa magonjwa.

**83. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kutoa kipaumbele katika sekta ya afya kwa kuwa inagusa maisha ya Watanzania na ustawi wa Taifa letu. Lengo la Chama ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya na siha bora ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za ujenzi wa Taifa na kuboresha maisha yao. Katika kipindi hicho, Chama kitasimamia Serikali katika kutekeleza yafuatayo:**

- (a) Kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto na kuzitoa bila malipo ili kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano;
- (b) Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vifaa saidizi na vitendanishi kulingana na mahitaji katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini;
- (c) Kuweka mazingira kwa wawekezaji/sekta binafsi kujenga viwanda vya kuzalisha dawa, vifaa, vifaa tiba, vifaa saidizi na vitendanishi kwa kutumia malighafi zinazopatikana ndani ya nchi ili kupunguza mzigo kwa Serikali wa kuagiza mahitaji hayo kutoka nje ya nchi;
- (d) Kujenga na kuimarisha vituo vya kutolea huduma za afya ili viweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. Hadi kufikia 2025 Serikali itaongeza vituo vya kutolea huduma za afya kwa asilimia 20 ya vituo 8,446 vilivyopo sasa; vipaumbele vitawekwa katika ujenzi wa vituo vya afya na ukamilishwaji wa maboma kwa kuzingatia uwiano wa kijiografia, idadi ya watu na wingi wa magonjwa;
- (e) Kuimarisha mfumo wa bima ya afya nchini ikiwemo mifuko ya bima za afya (NHIF na CHF) ili kufikia lengo la Serikali la kuwa na bima ya afya kwa wananchi wote;



- (f) Kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa hospitali 98 za halmashauri;
- (g) Kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika hospitali 28 za rufaa ngazi ya mkoa, hospitali za halmashauri za wilaya 125 kwa kukamilisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma (majengo, vifaa na watumishi);
- (h) Kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma katika hospitali za rufaa za kanda saba zilizopo na kuanza ujenzi katika kanda ambazo hazina hospitali;
- (i) Kuongeza udahili wa wanafunzi wa kada mbalimbali za afya kufikia 25,000 katika vyuo vya afya kwa kuimarisha miundombinu, na mfumo wa mafunzo wa kada hizo katika vyuo vya afya nchini;
- (j) Kuimarisha mfumo wa mafunzo ya wataalam bingwa na bobezi katika sekta ya afya ikiwa ni pamoja na kutumia utaratibu wa mafunzo ya kibingwa na bobezi wakiwa kazini (*Fellowship Training Programme*);
- (k) Kushirikiana na vyama vya kitaaluma vya kada za afya katika kusimamia uzingatiaji wa maadili na weledi katika utendaji wa watumishi wa afya nchini;
- (l) Kuajiri wataalam wa kutosha wenye ujuzi na kuboresha mazingira ya kazi ya watumishi wa sekta ya afya;
- (m) Kuhamasisha jamii umuhimu wa matumizi ya vyandarua vilivyowekwa dawa na upuliziaji wa viatilifu ukoko katika kuta za nyumba;
- (n) Kutekeleza mpango wa kuangamiza viluwiluwi vya mbu kwa kutumia viudadu vya kibaiolojia na usafi wa mazingira katika halmashauri ili kupunguza magonjwa yatokanayo na wadudu dhurifu;
- (o) Kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kupambana na magonjwa ya kuambukiza (Covid - 19, VVU na UKIMWI, TB, Homa ya Ini na Malaria) na yasiyoambukizwa (Shinikizo la damu, Kansa na Figo) pamoja na kununua na kusambaza dawa zake na kuhamasisha upimaji wake ili wananchi waweze kutambua hali zao na kuchukua hatua stahiki;
- (p) Kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi kufikia viwango vya kimataifa ili kukidhi mahitaji ya hapa nchini na wagonjwa kutoka nje ya nchi wanaohitaji huduma za tiba;
- (q) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya ikiwemo tiba mtandao, mafunzo, utawala, usimamizi wa fedha, dawa na bidhaa zote za dawa pamoja na uboreshaji wa ukusanyaji na matumizi ya takwimu za afya katika hospitali, hospitali za halmashauri za wilaya, vituo vya afya na zahanati;



- (r) Kumarisha maghala ya kutunzia dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi ili kuhakikisha vinapatikana kwa wakati karibu na wananchi. Aidha, maghala mapya matano yatajengwa katika mikoa ya Kagera, Simiyu, Ruvuma, Mtwara na Iringa;
- (s) Kusimamia tafiti za kimkakati za afya kwa ajili ya kupata suluhisho la matatizo ya kiafya yanayowakabili wananchi na kuhakikisha mipango mahsusi na maamuzi ya kiseru yanafanywa kwa mujibu wa taarifa zenye viwango vya ubora;
- (t) Kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini mkoani Lindi na Hospitali ya Uhuru Chamwino mkoani Dodoma;
- (u) Kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya na kuzifanya rafiki kwa wanawake, wanaume na vijana ikiwemo kutoa huduma ya msingi ya dharura ya afya ya uzazi na mtoto, huduma tembezi na mkoba;
- (v) Kuimarisha miundombinu na kujenga vituo vya damu salama katika mikoa mitano nchini ili kuvingejea uwezo wa kukusanya, kupima na kusambaza damu katika vituo vya damu salama kulingana na mahitaji;
- (w) Kutoa elimu na kuhamisha wananchi kuhusu kinga, kudhibiti na kuzuia Magonjwa Yasiyo ya Kuambukizwa (NCD), magonjwa mapya adimu na yasiyopewa kipaumbele kwa ngazi zote;
- (x) Kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za macho, afya ya kinywa na meno, koo, masikio, pua na vifaa tiba na watumishi wenye ujuzi katika ngazi zote za kutolea huduma za afya;
- (y) Kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi katika utoaji wa huduma za afya;
- (z) Kuimarisha mfumo wa upelekaji wa fedha moja kwa moja kwenye akaunti za vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi kwa kushirikisha wadau wote wanaotekeleza afua za afya;
- (aa) Kuimarisha mfumo wa mshitiri ili kuhakikisha kuwa bidhaa za afya zinapatikana kwa uhakika na kwa gharama nafuu katika ngazi zote za huduma; na
- (ab) Kuimarisha huduma za dharura katika Hospitali ya Kanda ya Benjamini Mkapa ili kumudu ongezeko la mahitaji ya huduma kutokana na Serikali kuhamishia Makao Makuu ya nchi Dodoma.





84.

### Mapambano Dhidi ya Magonjwa ya Mlipuko ikiwemo Corona

**Magonjwa ya mlipuko na yanayosambaa kwa kasi ni hatari kwa maisha ya wananchi na ulinzi na usalama wa Taifa. CCM itahakikisha nchi inakuwa na utayari wakati wote wa kuzuia, kudhibiti na kukabiliana na majanga haya kwa kushirikiana na wadau wengine. Janga la Corona lililoikumba dunia ikiwemo Tanzania limetupa funzo kubwa kuhusu umuhimu wa kujipanga kikamilifu katika kukabiliana na majanga ya aina hii punde yanapojitokeza. Katika kufikia azma hii, CCM itahakikisha Serikali inatekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuweka na kuimarisha mifumo na miundombinu ya kutambua, kudhibiti na kukabiliana na magonjwa ya mlipuko na yanayoenea kwa kasi;
- (b) Kuimarisha mpango wa Taifa wa utayari wa kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, ajali na majanga kwa kuboresha huduma za dharura na uokoaji ikiwemo miundombinu, na vitendea kazi;
- (c) Kuimarisha na kujenga uwezo wa kufanya utafiti kuhusu magonjwa ya mlipuko katika taasisi ya NIMR, vyo vikiu na taasisi nyingine za utafiti nchini;
- (d) Kuanzisha kituo kikubwa cha utafiti na uchunguzi wa mimea dawa na kuanzisha kiwanda cha kimkakati cha kuzalisha dawa zitokanazo na mimea yetu;
- (e) Kuimarisha uwezo wa wataalam wetu katika kuzuia na kutibu magonjwa ya mlipuko kwa kupatiwa vifaa na mafunzo ndani na nje ya nchi; na
- (f) Kujenga na kuimarisha maabara za uchunguzi wa magonjwa ya mlipuko, vituo vya kisasa vya kuwatenga wahisiwa (*isolation centres*) na kutoa tiba kwa wagonjwa.

### Lishe

85.

Lishe bora ni muhimu katika kuhakikisha Taifa linakuwa na jamii yenye nguvu kazi imara na uwezo mkubwa wa kuelewa na kukabiliana na mazingira yake. Kwa kuzingatia umuhimu huo Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kuisimamia Serikali kuandaa na kutekeleza mikakati na mipango mbalimbali ya kuongoza utekelezaji wa afua za lishe nchini kama vile Mpango Jumuiishi wa Taifa wa Utekelezaji wa Masuala ya Lishe (2016 - 2021). Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- (a) Kuimarisha huduma za lishe za wajawazito na wanawake wanaonyonyesha, vijana balehe, watoto wachanga kwa kuhakikisha elimu sahihi ya lishe inawafikia;
- (b) Kuongeza uwekezaji katika masuala ya lishe kwa halmashauri nchini kutenga shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato ya ndani ili zitumike kutekeleza afua za lishe;



- (c) Kuimarisha usimamizi wa masuala ya lishe kwa kuanzisha Kamati Elekezi za Kitaifa ambazo zimesaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa afua za lishe;
- (d) Kuimarishwa kwa uratibu wa masuala ya lishe katika ngazi ya Kitaifa, Mkoa na Halmashauri kwa kuanzisha kitengo cha lishe katika Ofisi ya Rais -TAMISEMI;
- (e) Kuimarisha huduma za matibabu ya utapiamlo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na jamii ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo watoaji wa huduma hizo na kuhakikisha upatikanaji wa mahitaji mfano chakula dawa na vifaa vya kutathmini ya hali ya lishe.

86.

**Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuhakikisha kuwa lishe bora inaendelea kuwa kipaumbele ili wananchi waweze kuwa na afya bora na maisha mazuri, na pia waweze kuchangia kuwepo kwa nguvu kazi imara na yenye tija kwa Taifa ambayo inaweza kushiriki kwenye shughuli za uzalishaji na hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi. Ili kufikia malengo hayo, Chama kitaelekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kutekeleza mikakati ya kupunguza idadi ya watoto chini ya miaka mitano wenye udumavu na ukondefu kwa kasi kubwa zaidi;
- (b) Kufanya tathmini ya kila mwaka kuhusu hali ya lishe na tathmini maalum kila baada ya miaka mitano na hatimaye kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha kwamba Taifa linakuwa na wananchi wenye afya bora na uwezo wa kuchangia ipasavyo katika shughuli za maendeleo ya Taifa lao;
- (c) Kuhakikisha hakuna ongezeko la uzito uliozidi kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano; na kupunguza idadi ya watoto wanaozaliwa na uzito pungufu yaani chini ya uzito wa kilogram 2.5 ili iwe chini ya asilimia 50;
- (d) Kupunguza kwa asilimia 50 viwango vya upungufu wa damu kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa yaani miaka 15 - 49; na kuongeza kiwango cha unyonyeshaji wa maziwa ya mama pekee kwa watoto chini ya miezi sita ili ifikie zaidi ya asilimia 50;
- (e) Kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu na mazao ya kilimo yenye viini lishe vingi, mbogamboga, matunda, mazao ya mifugo na uvuvi pamoja na uhamasishaji na uelimishaji wa ulaji wa vyakula hivyo;
- (f) Kuimarisha uhusiano wa wadau wa lishe na sekta binafsi katika kuzalisha bidhaa za vyakula viliyoongezewa virutubishi;



- (g) Kupanua wigo wa uelimishaji na uhamasishaji wa masuala ya lishe kupitia majukwaa mbalimbali ili kuelimisha juu ya mitindo bora ya maisha na kuzuia ongezeko la uzito uliozidi na kiriba tumbo; na
- (h) Kuongeza na kuwajengea uwezo wataalam wa afya kwa ajili ya kutoa huduma za lishe katika ngazi za mikoja, halmashauri pamoja na vituo vya kutolea huduma za afya.

### **Mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI**

87. Chama Cha Mapinduzi kinatambua kuwa VVU na UKIMWI una madhara makubwa kwa jamii na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Chama kinatambua kuwa mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI ni endelevu na yanahitaji juhudi za pamoja. Katika kipindi kilichopita msisitizo uliwekwa katika jitihada za kupunguza kasi ya maambukizi mapya, kupunguza unyanyapaa na kuendelea kutoa elimu ya Kinga Dhidi ya Maambukizi ya VVU. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), mafanikio yaliyopatikana katika kupambana na VVU na UKIMWI ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kupungua kwa kiwango cha maambukizi ya VVU na UKIMWI kwenye jamii kutoka asilimia 5.7 mwaka 2008 hadi asilimia 4.7 mwaka 2017 ambapo, kwa wanawake, kimeshuka asilimia 7.0 hadi 6.2 na wanaume kutoka asilimia 5.7 hadi 3.1;
- (b) Kupungua kwa vifo vitokanavyo na UKIMWI kwenye jamii kutoka vifo 200,000 kwa mwaka vilivyokisiwa mwaka 1990 hadi vifo 33,800 mwaka 2017;
- (c) Kupungua kwa maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT); na
- (d) Hadi kufikia Septemba 2018, WAVIU 1,068,282 walikuwa wanapata dawa za kufubaza VVU, ikilinganisha na WAVIU 575,850 mwaka 2012.

88. **Katika kipindi cha miaka mitano, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuisimamia Serikali kuendeleza mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kwa kuzingatia mikakati iliyoainishwa katika Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NMSF IV 2018/19 - 2022/23) kwa kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kuendeleza mikakati ya kudhibiti maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI, ikwemo maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto, Kifua Kikuu, Ukoma na Homa ya Ini;
- (b) Kuandaa mkakati endelevu wa kifedha kwa ajili ya kuimarisha Mfuko wa Udamini wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*AIDS Trust Fund - ATF*) ili kuwahudumia vyema waathirika;
- (c) Kupunguza kasi ya maambukizi mapya katika jamii kwa kuimarisha mikakati ya kupunguza maambukizo mapya kwa watoto na makundi



maalum ambayo yapo katika mazingira hatarishi zaidi katika kuambukiza na kuambukizwa virusi vya UKIMWI (VVU);

- (d) Kuongeza programu zenye ubunifu zinazozingatia umri na jinsia zinazoshughulikia utambuzi wa hatari za maambukizo ya VVU na mikakati ya kupunguza madhara kwa kutumia nadharia sahihi za kubadili tabia;
- (e) Kutumia uhamasishaji jamii wenye ufanisi ikiwemo redio za jamii kuibua uhitaji wa huduma za kinga, upimaji, matunzo na matibabu;
- (f) Kuimarisha ushiriki wa jamii kuwawezesha kushiriki katika kupanga, kutekeleza na kufuatilia afua za kijamii katika mazingira yao kwenye mapambano dhidi ya UKIMWI;
- (g) Kuhuisha na kujumuisha masuala ya UKIMWI (*mainstreaming*) kwenye taasisi na sekta zote ambazo zina mazingira yenye vichochezi vikuu vya UKIMWI, zikiwemo ujenzi, uchukuzi, uvuvi, madini;
- (h) Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya VVU na UKIMWI ili kupunguza maambukizi na unyanyapaa; na
- (i) Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa huduma za UKIMWI nchini kote ili kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwenye jamii.

### **Ustawi wa Jamii**

89. Chama Cha Mapinduzi kinaamini kuwa, kuinua na kuimarisha ustawi wa maisha ya mtu, familia na makundi yenye mahitaji maalum katika jamii ni nyenzo muhimu kwa mustakabali wa maendeleo endelevu na jumuishi. Kwa kutambua umuhimu huo, katika kipindi cha 2015 - 2020, mafanikio mengi yalipatikana ikiwemo ustawi wa wazee, watoto, familia na watu wenye ulemavu. Baadhi ya mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:-

### **Ustawi wa Wazee**

90. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Chama Cha Mapinduzi kiliendelea kuisimamia Serikali kutekeleza Sera ya Taifa ya Wazee ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- (a) Kuongezeka kwa idadi ya wazee waliopatiwa vitambulisho vya kuwawezesha kupata matibabu bila malipo kutoka 213,025 mwaka 2015 hadi kufikia wazee 1,042,403 mwaka 2020;
- (b) Wazee na wasiojiweza 2,135 wanaoishi katika makazi 16 yanayomilikiwa na Serikali walipatiwa huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu kati ya mwaka 2015 na 2020;
- (c) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa Wazee kwa kuanzisha madirisha 2,335 ya kutolea huduma za afya kwa wazee katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini;



- (d) Kuanzishwa kwa mabaraza ya wazee 8,183 ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa haki kwa wazee;
- (e) Kudhibiti mauaji ya wazee kwa kutekeleza Mkakati wa Kutokomeza Mauaji ya Wazee; na
- (f) Kuboresha makazi ya wazee kwa kukarabati na kujenga miundombinu mipya katika makazi ya wazee ya Kolandoto (Shinyanga), Nunge (Dar es Salaam), Njoro (Kilimanjaro), Magugu (Manyara) na Fungafunga (Morogoro).

91. **Katika kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa wazee, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itaekekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kuimarisha huduma za matibabu bila malipo kwa wazee;
- (b) Kuimarisha huduma za msingi kwa wazee wasiojiweza nchini katika makazi ya wazee yanayomilikiwa na kuendeshwa na Serikali pamoja na sekta binafsi;
- (c) Kukarabati na kujenga miundombinu katika makazi ya wazee;
- (d) Kuendeleza utekelezaji wa Mkakati wa Kutokomeza Ukatili na Mauaji ya Wazee;
- (e) Kutoa huduma za matunzo na kisaikolojia kwa wazee na watu wenye ulemavu;
- (f) Kuimarisha mabaraza ya wazee maeneo yote nchini; na
- (g) Kuongeza wigo wa mafao kwa wazee.

***Huduma za Watoto na Familia***

92. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Chama Cha Mapinduzi kiliendelea kuisimamia Serikali kutekeleza Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mtoto ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- (a) Kuimarisha hatua na mikakati ya kupambana na ukatili, unyanyasaji na udhalilishaji dhidi ya watoto ikiwemo kuimarisha kamati za ulinzi na usalama wa watoto katika maeneo yote nchini;
- (b) Kusimamia utoaji wa huduma ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali kwa watoto walio chini ya miaka mitano walio katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana ambapo vituo vimeongezeka kutoka vituo 744 mwaka 2015 hadi kufikia vituo 1,538 mwaka 2020;
- (c) Kusajili makao ya watoto ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za msingi za malazi, chakula, malezi, matunzo, ulinzi, afya na elimu kwa watoto walio katika mazingira hatarishi nchini. Mpaka mwaka



2020 yamesajiliwa jumla ya makao ya watoto 179 na kutoa huduma kwa jumla ya watoto 24,145;

- (d) Kukuza upatikanaji wa haki kwa haraka kwa watoto walio katika mkinzano na sheria ambapo mahakama za watoto zimeongezeka kutoka mahakama tatu mwaka 2015 hadi mahakama 141 zilizopo mwaka 2020. Aidha, mashauri 743 ya watoto yaliripotiwa na kushughulikiwa katika mahakama za watoto kwenye mikoa 26;
- (e) Kuongeza wigo wa malezi mbadala kwa watoto kupitia huduma ya kuasili na malezi ya kambo ambapo watoto waliopata huduma hiyo wameongezeka kutoka watoto 85 mwaka 2015 hadi kufikia watoto 342 mwaka 2020;
- (f) Kuongezeka kwa utoaji wa huduma za matunzo kwa watoto ambapo mashauri ya watoto yaliyoshughulikiwa na kutolewa uamuzi yaliongezeka kutoka mashauri 11,938 mwaka 2016 hadi mashauri 27,806 mwaka 2019;
- (g) Kuwezesha kaya 1,000,000 zenye umasikini uliokithiri kupata mafao ya kujikimu na kushiriki miradi ya jamii kupitia Programu ya Taifa ya Kuondoa Umasikini (TASAF); na
- (h) Kuanza ujenzi wa kituo kikubwa jijini Dodoma cha kuwatengamanisha watoto walio katika mazingira hatarishi kwa kuwapatia ujuzi, maarifa na makuzi ili waweze kujitegemea.

**93. Katika kuimarisha huduma za ustawi kwa watoto na familia, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kuimarisha, kusimamia na kufuatilia utoaji wa huduma katika makao ya watoto yanayomilikiwa na Serikali na taasisi binafsi na kujenga makao mapya kwa ajili ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi;
- (b) Kuunda kamati za ulinzi wa wanawake na watoto na kuzijengea uwezo ili kuhakikisha kuwa zinatekeleza afua za ulinzi na usalama wa wanawake na watoto na kulinda maadili chanya ya Taifa;
- (c) Kusimamia, kufuatilia na kuimarisha uanzishaji na uendelezaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo na vituo vya maendeleo ya awali ya mtoto katika ngazi ya jamii ili kuboresha malezi na makuzi ya kila mtoto;
- (d) Kuimarisha huduma ya malezi mbadala na kuasili ili kuwezesha watoto walio katika mazingira hatarishi kupata huduma za msingi za kifamilia;





- (e) Kuboresha uratibu, kusaidia na kusimamia vituo vya kupokea na kuhifadhi watoto waliokataliwa na familia zao na waliokimbia vitendo vya ukatili;
- (f) Kuimarisha huduma kwa watoto walio katika mkinzano na sheria kwa kuboresha mahabusu za watoto; kuboresha utoaji wa huduma katika shule ya maadilisho Irambo inayotunza watoto waliohukumiwa kutokana na makosa ya jinai;
- (g) Kukamilisha ujenzi wa mahabusu ya watoto mkoani Mtwara na kujenga mahabusu katika kanda ambazo hazina huduma hiyo ili kuboresha mazingira ya mahabusu za watoto;
- (h) Kujenga shule ya maadilisho katika makao makuu ya nchi Dodoma na nyingine katika kanda ya ziwa;
- (i) Kusaidia vyombo vya usimamizi wa sheria kutoa haki kwa watoto walio katika mkinzano na sheria;
- (j) Kusimamia uanzishaji wa nyumba salama kwa ajili ya hifadhi ya waathirika wa ukatili wa kijinsia katika maeneo mbalimbali nchini;
- (k) Kuendeleza utekelezaji wa Programu ya Kijamii ya Marekebisho ya Tabia kwa Watoto;
- (l) Kuimarisha huduma za usuluhisho wa migogoro ya ndoa na matunzo kwa watoto;
- (m) Kuendeleza utoaji wa elimu na uhamasishaji kuhusu utokomezaji wa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto; na
- (n) Kuimarisha mabaraza ya watoto katika kujadili masuala yanayowahusu yakiwemo ya maadili na uzalendo ili kujenga jamii imara yenye uwezo na uzalendo wa kitaifa.

#### ***Watu Wenye Ulemavu***

94.

Ustawi wa watu wenye ulemavu ni muhimu katika kuleta maendeleo yenye uwiano katika jamii. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inasisitiza usawa na haki. Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kuwatambua watu wenye ulemavu na kuwapatia kipaumbele katika masuala mbalimbali ikiwemo ajira na uteuzi, ujenzi wa miundombinu rafiki, huduma bora za afya, uzazi salama, marekebisho na utengamao pamoja na kukomesha vitendo vya ukatili na unyanyasaji vinavyoshusha utu wao vikiwemo ubaguzi, uonevu pamoja na mila potofu. Katika kipindi hicho, mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- (a) Kuanzishwa kwa Baraza la Ushauri la Taifa kwa ajili ya watu wenye ulemavu pamoja na kuundwa kwa Kamati za kuhudumia watu



wenye ulemavu katika ngazi ya Taifa, Mikoa, Wilaya, Vijiji na Mitaa/Vitongoji. Hadi kufika mwaka 2020 Kamati katika ngazi hizo zilikuwa zimeundwa katika mikoa (26), halmashauri (130), vijiji (5,024) na mitaa/vitongoji (2,284);

- (b) Kutungwa kwa sheria ya kuwezesha kiuchumi makundi maalam ya kijamii ambapo watu wenye ulemavu wameendelea kuwezesha kiuchumi kwa kupatiwa asilimia mbili ya mapato ya ndani ya halmashauri zote 185 nchini. Hadi mwaka 2019, jumla ya shilingi bilioni 3.87 zilikuwa zimetolewa kwa vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali na utoaji wa huduma vya watu wenye ulemavu nchini kote;
- (c) Kutambua na kuwalinda watu wenye ulemavu dhidi ya vitendo vinavyoshusha utu na hadhi yao vikiwemo: ubaguzi, uonevu, ukatili na mila potofu;
- (d) Kuwawezesha watu wenye ulemavu kushiriki katika shughuli za kijamii zikiwemo kuongeza fursa za elimu kwa kuwapatia vifaa maalum;
- (e) Kuanzishwa kwa Kitengo maalum katika muundo wa Serikali kinachoshughulikia Masuala ya watu wenye ulemavu;
- (f) Kuhamasisha uwekaji wa miundombinu na mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu katika majengo ya umma na maeneo mengine ya huduma za jamii; na
- (g) Kusimamia na kutoa msaada wa kisaikolojia kwa watu wenye ulemavu.

95.

**Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaelekeza Serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi na rafiki kwa watu wenye ulemavu ili waendelea kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya Taifa kwa kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2004 pamoja na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya Mwaka 2010 ili kuendana na mabadiliko ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiteknolojia;
- (b) Kuvifufua vyo vya ufundi maalum ili viweze kuwapatia mafunzo maalum ya stadi za kazi na utengamano (*rehabilitation*) watu wenye ulemavu ili waweze kuajiriwa au kujiajiri;
- (c) Kuboresha rejista ya watu wenye ulemavu itakayotoa taarifa sahihi za watu wenye ulemavu ili kuimarisha utoaji wa huduma na misaada;
- (d) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuwawezesha kiuchumi watu wenye ulemavu ili waweze kutoa mchango wao katika maendeleo ya Taifa;



- (e) Kujenga, kusimamia na kuhimiza uwepo wa miundombinu rafiki ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanafikia huduma mbalimbali kwa urahisi;
- (f) Kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuwezesha watu wenye ulemavu kujijiri na kuajiriwa;
- (g) Kuimarisha udhhibiti wa vitendo vya kikatili na unyanyasaji vinavyoshusha utu na hadhi ya watu wenye ulemavu vikiwemo ubaguzi, uonevu na mila potofu; na
- (h) Kuboresha na kusimamia utoaji wa msaada wa kisaikolojia kwa watu wenye ulemavu.

96. Chama Cha Mapinduzi kinatambua umuhimu wa kuwaondolea hofu Watanzania wanapokuwa katika mazingira mbalimbali yaliyo hatarishi hususan wanapokabiliwa na magonjwa ambayo tiba zake zinahitaji mhusika kuwa vizuri Kisaikolojia. Hivyo kimekuwa kikiweka mkazo kwa Serikali kuweka wataoa ushauri nasaha na msaada wa Kisaikolojia kwa makundi mbalimbali. Katika kipindi miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaelekeza Serikali kuendelea kutoa huduma za ushauri nasaha na msaada wa kisaikolojia kwa wananchi wote wenye uhitaji huo.

### **Maji na Usafi wa Mazingira**

97. Chama Cha Mapinduzi kinatambua kuwa maji ni msingi wa uhai wa binadamu na injini ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Upatikanaji wa uhakika wa huduma ya majisafi na salama na usafi wa mazingira huchangia sana katika kuzuia magonjwa na hivyo kuimarisha afya na kuboresha maisha ya wananchi kwa ujumla. Ni kwa sababu hizi, uimarishaji wa huduma ya maji imekuwa ni ajenda ya kudumu ya Chama tangu nchi yetu ilipopata Uhuru.

98. Katika kutekeleza Ilani ya CCM ya Mwaka 2015 - 2020, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi iliendelea kuchukua hatua madhubuti katika kuimarisha sekta ya maji nchini, ikiwemo (i) kuendelea kulinda na kutunza vyanzo vya maji kupitia Bodi za Maji za Mabonde nchini; (ii) kuendelea kukarabati na kujenga miundombinu mipya ya usambazaji maji, na (iii) kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa kusimamia sekta ya maji, ikiwa ni pamoja na kuanzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*Rural Water Supply and Sanitation Agency-RUWASA*).

99. Kutokana na hatua zilizochukuliwa katika kuimarisha sekta ya maji nchini, mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- (a) Nchi yetu imeendelea kuwa na rasilimali za maji za kutosha kukidhi mahitaji ya leo na vizazi vijavyo. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, nchi yetu ina wastani wa mita za ujazo bilioni 126 za raslimali za maji kwa mwaka, ambazo zinafaa kwa matumizi ya binadamu. Kiwango hiki ni sawa na wastani wa mita za ujazo 2,250 kwa mwaka kwa kila mtu, ikiwa ni juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 ambacho



ni kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa. Chini ya kiwango hicho nchi huhesabika kuwa na uhaba wa maji (*water stress*);

- (b) Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2019, jumla ya miradi ya maji 1,423 vijijini na mijini imeendelea kutekelezwa, ikiwemo miradi 1,268 ya vijijini na miradi 155 ya mijini. Jumla ya miradi 792 imekamilika ambapo miradi 710 ni ya vijijini na 82 ni ya mijini. Miradi 631 inaendelea kutekelezwa, ikiwemo miradi 558 ya vijijini na miradi 73 ya mijini. Baadhi ya miradi mikubwa iliyotekelezwa katika kipindi hiki ni pamoja na:
- (i) Upanuzi wa mitambo ya kuzalisha maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini na kuongeza uwezo wa kuzalisha maji kutoka mita za ujazo laki 300 kwa siku hadi kuzalisha mita za ujazo laki 502 kwa siku, na kupanua mtandao wa usambazaji maji jijini Dar es Salaam, na Miji ya Kibaha na Bagamoyo;
  - (ii) Miradi ya maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika miji ya Bukoba, Musoma, Mwanza, Nansio, Sengerema, Lamadi, Magu, Misungwi, Kagongwa-Isaka, Nzega, Tabora na Igunga;
  - (iii) Mradi wa maji kutoka Ziwa Tanganyika kwenda katika mji wa Ujiji Kigoma na vitongoji vyake;
  - (iv) Miradi ya maji katika halmashauri zote nchini;
  - (v) Miradi ya maji katika miji ya makao makuu ya mikoa mipya nchini, ikiwemo Bariadi, Njombe na Vwawa-Mlowo;
  - (vi) Miradi mikubwa na ya kimkakati katika miji ya Arusha, Kigoma, Lindi, Same, Mwanga, Orkusemet;
  - (vii) Mradi mkubwa wa maji katika miji 28 kupitia fedha za mkopo nafuu wa shilingi trilioni 1.2 kutoka Serikali ya India umeanza kutekelezwa;
  - (viii) Mradi wa maji mkubwa na wa kimkakati umeanza kutekelezwa wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya mazingira wa Simiyu (*Simiyu Climate Resilience Water Project*). Mradi huu una thamani ya shilingi bilioni 400, ukigharamiwa na Serikali ya Tanzania, Shirika la GCF na Serikali ya Ujerumani;
  - (ix) Mradi wa maji mkubwa na wa kimkakati kutoka Ziwa Victoria kwenda katika miji ya Mugango, Kiabakari na Butiama umeanza kutekelezwa; na



- (x) Ujenzi wa mabwawa katika mikoa yenye ukame umeanza kutekelezwa, ikiwemo mabwawa ya Seke Ididi (Kishapu - Shinyanga); Habiya (Itilima - Simiyu); Kawa (Nkasi - Rukwa); Matwiga (Chunya - Mbeya); Mwanjoro (Meatu - Simiyu); Igumila (Sikonge - Tabora); Mbuyuni (Monduli - Arusha); Kwagamacho (Mkinga - Tanga); Kiluluduga (Mkinga - Tanga); Doda (Mkinga - Tanga); Engikaret (Longido - Arusha); (Kwamaligwa (Kilindi - Tanga); Bambamwarongo (Kilindi - Tanga); Kakesio (Ngorongoro-Arusha); Sengenya (Nanyumbu - Mtwara); Wanging'ombe (Wanging'ombe - Njombe); na Mlilingwa (Morogoro) (watu 1831).
- (c) Upatikanaji wa huduma ya maji umeendelea kuimarika, ambapo idadi ya wananchi wanaopata majisafi na salama vijijini imeongezeka kutoka asilimia 47 mwaka 2015 hadi asilimia 70.1 mwaka 2020. Kwa upande wa mijini idadi imeongezeka kutoka asilimia 74 mwaka 2015 hadi asilimia 84 mwaka 2020.

100.

**Katika miaka mitano ijayo, lengo la CCM ni kuona kuwa nchi inaendelea kuwa na usalama wa maji na kwamba huduma ya majisafi na salama inaendelea kuimarishwa na kuwafikia zaidi ya asilimia 85 ya wakazi wa vijijini na zaidi ya asilimia 95 kwa mijini ifikapo mwaka 2025. Aidha, CCM inalenga kuhakikisha kuwa kaya nyingi zaidi mijini zinaunganishwa katika mtandao wa maji taka. Ili kufikia lengo hili, CCM itaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:**

- (a) Kutekeleza kikamilifu mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji (*Integrated Water Resources Management and Development Plans*);
- (b) Kutekeleza miradi ya ujenzi wa mabwawa ya kimkakati kwa lengo la kuimarisha uwezo wa kuhifadhi maji, yakiwemo mabwawa ya Kidunda, Lugola na Farkwa;
- (c) Kukamilisha utafiti na kuanza kutekeleza mradi wa kuchukua maji kutoka Ziwa Victoria kuyapeleka katika miji ya Singida na Dodoma na vijiji vya kandokando ya bomba kuu;
- (d) Kukamilisha miradi mikubwa ya maji inayoendelea nchini kote na kuhakikisha vijiji vyote vilivyopo kando kando ya miradi hiyo mikubwa vinanufaika;
- (e) Kubuni na kutekeleza miradi ya maji katika vijiji na miji iliyopo katika maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa;
- (f) Kupanua na kuboresha miradi ya maji ya kitaifa ya Wanging'ombe Mugango-Kiabakari, Handeni *Trunk Main* (HTM), Chalinze na Makonde;



- (g) Kujenga angalau bwawa moja la ukubwa wa kati katika kila wilaya ili kupunguza kiwango cha maji ya mvua kinachopotea kwenda baharini kwa ajili ya kuongeza vyanzo vya maji vya uhakika na kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama unakuwa endelevu;
- (h) Kuhamasisha ujenzi wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua katika majengo ya Serikali, asasi za umma na nyumba za watu binafsi;
- (i) Kuanza kutekeleza programu ya kuvuna maji ya mvua hasa katika maeneo kame, maeneo ya ufugaji na kwenye taasisi za huduma za jamii, hususan mashule na vituo vya kutolea huduma ya afya vijijini (zahanati, vituo vya afya na hospitali);
- (j) Kuhakikisha kuwa miradi yote ya maji mijini inakuwa na mfumo wa kuondoa majitaka;
- (k) Kutekeleza miradi ya kimkakati ya kujenga mfumo wa uondoaji wa majitaka katika miji yote ya makao makuu ya mikoa nchini;
- (l) Kuimarisha usimamizi na uhakiki wa visima vya maji ili kuhakikisha vinatoa majisafi na salama; na
- (m) Kuimarisha Mfuko wa Taifa wa Maji ili kuongeza uwezo wa kifedha katika kutekeleza miradi ya maji.





## SURA YA NNE

### SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA

101. Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ni nyezo muhimu katika kutatua changamoto mbalimbali za maendeleo hususan katika kuwezesha matumizi ya rasilimali kwa ufanisi zaidi. Kwa kutambua umuhimu huo, Chama katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015-2020), kimeendelea kuhimiza Serikali kuchukuwa hatua mbalimbali ili kuhakikisha masuala hayo yanayozingatiwa. Katika kipindi hicho mafanikio yafuatayo yamepatikana:-
- Kutolewa kwa mafunzo mbalimbali ya jinsi ya kuanzisha vituo vya ubunifu kwa taasisi mbalimbali za elimu ya juu ambayo yaliwezesha kuanzishwa kwa kumbi za ubunifu (*Innovation Hub*) na atamizi (*incubators*) katika vyuo Vikuu nchini ikiwa ni pamoja na; UDSM - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, SUA *Innovation Hub* (Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo), Bio-*Innovation Hub* (Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela), UDOM- *Innovation Space* (Chuo Kikuu cha Dodoma), *MUST Innovation Hub* (Chuo Kikuu cha Iringa), na Zanzibar *Technology and Business Incubator* (Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia);
  - Kukamilika kwa hatua ya kwanza ya ujenzi wa maktaba ya kisasa katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia - Mbeya yenye uwezo wa kuwahudumia wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja;
  - Kuibua na kutambua wabunifu wachanga 415 kupitia mashindano ya Kimataifa ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu ambapo kati yao wabunifu 60 mahiri wanaendelezwa ili ubunifu wao ufikie hatua ya kubiasharishwa na hivyo kuongeza fursa za ajira kwa vijana;
  - Kuanzishwa kwa vituo atamizi 17 kwa ajili ya kukuza na kuendeleza ubunifu na hivyo kuwezesha kuanzishwa kwa makampuni 94 yanayotokana na ubunifu;
  - Kukamilisha ujenzi wa uwekwaji wa vifaa vya kompyuta iliyo na uwezo mkubwa (*super computer*) katika vituo vipya vya kuendeleza ubunifu na ujasiliamali katika fani ya TEHAMA katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam;
  - Kutekeleza kwa jumla ya miradi 139 ya utafiti, miradi 47 ya ubunifu na miradi 29 ya kuboresha miundombinu ya maabara za utafiti katika Taasisi za Elimu ya Juu na utafiti. Aidha, watafiti 579 wamejengewa uwezo katika masomo ya ngazi ya Umahiri na Uzamivu;



- (g) Kuelimisha umma kuhusu matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii kwa kuandaa na kutoa makala 112 zilizorushwa kwenye redio na runinga; na
- (h) Kukamilika kwa awamu ya kwanza na kuanza kwa awamu ya pili ya ujenzi wa maabara changamano ya kisasa na ya aina yake Afrika Mashariki na Kati kwa ajili ya kudhibiti matumizi salama ya mionzi na kuendeleza sayansi na teknolojia za nyuklia katika Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) - Arusha.

102. ***Hivi sasa tunao Watanzania wengi waliofunzwa vizuri na wenye utaalumu. Wapo kwa sababu tulitumia rasilimali zetu kuwasomesha, lazima wapewe majukumu ya kutuhudumia na kutumia rasilimali tulizonazo katika Tanzania. Juhudi zao zisipuuzwe, eti kwa sababu bado hawajapata uzoefu; au kwa sababu hapo mwanzo kazi yao haikuwa nzuri sana, au haikufanywa kwa haraka, au haijafikia kiwango cha kimataifa. Wapeni nafasi! Tusipowapa nafasi wataalamu wetu nao wataendelea kuwa katika hali hiyo hiyo ambayo sasa inatuzuia kuwatumia. Baba wa Taifa Mwl Julius Kambarage Nyerere, 1987. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha kuwa sayansi, teknolojia na ubunifu vinatumika kikamilifu katika kuendesha sekta za kukuza uchumi kwa lengo la kufikia uchumi wa hadhi ya kipato cha kati ambao ni shindani, jumuishi na unaoongozwa na viwanda. Ili kutimiza azma hiyo, Chama kitaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-***

- (a) Kuimarisha mfumo wa uratibu wa shughuli za sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchangia kikamilifu katika ujenzi wa uchumi imara na endelevu;
- (b) Kutenga fedha kwa ajili ya kusomesha Watanzania nje ya nchi katika vyuo bora duniani katika sayansi, teknolojia na tiba ili kupata maarifa bora na ujuzi utakaochochea maendeleo nchini;
- (c) Kuweka mazingira wezeshi kwa wataalam wabobezi kutoka nje ya nchi kuja kufanya kazi nchini ili kuhawilisha maarifa na teknolojia kwa ajili ya maendeleo ya Taifa;
- (d) Kuweka kipaumbele katika kujenga na kuendeleza uwezo wetu na kuimarisha matumizi salama ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika maeneo ya kimkakati ikiwemo matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia na maendeleo ya teknolojia ya kidijitali (*digital technology*);
- (e) Kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kusimamia na kuendeleza masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu nchini;



- (f) Kuratibu uwekezaji katika maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu, hususan tafiti zinazochochea ugunduzi (*invention*) na zitakazowezesha nchi kupunguza utegemezi wa teknolojia kutoka nje;
- (g) Kuanzisha makampuni ya ndani ya kimkakati katika sekta mbalimbali ili kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu kwa ajili ya maendeleo endelevu;
- (h) Kujenga mfumo shirikishi na endelevu wa ubunifu (*national innovation system*) kwa kusimamia kila hatua ya ubunifu ili kuhakikisha ubunifu unakuwa fursa ya kiuchumi na unaongeza tija katika shughuli za uzalishaji na hivyo kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi;
- (i) Kuibua, kutambua na kuendeleza ubunifu na ugunduzi unaozalishwa nchini kwa ajili ya kutatua changamoto zinazoikabili jamii ya Watanzania;
- (j) Kuongeza na kuimarisha vituo atamizi kwa ajili ya kukuza na kuendeleza wabunifu ili kulea na kuwezesha vijana na wataalam kuendeleza ujuzi wao na kuanzisha makampuni madogo madogo yanayotokana na ubunifu na hivyo kuchochea kuzalisha ajira na kuongeza uzalishaji;
- (k) Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza mawazo ya ubunifu wenye mchango wa moja kwa moja katika maendeleo ya uchumi wa viwanda nchini;
- (l) Kuimarisha na kuhamasisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika uchumi wa kidijitali (*digital economy*) hususan Serikali mtandao, miundombinu ya TEHAMA katika Nyanja zote za uchumi na ulinzi wa mitandao;
- (m) Kuboresha utekelezaji wa sera na mikakati ya utafiti kwa kutenga fedha za kutosha na kuimarisha mifumo ya uratibu na usimamizi ili matokeo ya utafiti yaweze kutumika kwa tija na kuchangia katika utatuzi wa changamoto kwenye sekta zilizofanyiwa utafiti na hivyo kuongeza kasi ya uzalishaji viwandani na maendeleo ya Taifa kwa ujumla;
- (n) Kutenga fedha kwa ajili kuanzisha vituo vya umahiri vya sayansi na teknolojia (*centres of excellence*) katika taasisi za elimu ya juu nchini kwa kuzingatia maeneo ya kimkakati katika kujenga uchumi imara na endelevu;
- (o) Kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyuo vya sayansi na teknolojia pamoja na kukarabati karakana na kuziwekea vifaa vya kisasa vya kujifunzia na kufundishia;



- (p) Kuboresha na kuongeza miundombinu na vifaa vya mafunzo kwa vitendo kwenye vyuo vikuu na taasisi za umma zinazotoa mafunzo ya tiba nchini ikiwemo ujenzi wa hospitali (*teaching hospitals*) mahsusi za mafunzo na utafiti;
- (q) Kuanzisha kituo kikubwa cha utafiti na uchunguzi wa mimea dawa na kujenga kiwanda cha kimkakati cha kuzalisha dawa zinazotokana na mimea; na
- (r) Kuimarisha mafunzo ya walimu wa sayansi, teknolojia na ufundi katika ngazi za shule za msingi na sekondari, vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi na vyuo vya kati ili kuongeza uwepo wa nguvukazi ya kutosha na yenye ubora kwa ajili ya maendeleo ya viwanda nchini.

### **Uchumi wa Kidijitali (Digital Economy)**

103.

**Chama Cha Mapinduzi kinatambua kuwa uchumi wa kidigitali ni muhimu katika kuleta maendeleo kwa kuongeza ufanisi katika uzalishaji na utekelezaji wa shughuli mbalimbali na kutoa fursa za kuongeza vipato vya wananchi na Taifa kwa ujumla. Uchumi huo umeonekana kuwa eneo muhimu katika kuchangia kukuza uchumi nchini kama ilivyofanyika katika nchi nyingine za kipato cha kati. Aidha, uchumi wa kidijitali unarandana na mapinduzi ya nne ya viwanda yanayokuja na ambayo hayaepukiki. Hivyo basi, CCM itaendelea kusimamia Serikali kuhakikisha kuwa teknolojia mpya za kidijitali zinatumiwa kuongeza ufanisi katika sekta za uzalishaji na kuepuka madhara yanayoweza kutokea. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama kitaelekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuendeleza na kuongeza uwezo wa kitaalam na matumizi ya teknolojia mpya za kidijitali;
- (b) Kudhibiti athari hasi zinazoweza kutokea kutokana na matumizi ya teknolojia mpya za kidijitali;
- (c) Kurahisisha utoaji wa huduma mbalimbali za Serikali kwa umma kwa kuanzisha Vituo vya Huduma Pamoja (*One Stop Centre*) ili kuongeza ufanisi na kurahisisha upatikanaji wa huduma za Serikali;
- (d) Kuimarisha kituo cha utafiti, ubunifu na uendelezaji wa TEHAMA ikiwemo kujenga uwezo na kuongeza matumizi ya teknolojia mpya za kidijitali na *artificial intelligence*; na
- (e) Kuendeleza Serikali Mtandao inayozingatia usalama wa mifumo na taarifa za Serikali na kuwarahisishia watumishi wa umma utendaji kazi na wananchi kupata huduma kwa urahisi na ufanisi.



## SURA YA TANO

### ULINZI NA USALAMA

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA

104.

Uhakika wa amani, ulinzi na usalama ni nyenzo muhimu katika kuwawezesha wananchi kuishi na kuendelea na shughuli zao za maendeleo. Katika miaka mitano iliyopita, Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kuhakikisha kuwa mipaka ya nchi yetu inakuwa salama, Muungano wetu unaimarishwa, Mapinduzi matukufu ya Zanzibar yanalindwa, pamoja na kuwepo kwa umoja, mshikamano na utulivu. Chama Cha Mapinduzi kimesimamia serikali zake ili kuendeleza ipasavyo masuala ya ulinzi na usalama na kupata mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo:-

- (a) Nchi imeendelea kuwa na umoja, mshikamano, amani na utulivu, na hivyo kuwawezesha wananchi kuendelea kufanya kazi zao katika hali ya amani, utulivu na usalama;
- (b) Kuimarisha na kuboresha makazi ya maafisa na askari wa vyombo vya ulinzi na usalama kwa kujenga nyumba katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Polisi, Magereza, Idara ya Usalama wa Taifa na Uhamiaji;
- (c) Kuimarisha usalama wa raia na mali zao kwa kuhakikisha kila Kata ina kuwa na Askari wa Kata ambaye anashirikiana na Afisa Mtendaji Kata katika masuala ya ulinzi na kutoa taarifa za hali ya usalama katika vikao vya Kamati za Maendeleo za Kata;
- (d) Kuimarisha huduma za kiuhamiaji kwa kuanzishwa na kutumika kwa Mfumo wa Uhamiaji Mtadao ambao umewezesha: kutoa pasipoti za kielektroniki, kurahisisha huduma za kuhakiki hati za ukaazi kwa njia ya mtandao na kupunguza urasimu na muda wa upatikanaji wa hati za ukaazi pamoja na kuongeza maduhuli ya Serikali;
- (e) Kurahisisha uombaji na utoaji wa viza kwa wageni kwa njia ya mtandao na kudhibiti watu wanaoingia na kutoka nchini (*e-border management System*);
- (f) Kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuviongezea nguvu kazi, zana za kisasa na vitendea kazi kama vile magari, vifaa vya mawasiliano, magari ya kubebea wagonjwa pamoja na vifaa mbalimbali vya kuzima moto na maokozi na pikipiki;
- (g) Kuongezeka kwa maarifa, uzoefu na mbinu za kisasa za ulinzi wa amani katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kutokana na ushiriki katika operesheni za ulinzi wa amani katika nchi mbalimbali duniani;



- (h) Kuimarishwa kwa utendaji kazi wa vyombo vya ulinzi na usalama kwa kupatiwa mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Mafunzo hayo ya kitaalam na kitaaluma yalitolewa kwa maafisa wa vyombo vya ulinzi na usalama, wakaguzi na askari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Uhamiaji;
- (i) Kuendelea kuimarika kwa majeshi yetu kutokana na kushirikiana na mataifa mengine na asasi za kitaifa na kimataifa katika kupambana na makosa yanayovuka mipaka hasa ugaidi, uharamia, utakatishaji wa fedha haramu, biashara haramu ya dawa ya kulevywa na usafirishaji haramu wa binadamu;
- (j) Vyombo vya ulinzi na usalama vimeshirikiana na wananchi katika kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao;
- (k) Kurahisisha taratibu kwa wanaosafiri kwenda nje ya nchi kwa kuanzisha viza na pasi za kielektroniki;
- (l) Kuimarisha utambuzi wa Watanzania na raia wengineo kwa kuanzisha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuanzia mwaka 2010/11 ambapo Vitambulisho vya Taifa vilianza kutolewa; na
- (m) Kuimarika kwa mifumo ya ulinzi na usalama kwa kutambua na kusajili raia wa Tanzania, wageni wakazi na wakimbizi, ambapo hadi kufikia 2019 yafuatayo yamefanyika:-
  - (i) Kutambuliwa na kusajiliwa kwa jumla ya watu 21,511,321 na kuzalisha vitambulisho 5,787,869;
  - (ii) Kuzalishwa kwa namba za utambulisho (NIN) 16,321,689;
  - (iii) Kutambua na kusajili wakimbizi 200,074; na
  - (iv) Kuwezesha uunganishaji wa ofisi 126 za usajili na utambuzi za wilaya na makao makuu kupitia Mkongo wa Mawasiliano (*Optic Fibre*) kati ya wilaya 150 zinazopaswa kuunganishwa.

105. **Katika miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuhimiza serikali zake kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu, raia wake na mali zao ili kudumisha umoja, mshikamano, amani na utulivu ambazo ni tunu kuu za Taifa letu. Katika kufikia malengo hayo, Chama kitaelekeza Serikali kutekeleza yafuatayo: -**

- (a) Kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi na mipaka yake ili kudumisha Muungano, kulinda Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, umoja, mshikamano, amani na usalama wa raia na mali zao;





- (b) Kuendeleza jitihada za utatuzi wa changamoto za mipaka ya nchi yetu na nchi jirani;
- (c) Kuwawezesha ushirikiano wa vyombo vya ulinzi na usalama kufanya utafiti na ubunifu kwa kushirikiana na taasisi za utafiti;
- (d) Kuhusisha kikamilifu majeshi ya ulinzi na usalama katika kulinda miradi mikubwa ya kimkakati;
- (e) Kuhamasisha na kuelimisha wananchi juu ya masuala ya ulinzi, uzalendo wa kitaifa, usalama na umuhimu wa kushiriki katika ulinzi ikiwa ni pamoja na Jeshi la Akiba na ulinzi shirikishi ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu;
- (f) Kuimarisha mfumo wa ulinzi na usalama kwenye ngazi ya jamii ili kujenga mfumo wa kutambua, kutoa taarifa na kuchukua hatua za awali dhidi ya vihatarishi vya ulinzi na usalama vinavyojitokeza katika maeneo yao (kama ilivyokuwa kwenye mfumo wa nyumba kumi zamani);
- (g) Kuimarisha uwezo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama katika kushiriki shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda katika sekta ya ulinzi na maeneo mengine ya kimkakati;
- (h) Kuimarisha viwanda vya NYUMBU na Mzinga ili viweze kutimiza azma ya kuanzishwa kwake;
- (i) Kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ili viwe vyombo vya kuwapatia vijana ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa na pia kuwa vyombo mahiri vya huduma na uzalishaji mali hasa katika ujenzi, kilimo, ufugaji na uvuvi;
- (j) Kupanua na kuongeza idadi ya kambi za JKT na JKU ili kuwezesha vijana wengi zaidi wakiwemo wahitimu wote wa kidato cha sita kupata fursa ya mafunzo ili kujenga uzalendo na moyo wa kujitolea;
- (k) Kuliwezesha Jeshi la Polisi kuendelea na jukumu la kudhibiti hali ya uhalifu nchini, kudumisha hali ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kudhibiti ajali za barabarani na kuongeza kasi na ufanisi wa upelelezi wa kesi za makosa ya jinai na mengineyo;
- (l) Kuboresha mazingira ya kazi kwa kuwapatia makazi bora na kuongeza uwezo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia mafunzo ya kitaaluma na kitaalam, vitendea kazi na zana za kisasa zinazoendana na teknolojia ya kisasa;



- (m) Kuendeleza ushirikiano na vyombo vya ulinzi na usalama vya nje ya nchi pamoja na taasisi mbalimbali za kimataifa (*Interpol*) katika kukabiliana na kupambana na matishio ya kiusalama na makosa yanayovuka mipaka hususan ugaidi, makosa ya kimtandao (*cyber-crime*), uharamia, utakatishaji fedha haramu, biashara haramu ya madawa ya kulevya, usafirishaji haramu wa binadamu, ujangili na bidhaa bandia;
- (n) Kuliwezesha Jeshi la Magereza na Vyuo vya Mafunzo kuendelea na majukumu ya kutunza, kuhifadhi na kufundisha wahalifu na kuzalisha mali ili yaweze kujitegemea;
- (o) Kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutekeleza wajibu wake katika kuhakikisha usalama wa moto na maokozi katika maeneo mbalimbali nchini na hasa kwenye miradi mikubwa na ya kimkakati ikiwemo ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege, ujenzi wa viwanda, miradi ya umeme na gesi, ujenzi wa bomba la mafuta, treni ya umeme na uchimbaji wa madini;
- (p) Kuiwezesha Idara ya Uhamiaji kuendelea kutimiza wajibu wake wa kudhibiti uingiaji na utokaji wa watu nchini;
- (q) Kuwezesha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa kuendelea kutambua, kusajili na kutoa vitambulisho vya Taifa kwa raia wa Tanzania, wageni wakazi na wakimbizi kwa kuhakikisha:-
  - (i) Watu wote wenye sifa ya kusajiliwa na kupata utambulisho wa Taifa wanasajiliwa na kupatiwa vitambulisho; na
  - (ii) Taasisi zote za umma na binafsi zinaunganishwa na mfumo wa NIDA.

### **Kukabiliana na Majanga**

106. Nchi inapaswa kuwa katika hali ya utayari wakati wote kukabiliana na maafa au majanga yanayoweza kutokea kutokana na sababu mbalimbali ili kuokoa maisha na mali za wananchi. Kwa mantiki hiyo, Chama Cha Mapinduzi wakati wote kimeendelea kuhakikisha Serikali inaimarisha na kuvisimamia kikamilifu vyombo vya kukabiliana na maafa na majanga na kuhakikisha vinakuwa na mpango wa utayari wa kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali haraka pindi maafa yanapotokea. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), Chama kimeendelea kusimamia Serikali katika kukabiliana na majanga na maafa na kupata mafanikio yafuatayo:-

- (a) Kuendelea kutoa elimu ya usimamizi wa maafa kwa kamati za kudumu za Bunge na kamati za maafa katika mikoa kumi ya Songwe, Iringa, Arusha, Kilimanjaro, Lindi, Mara, Mwanza, Mtwara, Shinyanga na Rukwa. Vilevile, elimu kuhusu maafa imetolewa kwa umma kupitia



vyombo vya habari na maadhimisho ya siku ya maafa duniani kila mwaka;

- (b) Kuandaliwa kwa mipango ya kujiandaa na kukabili maafa ya katika halmashauri za wilaya nane ili kuwezesha halmashauri hizo kuwa na utayari wa kukabiliana na maafa pindi yanapotokea;
- (c) Kuongezeka kwa upatikanaji wa taarifa za uhakika za hali ya hewa katika maeneo mbalimbali nchini kutokana na kusimika vituo 51 vya kisasa vya kufuatilia taarifa hizo ikiwa ni vituo 15 vya kupima uwingi wa maji kwenye mabonde ya mito. Upatikanaji wa uhakiki wa taarifa za hali ya hewa umesaidia vyombo vya kuwa tayari kukabiliana maafa pindi dalili zinapojitokeza;
- (d) Kutolewa kwa misaada kibinadamu kufuatia maafa yaliyojitokeza katika halmashauri 54 zilizopo katika mikoa 17;
- (e) Kufanyika kwa ukarabati wa taasisi za umma 351 na nyingine kujengwa upya, na kurejesha miundombinu kufuatia tetemeko lililotokea mkoani Kagera mwaka 2016;
- (f) Kuanzishwa kwa Kituo cha Menejimenti ya Maafa na Mawasiliano ya Dharura ambacho kinatekeleza shughuli za operesheni na mawasiliano ya dharura nchini;
- (g) Kupatikana kwa eneo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kudumu cha menejimenti ya maafa na mawasiliano katika jiji la Dodoma; na
- (h) Kupeleka misaada ya kibinadamu kwa nchi jirani zilizopatwa na maafa ya kimbunga na mafuriko.

107.

**Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuhakikisha Serikali inaendelea kusimamia kikamilifu vyombo vinavyoshughulika na maafa kuwa na mpango wa utayari wa kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali haraka pindi maafa yanapotokea kwa kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kujenga na kuimarisha uwezo wa kitaifa wa uokozi katika maafa makubwa kama vile ajali za baharini, kwenye maziwa, migodini na mahala pengine;
- (b) Kuzijengea uwezo wizara, taasisi na mamlaka za serikali za mitaa kwa kuandaa mikakati ya kupunguza madhara ya maafa na mipango ya kujiandaa na kukabiliana na maafa;
- (c) Kuainisha maeneo yenye vihatarishi vikubwa vya kukumbwa na maafa/majanga na kuweka mfumo wa tahadhari ya awali kwa jamii;
- (d) Kutekeleza mikakati ya kitaifa, kikanda na kimataifa ya upunguzaji wa athari za maafa;



- (e) Kutoa elimu ya kuzuia na kukabiliana na maafa kwa umma na katika taasisi mbalimbali;
- (f) Kujenga uwezo wa wataalam kiujuzi na maarifa, na kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya kisasa katika kukabiliana na majanga/maafa mbalimbali;
- (g) Kuweka mikakati ya kushirikiana na sekta nyingine katika kuzuia na kukabiliana na maafa katika ngazi zote hususan ngazi za chini; na
- (h) Kujenga kituo cha kudumu cha Taifa cha menejimenti ya maafa na mawasiliano katika jiji la Dodoma.



## SURA YA SITA

### UTAWALA BORA, UTAWALA WA SHERIA NA MADARAKA YA WANANCHI

TUETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASIGGA MBEI PAMOJA

108. Uwepo wa utawala bora, utawala wa sheria na madaraka kwa wananchi ni matakwa muhimu yaliyoanishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar. Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kuzisimamia serikali zake kutekeleza misingi hiyo kwa kuhakikisha utawala bora, utawala wa sheria na madaraka kwa wananchi vinaimarishwa.

#### Utawala Bora

109. Maendeleo ya nchi na ustawi wa jamii unahitaji uwepo wa utawala bora katika nchi. Utawala bora unahakikisha kuwa utaratibu wa kufanya maamuzi na kutekelezwa kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa jamii unazingatia misingi ya utu, haki, ushirikishwaji, demokrasia, uwajibikaji, uwazi, utekelezaji, tija, ufanisi, usawa na ushiriki wa makundi yote. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015-2020), Chama Cha Mapinduzi kilihakikisha kuwa Taifa linakuwa na utawala bora unaozingatia misingi hiyo ili kutoa huduma bora kwa wananchi na kutokomeza umasikini katika jamii. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

- Kuimarika kwa hali ya amani na utulivu nchini kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa za kuhakikisha wananchi wanapata fursa ya kushiriki katika shughuli za maendeleo bila kuwepo bugudha;
- Kuimarika kwa uhuru katika utendaji kazi wa mihimili ya dola kwa kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa uhuru pasipo kuingiliana;
- Kutekeleza mikakati na maazimio ya kikanda na kimataifa yanayohusiana na utawala bora na haki za binadamu; na
- Kuimarika kwa matumizi sahihi ya rasilimali za nchi hali ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa kuchochea maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kiraia, kisiasa, kiutamaduni na utaifa.

110. **Katika kipindi cha Miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuhakikisha viongozi wanaoteuliwa ni waadilifu, wawajibikaji, wanaoleta matokeo chanya na kutumia rasilimali za umma kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Ili kufikia azma hiyo, Chama kitaelekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**

- Kuhakikisha kuwa madaraka kwa umma yanabaki kuwa ndio msingi wa utawala katika nchi;



- (b) Kuimarisha taasisi za utawala bora, maadili na uwajibikaji kama vile Ofisi ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi katika Utumishi wa Umma, TAKUKURU, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya ili ziweze kutimiza wajibu ipasavyo;
- (c) Kujenga jamii yenye ari na uhuru wa kujieleza, kuishi mahali popote nchini, kushiriki katika masuala ya kisiasa kwa kuzingatia maadili na sheria za nchi;
- (d) Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango na shughuli za Serikali;
- (e) Kusimamia nidhamu, uadilifu, uwazi na uwajibikaji miongoni mwa viongozi, watumishi wa umma na wafanyakazi wengine;
- (f) Kujenga jamii inayoheshimu na kuthamini utu, usawa na haki;
- (g) Kuimarisha ujumuishaji wa masuala yahasuyo haki na wajibu wa makundi maalum ikiwemo huduma kwa watu wenye ulemavu, unyanyasaji wa kimaumbile n.k. (anuai za jamii) katika shughuli mbalimbali za Serikali; na
- (h) Kutunga sheria ya usuluhishi ili pamoja na mambo mengine, itumike katika kusimamia masuala ya usuluhishi nchini.

### **Maadili katika Utumishi wa Umma**

111. Maadili ya viongozi na watumishi wa umma ni suala muhimu na la kipaumbele katika harakati za kujipatia maendeleo. Maadili ni msingi muhimu si tu katika mwitikio na dhamira ya uadilifu, uwazi, uwajibikaji na ari ya kutojijhusisha na masuala ya rushwa bali ni chemchem inayowafanya watumishi kujikita katika utoaji wa huduma bora kwa jamii bila upendeleo. Kwa kutambua umuhimu huo, Chama Cha Mapinduzi katika miaka mitano iliyopita (2015 - 2020) kimeendelea kutilia mkazo suala la maadili kwa kuchukua hatua zilizolenga kuimarisha nidhamu ya watumishi kwa lengo la kuwezesha utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kufanya marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Mwaka 1995 yaliyoongeza kifungu kinachotoa tafsiri ya mgongano wa masilahi kwa mtoto chini ya miaka 18; kuongeza jukumu la kufanya uhakiki wa tamko la rasilimali na madeni kwa viongozi wa umma kwa mujibu wa sheria na kumpa Kamishna wa Maadili mamlaka ya kuwaita viongozi wa umma kwa ajili ya mahojiano;
- (b) Kuandaa kanuni za sheria ya maadili ya viongozi wa umma (udhibiti wa mgongano wa masilahi) ili kuziba ombwe lililojitokeza kutokana na kukosekana kwa kanuni zinazofafanua baadhi ya vipengele katika





sheria kuhusu masuala ya mgongano wa masilahi kutokana na marekebisho ya sheria yaliyofanyika; na

- (c) Kuandaliwa kwa kanuni za maadili (utaratibu wa kushughulikia malalamiko ya ukiukwaji wa maadili katika baraza la maadili).

112. **Chama Cha Mapinduzi, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kitaendelea kuhakikisha suala la maadili ya viongozi na watumishi wa umma linatiliwa mkazo na kuimarishwa zaidi ili wananchi waendeleo kunufaika na huduma bora kulingana na matarajio yao. Ili kufikia malengo hayo, Chama kitaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kusimamia nidhamu, uadilifu, uwazi, uzalendo wa kitaifa, moyo wa kujitolea na uwajibikaji miongoni mwa viongozi na watumishi wa umma;
- (b) Kuongeza watumishi wenye sifa stahiki kwenye utoaji huduma na kuhimiza watumishi wa umma kufanya kazi kwa juhudi, maarifa, ubunifu na weledi katika kujenga taifa letu;
- (c) Kudhibiti migongano ya masilahi katika shughuli za Umma kwa kusimamia mifumo iliyopo;
- (d) Kujenga jamii inayoheshimu na kuthamini utu, haki, maadili na nidhamu; na
- (e) Kuimarisha Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ili iweze kuboresha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi.

### **Mapambano Dhidi ya Rushwa na Ufisadi**

113. Mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi ni suala muhimu kwa kuwa athari zake ni kubwa katika harakati za kufikia maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Endapo suala la rushwa litaendelea kutokuchukuliwa hatua stahiki, juhudi za kujenga uchumi imara ambao utachangia kupunguza kiwango cha umasikini wa wananchi hazitoweza kuzaa matunda. Chama Cha Mapinduzi kwa kutambua umuhimu wa kutokemeza adui rushwa na ufisadi, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015-2020), kiliisimamia Serikali kuendeleza vita dhidi ya rushwa na ufisadi kwa kuchukua hatua mbalimbali na kupata mafanikio makubwa.

114. Hatua hizo ni pamoja na kuendelea kuimarisha vyombo vinavyohusika na vita dhidi ya rushwa na ufisadi, hususan Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na ufisadi nchini kwa kufungua Ofisi mpya 21 katika Wilaya zote ambazo hazikuwa na Ofisi za TAKUKURU na kuanzishwa kwa Mahakama ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. Matokeo yaliyopatikana kutokana na hatua hizo ni pamoja na kuimarika kwa mifumo ya utoaji haki; kuongezeka uwajibikaji na uwazi miongoni viongozi na watumishi wa umma; na kuongezeka kwa kasi ya ushughulikaji wa mashauri yanayohusiana na rushwa na ufisadi.



115. Mafanikio hayo yamepatikana kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015-2020) ni kama ifuatavyo:-
- (a) Kuanzishwa kwa Mahakama ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi katika Mahakama Kuu ya Tanzania, hatua ambayo imeonesha nia ya Serikali kupambana kwa dhati na rushwa na ufisadi nchini;
  - (b) Kesi mpya za rushwa 3,350 zimefunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini ambapo watuhumiwa 1,268 wa kesi hizo walipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo au kulipa faini au vyote kwa pamoja;
  - (c) Kiwango cha kushinda kesi kilipanda kutoka asilimia 41 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 60.4 mwaka 2020;
  - (d) Kuongezeka kwa kasi ya utambuzi na urejeshaji mali au fedha zilizotokana na vitendo vya rushwa na ulimbikizaji mali kwa viongozi na watumishi wa umma ambapo shilingi bilioni 199.5 ziliokolewa na kutaifisha nyumba 6 na magari 5;
  - (e) Kuongezeka kwa mwamko wa wananchi kutoa taarifa kuhusu vitendo vya rushwa ambapo mwaka 2019 vitendo vya rushwa 8,234 viliripotiwa ikilinganishwa na vitendo 4,678 vya mwaka 2015. Hii imetokana na kuboresha mfumo wa kupokea na kulinda vyanzo vya taarifa (*whistle blowers*) na wananchi kuongeza imani kwa Serikali yao; na
  - (f) Miradi ya maendeleo 3,267 yenye thamani ya shilingi trilioni 10.11 ilifuatiliwa katika sekta za afya, maji, ujenzi na elimu kwa lengo la kuhakiki thamani halisi ya matumizi ya fedha za umma katika miradi hiyo.
116. **Chama Cha Mapinduzi, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kwa kutambua kuwa rushwa ni adui wa haki na kwamba hakitavumilia vitendo vya rushwa na ufisadi kwa namna yeyote ile. Ili kufikia malengo hayo, Chama Cha Mapinduzi kitaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-**
- (a) Kuimarisha mifumo na Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini (TAKUKURU) ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kupitia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007 ili kupunguza makosa ya rushwa kutokana na mabadiliko ya mienendo na vitendo vya rushwa;
  - (b) Kudhibiti matumizi mabaya ya ofisi na upotevu wa fedha za umma na kukabili vitendo vya rushwa katika maeneo mbalimbali;
  - (c) Kubuni na kutekeleza mikakati mipya ya kupambana na rushwa na ufisadi;



- (d) Kuhamasisha na kuishirikisha jamii katika mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi; na
- (e) Kutoa elimu na kuendelea kufanya tafiti mbalimbali ili kubaini na kuziba mianya mipya ya rushwa na ufisadi.

### **Demokrasia na Haki za Binadamu**

117.

Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kusimamia Serikali kuhakikisha kuwa demokrasia na haki za binadamu nchini zinalindwa na kuheshimiwa kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar. Vilevile, nchi yetu ni mwanachama wa Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa na imeridhia mikataba na itifaki mbalimbali za kikanda na kimataifa zinazohusu haki za binadamu na kuendelea kutekeleza haki hizo kupitia mipango na programu mbalimbali za Serikali. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015-2020), mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- (a) Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa haki za elimu, afya na maji safi na salama na huduma nyingine muhimu;
- (b) Kuimarika kwa mfumo wa demokrasia ya kubadilishana viongozi wa nchi kwa njia ya amani katika pande zote za muungano na kuifanya nchi yetu kuwa nchi ya kwanza katika ukanda huu kuwa na msingi wa mfumo imara wa kubadilishana madaraka;
- (c) Ushirikishwaji wa wananchi moja kwa moja au kupitia kwa wawakilishi wao katika uongozi na utawala wa nchi;
- (d) Kuimarika kwa upatikanaji wa haki kwa kuboresha mhimili wa Mahakama ya Tanzania kwa kuijengea miundombinu ya utoaji haki, upatikanaji haraka wa nyaraka zinazohusiana na mashauri na kutungwa kwa mwongozo wa mwaka 2018 wa kushughulikia mashauri yanayohusiana na makundi maalum ndani ya kipindi kisichozidi miezi sita;
- (e) Wananchi wameendelea kupata haki mbalimbali ikiwemo uhuru wa kutoa mawazo, kupiga na kupigiwa kura, faragha, haki ya kumiliki mali, haki ya kuishi popote, usawa mbele ya sheria, haki ya watu kuwa na amani na usalama, haki ya kuishi na haki ya watu kujitawala kwa kuhakikisha kwamba Taifa linaendelea kutafsiri uhuru tulioupata mwaka 1961 na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964 kwa vitendo;
- (f) Kuandaa na kukubaliwa kwa taarifa ya pili ya nchi ya haki za binadamu chini ya mfumo wa Umoja wa Mataifa wa mapitio katika kipindi maalum na kuiwasilisha kwenye Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa mwaka, 2016. Kutokana na taarifa hiyo, mapendekezo 227 yamepokelewa na 131 kuridhiwa yanayoendana na misingi ya katiba, sheria, sera, mila na desturi za watu wa Tanzania;



- (g) Kuimarisha juhudi za kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wazee kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu wa 2013 na kutunga Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017 ili kuhakikisha Serikali, asasi za kiraia na wananchi wanatekeleza wajibu wa kulinda na kukuza haki za binadamu;
- (h) Kuimarisha mifumo ya ulinzi, uhifadhi na uendelezaji wa haki za watoto, wanawake na wazee kupitia sekta mbalimbali kwa kuendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa kutokomeza Ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wazee Tanzania wa mwaka 2017 hadi 2022;
- (i) Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mamlaka aliyopewa kwa mujibu wa katiba kuwaachia huru wafungwa 42,774 waliokidhi vigezo kutoka magerezani katika kipindi cha miaka mitano iliyopita; na
- (j) Kuimarika kwa hali ya demokrasia nchini kutokana na nchi yetu kuendelea kuheshimu sheria na utamaduni wa kufanya uchaguzi mara kwa mara kwa lengo la kuwawezesha wananchi kuwachagua viongozi wanaowataka.

**118. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuheshimu na kulinda misingi ya demokrasia na haki za binadamu kwa ajili ya ustawi wa Taifa kwa kuzingatia Katiba ya Nchi. Lengo la Chama Cha Mapinduzi katika kipindi hiki ni kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kupata haki kwa mtu mmoja mmoja na makundi mbalimbali. Ili kutimiza azma hiyo, Chama Cha Mapinduzi kitaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kuelimisha wananchi kutambua haki zao na kutumia fursa zilizopo kujiendeleza kwa kuzingatia matakwa na misingi ya katiba na sheria za nchi;
- (b) Kuheshimu na kuzingatia mifumo ya kulinda haki za binadamu, kwa mtu mmoja mmoja, makundi na jamii kwa ujumla;
- (c) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kukuza, kulinda na kutekeleza misingi ya haki za binadamu na wajibu wao;
- (d) Kuweka mazingira rafiki kwa wananchi kufikia vyombo vinavyosimamia haki katika ngazi zote; na
- (e) Kuweka mazingira wezeshi ya haki kwa wananchi kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa.



### **Katiba na Utawala wa Sheria**

119. Utawala wa sheria ni muhimu katika kuhakikisha kuna uzingatiwaji wa misingi ya utoaji haki. Katika kuimarisha utawala wa sheria nchini kama moja ya nguzo kuu za utawala bora na demokrasia, kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020, Serikali imeendelea kuimarisha mifumo na misingi ya utawala wa sheria na kupata mafanikio yafuatayo:-
- (a) Kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu sheria mbalimbali kwa kutafsiri sheria 157 kutoka Lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili ikilinganishwa na sheria 50 zilizokuwa zimetafsiriwa hadi mwaka 2010;
  - (b) Kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wote na kwa usawa kwa kutunga Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017; na Kanuni na Maadili kwa Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria za Mwaka 2018;
  - (c) Tija na ufanisi katika kutoa huduma za kisheria kwa umma na kwa Serikali umeongezeka kutokana na kuboreshwa kwa muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuanzishwa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;
  - (d) Huduma za mahakama zimendelea kuboreshwa kupitia Mkakati wa kuboresha Mahakama nchini ambapo: ujenzi wa Mahakama Kuu mbili katika mikoa ya Kigoma na Mara na ukarabati katika Mahakama ya Mbeya umekamilika; ujenzi wa mahakama 15 za wilaya ambazo ni pamoja na Kibaha, Bagamoyo, Kigamboni, Ilala, Longido, Kilwa, Ruangwa, Chato, Mkuranga, Kondoa, Bukombe, Kasulu na Chunya umekamilika. Vilevile, ujenzi wa mahakama tano za Hakimu Mkazi ikiwemo za Geita, Njombe na Simiyu umekamilika;
  - (e) Kuwa na wasajili wasaidizi katika halmashauri zote ambao wamewezesha uratibu na utoaji wa msaada wa kisheria kwa mafanikio makubwa kwa wananchi;
  - (f) Kuimarisha utendaji wa mabaraza ya ardhi na kuyaingiza katika mfumo wa kawaida wa utoaji haki;
  - (g) Kusogeza huduma za kisheria karibu na wananchi kwa kuanzisha huduma ya mahakama zinazotembea ikiwa ni pamoja na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika uendeshaji wa mashauri;
  - (h) Kuimarisha usimamizi wa biashara ya madini nchini kwa kutunga Sheria (*The Mining Act Cap. 123*) na kanuni zake kwa ajili ya uanzishwaji wa masoko ya madini ambayo yamekuwa na manufaa kwa watu, jamii na Taifa kwa ujumla;
  - (i) Kuwaachilia mahabusu 2,812 waliokuwa wameshikiliwa magerezani kwa muda mrefu kupitia Ofisi ya Mwendesha Mashitaka ya Taifa kwa utaratibu wa kuwafanyia mapitio katika kila gereza; na



- (j) Kuboresha ufanisi na ubora wa huduma za mahakama kwa kuajiri jumla ya watumishi 1,414 wa kada mbalimbali ukiwemo uteuzi wa majaji 52 wa Mahakama Kuu na majaji 17 wa Mahakama ya Rufani pamoja na mahakimu 319.

**120. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendeleza juhudi za kuimarisha utawala wa sheria nchini kwa kuelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kulinda haki za kikatiba za wananchi wanaoshiriki katika mijadala mbalimbali inayohusu maendeleo ya Taifa lao na kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya katiba na sheria ili kuimarisha misingi ya ukatiba (*constitutionalism*), demokrasia, utawala bora na utawala wa sheria;
- (b) Kuchukua hatua zaidi za kupunguza mrundikano wa kesi mahakamani;
- (c) Kuimarisha mfumo wa wasajili wasaidizi katika halmashauri zote ili kuwezesha uratibu na utoaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi, ikiwemo msaada wa huduma za kisheria kwa masuala ya mirathi na ndoa;
- (d) Kuhakikisha huduma bora za sheria zinapatikana kwa wakati na kwa gharama nafuu kwa kuongeza wataalam, miundombinu, vitendea kazi na kusogeza huduma karibu na wananchi;
- (e) Kuimarisha vyombo vya sheria kwa kuongeza wigo wa huduma za utoaji wa haki nchini;
- (f) Kuboresha miundombinu ili kuweka mazingira wezeshi ya kufanyia kazi kwa kujenga majengo ya mahakama katika ngazi mbalimbali, kujenga ofisi za mashtaka katika ngazi ya wilaya na kujenga ofisi za taasisi za makao makuu - Dodoma;
- (g) Kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kutoa huduma za kimahakama na kwenye uandishi wa nyaraka za kisheria;
- (h) Kujenga mifumo ya TEHAMA na kuendelea kuhimiza matumizi yake katika utoaji haki;
- (i) Kuharakisha upelelezi wa mashtaka ili kuharakisha upatikanaji haki nchini;
- (j) Kuzingatia matumizi ya adhabu mbadala ili kupunguza mlundikano wa mahabusu, wafungwa magerezani na kupunguza gharama za uendeshaji wa kesi;





- (k) Kuimarisha Tume ya Utumishi wa Mahakama ili iweze kusimamia kwa ufanisi maadili na nidhamu katika utumishi wa mahakama; na
- (l) Kuimarisha utendaji kazi wa watumishi katika sekta ya sheria kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ili kuongeza weledi na ubobezi katika tasnia husika na kuendana na kasi ya mabadiliko ya sheria kikanda na kimataifa.

### **Serikali za Mitaa**

121. Serikali za Mitaa ni vyombo vya wananchi kwa ajili ya kujiamulia mambo yao ikiwemo shughuli za maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Serikali hizi zimeundwa kwa ajili ya kupeleka madaraka na huduma karibu na wananchi na kuhakikisha wananchi wanashirikishwa katika uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo vijijini na mijini. Serikali za Mitaa zimeendelea kuimarika na kutoa huduma bora kwa wananchi. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020) mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- (a) Kurekebishwa kwa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 ili kuimarisha utoaji na usimamizi wa mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kutokana na sheria hiyo, mamlaka za serikali za mitaa zimetakiwa kutenga kiwango cha asilimia 10 ya mapato ya ndani na kuwapatia wanawake asilimia 4, vijana asilimia 4 na watu wenye ulemavu asilimia 2;
- (b) Mikopo ya shilingi bilioni 93.2 imetolewa ambapo vikundi vya wanawake vimepata shilingi bilioni 37.3, vikundi vya vijana shilingi bilioni 37.3 na vikundi vya watu wenye ulemavu shilingi bilioni 18.6 Mikopo hiyo imenufaisha jumla ya vikundi 32,553 vikiwemo vikundi 20,542 vya wanawake, vikundi 10,741 vya vijana na vikundi 1,270 vya watu wenye ulemavu;
- (c) Kuondolewa kwa kodi zenye kero ambapo ushuru wa mazao umepunguzwa kutoka asilimia 5 hadi asilimia 3 kwa mazao ya kibiashara na chakula yanayozidi tani moja na kuondolewa ushuru kwa wafanyabiashara wadogo wanaofanya shughuli zao katika maeneo yasiyokuwa rasmi;
- (d) Kuongeza udhibiti wa mapato ya ndani ya halmashauri kupitia mifumo ya kielektroniki ambapo halmashauri zimekusanya jumla ya shilingi trilioni 2.54 kati ya shilingi trilioni 2.99 zilizokadiriwa sawa na asilimia 85 ya lengo;
- (e) Miradi ya kimkakati yenye thamani ya shilingi bilioni 132.92 imetekelezwa katika halmashauri 18 na kuziwezesha mamlaka ya serikali za mitaa kuongeza mapato ya ndani ya halmashauri;
- (f) Majengo 70 ya utawala ya halmashauri yamejengwa ili kuboresha mazingira ya kufanyia kazi. Kati ya hayo, majengo 13 yamekamiliwa katika halmashauri za wilaya za Gairo, Itigi, Mkinga, Mkalama, Ikungi, Nanyamba, Rorya na Kilindi, Itilima, halmashauri za miji za Newala,



Mafinga na Njombe na halmashauri ya manispaa ya Kigamboni na halmashauri 57 zinaendelea na ukamilishaji wa miradi;

- (g) Kuimarisha usimamizi wa Serikali za Mitaa ambapo ofisi nne za wakuu wa mikoa ya Njombe, Songwe, Geita na Dodoma zimejengwa. Aidha, nyumba za wakuu wa mikoa minne ya Simiyu, Mwanza, Njombe na Songwe zimekamilika. Vilevile, nyumba tatu za makatibu tawala wa mikoa ya Simiyu, Njombe na Songwe zimekamilika;
- (h) Kuboreshwa kwa mazingira ya kazi kwenye ofisi za wilaya kwa kujenga na kukarabati Ofisi 12 za wakuu wa wilaya katika wilaya za Mwanga, Kigamboni, Ubungo, Wanging'ombe, Kalambo, Muleba, Biharamulo, Ruangwa, Busega, Mbinga, Nyamagana na Ikungi. Vilevile, nyumba nne za Wakuu wa Wilaya za Wanging'ombe, Mlele, Kyerwa na Kalambo zimejengwa na kukamilika na nyumba tano za makatibu tawala wa wilaya za Mlele, Tanganyika, Kyerwa, Kaliua na Itilima zimejengwa na zinatumika;
- (i) Kuboreshwa kwa usimamizi wa Serikali za Mitaa, ambapo ofisi 73 za maafisa tarafa zimejengwa katika mikoa ya Katavi, Tanga, Dar es Salaam, Kagera, Shinyanga, Kigoma, Lindi, Mbeya, Mtwara na Ruvuma;
- (j) Kupatia ufumbuzi wa kero za wafanyabiashara ambapo wafanyabiashara ndogo ndogo wametengewa maeneo ya kufanya shughuli zao na kupewa vitambulisho maalum vinavyowawezesha kufanya biashara bila bugudha. Jumla ya vitambulisho 1,591,085 vimetolewa kwa wafanyabiashara wadogo na kiasi cha shilingi bilioni 30.5 kimekusanywa;
- (k) Kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa kununua na kugawanywa mashine za kukusanyia mapato (*Point of Sale – POS*) 7,832;
- (l) Kurahisisha upatikanaji wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA katika halmashauri, mikoa, taasisi na wizara mbalimbali kwa kusanifu na kujenga Mifumo ya Mtandao Kiambo (LAN) na Mtandao Mpana (WAN) ambao imeunganishwa na Mikoa 26 na halmashauri 185 za Tanzania Bara. Vilevile, mfumo huu umewezesha na kuimarika kwa matumizi ya fedha katika serikali za mamlaka za mitaa ambapo halmashauri zilizopata hati inayoridhishwa zimeongezeka kutoka 138 mwaka 2015 hadi kufikia 176 mwaka 2018;
- (m) Kurahisisha urasimishaji wa biashara, kupunguza urasimu wa utoaji huduma za biashara na kuongeza idadi ya biashara zinazosajiliwa na halmashauri na kuongeza mapato ya ndani kwa kuanzishwa vituo 13 vya utoaji huduma za biashara na uwekezaji (*One Stop Business Centres*) katika halmashauri 16 za mikoa ya Dodoma na Kigoma;



- (n) Kuimarisha usafi wa mazingira na afya za wananchi kwa kujenga madampo saba ya kisasa katika majiji ya Dodoma, Tanga, Mbeya, Kigoma, Mtwara, Mwanza na Arusha na kukarabati madampo mawili katika halmashauri za manispaa za Moshi na Lindi. Aidha, magari 54 kwa ajili ya kusomba taka, mitambo mikubwa 10 kwa ajili ya kupakia taka, ununuzi wa *skip bucket* 231;
- (o) Kuboresha mazingira ya usafiri na kuongeza mapato ya halmashauri kwa kujenga stendi tisa za mabasi katika manispaa za Iringa, Songea, Sumbawanga, Singida, miji ya Njombe, Mpanda, Kibaha, Korogwe na Bariadi;
- (p) Kuboresha mazingira ya kufanyia biashara na kuongeza mapato ya halmashauri kwa kujenga masoko ya kisasa 12 katika halmashari ya manispaa za Temeke masoko sita (Kijichi, Makangalawe, Mbagala, Kilakala, Mtoni na Mbagala) Ilala tatu, (Kigalagila, Bomubomu, Minazi Mirefu), Kinondoni moja (Bwawani), Mtwara/Mikindani moja na Halmashauri ya Jiji la Dodoma soko moja;
- (q) Kuwapatia wananchi maeneo ya kupumzikia na kuongeza mapato kwa kujenga maeneo manne ya mapumziko (*recreational parks*) katika jiji la Dodoma na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara/Mikindani. Vilevile vituo vitatu vya kuegesha malori ya mizigo vimejengwa katika halmashauri za Manispaa ya Sumbawanga, Mji wa Bariadi na Jiji la Dodoma;
- (r) Kuboresha huduma za machinjio kwa kujenga machinjio tano za kisasa katika halmashauri za Lindi, Songea, Shinyanga na Geita;
- (s) Kuboresha maeneo ya makazi yasiyopangwa (*Resettlement Scheme*) katika kata 14 za jiji la Dar es Salaam kwa kuboresha barabara za mitaa, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita 40; na
- (t) Kubuni, kusanifu na kutengeneza mifumo ya TEHAMA ambayo imesaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali na kuongeza uwazi na uwajibikaji. Mifumo hiyo ni pamoja na:-
- (i) Kuboresha mtandao kiambo kwa halmashauri 147 na mtandao mapana wa OR-TAMISEMI kwa mikoa 26 na halmashauri 185 (*LAN and WAN Improvement*). Aidha, mtandao huu umeunganisha wizara tatu na taasisi 15 za Serikali na umewezesha kurahisisha upatikanaji wa mifumo ya TEHAMA kwa njia ya kielektroniki na uendeshaji wa mikutano kwa video (*video conference*) kati ya ofisi za wakuu wa mikoa yote nchini na taasisi nyingine;



- (ii) Kuwekwa kwa mfumo wa usimamizi wa fedha za umma wa *Epicor* kwa halmashauri 185 ambao umesaidia kudhibiti matumizi ya fedha za umma;
  - (iii) Kudhibiti matumizi ya fedha za umma katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma kwa kusimika mfumo wa usimamizi wa fedha na utoaji wa taarifa za kihesabu wa FFARS katika vituo zaidi ya 26,000 vya kutolea huduma za afya na elimu;
  - (iv) Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuweka mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS) unaotumika katika halmashauri 185 ambao umesaidia kupunguza mianya ya rushwa na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato;
  - (v) Kuongeza uwazi, uwajibikaji na kupunguza gharama za maandalizi na uwasilishaji wa bajeti kwa kufanya maboresho ya mfumo wa uandaaji wa mipango na bajeti kwa mamlaka ya serikali za mitaa (PlanRep);
  - (vi) Kuongeza ukusanyaji wa mapato na utoaji wa huduma kwa kuboresha mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa vituo vya kutolea huduma za afya wa GoTHOMIS unatumika katika vituo 518 vya kutolea huduma za afya;
  - (vii) Kuhabarisha umma kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Serikali katika mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa kusanifu mfumo wa utengenezaji na uendeshaji wa tovuti za Serikali uitwao GWF unaotumika katika mikoa 26, halmashauri 185, hospitali za mikoa 26 na taasisi 4;
  - (viii) Kusanifu mfumo unaoweza mifumo mbalimbali kubadilishana taarifa na hivyo kuwezesha upatikanaji na ubadilishanaji taarifa sahihi kwa wakati; na
  - (ix) Kurahisisha na kupunguza gharama ya zoezi la uchakataji wa maombi ya kazi kwa kusanifu mfumo kwa ajili ya maombi ya ajira za afya na walimu (HSRS na OTEAS).
- (u) Kuwapatia viongozi wa mikoa na wilaya vitendea kazi pamoja na kuwajengea uwezo katika maeneo ya uongozi na utawala bora, usimamizi na ufuatiliaji kama ifuatavyo:-
- (i) Kujenga uwezo wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kutoa huduma kwa wananchi kwa kutoa magari 123 yakiwemo 15 ya wakuu wa mikoa, saba ya makatibu tawala wa mikoa, 38 ya wakuu wa wilaya, 51 ya makatibu tawala wa wilaya, na 10 kwa ajili ya wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa. Aidha, pikipiki 413 zilinunuliwa kwa ajili ya maafisa tarafa;



- (ii) Kuboresha utoaji wa huduma kwenye mazingira magumu ya halmashauri zenye visiwa kwa kununua boti saba kwa halmashauri za Ludewa, Kibiti, Rufiji, Mafia, Ukerewe, Kigoma na Nyasa;
- (iii) Kuongeza uwezo wa uongozi na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa wakuu wa mikoa 26, makatibu tawala wa mikoa 26, wakuu wa wilaya 139 na wakurugenzi wa mamlaka za serikali mitaa 185 kwa kutoa mafunzo ya utawala bora na uongozi kwa viongozi hao;
- (iv) Kujenga uwezo wa usimamizi wa shughuli za Serikali katika ngazi ya Tarafa na Kata kwa Rais kufanya kikao kazi kwa Maafisa Tarafa 570 na Watendaji wa Kata 3,956 nchini. Vilevile, uwezo kuhusu uandaaji wa mipango na bajeti umejengwa kwa watumishi 659 wa ngazi ya mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;
- (v) Kujenga uwezo wa wananchi 1,500 katika mikoa ya Kigoma na Dodoma kwa kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali, uandaaji wa maandiko ya miradi kwa ajili ya kuwaunganisha na taasisi za fedha ili kupata mikopo na kukuza vipato vyao;
- (vi) Kuboresha uandishi wa Sheria Ndogo kwa kutoa mafunzo kuhusu Uandishi wa Sheria na tafsiri kwa Wanasheria 211 wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;
- (vii) Kuongeza uadilifu na uwajibikaji katika mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa kutoa mafunzo kwa kamati za kudhibiti uadilifu katika mikoa na halmashauri zote 185 nchini;
- (viii) Kuwajengea uwezo wa usimamizi wa rasilimaliwatu, utatuzi wa migogoro na mfumo wa uendeshaji serikali za mitaa kwa kutoa mafunzo elekezi kwa maafisa utumishi wa mikoa 26 na maafisa utumishi wa mamlaka za serikali za mitaa 185;
- (ix) Kuboresha uendeshaji wa mabaraza ya madiwani na usimamizi wa miradi katika mamlaka za serikali za mitaa kwa kutoa mafunzo kwa mameya na wenyeviti wa halmashauri 185, wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa 185 na wakuu wa idara ya utawala na rasilimaliwatu 184; na
- (x) Kuboresha utendaji kazi katika sekta ya elimu kwa kutoa mafunzo ya ujazaji fomu za OPRAS kwa walimu 880 wanaofundisha darasani katika kanda nne ambazo ni Kanda ya Kati na Kaskazini (Dodoma), Kanda ya Mashariki (Morogoro), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kusini (Iringa), Kanda ya Magharibi (Katavi).



122. **Kwa kutambua umuhimu wa kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi katika hali iliyo shirikishi, Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kitahakikisha kuwa Serikali za Mitaa zinaendelea kuboreshwa kwa lengo la kuinua ubora wa huduma kwa wananchi. Ili kufikia lengo hilo, Chama kitaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kuimarisha mifumo ya kitaasisi na uwezo wa viongozi na watendaji wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwenda vijijini kusikiliza na kushughulikia kero na malalamiko ya wananchi kwa wakati, kwa haki na uadilifu. Aidha, kuwapokea, kuwasikiliza na kuwahudumia wananchi wanaotembelea ofisi hizo kwa weledi, hekima na busara;
- (b) Kufanya mapitio ya sheria ya tawala za mikoa na sheria za serikali za mitaa ili kuendana na uboreshaji wa mifumo ya utoaji huduma kwa wananchi;
- (c) Kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha makusanyo ya mapato katika vyanzo vilivyopo ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi;
- (d) Kuimarisha serikali za mitaa ili ziendelee kuwa chombo cha kuwapa wananchi uwezo na sauti ya kuamua na kushiriki kwa karibu katika shughuli za maendeleo;
- (e) Kujenga uwezo wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kwa mafunzo, mifumo na vitendea kazi ili kuiwezesha kutoa huduma kwa wananchi;
- (f) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji na udhibiti wa mapato katika halmashauri zote nchini;
- (g) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za kijamii hususan afya, elimu, maji na miundombinu ya kiuchumi katika halmashauri zote nchini pamoja na kuongeza idadi ya wataalam mbalimbali;
- (h) Kubuni na kuibua miradi ya kimkakati ambayo itaboresha utoaji wa huduma katika mamlaka za serikali za mitaa na kuongeza mapato ya ndani na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu;
- (i) Kuimarisha utekelezaji wa maboresho ya serikali za mitaa kupitia sera na sheria mbalimbali ili kuendana na dhana ya kupeleka madaraka karibu na wananchi;
- (j) Kuimarisha Bodi ya Mikopo ya mamlaka za serikali za mitaa kwa kuhamasisha uchangiaji wa kila halmashauri;





- (k) Kuandaa sera ya maendeleo ya miji na kuendelea na utekelezaji wa programu ya uendelezaji wa miundombinu katika majiji, manispaa na miji ili iwe ya kisasa itakayochangia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi. Kipaumbele kitakuwa ni kuendeleza miji inayochipukia ili kuzuia uendelezaji usiozingatia taratibu za mipango miji;
- (l) Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kujenga ofisi za wakuu wa mkoa, wilaya, tarafa, kata na vijiji na nyumba za watumishi kwa kuweka kipaumbele katika maeneo ambayo hayana ofisi na nyumba za viongozi na watumishi;
- (m) Kuboresha mazingira ya kufanyia biashara na uwekezaji katika mamlaka za serikali za mitaa kwa kutenga maeneo ya uwekezaji na kuzipatia ufumbuzi kero za wafanyabiashara wadogo;
- (n) Kusimamia kikamilifu suala la utawala bora, uadilifu, uwajibikaji na matumizi sahihi ya rasilimali za umma pamoja na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika mamlaka hizo ili itekelezwe kwa kiwango kinachokusudiwa na kuhakikisha kuwa ubora wa miradi unalingana na thamani ya fedha iliyotumika (*value for money*);
- (o) Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa masuala yote yaliyoanishwa kwenye sheria za serikali za mitaa kama vile ulinzi wa amani, utulivu wa jamii na usalama;
- (p) Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa masuala mtambuka katika mamlaka za serikali za mitaa ikiwemo uhifadhi wa mazingira, usawa wa kijinsia, mapambano dhidi ya UKIMWI, mapambano dhidi ya rushwa na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na
- (q) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na utoaji wa huduma kwa wananchi ili kuchochea uchumi wa maeneo husika na kuongeza ajira.

### **Vyombo vya Habari**

123. Habari ni moja kati ya haki za msingi za binadamu kwa kuwa kila mwananchi anayo haki ya kupokea au kutoa habari kuhusu masuala mbalimbali yakiwemo ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kutokana na umuhimu wa sekta ya habari, vyombo vya habari vimepewa jukumu kubwa la kutoa habari, kuburudisha na kuelimisha jamii kuhusu matukio na masuala mbalimbali yanayojitokeza ndani na nje ya nchi. Upatikanaji wa habari sahihi na kwa wakati huchangia katika kukuza na kuimarisha demokrasia na utawala bora.

124. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), Chama Cha Mapinduzi kilichukua hatua za kusimamia sekta ya habari kikamilifu. Lengo kuu likiwa ni kuhakikisha wananchi wanapata habari sahihi na zenye uhakika kuhusu masuala mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi.



Mafanikio yaliyopatikana kutokana na hatua hiyo ni pamoja na wananchi kuongezewa wigo wa kupata habari ikiwa ni matokeo ya kuongezeka kwa idadi ya vyombo vya habari nchini. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na:-

- (a) Kuimarishwa kwa mazingira ya uwekezaji katika tasnia ya habari ili kupanua wigo wa wananchi kupata habari ambapo hadi mwaka 2020 jumla ya magazeti na majarida 231, redio 183 na televisheni 43 vimesajiliwa. Aidha, televisheni za mtandao zilizosajiliwa ni 264, blogs 85, redio mtandao 21 na Majukwaa ya Mtandaoni (*Online Forums*) sita;
- (b) Kuanzishwa kipindi maalum cha “TUNATEKELEZA” kinachorushwa hewani na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) chenye lengo la kuwawezesha wananchi kupata habari kuhusu utekezaji wa shughuli za Serikali katika Sekta mbalimbali ambapo jumla ya vipindi 212 viliratibiwa na kurushwa hewani;
- (c) Kuimarisha utoaji wa taarifa na ufafanuzi wa masuala mbalimbali kupitia mikutano 64 ya waandishi wa habari iliyoratibiwa na wizara na taasisi za umma na kuanzishwa kwa MAELEZO TV, *Blog* ya MAELEZO, *Tweeter* ya Msemaji Mkuu wa Serikali na Tovuti maalum. Aidha, Jarida Maalum la **NCHI YETU** linaloelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano lilichapishwa na jumla ya nakala 15,000 zilisambazwa;
- (d) Kuimarisha weledi katika tasnia ya habari kwa kutunga Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya Mwaka 2016 na Kanuni zake za Mwaka 2017;
- (e) Kuimarishwa kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kwa kuliunganisha na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuongeza ufanisi;
- (f) Kuongezeka kwa usikivu wa Redio za TBC kutoka wilaya 87 mwaka 2017 hadi wilaya 102 mwaka 2019;
- (g) Kuimarika kwa urushaji wa matangazo moja kwa moja kupitia kituo cha utangazaji cha TBC ambapo Shirika limeimarishwa kwa kuongezewa vifaa vya kisasa (*Live-U equipment*) vinne kwa ajili ya kurushia matangazo ya moja kwa moja kwa njia ya intaneti na kifaa kimoja cha kurushia matangazo ya moja kwa moja kwa njia ya satelaiti na kuweza kurusha matangazo mubashara sehemu nne tofauti kwa wakati mmoja;
- (h) Kuanzishwa Chaneli ya Utalii (*Tanzania Safari Channel*) kwa ajili ya kutangaza fursa za utalii, maliasili, utamaduni na urithi mwingine wa nchi yetu; na



- (i) Kuboresha mazingira ya maandishi wa habari ikiwa ni pamoja na kuwatambua, ambapo wastani maandishi wa habari 729 walipewa vitambulisho kwa kila mwaka.

**125. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuhakikisha sekta ya habari inaboreshwa ili kuwaongezea wananchi fursa ya kupata habari kwa kuongeza wigo wa upashanaji wa habari. Ili kufikia malengo hayo, Chama kitaelekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa sahihi kwa urahisi zaidi na kwa wakati kwa mujibu wa sheria kwa kuendelea kutekeleza Sheria ya Huduma za Habari Na. 12 ya Mwaka 2016;
- (b) Kuhakikisha kuwa uhuru wa vyombo vya habari unaimarishwa na kulindwa, na kwamba wamiliki na wanahabari wanazingatia maadili na weledi katika kazi zao;
- (c) Kuhakikisha wanahabari wanapatiwa mikataba ya ajira inayozingatia sheria za kazi;
- (d) Kuhakikisha uhuru wa kupata na kutoa habari unaendelea kutekelezwa kwa mujibu wa sheria na wadau wote wanatimiza wajibu wao;
- (e) Kuimarisha uwezo wa Idara ya Habari - MAELEZO kwa kuipatia rasilimali watu na vitendea kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi;
- (f) Kuliimarisha Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) kwa kulijengea uwezo wa rasilimaliwatu, fedha na vifaa vya kisasa ili liweze kufikisha matangazo ya redio na televisheni nchini kote kwa ubora na usikivu mzuri ikiwa ni pamoja na kuanzisha ofisi na studio za kisasa makao makuu ya nchi jijini Dodoma na kwenye kanda zote za TBC;
- (g) Kuiwezesha TBC kuimarisha chaneli za kimataifa ili liendelee kuitangaza nchi yetu kimataifa;
- (h) Kuhamasisha matumizi ya mitandao ya kijamii ili kuongeza upatikanaji wa habari; na
- (i) Kuhamasisha ushiriki wa vyombo vya habari katika kuitangaza vema Tanzania ndani na nje ya nchi.

**Jumuiya na Asasi za Kijamii na Kiraia**

- 126.** Chama Cha Mapinduzi kinatambua umuhimu wa mchango wa jumuiya na asasi za kijamii na kiraia katika kuimarisha demokrasia, haki za binadamu na maendeleo ya nchi na watu wake. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015–2020), Chama kimesimamia Serikali kuweka mazingira



wezeshi ya ushiriki wa jumuiya na asasi za kiraia katika ajenda za maendeleo na kupata mafanikio yafuatayo:-

- (a) Kuongezeka kwa usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoka 4,203 mwaka 2015 hadi 10,351 mwaka 2020;
- (b) Kuimarisha uwazi na uwajibikaji wa jumuiya na asasi za kijamii na kiraia kwa kuboresha sheria inayohusu mifumo ya usajili na uratibu wa jumuiya hizo ikiwemo marekebisho ya kanuni;
- (c) Kuandaa mwongozo wa uratibu wa jumuiya na asasi za kijamii na kiraia ili kuwezesha utendaji wa jumuiya hizo ufanyike kwa ufanisi, tija na kuzingatia masilahi ya Taifa; na
- (d) Kuweka mfumo wa kielektroniki wa taarifa za jumuiya na asasi za kijamii na kiraia ili kurahisisha uratibu wa upatikanaji wa taarifa kuhusu utekelezaji wa shughuli za asasi za kijamii na kiraia.

127. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama kitaendelea kusimamia Serikali kuhakikisha inaweka mazingira wezeshi kwa Jumuiya na Asasi za Kijamii na Kiraia ili ziendeleo kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi kwa kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kuimarisha mazingira wezeshi na ushirikiano baina ya Serikali na jumuiya na asasi za kijamii na kiraia ili kuwezesha kutoa mchango mkubwa zaidi katika kuimarisha demokrasia, haki za binadamu na maendeleo ya watu;
- (b) Kuimarisha uratibu wa jumuiya na asasi za kijamii na kiraia ili kuhakikisha jumuiya hizo zinatekeleza majukumu yake kwa kufuata dhana ya uwazi na uwajibikaji kwa wananchi kwa kuzingatia vipaumbele vya nchi;
- (c) Kuimarisha mifumo ya kisera na kisheria ambayo itasaidia jumuiya na asasi za kijamii na kiraia kufanya kazi kwa ufanisi, tija na kuzingatia masilahi ya Taifa; na
- (d) Kutambua michango jumuiya na asasi za kijamii na kiraia kwenye miradi ili kuhakikisha jumuiya hizo zinakuwa na tija na kuongeza mchango wake katika pato la Taifa.

### **Wafanyakazi na Vyama vya Wafanyakazi**

128. Nchi yetu imeendelea kutambua mchango mkubwa wa wafanyakazi katika ujenzi wa uchumi kutokana na nafasi yao katika uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma kwa jamii. Kutokana na umuhimu huo, wafanyakazi wamekuwa wakipatiwa fursa ya kujiunga na vyama mbalimbali vya wafanyakazi. Vyama hivyo, ni huru na vimeendelea kuundwa na kusimamiwa na wafanyakazi wenyewe kwa lengo la kutetea masilahi yao mahali pa kazi. Chama Cha



Mapinduzi kwa kutambua umuhimu wa wafanyakazi na vyama vyao, kimeendelea kusimamia Serikali kuweka mazingira wezeshi ya kuongeza fursa za majadiliano kati ya waajiri na wawakilishi wa wafanyakazi nchini.

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMBA

129. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015-2020), mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa ufanisi mahala pa kazi kutokana na kupungua kwa migomo na migogoro kati ya wafanyakazi na waajiri. Aidha, masilahi na mazingira ya kazi yameendelea kuboreshwa. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na:-
- (a) Kuongezeka kwa vyama vya wafanyakazi kutoka 31 mwaka 2015 hadi kufikia vyama na mashirikisho 35 mwaka 2020;
  - (b) Kuimarisha mifumo ya kushughulikia mishahara na masilahi katika sekta ya umma na binafsi;
  - (c) Kima cha chini cha mishahara katika sekta binafsi kimeongezeka kati ya asilimia 25 hadi 45 ya viwango vya mishahara vya mwaka 2015 kutokana na kuandaliwa utaratibu wa kisheria uliowezesha waajiri katika sekta binafsi kulipa viwango vya mishahara hata zaidi ya kiwango kinachowekwa kama kima cha chini pale mbapo wanaona itaongeza motisha kwa wafanyakazi wao kufanya kazi kwa bidii zaidi;
  - (d) Kupungua kwa kodi ya mapato katika mishahara ya wafanyakazi (PAYE) kutoka asilimia 12 mwaka 2015 hadi asilimia 9 mwaka 2020;
  - (e) Kufanyika kwa marekebisho katika sheria za kazi na kuwawezesha wafanyakazi kujiunga katika vyama huru vya wafanyakazi ili kushughulikia masilahi yao na kuongeza tija na uzalishaji sehemu za kazi;
  - (f) Kuboresha usalama mahali pa kazi kwa kuwezesha utoaji wa matibabu na fidia ambapo wafanyakazi 408,252 walipimwa afya na waajiri wao;
  - (g) Kuboresha mazingira ya kazi katika maeneo yaliyo hatarishi kwa wafanyakazi ambapo kaguzi 562,962 zimefanyika kujumuisha kaguzi za umeme, mitambo ya kuzalisha mvuke (*boilers*), mitungi ya hewa na mvuke, zana za kunyanyulia vitu vizito na vipimo vya mazingira ikiwa ni wastani wa kaguzi 150,000 kwa mwaka kwa lengo la kuhakikisha waajiri wanafuata sheria za kazi ipasavyo;
  - (h) Wafanyakazi na waajiri 656,900 walipatiwa mafunzo kuhusu usalama na afya mahali pa kazi katika kusaidia kuboresha mifumo ya usimamizi wa afya na usalama mahali pa kazi. Aidha, wafanyakazi wapatao 2,670,000 na waajiri 10,690 wamepewa elimu kuhusu sheria na miongozo mbalimbali ya kazi;
  - (i) Muda wa kushughulikia utatuzi wa migogoro kwenye hatua ya usuluhishi umepungua kutoka siku 30 hadi siku zisizozidi 15. Aidha,



migogoro 24,281 imesuluhishwa ambapo uamuzi ulitolewa kwa migogoro 16,200 na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA). Vilevile, mabaraza ya wafanyakazi 688 yameundwa katika taasisi za sekta binafsi;

- (j) Kuendelea kushirikisha wafanyakazi katika hatua za maamuzi kupitia mabaraza ya wafanyakazi ili kuimarisha mahusiano mahala pa kazi;
- (k) Kuboresha sheria na muundo wa kitaasisi wa kusimamia mafao ya wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kuunganisha taasisi za mifuko ya pensheni (*PPF, PSPF, LAPF na GEPP*) na kuanzisha mfuko wa *PSSSF* ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuboresha mafao; na
- (l) Kuongeza wigo wa hifadhi ya jamii kwa kuendelea kuimarisha Mfuko ya Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko ya Afya ya Jamii (CHF).

**130. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, lengo la Chama Cha Mapinduzi ni kuendelea kuweka mazingira rafiki ya utendaji wa vyama vya wafanyakazi ili viendeele kuwa nguzo muhimu katika kujenga mahusiano mahala pa kazi na kuboresha masilahi na haki za wafanyakazi. Ili kufikia lengo hilo, Chama kitaelekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi ili kuhakikisha kuwa ajira zaidi zinazalishwa ili kukidhi mahitaji;
- (b) Kuendeleza majadiliano stahiki kuhusiana na uboreshaji wa masilahi ya wafanyakazi pamoja na masuala mengine yanayohusu uzingatiji wa haki na wajibu wa wafanyakazi na waajiri;
- (c) Kuimarisha taasisi za hifadhi ya jamii na kuhamasisha wananchi, hususan wafanyakazi kwenye sekta rasmi na isiyo rasmi kujiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii;
- (d) Kuboresha na kuimarisha mfumo wa fidia ya wafanyakazi ili uweze kuwahudumia wafanyakazi vizuri zaidi;
- (e) Kuimarisha mfumo wa kitaasisi unaoshughulikia migogoro baina ya waajiri na wafanyakazi;
- (f) Kujenga uwezo wa waajiri na wafanyakazi kuhusu afya na usalama mahala pa kazi;
- (g) Kuendeleza mipango ya kuboresha masilahi ya wafanyakazi ili waweze kumudu gharama za maisha;





- (h) Kuboresha mishahara ya watumishi wa umma kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi wa Taifa na tija ya wafanyakazi;
- (i) Kuhakikisha kuwa masilahi ya watumishi wa umma ikiwemo upandishaji vyeo kwa mujibu wa miundo ya utumishi wa kada mbalimbali yanazingatiwa;
- (j) Kuendeleza mipango ya usimamizi wa rasilimaliwatu kwa kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa watumishi wa umma wanakuwa na sifa stahiki na wanafanya kazi kwa uadilifu, uwajibikaji, weledi, bidii na maarifa ili kuimarisha utoaji huduma bora kwa wananchi;
- (k) Kuridhia na kutekeleza mikataba ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) yenye masilahi kwa Taifa na wafanyakazi;
- (l) Kuboresha mazingira ya utendaji wa wafanyakazi wa sekta ya umma na sekta binafsi ikiwemo kuimarisha mabaraza ya wafanyakazi, kuhimiza majadiliano ya pamoja kati ya waajiri na wafanyakazi na kuhakikisha wafanyakazi wanapewa mikataba ya kazi kwa mujibu wa sheria;
- (m) Kuimarisha mifuko ya hifadhi ya jamii na misaada ya kijamii ili kutoa huduma bora na endelevu kwa makundi mbalimbali ya kijamii na kwa wananchi wengi zaidi;
- (n) Kuhamasisha vyama na taasisi za kitaaluma kuendelea kujenga utawala bora, kuhimiza uzingatiaji wa maadili ya kitaaluma, na kuhimiza weledi katika utekelezaji wa wajibu;
- (o) Kuandaa sera ya kinga ya jamii (*social protection policy*) ili kuhakikisha makundi mbalimbali ya kijamii katika Taifa letu yanakuwa na hifadhi na kinga ya kijamii; na
- (p) Kusimamia uwekezaji wa mifuko ya hifadhi ya jamii ili kuwanufaisha wachangiaji.



## SURA YA SABA

### MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA

131. Ushirikiano wa nchi yetu na nchi nyingine ni fursa muhimu katika kuleta maendeleo na kudumisha amani. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 – 2020), Chama Cha Mapinduzi kilielekeza Serikali kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa, hususan katika eneo la diplomasia ya siasa na uchumi ambayo inawezesha nchi yetu kunufaika na fursa za kiuchumi zinazopatikana nje ya nchi yetu. Pamoja na mikakati mingine, Chama kilielekeza Serikali kuendelea kushiriki katika masuala mbalimbali ya kikanda na kimataifa ili kutumia fursa za kiuchumi na kijamii. Kupitia hatua hizo, mafanikio yafuatayo yalipatikana:-
- (a) Kuimarisha na kudumisha mahusiano ya kidiplomasia na nchi nyingine kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufungua ofisi mpya za ubalozi nane katika nchi za Algeria, Uturuki, Korea Kusini, Qatar, Sudan, Israel, Cuba na Namibia;
  - (b) Kuongezeka kwa fursa za biashara na uwekezaji kupitia utekelezaji wa diplomasia ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na kufanya makongamano, mikutano baina ya nchi na nchi, jumuiya za kikanda na kimataifa, na uratibu wa maonyesho ya biashara na utalii. Baadhi ya nchi zilizohusika ni: Uturuki, Oman, Vietnam, Misri, Kenya, China, Marekani, Ujerumani, Sweden, na Japan. Aidha, baadhi ya jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa tulizoshirikiana nazo ni pamoja na EAC, SADC, UNCTAD, WTO na Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa;
  - (c) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za Umoja wa Mataifa ikiwemo mikutano ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ili kulinda na kutetea masilahi ya nchi na kushiriki katika kuimarisha amani na usalama, haki, usawa na maendeleo kwa wote duniani;
  - (d) Kuimarisha ushirikiano wa kikanda ikiwa ni pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ambapo Tanzania ilikuwa Mwenyekiti kwa miaka miwili mfululizo kuanzia mwaka 2015/16 na mwaka 2016/17. Vilevile, utangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeimarishwa kwa kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha na Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Tanzania imeendelea kushiriki katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ikiwa ni pamoja na kushika nafasi ya Makamu Mwenyekiti (2018/19) na Mwenyekiti wa Jumuiya (2019/20);



- (e) Kushiriki katika juhudi za kuleta amani duniani kwa kupeleka vikosi vya kulinda amani ambapo jumla ya walinda amani 2,303 wameshiriki kwenye misheni sita za Umoja wa Mataifa. Misheni hizo ni MONUSCO (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo), UNAMID (Darfur, Sudan), UNIFIL (Lebanon), UNMISS (Sudan Kusini), UNISFA (Abyei, Sudan) na MINUSCA (Jamhuri ya Afrika ya Kati). Aidha, Tanzania imeshiriki kikamilifu katika kuongoza juhudi za kuleta suluhisho la kisiasa nchini Lesotho na Burundi;
- (f) Kufanikiwa kudumisha ushirikiano na nchi zote jirani kwa kuratibu na kushiriki katika mikutano na mataifa hayo. Mikutano hiyo ni pamoja na Tanzania na Msumbiji (Mtwara, Ruvuma na majimbo ya Niassa na Cabo Delgado ya Msumbiji), Tanzania na Rwanda (Kagera na Jimbo la Mashariki la Rwanda);
- (g) Kuimarisha mahusiano ya kimataifa kwa kutembelewa na wakuu wa nchi na serikali mbalimbali. Miongoni mwa wakuu wa nchi na Serikali waliokuja nchini ni pamoja na kutoka: India, Morocco, Zimbabwe, Uganda, Rwanda, Burundi, Msumbiji, Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Afrika Kusini, Vietnam na Uturuki;
- (h) Kuimarisha mahusiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine kwa ziara za viongozi wetu nje ya nchi. Miongoni mwa ziara hizo ni: Ziara za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nchi za Kenya, Rwanda, Uganda, Malawi, Afrika Kusini, Namibia na Zimbabwe; ziara za Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Niger, Zimbabwe, Afrika Kusini, Namibia, Angola na Eswatini; ziara za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nchini Comoro, Indonesia, Djibouti, Kenya na UAE; na ziara za Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Mauritius, Misri, Ethiopia, Urusi, Canada, Uingereza, Cuba, China na Japan;
- (i) Kudumisha ushirikiano na taasisi mbalimbali za kimataifa kwa kuratibu ziara za viongozi na wataalam waliokuja nchini kwa masuala mbalimbali ya kijamii na kimaendeleo wakiwemo: Rais wa Benki ya Dunia; Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika; Rais wa Benki ya Mashariki na Kusini mwa Afrika. Makubaliano yaliyofikiwa wakati wa ziara hizo yamesaidia kuchochea maendeleo ya nchi katika nyanja mbalimbali;
- (j) Kushiriki kikamilifu katika majadiliano yaliyoweza kuanzishwa kwa eneo huru la biashara barani Afrika (*Continental Free Trade Area*);
- (k) Kushawishi nchi za jumuiya ya SADC kupitisha azimio la kutaka vikwazo vya kiuchumi dhidi ya Zimbabwe viondolewe; na
- (l) Kuendeleza msimamo wa Tanzania kuhusu masuala muhimu ya dunia kwa kushiriki kwenye majukwaa yanayopaza sauti kuhusu



kuwepo kwa usawa duniani ikiwemo G 77 + China, Harakati za Nchi Zisizofungamana na Siasa za Upande Wowote (NAM) na WTO.

132. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha kuwa mahusiano ya nchi yetu kikanda na kimataifa yanaendelea kuimarishwa katika maeneo mbalimbali. Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kuwa mstari wa mbele katika masuala ya kuimarisha amani, uhuru, na masilahi ya Taifa katika nyanja za kimataifa ikiwa ni pamoja na kutumia fursa za kiuchumi zitokanazo na mahusiano hayo. Ili kuifikia azma hiyo, Chama kitaelekeza Serikali kutekeleza yafuatayo: -**

***Diplomasia ya Siasa***

- (a) Kuboresha utekelezaji wa mipango ya kuimarisha diplomasia ya siasa ya kimkakati kwa ajili ya kulinda amani, uhuru, masilahi ya Taifa na kuimarisha ujirani mwema;
- (b) Kuboresha na kuimarisha uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine na taasisi za kimataifa;
- (c) Kuimarisha sauti ya Tanzania na taswira yake katika medani ya uhusiano wa kikanda na kimataifa;
- (d) Kupigania mfumo wa haki wa utawala, siasa na uchumi duniani; na
- (e) Kushawishi na kuhamasisha matumizi Kiswahili kama lugha ya diplomasia katika jumuiya mbalimbali za kikanda na kimataifa.

***Diplomasia ya Uchumi***

- (a) Kukuza mahusiano ya kiuchumi na mataifa, jumuiya za kikanda na taasisi nyingine za kimataifa;
- (b) Kulinda uchumi na masilahi mapana ya Taifa kwa kutumia jiografia ya nchi kimkakati na ushawishi wa kihistoria, hususan kwenye Ukanda wa Kusini;
- (c) Kuhakikisha kuwa balozi zetu zinakuwa kiungo muhimu cha kukuza uwekezaji na upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma zetu;
- (d) Kuweka mazingira wezeshi na kuendelea kuratibu na kuhamasisha ushiriki wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi (*Diaspora*) ili waweze kuzitangaza fursa zinazopatikana nchini na kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo hususan ya kiuchumi ya nchi yetu; na
- (e) Kulinda na kutetea misingi ya Taifa letu ndani na nje ya nchi kwa kuweka msisitizo katika diplomasia ya uchumi.

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA



***Mambo Mtambuka ya Kidiplomasia***

- (a) Kujenga au kununua majengo kwa ajili ya balozi za Tanzania kwenye nchi ambazo kwa sasa yanakodishwa ili kupunguza gharama na kuleta mapato kwa Serikali;
- (b) Kuzihamasisha balozi na jumuiya za kimataifa kufungua ofisi ndogo za uwakilishi Zanzibar;
- (c) Kufungua balozi na konseli kuu mpya kwa kadri itakavyohitajika;
- (d) Kuhamasisha balozi hapa nchini kuhamia Makao Makuu ya Nchi Dodoma;
- (e) Kuendeleza jitihada za kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi kwenye jumuiya za kikanda zinazohusu nchi yetu; na.

***Jumuiya ya Afrika Mashariki***

- (a) Kushiriki kikamilifu katika kuimarisha utangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- (b) Kubuni na kuijumuisha katika programu za Jumuiya miradi ya kipaumbele na itakayochangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu;
- (c) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuhakikisha Tanzania inanufaika kikamilifu katika shughuli za uchumi na soko la pamoja la Afrika Mashariki; na
- (d) Kuendeleza mipango ya kutumia ipasavyo fursa za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuzingatia masilahi mapana ya Taifa.

***Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika***

- (a) Kuendeleza mafungamano ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kuendelea kuweka mazingira bora yatakayowezesha Tanzania kushiriki kikamilifu katika uchumi wa kikanda;
- (b) Kuweka mikakati ya kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili ili kutumia fursa inayotokana na lugha hiyo kuridhiwa kuwa lugha rasmi ya nne ya kazi katika SADC;
- (c) Kuimarisha ushirikiano wa nchi wanachama wa SADC katika kukabiliana na masuala mbalimbali yakiwemo uharamia, ugaidi, usafirishaji wa dawa za kulevya; biashara haramu ya silaha na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu; na
- (d) Kujenga uelewa mkubwa zaidi miongoni mwa mataifa ya Afrika kuhusu urithi wa ukombozi na mchango mkubwa wa Tanzania katika ukombozi wa Afrika hususan Afrika ya Kati na Kusini mwa Afrika.



### ***Umoja wa Afrika***

- (a) Kushiriki kikamilifu katika juhudi za kuimarisha umoja na mshikamano wa Bara la Afrika;
- (b) Kuendeleza ushiriki wa nchi yetu katika usuluhishi na upatanishi pamoja na ulinzi wa amani katika nchi za Afrika; na
- (c) Kuitangaza lugha ya Kiswahili katika Umoja wa Afrika kama urithi wa utamaduni wa Mtanzania na Mwafrika kwa ujumla.

### ***Umoja wa Mataifa***

- (a) Kushiriki katika kujenga mfumo bora na wa haki duniani unaojali masilahi ya mataifa yote hususan mataifa ya Afrika na ya Kusini mwa dunia;
- (b) Kuendeleza misingi ya nchi yetu kuwa isiyofungamana na upande wowote;
- (c) Kushiriki katika kuimarisha Umoja wa Mataifa ili uwe chombo cha haki na usawa kwa mataifa yote kwa kushiriki katika juhudi za kufanya mageuzi ya mfumo wa Umoja wa Mataifa;
- (d) Kushirikiana na nchi na taasisi za kimataifa katika usuluhishi na upatanishi pamoja na ulinzi na usalama wa dunia; na
- (e) Kushiriki katika juhudi za kufanya mabadiliko katika mfumo wa biashara wa dunia kwa ajili ya kutetea masilahi ya nchi yetu na nchi zinazoendelea kwa ujumla.

### ***Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote (Non-Alignment Movement)***

- (a) Kushiriki kikamilifu katika mikutano ya majadiliano ya shughuli za umoja huu ili kuendeleza umoja na kulinda masilahi ya nchi yetu; na
- (b) Kushiriki katika kuimarisha na kuhuisha umoja huu katika mazingira mapya.

### ***Jumuiya ya Madola (Common Wealth)***

Kushiriki kikamilifu katika shughuli za Jumuiya ya Madola kwa manufaa ya Taifa letu na Jumuiya hiyo kwa ujumla.

### ***Jumuiya Nyingine za Kimataifa***

Kuimarisha ushiriki katika jumuiya nyingine za kimataifa zikiwemo *Indian Ocean Rim Association, Indian Ocean Tuna Commission, South South Commission, South West Indian Ocean Fisheries Commission.*





## SURA YA NANE

### MAZINGATIO MAALUM YA ILANI KUHUSU ZANZIBAR

#### Utangulizi

133. Kwa kuzingatia mazingira maalum ya Zanzibar, CCM inaendelea kuwa na sehemu maalum katika Ilani yake kwa ajili ya kutekeleza sera zake kwa Zanzibar. CCM inathamini, kuenzi na kutekeleza sera za msingi za Mapinduzi zilizoasisiwa na Chama cha ASP ikiwa ni pamoja na kugawa ardhi kwa wanyonge, kutoa huduma ya afya na elimu bure kwa wote, kuwapatia wananchi makaazi bora, kuondoa dhuluma na kujenga ujamaa.
134. Ilani hii ni muendelezo wa utekelezaji wa Mwelekeo wa Sera za CCM za miaka ya tisini na elfu mbili ambazo ziliendeleza mageuzi ya kiuchumi na kijamii na kupunguza umasikini kwa kukuza uchumi unaonufaisha wananchi walio wengi; kukuza uwezo wa rasilimali watu; kutoa huduma bora kwa wananchi wote; kuhifadhi mazingira na kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kushikamana na misingi ya utawala bora. Wazanzibari wameendelea kuridhika na kuzikubali sera hizo na hivyo kuichagua CCM kuongoza SMZ kupitia chaguzi zote zilizopita.
135. Katika kipindi cha mwaka 2020 - 2025 cha Awamu ya Nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Ilani hii ya uchaguzi imeweka bayana dhamira ya CCM katika kuwajengea Wazanzibari misingi imara ya kiuchumi na kijamii, utawala bora pamoja na kuimarisha huduma za jamii. Utekelezaji wa makusudio hayo unakwenda sambamba na malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya Mwaka 2050, mikakati na mipango ya maendeleo ya kipindi cha miaka mitano ijayo (2020-2025).
136. Katika miaka mitano ijayo kwa mazingatio maalum ya Zanzibar CCM itaisimamia SMZ kuzingatia misingi ya vipaumbele vifuatavyo:-
- (a) Kuendeleza jitihada za kuwaunganisha Wazanzibari wote na kubaki kuwa wamoja;
  - (b) Kuhakikisha maendeleo ya uchumi yanazingatia usawa na yananufaisha maeneo yote ya Zanzibar;
  - (c) Kuimarisha upatikanaji wa ajira kwa vijana kwa kuzalisha ajira angalau 300,000 kwenye sekta rasmi na isiyo rasmi ifikapo mwaka 2025;
  - (d) Kupitia upya mfumo wa elimu ya ufundi na amali ili uweze kusajili vijana wengi zaidi na kuzalisha wataalam mahiri wa ngazi ya msingi na ya kati wenye ujuzi katika fani zao na uwezo wa kujiajiri na kuajirika mahali popote duniani; na



- (e) Kuibua na kuendeleza sekta mpya za uchumi ikiwemo uchumi wa buluu (*blue economy*), ubunifu (*creative industry*) na uchumi wa kidigitali (*digital economy*)
- (f) Kuendeleza kilimo cha kisasa kilichoungana vyema na sekta za huduma na viwanda kinachozingatia udogo wa ardhi ya Zanzibar, utajiri wa rasilimali za baharini na kuzitumia ipasavyo rasilimali hizo.

### Hali ya Uchumi

137. Ilani ya CCM ya uchaguzi ya mwaka 2015 - 2020 ilielekeza SMZ kuchukua hatua mbalimbali za kimaendeleo ikiwemo kufanya mapitio ya mipango ya kukuza uchumi na kuandaa mikakati imara inayoweza kufikiwa malengo ya mikakati hiyo na kuweka mazingira yatakayoweza uchumi wa Zanzibar kufikia kiwango cha uchumi wa kipato cha kati. Vile vile, mfumko wa bei kubaki katika tarakimu moja na kuimarisha wastani wa pato la kila mwananchi, kudhibiti na kuongeza mapato ya ndani kufikia shilingi bilioni 800 pamoja na kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ya Serikali.
138. SMZ imetekeleza Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 - 2020 na kupata mafanikio makubwa kama ifuatavyo:-
- (a) Kufanya mapitio ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA II) uliomalizika mwaka 2015 na kuwezesha kuandaa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Awamu ya Tatu (MKUZA III) ulioanza kutekelezwa mwaka 2016. Tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2020 imefanywa na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 imeandaliwa;
  - (b) Kuongeza Pato la Taifa kutoka thamani ya shilingi trilioni 2.4 mwaka 2015 hadi kufikia thamani ya shilingi trilioni 3.1 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 30.6. Uchumi wa Zanzibar umekuwa kwa wastani wa asilimia 6.8 kwa mwaka katika kipindi hicho uliopelekea kuongezeka kwa pato la mwananchi mmoja mmoja kutoka wastani wa shilingi 1,666,000 (USD 834) mwaka 2015 hadi shilingi 2,549,000 (USD 1,114) mwaka 2019. Kisekta, uchumi wa Zanzibar umeendelea kuchangiwa zaidi na sekta ya huduma (asilimia hamsini) na sekta ya kilimo imechangia wastani wa asilimia ishirini na hivyo kuashiria kuendelea kufanikiwa kwa mageuzi ya msingi ya kiuchumi;
  - (c) Kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani kutoka shilingi bilioni 428.511 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 748.9 mwaka 2019;
  - (d) Kupunguza utegemezi wa bajeti na kufikia asilimia 5.7 na kuvuka lengo lililoainishwa katika Ilani la kufikia asilimia 7 ifikapo 2020;
  - (e) Kudhibiti kasi ya mfumko wa bei kubaki kwenye tarakimu moja katika kipindi chote cha utekelezaji wa Ilani kutoka asilimia 5.7 mwaka 2015 hadi asilimia 2.7 mwaka 2019;



- (f) Kutunga Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali ya Mwaka 2016, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2016 sambamba na kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali (ZPPDA) na Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani kwa lengo la kudhibiti matumizi ya rasilimali;
- (g) Kuimarisha Mfumo wa Udhibiti na Usimamizi wa Matumizi ya Serikali (IFMS) kwa kuweka toleo jipya la *EPICOR* na kuziunganisha moja kwa moja taasisi zinazokusanya mapato kwa kutoa risiti za makusanyo kwa wakati pamoja na kufanya malipo kupitia akaunti za benki; na
- (h) Kuongeza usimamizi wa fedha kwa kuwapatia mafunzo watendaji 444 kuhusu usimamizi wa fedha (CPA, IPSAS na IFRS), ununuzi na uondoshaji wa mali chakavu na usimamizi wa mitaji ya umma.

**139. CCM itaendeleza kasi ya mageuzi ya uchumi na kuwa wa kisasa, himilivu na unaonufaisha wananchi walio wengi hasa vijana. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, CCM itaelekeza SMZ kuhakikisha kwamba :-**

- (a) Uchumi unaendelea kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 8 na kuinua ustawi wa Wazanzibari kwa kuongeza wastani wa pato la mtu kuelekea Kiwango cha Juu cha Wastani wa Nchi za Uchumi wa Kati (UMIS);
- (b) Kutengeneza fursa mpya za ajira rasmi na sekta zisizo rasmi 300,000 ifikapo mwaka 2025 hususan kwa vijana ili kusaidia kupunguza umasikini;
- (c) Kunakuwepo utulivu wa uchumi ambao ni shirikishi na endelevu kwa kufanya yafuatayo:-
  - (i) Kudhibiti mfumko wa bei na kubaki kwenye tarakimu moja;
  - (ii) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kutoka wastani wa shilingi bilioni 800.0 kwa mwaka 2019 hadi shilingi trilioni 1.55 mwaka 2025;
  - (iii) Kuendelea kupunguza asilimia ya utegemezi wa bajeti ili usizidi kiwango cha tarakimu moja na hivyo kuwa na uhakika wa kuendeleza mipango ya maendeleo ya nchi yetu;
  - (iv) Kusimamia deni la Taifa liendeleo kuwa himilivu na kuhakikisha kuwa mikopo yote ina tija kubwa kwa maendeleo;
  - (v) Kuongeza uzalishaji wa bidhaa hasa za viwandani kwa ajili ya mauzo ya nje ya nchi na katika soko la kikanda;



- (vi) Kuimarisha sekta ya huduma hususan utalii na usafirishaji ili iendelee kutoa mchango mkubwa zaidi katika uchumi;
- (vii) Kutumia kikamilifu rasilimali za ndani kwa kuleta maendeleo ya kiuchumi;
- (viii) Kuimarisha sekta ya fedha kwa kupanua huduma za fedha na mitaji hadi vijijini kwa lengo la kuwafikia wananchi wengi; na
- (ix) Kuendeleza sekta mpya za uchumi ikiwemo sekta ya mafuta na gesi asilia, uchumi wa buluu (*blue economy*), sekta ya ubunifu (*creative industry*) na uchumi wa kidijitali (*digital economy*) ili zitoe mchango katika pato la Taifa.

### Mchango wa Sekta Binafsi

140.

CCM inatambua umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi katika kukuza uchumi kwa nchi na wananchi kwa ujumla. Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya Mwaka 2015 - 2020 ilielekeza SMZ kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji zaidi. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita mafanikio yalipatikana kama ifuatavyo:-

- (a) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika uendelezaji wa shughuli za kiuchumi ikiwemo uzalishaji viwandani; kilimo, ufugaji na uvuvi; usafirishaji angani, baharini na nchi kavu; na sekta ya huduma ikiwemo utalii, sekta ya fedha, afya na elimu;
- (b) Ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi umeimarishwa kwa kutungwa na kutekelezwa kwa Sheria ya Mashirikiano ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership - PPP*) ya Mwaka 2015 na Sheria ya Baraza la Biashara ya Mwaka 2017. Kutokana na sheria hizo, mabaraza na majukwaa ya biashara yamefanyika. Aidha, jumla ya miradi 13 imefanyiwa upembuzi yakinifu ikiwemo ujenzi wa vituo vya daladala Kijangwani, Chuini na Chanjaani; ujenzi wa masoko sita yaliyopo Chuini, Mwanakwerekwe, Mombasa, Mkokotoni, Jumbi na Machomane; ujenzi wa Kituo cha Maonesho ya Biashara na Mikutano; ujenzi wa mabweni ya wanafunzi SUZA, Tunguu; ujenzi wa maegesho ya gari Mlandege; na mradi wa nishati mbadala/jadidifu ya jua kwa majengo ya Serikali kwa kutekelezwa kwa njia ya PPP;
- (c) Kuendeleza ujenzi wa miji ya kisasa kupitia miradi wa “*Fumba Town Development (FTD)*” na “*Fumba Up Town Living*”. Jumla ya nyumba 230 zimeshajengwa kati ya nyumba 1,400 zinazokusudiwa kujengwa. Kwa upande wa Micheweni-Pemba, kazi ya kuandaa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi iliyotengwa kwa maeneo huru imekamilika;
- (d) Kutungwa Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 2018 ambayo imeipa nguvu taasisi ya kusimamia vitega uchumi kuwa kituo imara cha ufanikishaji (*One Stop Centre - OSC*); na



- (e) Kushuka kwa riba ya mikopo kutoka wastani wa asilimia 18 mwaka 2015 hadi asilimia 14 mwaka 2020, hivyo jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni hamsini imetolewa kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza miradi ya uwekezaji katika sekta mbalimbali za kukuza uchumi.

**141. Mitaji binafsi ni chanzo muhimu cha uwekezaji ili kusaidia kuleta maendeleo nchini. Hatua zitaendelea kuchukuliwa kuhamasisha na kuimarisha mazingira ya uwekezaji na uendeshaji biashara kwa lengo la kuvutia uwekezaji binafsi wa ndani na kutoka nje, na kuongeza mijadala ya wazi na yenye tija baina sekta za umma na sekta binafsi. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, CCM itaelekeza SMZ kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kubuni na kutekeleza miradi yenye tija kwa njia ya Ushirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
- (b) Kufanya mijadala baina ya sekta ya umma na sekta binafsi kupitia baraza na jukwaa la biashara kwa lengo la kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini;
- (c) Kuendeleza Maeneo Maalum ya Kiuchumi (FEZs) na utoaji vivutio kwa wazawa, diaspora na wageni vitakavyochochea uwekezaji nchini;
- (d) Kuwawezesha wawekezaji wa ndani kwa kuwapatia mitaji na mikopo na huduma nyengine za kibiashara;
- (e) Kuboresha uwekaji wa mazingira bora yatakayorahisisha na kupunguza gharama za uwekezaji nchini; na
- (f) Kupanua wigo na kuwaunganisha wawekezaji wa ndani kuweza kutumia fursa za uwekezaji zilizopo Afrika Mashariki, jumuiya nyengine za kikanda na kimataifa.

**Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kupambana na Umasikini**

**142. CCM inaendelea na mapambano dhidi ya umasikini kama yalivyoasisiwa na Chama Cha Afro Shirazi chini ya uongozi wa Rais wa kwanza wa Zanzibar Sheikh Abeid A. Karume mara baada ya Mapinduzi. Katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 ilielekeza SMZ kuchukua hatua za kupunguza umasikini Zanzibar na kuwawezesha wananchi kiuchumi. Katika kipindi hicho mafanikio yafuatayo yamepatikana:-**

- (a) Hali ya maisha ya wananchi imeendelea kustawi na umasikini wa mahitaji ya msingi umepungua;
- (b) Jumla ya mikopo 1,603 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.45 imetolewa katika shehia 305 Unguja na Pemba na kunufaisha watu 20,614 wakiwemo wanawake 11,873 na wanaume 8,741



kupitia Mfuko wa Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi uliotokana na kuunganishwa Mfuko wa Kujitegemea na Mfuko wa Jakaya Kikwete (JK) na Amani Karume (AK);

- (c) Kuboresha na kuongeza kasi ya utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III) katika shehia 204 (Unguja 126 na Pemba 78) ambapo miradi 544 yenye thamani ya shilingi bilioni 41.1 imeanzishwa. Miradi hiyo inahusu ujenzi wa skuli za maandalizi, ujenzi wa matuta ya kuzuia maji ya bahari katika mabonde ya kilimo, hifadhi ya mazingira, ukarabati wa njia za ndani na utoaji wa ruzuku kwa kaya maskini. Jumla ya kaya masikini 32,994 zimenufaika na miradi hiyo;
- (d) Jumla ya shilingi bilioni 5 zimetolewa kwa vijana wakiwemo wajasiriamali wanawake kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi. Aidha, Programu ya Ajira kwa Vijana imeanzishwa na kunufaisha jumla ya vijana 3,050 wanaojishughulisha na kilimo, ufugaji na uvuvi;
- (e) Miradi 307 ya maendeleo ya wananchi yenye thamani ya shilingi billioni 4.32 imetekelezwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo iliyohusisha miradi ya afya 12, majisafi na salama 101, ujenzi wa barabara 28, umeme 23, elimu 127, madaraja 13 na masoko matatu;
- (f) Kituo cha kulea na kukuza wajasiriamali kimeendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali na masoko kwa vijana 1,069 (253 wanaume na 816 wanawake) ya ujasiriamali na masoko. Kampuni ndogo 45 za biashara zimeanzishwa kupitia kituo hicho na jumla ya mashine 35 zikiwemo mashine za sabuni, mwani, asali, mtindi, vitunguu saumu, bekari na mashine za kukatia mbatata zimenunuliwa na kufungwa kituoni hapo;
- (g) Vikundi vya kiuchumi 250 na wajasiriamali 6,000 wakiwemo wahitimu wa vyuo vikuu 250 wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali ili kubadili mitazamo yao na kuwajengea uwezo wa kujiajiri;
- (h) Jumla ya shilingi milioni 32 zimetolewa kwa kampuni saba za vijana kutoka katika Mfuko wa Ubunifu (*Innovation Fund*) na Mfuko wa Mtaji wa Kuanzisha Biashara inayoendeshwa na kituo hicho; na
- (i) Vituo vinne vya kutoa huduma bora za ujasiriamali kwa wananchi vimeanzishwa katika Wilaya ya Kaskazini "A", Kaskazini "B", Wilaya ya Kati (Unguja) na Wilaya ya Mkoani (Pemba) na kupatiwa vifaa mbalimbali. Matayarisho ya ujenzi wa kituo cha kulea na kukuza wajasiriamali Pemba yameanza.

143. **CCM inatambua kuwa umasikini ni miongoni mwa maadui watatu wakubwa walioainishwa katika sera za waasisi wa Taifa letu, hivyo CCM itaendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi ili waweze kupambana na umasikini, kujitegemea na kuchangia katika maendeleo ya Taifa. Katika miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kufanya yafuatayo:-**





- (a) Kuimarisha sekta zinazotegemea nguvu kazi shadidi (*labour intensive*) na zinazotumia malighafi za ndani;
- (b) Kuwahamasisha wananchi kufanya kazi kwa bidii kwa masilahi yao wenyewe na Taifa kwa ujumla;
- (c) Kuanzisha, kusajili na kuhamasisha vikundi vya wajasiriamali kuungana pamoja katika kutafuta soko la uhakika na lenye tija;
- (d) Kutumia utaratibu wa ugatuzi kwa kupeleka rasilimali katika maeneo yenye kiwango kikubwa zaidi cha umasikini;
- (e) Kuhamasisha taasisi za fedha kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana, wanawake na makundi maalum na kuweka utaratibu maalum wa udhamini wa mikopo;
- (f) Kuendeleza na kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III-2) na kuendelea kubuni mipango na miradi ya kusaidia jamii kupambana na umasikini;
- (g) Kuhakikisha kuwa asilimia 75 ya ardhi imetambuliwa na kurasimishwa kwa Unguja na Pemba kupitia utekelezaji wa programu ya MKURABITA ili kuwapa wananchi fursa zaidi za kutumia ardhi yao katika kujiletea maendeleo. Hali kadhalika, wajasiriamali 150 watasajiliwa na kupatiwa mafunzo kila wilaya na hivyo kufikia jumla ya wafanyabiashara 1,650;
- (h) Kuimarisha mifuko ya uwezeshaji ili iweze kuwanufaisha Wazanzibari wengi ambapo jumla ya shilingi bilioni 46 zitatolewa kwa wajasiriamali kwa masharti nafuu;
- (i) Kujenga vituo sita vya ushauri wa kibiashara kwa wajasiriamali na kuimarisha vituo vinne vilivyopo ili kuwa na kituo katika kila wilaya; na
- (j) Kuendeleza kituo cha ubunifu (*Barefoot center*) kuwa kituo cha mfano cha kukuza vipaji katika kanda ya Afrika Mashariki na kuanzisha vituo atamizi (*incubators*) viwili Unguja na Pemba.

### Sekta za Uzalishaji Mali

144.

Katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 iliielekeza SMZ kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, kusimamia matumizi endelevu ya maliasili, kuimarisha viwanda, biashara, mawasiliano, usafirishaji na utalii kwa lengo la kukuza uchumi. Mafanikio kwa kila sekta ni kama yafuatavyo:-

#### **Kilimo**

- (a) Kuongezeka uzalishaji wa mazao ya chakula mbali na mpunga kutoka tani 281,226 mwaka 2015 hadi tani 404,285 mwaka 2019;



- (b) Kuongezeka uzalishaji wa mpunga kutoka tani 29,083 mwaka 2015 hadi tani 47,507 mwaka 2018 ambapo tija ya uzalishaji kwa hekta imeongezeka kutoka wastani wa tani 2.5 kwa hekta mwaka 2015 hadi wastani wa tani 4.5 kwa hekta mwaka 2019 kwa mpunga wa umwagiliaji maji kwa kutumia teknolojia shadidi. Vilevile, tija katika uzalishaji wa mpunga kwa kutegemea mvua imeongezeka kutoka tani 0.9 hadi 1.5 kwa hekta;
- (c) Kufanya mapitio ya sera, sheria na kanuni ikiwemo Sera ya Kilimo, Sera ya Minazi, Sera ya Misitu na Mpango Mkakati wa Kilimo, Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya ya mbegu za mimea-PBR, Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Sheria ya Mbegu, Sheria ya Uhifadhi na Utibabu wa Mimea na Sheria ya Viatilifu;
- (d) Kuanzisha Wakala wa Serikali wa Matrikta na Zana za Kilimo na kununua matrikta 33 yenye thamani ya bilioni 1.383 na kuongeza bajeti ya pembejeo kwa zao la mpunga kutoka shilingi bilioni 1.5 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 2.2 mwaka 2020 iliyowanufaisha wakulima wadogo wadogo 70,719;
- (e) Kuongezeka kwa eneo lenye miundombinu ya umwagiliaji maji kutoka hekta 810 mwaka 2015 hadi hekta 2,527 mwaka 2020;
- (f) Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mboga kutoka tani 90.4 mwaka 2015 hadi tani 106.6 mwaka 2020;
- (g) Kutayarisha Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Zanzibar kwa miaka kumi (*Zanzibar - Agriculture Sector Development Project Z-ASDP*);
- (h) Kutayarisha na kutekeleza mpango wa kufufua mazao ya Karafuu na Nazi kwa kuwapatia wakulima miche ya mikarafuu (3,207,107) na minazi (186,631) bure;
- (i) Kupandishwa hadhi Chuo cha Kilimo cha Kizimbani kuwa Skuli ya Sayansi ya Kilimo katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA). Wahadhiri 12 wamepatiwa mafunzo katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu (6) na Uzamili (6) na wanafunzi 357 wa Cheti na Diploma wamehitimu katika chuo hicho;
- (j) Kuongezeka kwa uzalishaji wa Karafuu kutoka tani 3,321.7 mwaka 2015 hadi kufikia tani 8,277 mwaka 2018;
- (k) Kuendelea na udhibiti wa nzi wa matunda ambapo jumla ya mitego 5,080 ya kunasia imesambazwa kwa wakulima Unguja na Pemba. Wakulima 114 (Pemba 50, Unguja 64) wamepatiwa mafunzo juu ya mbinu mchanganyiko za udhibiti wa nzi wa matunda;
- (l) Kukamilisha ukarabati wa ghala la hifadhi ya chakula lenye uwezo wa kuhifadhi tani 600 pamoja na ununuzi wa vifaa vya hifadhi ya chakula. Jumla ya tani 338 za mchele zimehifadhiwa;



- (m) Kutoa mafunzo ya chakula na lishe bora kwa jumuiya 20 za wakulima wa Mpunga kwa wakulima 950 (Unguja 450 na Pemba 500) na ugawaji wa mbegu za viazi lishe katika skuli mbili za msingi umefanyika;
- (n) Kuviwezesha vikundi saba vya wananchi vinavyojishughulisha na kilimo kwa kuvipatia vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 479 kwa ajili ya kukoboa Mpunga; kusarifu matunda; kusarifu Mwani; kusarifu Maziwa; pamoja na mashine ya kukaushia Daga;
- (o) Kufunga pampu za maji zinazotumia nishati ya jua kwa matumizi ya umwagiliaji katika maeneo kumi ya wakulima wa mboga na vikundi vinane (vitano Unguja na vitatu Pemba) vya wakulima vimepatiwa mkopo wa shilingi milioni 71. Jumla ya wakulima wa mboga 417 wameunganishwa na masoko kwa kuuza mazao yao katika masoko makuu na hoteli za kitalii ambapo wamepata shilingi bilioni 1.07. Vile vile, vikundi vya wakulima vijana 14 wa Unguja na 12 wa Pemba vimepatiwa ekari 11 katika mashamba yaliyopo maeneo mbalimbali;
- (p) Kushajiika kwa wakulima wa alizeti na kununua mitambo miwili ya kukamulia mafuta yenye uwezo wa kukamua tani 6.5 kwa siku;
- (q) Kujenga masoko matatu ya bidhaa za kilimo katika vijiji vya Konde, Tibirinzi kwa Pemba na Kinyasini kwa Unguja pamoja na ukarabati wa vyumba vya baridi katika soko la Mombasa (Unguja) na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi na Usarifu wa Mazao Pujini (Pemba); na
- (r) Kufanya uhakiki na tathmini na kuorodhesha vikundi 117 vya kilimo (uvuvi, ufugaji, maliasili na wajasiriamali wengine). Aidha, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imevipatia mikopo nafuu vikundi viwili (Kilimo Mkombozi cha Mkokotoni na wakulima SACCOS cha Bumbwisudi) kwa kuwanunulia matrekta mawili.

145. **Sekta ya Kilimo inayo nafasi maalum kwa maendeleo ya wananchi. Mkazo maalum utawekwa katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Zanzibar (Z-ASDP) ikiwa ni jitihada zitakazochangia kuleta mapinduzi ya kilimo. Aidha, lengo litakuwa ni kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula na kuwa na ziada kwa matumizi ya sekta nyengine za kiuchumi kama vile viwanda, huduma na biashara. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, CCM itaelekeza SMZ kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika hekta za mpunga 2,500 katika mabonde ya Cheju, Kilombero, Chaani, Kibokwa, Kinyasini kwa Unguja na Mlemele na Makwararani kwa Pemba pamoja na uhamasishaji wa umwagiliaji kwa matone kwa mazao mengine na matumizi ya “greenhouse” katika hekta 400;
- (b) Kuimarisha uhifadhi wa akiba ya chakula tani 850 za mpunga pamoja na ujenzi wa maghala matatu (mawili - Pemba na moja - Unguja) ya uhifadhi wa chakula yenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 4,250;



- (c) Kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji, usarifu na usafirishaji wa mazao ya chakula na biashara yakiwemo ndizi kutoka tani 65,321 hadi 110,250, mboga na matunda kutoka 45,955 hadi tani 65,834, muhogo tani 177,299 hadi tani 192,429, viazi vitamu tani 53,996 hadi tani 65,482 na mpunga kutoka tani 47,507 hadi 61,500 kwa mwaka;
- (d) Kuongeza uzalishaji wa mazao ya viungo na nazi ikiwemo karafuu kutoka tani 8,227 hadi tani 10,000, Nazi kutoka tani 80,500,000 hadi 126,000,000 na kuongeza uzalishaji wa miche 500,000 ya Karafuu, 500,000 ya Nazi kila mwaka na kuwapatia wananchi bila ya malipo. Mazao mengine ya viungo yatakapopewa kipaumbele ni pamoja na Kungumanga, Vanila, Pilipili Manga, Manjano na Mdalasini;
- (e) Kujitoshesha kwa mazao ya chakula cha mizizi, matunda, mboga na jamii ya kunde kwa kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka 10 wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (Z-ASDP) ikiwemo kuimarisha uzalishaji wa mazao mkakati kiwilaya, usarifu na uongezaji wa thamani;
- (f) Kuwaunganisha wakulima, wafugaji na wavuvi na masoko na kujenga masoko manne ya mazao ya kilimo katika wilaya za Kaskazini B, Kati, Kusini kwa Unguja na Mkoani kwa Pemba;
- (g) Kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora zenye uzazi mwingi, zinazohimili maradhi, wadudu pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi;
- (h) Kuimarisha afya na hifadhi ya mimea kwa kudhibiti wadudu na maradhi ya mimea;
- (i) Kununua pembejeo za kilimo ikiwemo mbolea tani 1,800 (tani 900 kupandia na tani 900 za kukuzia), mbegu tani 350, dawa ya kuulia magugu lita 30,000 pamoja na kuimarisha usimamizi na udhibiti wa viwango na ubora wa pembejeo, mazao na bidhaa za kilimo; na
- (j) Kununua matrekta 50, vipuri pamoja na mashine 10 ndogo za kuvunia na kutoa huduma za utayarishaji wa ardhi.

### **Mifugo**

146. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita SMZ iliendeleza vyema sekta ndogo ya mifugo na kupata mafanikio yafuatayo:-

- (a) Kuongeza idadi ya wafugaji kutoka 109,533 mwaka 2015 hadi 137,003 mwaka 2020;
- (b) Kuongezeka kwa uzalishaji wa maziwa kutoka lita milioni 34 mwaka 2015 hadi lita milioni 40.8 mwaka 2020;



- (c) Kuongezeka kwa uzalishaji wa mayai kutoka milioni 95.8 mwaka 2015 hadi kufikia milioni 184.5 mwaka 2020;
- (d) Kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wafugaji 6,545 kuhusu mbinu bora za ufugaji, utoaji wa huduma pamoja na ukamuaji na uhifadhi wa maziwa;
- (e) Kukarabati mtambo wa kuzalisha gesi ya kuhifadhia mbegu za uzazi (*Liquid Nitrogen Plant*) ambapo jumla ya lita 3,374 za gesi hiyo zilizalishwa na jumla ya ngombe 5,550 walipandishwa kwa sindano. Vituo vinne vya utoaji wa huduma za mifugo ikiwemo Ole-Kianga, Pageni, Fuoni, Unguja Ukuu, Magomeni Chake na kituo kimoja cha karantini Gando Nziwengi Pemba vilifanyiwa matengenezo;
- (f) Kutoa chanjo 1,040 dhidi ya maradhi ya vibuma (ECF). Jumla ya wanyama 141,990 walitibiwa na wanyama 241,832 walipatiwa huduma za kinga na tiba kwa maradhi mbalimbali ya mifugo ikiwemo kimeta, chambavu, magonjwa ya ngozi na kichaa cha mbwa;
- (g) Kuhamasisha matumizi ya biogesi na ujenzi wa mitambo minne ya biogesi ulifanyika kwa wafugaji wenye ng'ombe wa maziwa. Utafiti wa kuelewa ubora wa maziwa yanayozalishwa Zanzibar umefanywa, ambapo sampuli 300 kutoka wilaya sita za Unguja na Pemba zilikusanywa na kuchunguzwa;
- (h) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi watano na kuongeza idadi ya madaktari na madaktari wasaidizi wa mifugo kutoka 5 mwaka 2015 hadi 13 mwaka 2020 na madaktari 32 wanaendelea na masomo; na
- (i) Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika sekta ya mifugo kwa ufugaji, usarifu wa maziwa na nyama ya kuku, utotoaji wa vifaranga na uzalishaji wa chakula cha mifugo.

147. **CCM inatambua fursa iliopo katika kuzalisha ajira na kuendeleza sekta za viwanda, biashara na huduma kupitia sekta ya mifugo. Katika utekelezaji wa Ilani hii, Chama kitaelekeza SMZ kuimarisha ufugaji, kuongeza uzalishaji, tija na ubora wa bidhaa za mifugo ili kuwezesha kujitosheleza kwa mahitaji ya jamii na kupata ziada kwa matumizi ya sekta nyengine za kiuchumi kwa kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kuendeleza sekta ya mifugo kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia inayokidhi mahitaji ya sasa ya kiuchumi na kijamii;
- (b) Kuongeza uzalishaji, tija, ubora na usalama wa bidhaa za mifugo ili kukidhi mahitaji na viwango vya soko la ndani na nje ikiwemo kuongeza idadi ya mayai kutoka 148,400,862 hadi 154,350,000, maziwa kutoka lita 6,046,733 hadi 11,000,000, nyama ya kuku kutoka tani 4,970 hadi 9,000, nyama ya ng'ombe kutoka tani 3,363 hadi 6,000 na nyama ya mbuzi kutoka tani 26 hadi 31;



- (c) Kudhibiti ubora wa pembejeo za mifugo zinazolingia nchini ikiwemo vyakula, dawa na chanjo na kuhamasisha matumizi sahihi;
- (d) Kupunguza gharama za uzalishaji wa mazao ya mifugo kwa kuimarisha upatikanaji wa aina bora za mifugo, vyakula na pembejeo za mifugo;
- (e) Kuimarisha miundombinu na nyenzo za uzalishaji wa mifugo kwa kufanya yafuatayo:-
  - (i) Kuimarisha vituo vya upandishaji wa ng'ombe kwa njia ya sindano (AI Centres) na kutumia teknolojia ya kuhamishia mimba (embryo transfer); na
  - (ii) Kushajiisha utayarishaji na utumiaji wa malisho na vyakula bora vya kutosha vya mifugo;
  - (f) Kuendeleza vituo vitatu vya kukusanyia maziwa vilivyopo na kuanzisha vituo vipya vitano ili kutoa maziwa yenye ubora;
  - (g) Kujenga machinjio mawili ya kisasa moja Unguja na moja Pemba;
  - (h) Kuimarisha huduma za maabara tatu za uchunguzi wa maradhi na moja ya ubora wa chakula cha mifugo;
  - (i) Kuimarisha huduma za ugani kwa kuongeza idadi ya wataalam wa uzalishaji, kinga na tiba kwa wastani wa wataalam wawili kwa ngazi ya shahada ya kwanza katika wilaya na wataalam 10 kwa ngazi ya stashahada kwa kila wilaya, kuwaendeleza na kuwapatia nyenzo watoa huduma za mifugo vijijini (CAHWS);
  - (j) Kuanzisha viwanda viwili vya uzalishaji wa vyakula vya mifugo vyenye viwango na ubora;
  - (k) Kutoa kinga dhidi ya maradhi yasiyo na mipaka (*transboundary animal diseases*), kuimarisha vituo vya udhibiti wa uingizaji wa wanyama (*quarantines*) na kutoa huduma za utibabu wa mifugo kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya;
  - (l) Kuhamasisha wafugaji na jamii kutumia teknolojia ya kisasa kuongeza uzalishaji wa malisho ya mifugo katika eneo dogo na kuanzisha mashamba ya kisasa matatu ya uzalishaji wa malisho ya mifugo (Unguja 2 na Pemba 1);
  - (m) Kutekeleza mikakati ya kulinda haki za wanyama dhidi ya matumizi mabaya, lishe duni na maradhi; na
  - (n) Kuhamasisha ufugaji bora na wa kisasa (*intensive farming*) unaohimili uhaba wa rasilimali ardhi ya Zanzibar.





### Uvuvi na Mazao ya Baharini

148. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, SMZ iliendeleza vyema sekta ndogo ya uvuvi na mazao ya baharini kwa kutekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuanzisha Kampuni ya Uvuvi ya Zanzibar (*Zanzibar Fisheries Company ZAFICO*) na kununua boti mbili za uvuvi zenye uwezo wa kuvua tani 70 katika kina kirefu cha maji kwa thamani ya shilingi bilioni 2.26, ununuzi wa gari ya kusafirishia samaki tani 10, na ujenzi wa vyumba vya baridi. Vile vile, matayarisho ya ujenzi wa gati ndogo katika bandari ya Malindi kwa ajili ya kuegesha boti za uvuvi za kampuni ya ZAFICO yamefanyika;
- (b) Kununua vihori 500 vyenye thamani ya shilingi milioni 425 na kuwapatia wakulima wa Mwani wa Unguja na Pemba;
- (c) Kuendelea na ujenzi wa soko la samaki na diko la kisasa katika bandari ya Malindi lililogharimu shilingi bilioni 26.5, litakaloajiri wavuvi, wachuuzi na wafanya biashara wapatao 6,500;
- (d) Kununua boti tatu za doria zenye thamani ya shilingi milioni 583.2;
- (e) Kujenga kituo cha kuzalishia vifaranga vya samaki milioni 10, majongoo 70,000 na kaa 50,000 kwa mwaka. Jumla ya vifaranga 240,000 vya majongoo bahari vimezalishwa na kusambazwa katika mashamba ya mfano Unguja na Pemba. Vikundi 158 (Unguja 72, Pemba 86) vya wafugaji wa majongoo vimepatiwa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji wa mazao ya baharini ikiwemo samaki, majongoo na kaa;
- (f) Kuendelea na ujenzi wa ofisi na maabara ya taasisi ya utafiti wa uvuvi na mazao ya baharini uliogharimu jumla ya shilingi bilioni 1.6;
- (g) Kuendelea kutoa huduma shirikishi za uhifadhi katika maeneo ya Menai, MIMCA na PECCA pamoja na ujenzi wa majengo mapya ya ofisi za wavuvi katika hifadhi mpya za Tumbatu (TUMCA), Mazizini (CHABAMCA) na ujenzi wa kituo cha doria (MCS) katika Kisiwa cha Pungume umekamilika pamoja na kutoa mafunzo kwa wavuvi na wanajamii 450 kuhusiana na uhifadhi, uendeshaji na utunzaji wa mazingira;
- (h) Kufanya doria shirikishi 579 katika maeneo ya hifadhi za bahari zilizopelekea kukamatwa wavuvi haramu 8,750;
- (i) wanaojishughulisha na uvuvi wa kina kirefu cha bahari kutoka 34,000 mwaka 2015 hadi 50,000 mwaka 2020 pamoja na kutoa mafunzo kwa wavuvi 26 katika Chuo cha Uvuvi Mbegani;
- (j) Kuongeza uzalishaji wa Mwani kutoka tani 9,908 mwaka 2015 kufikia 16,724 mwaka 2020. Mafunzo ya kilimo cha Mwani katika kina kirefu cha maji yalifanyika kwa vijiji 48 na Kamati 81 za wakulima wa Mwani zilipatiwa vifaa vya kulimia Mwani vikiwemo roli 1,222 za Kamba na Taitai 2,250;



- (k) Kusomesha vikundi 72 vya wakulima wa Mwani, ufugaji wa samaki, Chaza, Kaa, Kamba na Majongoo na mazao mengine ya baharini kuhusu kuimarisha masoko yao na kuongeza uzalishaji; na
- (l) Kuunda vikundi shirikishi vya usimamizi wa uvuvi wa Pweza na kukamilisha miongozo ya utekelezaji katika maeneo ya Kisiwa Panza, Kokota na Mwambe.

149. **Zanzibar ina fursa maalum ya kuendeleza uchumi wake kupitia rasilimali za baharini. Katika utekelezaji wa Ilani hii, CCM itaelekeza SMZ kuimarisha uvuvi na kuongeza uzalishaji na thamani ya samaki na mazao mengine ya baharini ili kuwezesha kujitosheleza kwa mahitaji ya jamii na kupata ziada kwa matumizi ya sekta nyengine za kiuchumi na soko la nje kwa kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kukamilisha utayarishaji wa sera mpya ya uvuvi Zanzibar na kufanya mapitio ya Sheria ya Uvuvi Na. 7 ya Mwaka 2010, Kanuni Kuu za Uvuvi za Mwaka 1993 pamoja na Kanuni ya Maeneo ya Hifadhi za Bahari ya Mwaka 2014 na kuanzisha sheria ndogo ndogo za usimamizi wa rasilimali za uvuvi (Pweza, samaki wa miamba) katika vijiji vilivyopo pembezoni mwa bahari;
- (b) Kukamilisha mapitio ya mipango mikuu ya maeneo matano ya hifadhi ambayo ni Menai, PECCA, CHABANCA, TUMCA na MIMCA;
- (c) Kutekeleza Mpango Mkuu wa Uvuvi (*Fisheries Master Plan*) na kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu;
- (d) Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya uvuvi ikiwemo ukarabati wa soko la samaki la Tumbe na Nungwi, ujenzi wa gati ndogo ya vyombo vya uvuvi na soko la samaki katika bandari ya Malindi pamoja na kuanzisha kituo cha kupokelea vifaranga vya samaki Pemba;
- (e) Kujenga viwanda vitano; kiwanda cha kukaushia daga katika eneo la Mkokotoni, viwanda viwili vya kusarifu samaki na mazao ya baharini Unguja na Pemba na viwili vya kuzalisha chakula cha samaki na mazao ya baharini Unguja na Pemba;
- (f) Kuongeza kituo kidogo cha ulinzi na doria za baharini katika eneo la Jambiani;
- (g) Kuongeza uzalishaji wa samaki jamii ya Jodari katika bahari kuu na ufugaji maalum wa samaki kwa kutumia vizimba (*cage farming*) kutoka tani 36,728 hadi tani 44,450 kwa mwaka kupitia ZAFICO;
- (h) Kujenga miundombinu kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa Kampuni ya Uvuvi ya Zanzibar (ZAFICO) ikiwemo vyumba vya baridi vya kuhifadhia samaki, mtambo wa kuzalishia barafu na ujenzi wa



bandari ya kuegesha boti pamoja na ununuzi wa boti nne za uvuvi wa bahari kuu;

- (i) Kuongeza uzalishaji wa mwani kutoka tani 16,723.8 hadi tani 21,000 kwa mwaka;
- (j) Kutoa taaluma bora zaidi ya ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kibiashara, mafunzo kwa wavuvi vijana kuwawezesha kuvua katika kina kirefu na kuendelea kuwajenga uwezo wataalam juu ya uzalishaji wa vifaranga vya samaki Kaa na Majongoo katika kituo cha kutotolea vifaranga vya samaki (*hatchery*) kilichopo *Beit el Ras*;
- (k) Kuzalisha na kusambaza vifaranga milioni 10 vya samaki, Kaa na Majongoo kibiashara kwa mwaka kwa wanajamii na kuanzisha mashamba 12 ya mfano ya ufugaji wa Majongoo kibiashara (Unguja 6 na Pemba 6) pamoja na kuanzisha ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba (*cage farming*) vyenye uwezo wa kuzalisha tani 40,000 kwa mwaka;
- (l) Kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira ya baharini kwa jamii katika kulinda rasilimali za bahari, kuzijengea uwezo kamati za uvuvi 91 (58 Unguja na 33 Pemba) ili kuongeza ufanisi katika shughuli zao na kuhamasisha jamii katika kusimamia rasilimali za bahari kwa kuanzisha maeneo ya ufugaji wa Pweza na samaki wa miamba;
- (m) Kuimarisha doria/ulinzi shirikishi katika maeneo ya maji ya ndani na kununua boti tano za uvuvi zitakazofika katika bahari kuu ili kudhibiti uvuvi haramu. Aidha, jamii itashajihishwa kuweka matumbawe bandia katika maeneo ya hifadhi za bahari ili kuongeza uzalishaji wa samaki;
- (n) Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi ikiwemo kutoa mafunzo na uendeshaji wa kituo cha kutotolea vifaranga vya samaki (*hatchery*); na
- (o) Kuwawezesha wakulima wa Mwani kwa kuwapa mafunzo na nyenzo ili kuweza kulima mwani wenye thamani, tija na gharama ndogo za uzalishaji ikiwemo aina ya *Cottonii* na *Glacillaria*. Vilevile, jumuiya za wakulima wa mwani zitaimarishwa kwa kuwapatia nyenzo zitakazosaidia kufanya usarifu wa mwani.

### **Maliasili**

150. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, SMZ iliendeleza vyema sekta ndogo ya maliasili kwa kutekeleza yafuatayo:-

- (a) Kufanya mapitio ya Sera ya Misitu ya Mwaka 1995, Sheria ya Misitu ya Mwaka 1996 na Mpango wa Usimamizi wa Misitu 2015-2025;



- (b) Kuandaa na kutekeleza kanuni za usimamizi na uhifadhi wa misitu na wanyamapori na mwongozo juu ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Wanyamapori, miti na mimea iliyo hatarini kutoweka (*Convention of International Trade of Endangered Species CITES*);
- (c) Kufanya doria 623 Unguja na Pemba na kukamata Makobe 850 ambayo yaliingizwa nchini kinyume na sheria. Kukamata na kuteketeza misumeno ya moto 346 (Unguja 206 na Pemba 140). Aidha, gari 130 za mizigo na gari 15 za ng'ombe zinazosafirisha maliasili kinyume na taratibu zilikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria;
- (d) Kupanda miti:
- (i) Hekta 99.5 katika maeneo matano yaliyochimbwa mchanga yakiwemo Mangapwani, Zingwezingwe, Donge Chechele, Kidanzini na Fujoni Wilaya ya Kaskazini B Unguja;
  - (ii) Hekta 369.1 katika mashamba ya watu binafsi na maeneo ya misitu ya jamii ikiwemo Chaani, Kibele, Dunga, Unguja Ukuu, Maziwa Ng'ombe, Tumbe, Selem, Makuwe, Gando, Kiwengwa, Masingini na Jozani;
  - (iii) Hekta 163.5 za Mikoko Unguja na Pemba; na
  - (iv) Hekta 710 katika maeneo yaliyo wazi, ikiwemo miti ya matunda, misitu, viungo pamoja na mikarafuu.
- (e) Kutoa taaluma ya kuanzisha vikundi vya ushirika, kuandaa vitalu vya miti na kutengeneza majiko sanifu kwa wanawake 45 wa Shehia za Kitogani na Muyuni. Madiwani na viongozi 25 (10 wanawake na 15 wanaume) wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B Unguja walipata semina ya kuongeza uelewa juu ya sheria ya maliasili na maamuzi ya Serikali kusimamia uchimbaji wa mchanga;
- (f) Hifadhi nne za Taifa za Jozani (*Biosphere Reserve*), Masingini, Kiwengwa-Pongwe na Ngezi-Vumawimbi zimepandishwa hadhi kwa mujibu wa Sheria ya Misitu ya Mwaka 1996;
- (g) Kuimarisha miundombinu ya hifadhi ya msitu wa maumbile Masingini kwa ajili ya utalii ikiwemo ujenzi wa sehemu za mapumziko, huduma za ofisi ya kituo, njia za kupitia watalii, mnara wa kuangalia haiba ya mji wa Zanzibar, ujenzi wa vyoo na mkahawa;
- (h) Kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali zisizorejeshika ikiwemo mchanga, kifusi, kokoto na mawe kwa kutayarisha mpango maalum wa uratibu na udhibiti wa matumizi holela ambao umewezesha ongezeko la mapato kutoka shilingi milioni 558 kwa mwaka 2015 na kufikia shilingi bilioni 16.5 mwaka 2020;



- (i) Kuhamasisha jamii katika uhifadhi na kuendeleza miradi ya jamii nje ya misitu ambapo mwaka 2020 jumla ya shilingi bilioni 1.43 zimegaiwa kwa wanajamii wanaozunguka Hifadhi ya Taifa ya Jozani;
- (j) Wafugaji 962 wa nyuki walitambuliwa (524-wanawake na 438 wanaume) na tani 13.3 za asali zilizalishwa Unguja na Pemba pamoja na ujenzi wa mabanda ya kisasa ya mfano 3 ya nyuki (2 Unguja 1 Pemba) yenye mizinga 40 kila moja;
- (k) Jumla ya miche 4,827,561 (2015-2018) imeoteshwa katika vitalu vya Serikali na miche 2,593,215 imeoteshwa na wanajamii inayojumuisha miti ya misitu, matunda na viungo; na
- (l) Miche ya mikarafuu 1,793,303 imeoteshwa (1,309,050 katika vitalu vya Serikali na 484,253 vya watu binafsi). Aidha, vitalu binafsi 101 vimepatiwa mafunzo na vifaa vya uoteshaji miche. Vilevile, Serikali imeanzisha mashamba ya mbegu za miche ya minazi miwili (ekari 5.3 Selemu Unguja na ekari nne Tumbe Pemba) pamoja na uzalishaji wa miche ya minazi 186,506 Unguja na Pemba na kusambazwa kwa wananchi bure.

**151. Maliasili ni muhimu sana kwa maendeleo, ustawi wa jamii na hifadhi ya mazingira. CCM inaelewa umuhimu wa kuzitambua na kuzitunza kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho. Hivyo, mkazo mkubwa utawekwa katika uendelezaji na uhifadhi wa maliasili pamoja na kuwa na matumizi endelevu. Katika Ilani hii, CCM itaelekeza SMZ kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Misitu ya Mwaka 2020 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2015 na kuendeleza mipango mikakati ya usimamizi wa matumizi endelevu ya hifadhi za misitu na maliasili zisizorejesheka itakayotoa fursa za maendeleo na ajira kwa jamii;
- (b) Kufanya matumizi mbadala ya maeneo ya mashimo yaliyochimbwa mchanga na kifusi ili kuleta tija kiuchumi na kijamii, pamoja na kuweka vizuri haiba ya maeneo hayo;
- (c) Kufanya utafiti wa rasilimali mbadala wa rasilimali zisizorejesheka na kuendelea kudhibiti na kusimamia matumizi endelevu ya maliasili hizo ikiwemo mchanga, kifusi, mawe na kokoto kwa kushirikiana na halmashauri husika;
- (d) Kutoa taaluma ya udhibiti na matumizi endelevu ya misitu ya jamii 57 (COFMA) pamoja na kuanzisha misitu mipya ya jamii miwili (Mtambwe na Uzi-Vundwe) kwa kushirikiana na halmashauri na mabaraza ya vijana katika wilaya za Unguja na Pemba;



- (e) Kufanya sensa ya miti ya Zanzibar (*Wood Biomass Survey*) ili kujua mabadiliko ya uoto wa asili, wingi wa misitu pamoja na kujua idadi ya mikarafuu iliopo hivi sasa;
- (f) Kutayarisha mipango mipya ya usimamizi wa misitu ya jamii 20 ambayo ni Kikungwi, Mzuri, Fujoni, Tumbatu Jongowe, Tumbatu Uvuvini, Tumbatu Gomani, Makoba, Mto wa Pwani na Kigunda Unguja na Kiuyu Mbuyuni, Shanate, Makangale, Kipange, Wingwi Mapofu, Wingwi Mtemani, Majenzi Micheweni, Kiweni, Makoongwe, Wambaa na Pujini Pemba;
- (g) Kuongeza idadi ya uzalishaji wa Paa Nunga kutoka 300 mwaka 2020 hadi zaidi ya 600 mwaka 2025 na Paa Chesi wa Pemba kutoka 1,500 mwaka 2020 hadi zaidi ya 2,000 mwaka 2025 katika hifadhi za Kiwengwa, Jozani na Kisiwa cha Pungume kwa Unguja na Ngezi na Msitu Mkuu kwa Pemba;
- (h) Kutumia hifadhi misitu ya Mtambwe Kusini na Mtambwe Kaskazini kwa Pemba na misitu ya Uzi Ng'ambwa na Kisiwa cha Vundwe kwa Unguja ili kuimarisha utalii wa kimaumbile kwa kupandisha hadhi na kuongeza vivutio vya kitalii;
- (i) Kusimamia misitu ya jamii ili kuongeza tija kwa kufanya mambo ya msingi yafuatayo:-
  - (i) Kurejeshea miti ya misitu katika maeneo yaliyoathirika na ukataji ovyo wa miti;
  - (ii) Kutekeleza miradi ya mbinu mbadala na kutoa mafunzo husika kwa miradi itakayobuniwa; na
  - (iii) Kuendeleza uzalishaji wa miche ya miti milioni 2.5 (miti ya misitu milioni 1.5 na miti ya matunda milioni 1) na kuisambaza kwa jamii.
- (j) Kutoa elimu ya uzalishaji miche kwa mabaraza ya vijana na skuli, utoaji wa nyezo kwa ajili ya uanzishaji wa vitalu vya jamii pamoja na uoteshaji na upandaji wa miti ya mikoko katika maeneo yaliyoathirika na mmong'onyoko wa fukwe na kuyatumia maeneo hayo kwa ufugaji wa kaa na mazao mengine ya baharini;
- (k) Kupanda miti hekta 160 katika maeneo yaliyoathirika na moto ya msitu wa hifadhi wa Kiwengwa na Jozani;
- (l) Kujenga mabanda matatu ya mfano ya kufugia nyuki (yenye uwezo wa kuchukua mizinga 40 kila moja) kwa kila wilaya kwa madhumuni ya kushajiisha ufugaji wa nyuki;





- (m) Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika misitu ya hifadhi ya Masingini, Kiwengwa na Ngezi; na
- (n) Kuimarisha njia zinazopitika (*nature trail*) na miundombinu ya ugunduzi wa awali wa moto; kuongeza visima vya maji ndani ya misitu ya hifadhi; na kutoa mafunzo ya awali ya kukabiliana na majanga ya moto;

### **Utalii**

152. Katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, CCM ilielekeza SMZ kuendelea kusimamia, kuendeleza na kutangaza sekta ya utalii ili iweze kuleta tija zaidi kwa Taifa na watu wake. Katika kipindi hicho mafanikio yameendelea kupatikana yakiwemo yafuatayo:-

- (a) Kuongezeka kwa idadi ya watalii mwaka hadi mwaka kutoka 294,243 mwaka 2015 hadi 538,264 mwaka 2019 na hivyo kuvuka lengo la Ilani la kupokea watalii laki tano ifikapo mwaka 2020;
- (b) Kuongezeka wastani wa siku za ukaazi kwa mtalii kutoka siku sita mwaka 2016 hadi siku saba mwaka 2020 na kuongezeka kwa wastani wa matumizi kwa mgeni kutoka Dola za Kimarekani 102.6 mwaka 2016 hadi Dola za Kimarekani 262 mwaka 2019;
- (c) Kufanya mapitio ya sera ya utalii, kuandaa kanuni mpya za utalii na kuimarishwa kwa kamati za utalii za wilaya kwa azma ya kuharakisha utekelezaji wa mkakati wa “Utalii kwa Wote”;
- (d) Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za utalii kwa kuanzisha utaratibu maalum wa kushirikisha Kamisheni ya Utalii, Bodi ya Mapato, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Idara ya Uhamiaji, Idara ya Forodha ya TRA, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na kampuni za kushughulikia abiria viwanja vya ndege na bandarini;
- (e) Kuongezeka kwa idadi ya vyumba vya kulaza wageni kutoka 8,016 mwaka 2015 hadi 10,704 mwaka 2020. Aidha, hoteli za daraja la juu zimeongezeka kutoka 26 mwaka 2015 hadi 43 mwaka 2020;
- (f) Kuunganisha Chuo cha Utalii (*ZiTOD*) na Chuo Kikuu cha Zanzibar (*SUZA*). Walimu sita wamepatiwa mafunzo ya juu na jumla ya wanafunzi 983 (wanawake 386 na wanaume 597) wamehitimu masomo yao katika ngazi ya Shahada na Stashahada;
- (g) Kuanzisha mifumo ya kisasa ya kuitangaza Zanzibar kwa lugha tano (Kingerezea, Kijerumani, Kifaransa, Kichina na Kiarabu) kupitia tovuti na kuanzisha matukio na matamasha mapya ya utalii kama vile Tamasha la Michezo na Utalii (Pemba) na Tamasha la Utalii Zanzibar (Unguja) ambalo lilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 150 wakiwemo wasambazaji wakubwa saba wa utalii na wananchi 4,022, mbio za *marathon* za Mji Mkongwe (Zanzibar *Stone Town Marathon*) na “Zanzibar Trail”. Aidha, matamasha ya Sauti ya Busara, Tamasha



la Nchi za Jahazi (ZIFF) na Tamasha la Chakula cha Kimakunduchi yameimarishwa;

- (h) Kuimarisha utekelezaji wa Programu ya Matokeo kwa Ustawi (R4P), kuandaa na kutekeleza Mpango wa Kuimarisha Sekta ya Utalii na taasisi zinazosimamia sekta hiyo. Vilevile, Mpango wa Kuimarisha Utalii wa Viungo (*Spice Tourism*), Mpango wa Muda wa Kati wa Kuimarisha Utalii (*Integrated Strategic Action Plan - ISAP*) na Mpango wa Muda Mrefu wa Kuimarisha Utalii kupitia mradi wa “*Boost Inclusive Growth for Zanzibar*” (*BIG Z*) imeandaliwa;
- (i) Kushirikiana na sekta binafsi katika kushiriki maonesho ya utalii ya kitaifa na kimataifa na mikutano ya wazi (*road shows*), kuiendeleza Ofisi ya Uwakala wa Utangazaji Utalii Nchini India na kuibuliwa masoko mapya ya utalii ya India, China, Uturuki na Urusi;
- (j) Kuandaliwa vipindi maalum na waandishi wa habari 19 kutoka vyombo vya nchi za nje ikiwemo *China Travel Channel*, *Brazil*, *Uingereza - Reuters*, *France 4K Travel Chanel*, *BBC* na *Malaysia* ambao walitembelea maeneo ya utalii nchini;
- (k) Kuhamashisha jamii kushiriki katika utalii wa ndani ikiwemo kutoa mafunzo ya utalii kwa wafuatao:-
  - (i) Wanafunzi 680 kutoka skuli za sekondari, vijana 325 kutoka mabaraza ya vijana 185 na vijana 140 kutoka katika Asasi ya Umoja wa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu;
  - (ii) Kamati za utalii za wilaya 11 za Unguja na Pemba;
  - (iii) Vikundi 45 vya vijana vinavyotoa huduma za kitalii katika mashamba ya viungo yaliyopo Kizimbani na maeneo yaliyopo karibu na kijiji hicho;
  - (iv) Watoa huduma 45 wamepatiwa mafunzo juu ya namna bora ya kuendesha shughuli zao za utalii wa pomboo - Kizimkazi; na
  - (v) Wanavikundi 70 kutoka katika wilaya za Mkoani, Chake Chake, Wete, Micheweni na Mjini wanaojishughulisha na utengenezaji na uuzaji wa bidhaa za utalii.
- (l) Kuhamasika zaidi wawekezaji wa nje na ndani kuwekeza katika ujenzi wa hoteli za daraja za juu kama vile Hotel za Verde (Mtoni), White Paradise Zanzibar (Pongwe), Zanzi Blue Resort, Madinat Al Bahari (Mbwani) na Zuri ambazo zimeongeza ubora wa huduma za utalii na ajira Zanzibar;
- (m) Kuimarika kwa ulinzi na usalama kwa watalii, wawekezaji na mali zao katika maeneo ya uwanja wa ndege, Bandarini, Mji Mkongwe na baadhi ya maeneo ya Barabara kuu zinazoingilia maeneo ya Mkoa wa



Mjini Magharibi kupitia mradi wa Zanzibar Salama kwa kufungwa Kamera za ulinzi na kuanzishwa. Vilevile, ulinzi katika maeneo mengine ya utalii umeimarishwa kwa kuanzisha Wakala wa Ulinzi wa Jeshi la kujenga Uchumi.

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAJAJA

153. **Utalii ni Sekta kiongozi kwa uchumi wa Zanzibar katika kuchangia pato la Taifa, fedha za kigeni na kutoa fursa nyingi za ajira. Kwa kutambua kuwa Zanzibar ina vivutio vingi vya kipekee vya utalii, mkazo mkubwa utawekwa katika ushirikishwaji wa jamii, kuimarisha mazingira ya uwekezaji na kuongeza idadi ya watalii wa daraja la juu na watakaokaa kwa muda mrefu. Katika Ilani hii, CCM itaelekeza SMZ kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kutekeleza Mpango Shirikishi wa Uendelezaji Utalii (ISAP) na Mradi wa “BIG Z” ili kuongeza thamani ya utalii wa Zanzibar kwa kupanua wigo, ubora na upekee wa bidhaa zinazotolewa kwa wageni na hivyo kupelekea:-
  - (i) Kuongezeka kwa idadi ya wageni kutoka 538,264 mwaka 2019 hadi kufikia 850,000 mwaka 2025;
  - (ii) Kuongezeka kwa siku za ukaazi kutoka wastani wa siku saba mwaka 2019 hadi kufikia siku nane mwaka 2025; na
  - (iii) Kuongezeka kwa matumizi ya mgeni kutoka wastani wa Dola za Kimarekani 262 kwa siku mwaka 2019 hadi kufikia Dola za Kimarekani 350 mwaka 2025.
- (b) Kuendeleza utekelezaji wa dhana ya utalii kwa wote kwa kuwahamasisha wananchi kutoa huduma za utalii na kufanya utalii wa ndani;
- (c) Kuimarisha maeneo na vivutio vya utalii ikiwemo zoni za utalii za Kaskazini, Mashariki na Kusini kwa Unguja na Kaskazini na Kusini Pemba;
- (d) Kukitangaza zaidi kisiwa cha Pemba kwa utalii endelevu na unaozingatia mazingira na kuongeza idadi ya watalii wanaokitembelea kutoka 30,000 mwaka 2018 hadi 150,000 mwaka 2025;
- (e) Kuongeza idadi ya vyumba vya kulaza wageni kutoka 10,704 mwaka 2019 hadi vyumba 15,350 mwaka 2025. Aidha, mkazo utaweka katika kushajiisha uwekezaji zaidi katika ujenzi wa hoteli za daraja la juu na kuongeza vyumba kutoka 2,980 mwaka 2020 hadi vyumba 7,626 mwaka 2025;
- (f) Kuimarisha utalii wa meli (*cruise tourism*) na kuongeza idadi ya meli za kitalii zinazotembelea Zanzibar kutoka 6 mwaka 2018 zilizoleta watalii 758 hadi meli 40 mwaka 2025 zenye wageni 14,250;



- (g) Kufundisha vijana 4,500 kwenye fani za utalii, ukarimu, uongozaji watalii na usafirishaji ifikapo mwaka 2025;
- (h) Kuendeleza utalii wa matamasha, ikolojia, mikutano, michezo, viungo, biashara na utamaduni;
- (i) Kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi katika kuvutia, kuhudumia na kutanua mazao ya utalii;
- (j) Kuandaa chapa ya utalii ya Zanzibar (*branding*) na kuendelea kuitangaza Zanzibar kama kituo cha utalii kwa kushirikiana na sekta binafsi, ofisi za balozi za Tanzania nje, watu maarufu (*celebrities*) na jumuiya za wana-diaspora wa Tanzania, kutumia vyombo vya habari vya kimatifa na kuimarisha matamasha ya utalii yaliyopo na kuanzisha mapya, pamoja na kuendelea kuimarisha mifumo ya utangazaji yanayoendana na mabadiliko ya TEHAMA;
- (k) Kuimarisha ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za utalii ikiwemo kwa kufanya utafiti wa utokaji wa wageni (*Tourist exit survey*) na utafiti wa kujua uwezo wa kupokea wageni kwa kisiwa cha Unguja, Pemba na visiwa vidogo vidogo (*carrying capacity*) ili kuwa na utalii endelevu; na
- (l) Kutekeleza mapendekezo ya Programu ya Matokeo kwa Ustawi (R4P) kwa kuimarisha ulinzi kupitia kikosi maalum na ushirikishwaji wananchi.

### **Mambo ya Kale na Utunzaji Kumbukumbu za Taifa**

154.

Mambo ya Kale ni urithi adhimu kwa utambulisho wa nchi, maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii ya Zanzibar. Yakitumiwa vyema, mambo ya kale yanaweza kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya utalii, uhifadhi wa historia na urithi wa utamaduni. Katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, CCM iliielekeza SMZ kutunza kumbukumbu za Taifa, kuhifadhi na kuendeleza mambo ya kale na mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- (a) Kuendeleza Makumbusho ya *Livingstone* kwenye Jengo la *Livingstone* Kinazini kwa kushirikiana na sekta binafsi;
- (b) Kufanya matengenezo makubwa ya majengo ya kihistoria ya Kasri ya Bikhole (Bungi), Mwinyi Mkuu (Dunga), eneo la kihistoria la Mvuleni, Ngome ya Wareno (Fukuchani), Makumbusho ya Viumbe Hai Mnazimmoja kwa Unguja na Makumbusho ya Chake Chake na Mkamandume kisiwani Pemba. Vilevile, majengo ya kihistoria ya *Beit el Ajaib*, Jumba la Wananchi Forodhani, Kasri ya Mtoni, Jengo la Tip Tip na Ngome Kongwe yamefanyiwa matengenezo;
- (c) Kuandaa kitabu chenye taarifa sahihi za maeneo mbalimbali ya kihistoria. Kitabu hicho kitatumika kama nyenzo ya kutolea maelezo kwa watalii na wageni wengine;



- (d) Kuanzisha makumbusho ya kumbukumbu za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964 katika eneo la Michenzani;
- (e) Kuimarisha Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu kwa kupatiwa vifaa vya kisasa vinavyoiwezesha na kuendelea na Mpango wa Kuhuisha Nyaraka na Kuzihifadhi Katika Mfumo wa Kielektroniki;
- (f) Kutoa mafunzo kwa watendaji watano katika fani za uhifadhi, utunzaji wa kumbukumbu na historia;
- (g) Kuandaa sera ya urithi wa mambo ya kale na kufanya utafiti katika visiwa 13 visivyoishi watu, sita Unguja na saba Pemba. Visiwa hivyo ni Kwale, Pungume, Nyemembe, Miwi, Vundwe na Daloni na kwa upande wa Pemba ni Mtangani (Kuji), Pembe, Funzi, Kokota, Njao, Mbale, na Njiauze; na
- (h) Kuimarisha usalama wa eneo la utunzaji wa nyaraka kwa kulipa fidia kwa jengo la makaazi binafsi.

**155. Kwa kutambua kuwa nchi yetu ina utajiri mkubwa wa historia na mambo ya kale, mkazo utawekwa katika kuwashajiisha wananchi na wawekezaji katika kuhifadhi, kuhuisha na kutumia rasilimali hiyo kwa kuongeza kipato na kukuza uchumi ikiwa ni sehemu ya kupanua wigo wa bidhaa za utalii na uendelezaji wa juhudi za kueleemisha jamii kuhusu historia na urithi wa nchi yetu. Katika Ilani hii, CCM itaelekeza SMZ kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kuendeleza na kuhifadhi urithi wa dunia wa Mji Mkongwe;
- (b) Kudhibiti na kusimamia uhifadhi wa mambo ya kale kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo;
- (c) Kusimamia, kuendeleza na kuimarisha utunzaji wa uhifadhi wa vivutio asilia na vya kiutamaduni (*natural and cultural heritage*) kwa kushirikiana na wadau wengine;
- (d) Kukamilisha na kuanza utekelezaji wa sera na sheria ya mambo ya kale, mpango mkuu wa kuendelea na kuhifadhi maeneo ya kihistoria, Mpango Mkakati wa Kuendeleza Makumbusho na kuanzisha Wakala wa Urithi Zanzibar;
- (e) Kuendeleza Makumbusho ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Mwaka 1964 yaliyopo Michenzani, kufufua nyumba ya Afro Shiraz Party (ASP) Kijangwani na kuanzisha Makumbusho ya Sheikh Abeid Amani Karume na waasisi/viongozi wengine wenye mchango mkubwa wa kuyaenzi na kuyadamisha Mapinduzi ya Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964;
- (f) Kushirikisha wananchi katika kuyatunza, kuyahifadhi na kuyatumia maeneo ya utamaduni na mambo ya kale;



- (g) Kuandaa makala (*documentaries*) na kuandika vitabu vyenye taarifa mbalimbali za maeneo ya historia kwa ajili ya kuweka kumbukumbu na kutangaza utalii;
- (h) Kufanya tafiti tano za ikolojia Unguja na Pemba ili kujua upana wa historia iliyopo katika maeneo hayo;
- (i) Kuyafanyia matengenezo makubwa maeneo ya kihistoria ya Makumbusho ya Mnazimmoja, Chwaka-Tumbe (Msikiti Chooko na kaburi kubwa la Haroun na makaburi ya Mazrui), Makumbusho ya Chake Chake na kuendeleza eneo la historia la mji uliozama Ras Mkumbuu;
- (j) Kuhifadhi na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria Pemba ikiwemo Mji wa Kale wa Jambangome, Msikiti wa Kichokochwe na Mfufuni (Kangani);
- (k) Kuandika na kuweka kumbukumbu ya historia ya Zanzibar ya kisiasa, kijamii na kiuchumi kabla na baada ya Mapinduzi Matukufu ya Mwaka 1964;
- (l) Kuboresha utekelezaji wa mikakati ya kukuza utalii wa ndani;
- (m) Kujenga kituo cha Taifa cha Kuhifadhia Kumbukumbu Tuli (*dormant record*);
- (n) Kuhami mali za kale ili zisichukuliwe na kupotea pamoja na kuchukua hatua za kurejesha zilizochuliwa; na
- (o) Kuanzisha makumbusho ya kisasa ambayo yataeleza historia mpya ya maendeleo ya Zanzibar baada ya Mapinduzi (*Post Revolution Era*).

### **Viwanda na Biashara**

156. Katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, CCM iliielekeza SMZ kuandaa na kutekeleza sera mpya ya biashara, sera ya uendelezaji wa viwanda vidogo na vya kati, kuwapatia mafunzo, mitaji na huduma za kiufundi wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati (SME's). Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, sekta ya viwanda na biashara imepata mafanikio yafuatayo:-

- (a) Kuanzisha Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati kwa kutunga sheria yake sambamba na Sheria ya Biashara, Sheria ya Utoaji Leseni za Biashara na Usajili, Sheria ya Kumlinda Mlaji, Sheria ya Kuimarisha Ushindani Halali, na Sheria ya Mizani na Vipimo;
- (b) Kutengeneza mashine tano za teknolojia rahisi kwa kuwatumia vijana waliomaliza vyuo vya ufundi ikiwemo nne za uzalishaji wa sabuni na moja ya kutengeneza vikoi;





- (c) Kukamilishwa utafiti wa kuendeleza uzalishaji dagaa;
- (d) Kuwapatia mafunzo wajasiriamali 412 ikiwemo ya uzalishaji na usarifu bora wa bidhaa zikiwemo maziwa, Mwani na matumizi ya vifungashio;
- (e) Kuyapima maeneo matatu ya viwanda ya Dunga, Nungwi na Chamanangwe. Mpango Mkuu wa matumizi ya eneo la Chamanangwe umeandaliwa;
- (f) Kufanya kongamano la biashara na uwekezaji nchini China (*Zanzibar China Business Forum*);
- (g) Kufufua kiwanda cha nguo cha Cotex (Basra) kwa kufanya matengenezo ya majengo, kujenga barabara ya kufika katika kiwanda na kufunga mashine;
- (h) Kufanya utafiti wa utoaji wa leseni na kuandaa misingi, vigezo, miongozo na taratibu fupi kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa leseni;
- (i) Kuendelea kusimamia vyema biashara ya zao la Karafuu kwa masilahi ya nchi na wakulima;
- (j) Kuandaa tamasha la biashara kila mwaka kwa lengo la kuwaunganisha wafanyabiashara na soko pamoja na kuwashajiisha na kuwasaidia wafanyabiashara kutumia soko la ndani, kikanda na kimataifa kuuza bidhaa zao;
- (k) Kuanzisha maabara ya upimaji wa bidhaa za umeme, mafuta ya nishati na vyakula vyenye kemikali;
- (l) Kuongezeka kwa idadi ya viwango vya bidhaa kutoka 85 mwaka 2015 hadi 293 mwaka 2020. Aidha, bidhaa zenye alama ya ZBS zimeongezeka kutoka bidhaa moja mwaka 2015 hadi kufikia 27 mwaka 2020;
- (m) Kuanzisha viwanda vya kusarifu mafuta ya mimea ikiwa ni pamoja na Mikaratusi, Milangilangi, Michaichai, Mwani pamoja na vya kusarifu chumvi na dagaa; na
- (n) Kuongeza mazao ya Karafuu kwa kuanza kuchakata mafuta kutoka katika majani ya mkarafuu.

157. **Sekta za viwanda na biashara zina nafasi maalum katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi. Katika Ilani hii, CCM itaendelea kuelekeza SMZ kubuni mikakati itakayoimarisha urari wa biashara na usafirishaji wa mazao na bidhaa za kimkakati, pamoja na kushajiisha ujenzi wa viwanda vidogo na vya kati vinavyohimili ushindani katika wingi na ubora wa bidhaa kwa kutekeleza yafuatayo:-**



- (a) Kushajiisha uwekezaji zaidi wakiwemo wawekezaji wa ndani katika kuanzishwa na kuendeleza viwanda nchini hasa vyenye kutumia malighafi za ndani ili kupunguza uingizaji wa bidhaa nchini kwa kuweka mkazo katika viwanda vidogo na vya kati vinavyotumia malighafi kutokana na mazao ya kilimo, mifugo na bahari;
- (b) Kuongeza mchango wa sekta ya viwanda kutoka asilimia 18 mwaka 2018 hadi asilimia 22.5 mwaka 2025;
- (c) Kuainisha na kuendeleza maeneo yaliyotengwa kwa maendeleo ya viwanda na ugunduzi katika mikoa sambamba na ukuzaji wa uwezo wa ujasiriamali. Vilevile, mipango ya matumizi wa maeneo ya viwanda yaliyopo Nungwi na Dunga itaandaliwa;
- (d) Kuongeza udhibiti wa ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini kwa kuanzisha maabara za ugezi (*calibration*), uhandisi vimelea (*food microbiology*). Aidha, maabara za upimaji chakula kemikali na maabara ya upimaji wa vyombo vya moto zitaimarishwa;
- (e) Kuzifanya maabara za ZBS kutambulika katika ukanda wa Afrika na duniani kote kwa kupata ithibati (*accreditation*) kutoka Shirika la SANAS (*South African National Accreditation*);
- (f) Kuimarisha chapa ya Zanzibar (*branding*) katika kukuza biashara, kusimamia na kuhakikisha ubora wa bidhaa na huduma kwa kuzingatia viwango na mahitaji ya soko na kusimamia haki za wabunifu (*intellectual property rights*);
- (g) Kuimarisha mamlaka ya udhibiti wa viwango vya usafirishaji wa bidhaa ikiwemo samaki na mazao ya baharini kwa mujibu wa mahitaji ya kitaifa, kikanda na kimataifa;
- (h) Kuratibu maonesho ya biashara ya Zanzibar ambayo yatafanyika mara mbili kwa mwaka;
- (i) Kujenga kituo cha Kimataifa cha Mikutano na Maonesho ya Biashara katika eneo la Nyamanzi/Dimani;
- (j) Kuratibu ushiriki wa wajasiriamali wa Zanzibar katika Maonesho ya Biashara ya Kitaifa na Kimataifa;
- (k) Kuimarisha eneo tengefu la viwanda vitakavyotumia malighafi inayopatikana ndani ya nchi ili kukuza na kuendeleza wajasiriamali;
- (l) Kushiriki ipasavyo katika utangamano wa kikanda (EAC, SADC, IORA, ACP) na kuhamasisha matumizi ya fursa za masoko ya kanda hizo; na
- (m) Kukamilisha na kusimamia mfumo wa kielektroniki na wa kitaasisi wa utoaji wa leseni za biashara.



### Huduma za Fedha

158. Huduma za fedha, ikiwemo za kibenki na mifumo ya malipo, masoko ya mitaji, bima, hifadhi za jamii, na huduma ndogo ndogo za fedha (*microfinance*), ndio mlizamu wa kuimarisha uchumi. Katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, Chama kilielekeza SMZ kusimamia na kuendeleza huduma za fedha ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-
- (a) Kuendelea kukua kwa huduma za fedha kwa wastani wa asilimia 9 kwa mwaka;
  - (b) Kuimarika huduma za kibenki kwa kuongeza idadi ya benki kufikia 13 mwaka 2019 zenye jumla ya amana ya shilingi bilioni 897 na mikopo ya shilingi bilioni 390 mwaka 2019;
  - (c) Kuongezeka kwa idadi za mashine za kutolea fedha zilizowekwa maeneo mbalimbali mijini na vijijini kutoka 45 mwaka 2015 hadi 466 mwaka 2020;
  - (d) Kuimarika kwa huduma za bima ambapo kampuni za bima zimeongezeka kutoka kampuni tano mwaka 2015 hadi kufikia 10 mwaka 2019;
  - (e) Kufanyika kwa utafiti wa upatikanaji na utumiaji wa fedha Zanzibar (*Finscope*) na matokeo yake yamesaidia kuandaa sera na mikakati ya kuimarisha sekta ya fedha;
  - (f) Kufanya utafiti wa kuangalia huduma jumuishii za fedha (*financial inclusion*);
  - (g) Kuanzisha idara inayosimamia sekta ya fedha katika Wizara ya Fedha na Mipango; na
  - (h) Kukamilisha sera ya huduma ndogo ndogo za kifedha.
159. **Huduma za fedha ni muhimu katika kuimarisha na kuharakisha miamala ya kiuchumi. CCM itaelekeza SMZ kuimarisha huduma za fedha zikiwemo mabenki, bima, soko la mitaji na usalama katika uwekezaji ili kukidhi mahitaji halisi ya wawekezaji na wananchi walio wengi kwa kutekeleza yafuatayo:-**
- (a) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa sekta ya fedha;
  - (b) Kufanya maandalizi na kuanzisha soko la mitaji la Zanzibar;
  - (c) Kuboresha utoaji huduma za fedha na za kibenki kwa kupanua wigo wa matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika sekta za fedha na benki;
  - (d) Kukuza huduma za bima kwa sekta isiyo rasmi kwa kuzingatia maeneo ya vijijini ambayo hayafikiwi na huduma hizo;



- (e) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Miamala Salama ya Mwaka 2008 na kuandaa sheria ya huduma ndogo ndogo za kifedha;
- (f) Kuimarisha huduma za kifedha kwa mfumo wa uchumi wa kiislam; na
- (g) Kuimarisha Benki ya Watu wa Zanzibar ili iweze kutoa huduma bora zaidi na kuwafikia wateja wengi zaidi.

### Vyama vya Ushirika

160.

Moja ya hatua za kuongeza ajira na kupunguza umasikini ni uwepo, uanzishwaji na uendelezaji wa vyama vya ushirika. Katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, CCM ilielekeza SMZ kusajili, kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika, kuanzisha vyama vikuu vya kisekta na kutoa mafunzo ambapo mafanikio yafuatavyo yamepatikana:-

- (a) Kukamilisha mapitio ya sera ya maendeleo ya ushirika na kutunga Sheria ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2018;
- (b) Jumla ya wanachama wanaowakilisha familia 34,005 wamefikiwa na huduma za fedha kupitia SACCOS mbalimbali. Aidha, taarifa za vyama hai 1,178 zimekusanywa na kuingizwa katika mfumo, sawa na asilimia 32 ya vyama vyote 3,729 vilivyosajiliwa;
- (c) Kusajili vyama vipya 897 (674 Unguja na 223 Pemba), kati ya hivyo 874 ni vya uzalishaji na 23 ni vya SACCOS;
- (d) Kutoa mafunzo kwa SACCOS 215 zenye wanachama 12,279 kwa ajili ya kuimarisha uendeshaji wa SACCOS, katika fani za uongozi, utunzaji wa vitabu, uimarishaji wa mitaji, kuandaa mipango ya biashara, udhibiti wa muda na mabadiliko ya mtazamo. Aidha, waandishi wa habari 47 wamepatiwa mafunzo na vipindi 120 vilivyoelimisha jamii kuhusu SACCOS viliandaliwa na kurushwa hewani kupitia televisheni na redio;
- (e) Kukagua vyama vya ushirika 2,318 Unguja na Pemba, vyama 356 vimekaguliwa hesabu zake na vyama 1,962 vimefanyiwa ukaguzi wa kawaida. Mitaji ya vyama vya akiba na mikopo imekuwa na kufikia bilioni 12.8 hadi mwaka 2017; na
- (f) Kuhamasisha uundaji wa vyama vikuu viwili vya sekta ya kilimo (Unguja na Pemba). Pia chama kikuu cha kitaifa cha huduma za fedha (Faraja Union Ltd) kimeundwa na kimeanza shughuli zake za kulinda masilahi ya wanachama wake kwa kujenga mtaji wa pamoja.

161.

**CCM inatambua kuwa Ushirika ni njia mojawapo ya kuwaunganisha wazalishaji kupata mitaji na masoko. Katika Ilani hii, Chama kitaelekeza SMZ kuhakikisha kuwepo kwa mitaji ya uhakika kwa ajili ya shughuli za uzalishaji na kutanua mtandao wa masoko kwa wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyabiashara na wazalishaji wadogo na wa kati kupitia vyama vyao vya ushirika kwa kutekeleza yafuatayo:-**



- (a) Kuhakikisha kuwa wajasiriamali wanaungana pamoja kuunda vyama vya ushirika katika kutafuta na kuhudumia masoko ya bidhaa zao;
- (b) Kusimamia usajili wa vyama vya ushirika 1000, kukagua vyama vya ushirika 2,000 na kuvipatia mafunzo vyama 2,000 juu ya uendeshaji na usimamizi wa vyama hivyo, pamoja na kuvisaidia katika utatuzi wa migogoro inayojitokeza; na
- (c) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za fedha kwa vyama vya ushirika kwa kuviunganisha kwenye SACCOs, makampuni na taasisi za fedha.

### **Uchumi wa Rasilimali za Maji/Uchumi wa Buluu (Blue Economy)**

162.

**Zanzibar imezungukwa na Bahari ya Hindi na ipo karibu na mwambao wa mashariki ya Afrika, hivyo inazo fursa adhimu za kutumia eneo lake la bahari, nafasi yake ya kijiografia na rasilimali za bahari kuharakisha maendeleo yake ya kiuchumi. Ili kuratibu vyema matumizi ya bahari na rasilimali zake katika kujenga Uchumi wa Buluu, CCM itaelekeza SMZ kufanya mambo yafuatayo:-**

- (a) Kuandaa Mpango mahsusi wa matumizi ya maeneo ya bahari (*Marine Spatial Plan*) na kuanza kuutekeleza;
- (b) Kujenga miundombinu ya kimkakati ya kuifanya Zanzibar kuwa kituo maalum cha biashara, usafiri na usafirishaji baharini (*marine transportation*);
- (c) Kuwa kituo cha kanda cha uvuvi na mazao ya baharini;
- (d) Kutumia mazao ya baharini ikiwemo samaki, mwani na chumvi kama chachu ya maendeleo ya viwanda;
- (e) Kutumia bahari na fukwe kwa ajili ya:-
  - (i) Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia;
  - (ii) Kuendeleza zaidi utalii wa bahari, fukwe n.k; na
- (f) Kuweka mfumo bora wa kitaasisi wa kuratibu maendeleo ya Uchumi wa Buluu.

### **Matumizi Bora ya Teknolojia**

163.

**CCM inatambua faida ya maendeleo makubwa ya teknolojia duniani katika mageuzi ya kiuchumi. Katika miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kuhakikisha kuwepo kwa watu wenye weledi wa kuandaa na kufanya matumizi sahihi ya teknolojia iliyo salama, wezeshi na rahisi katika shughuli za kiuchumi na kijamii kwa kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kujenga utaalum wa upeo maalum wa teknolojia ya dijitali, utengenezaji na matumizi ya roboti, fani zote za TEHAMA na fani ya “*Artificial Intelligence*” kwa kushirikiana na sekta binafsi;



- (b) Kuanzisha timu (*pool*) ya wataalam wa hadhi ya juu kuwezesha mafunzo vijana 25 kwa kutumia ufadhili (*scholarship*) maalum kwa vyuo vikuu na taasisi mahiri za teknolojia duniani;
- (c) Kuimarisha Taasisi ya Ufundi ya Karume (KIST) na kuzipandisha hadhi skuli za ufundi za Mikunguni Unguja na Kengeja Pemba kuwa taasisi za ufundi zenye hadhi maalum;
- (d) Kusisitiza mafunzo ya vitendo na umahiri (*precision technology & tooling*);
- (e) Kuanzisha vituo atamizi (*incubators*) na kongano (*Clusters*) maalum za teknolojia pamoja na kuendeleza na kusaidia wahitimu wa vituo hivyo kuanzisha makampuni;
- (f) Kutumia wataalam wa ndani katika kuimarisha matumizi ya teknolojia kwa kuandaa program za ufundi na teknolojia (*benchmarking*);
- (g) Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji wa teknolojia; na
- (h) Kuanzisha maeneo maalum ya matengenezo ya vifaa vya kielektroniki ili kuongeza fursa za ajira kwa vijana.

### **Sekta za Miundombinu ya Kiuchumi**

164.

Sekta ya usafiri na usafirishaji ina umuhimu mkubwa katika kukuza shughuli za uchumi na kijamii, na kuiunganisha Zanzibar na mwambao wa Afrika na dunia kwa ujumla. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita SMZ imeimarisha miundombinu ya usafiri na usafishaji na mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

#### **Barabara**

- (a) Jumla ya kilomita 90.5 za barabara za Unguja zimejengwa kwa kiwango cha lami katika kisiwa cha Unguja:
  - Jendele–Cheju–Kaebona (km 11.7) ;
  - Koani –Jumbi (km 6.3) ;
  - Bububu (Polisi) – Mahonda - Kinyasini – Mkokotoni (km 33.8) ;
  - Matemwe – Muyuni (km 7.6) ;
  - Mwanakwerekwe - Fuoni – Jumbi (km 7);
  - Fuoni – Kombeni (km 8.6) ;
  - Pale – Kiongole (km 4.6);
  - Melitano - Kwarara (km 3);
  - Donge – Muwanda (km 4.2);
  - Nyumba Mbili – Mpendae (km 1.2);
  - Kijitoupele – Fuoni – Mambosasa (km 2.5).





- (b) Jumla ya kilomita 13.54 zimejengwa kwa kiwango cha lami katika halmashauri za Zanzibar, barabara hizo ni:
- Msingini ( km 0.65);
  - Soko kongwe – Skuli ya Ngomeni (km 0.33);
  - Chake Hospital – Tibirinzi ( km 0.45);
  - Kilimani estate (km 0.55);
  - Kikwajuni – Maisara ( km 0.32);
  - Mitiulaya – Muembeladu Hospital (km 0.32);
  - Mzunguko wa mnara wa kisonge (km 0.30);
  - Misufini mpaka kwa Biziredi (km 0.65);
  - Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar (km 0.22);
  - Magogoni – Kinuni Skuli (km 3);
  - Nyarugusu – Kijitoupele (km 1.65);
  - Kijitoupele – Mambosasa (km 2);
  - Mambosasa – Mwera ( km 3.4).
- (c) Jumla ya kilomita 23 zimejengwa kwa kiwango cha kifusi ambazo ni:
- Jozani – Charawe – Ukongoroni – Bwejuu;
  - Mbuyu maji – Kiwengwa (km 2.5);
  - Mkwajuni – Kijini (km 9.4);
  - Mfurumatonga – Mlilile (km 3);
  - Kilombero - Mgonjoni (km 3.5);
  - Kinduni – Kichungwani (km 2).
- (d) Jumla ya kilomita 55.1 zimejengwa kwa kiwango cha lami katika kisiwa cha Pemba:
- Ole – Kengeja (km 35),
  - Mkanyageni – Kangani (km 6.5),
  - Mgagadu - Kiwani (km 7.6),
  - Wawi – Mabaoni (km 3),
  - Kuyuni - Ngombeni (km 3).
- (e) Jumla ya kilomita 30 kwa kiwango cha kifusi Pemba
- Kipapo – Mgelema – Wambaa (km 6);
  - Mgagadu – Kiwani (km 8.8);
  - Finya – Kicha (km 4.5);
  - Konde – Makangale;
  - Micheweni – Kiuyu;
  - Pujini – Kibaridi (km 2);
  - Mtambwe – Chanjaani (km 1);
  - Pandani – Mlindo (km 3).
- (f) Jumla ya kilomita 127.8 zimefanyiwa upembuzi yakinifu, usanifu na kuandaliwa michoro ya kina Unguja na Pemba:
- Tunguu – Makunduchi (km 48);
  - Mkoani – Chake Chake (ikiwemo Chanjaani - Airport) (km 43.5);
  - Fumba – Kisauni (km 12);



- Mkwajuni – Kijini (km 9.4);
- Umbuji – Uroa (km 6.9);
- Kichwele – Pageni (km 4.8);
- Unguja Ukuu – Uzi Nga'mbwa (km 3.2).

- (g) Kukamilika kwa ujenzi wa daraja la kisasa la Dk. Shein katika eneo la Kibonde Mzungu. Eneo la Mwanakwerekwe limenyanyuliwa mita mbili kwa umbali wa mita 400 kutoka Sokoni Mwanakwerekwe hadi Makaburini. Ujenzi wa msingi wa maji ya mvua yaliyokuwa yanatuwama barabarani eneo la Kiembesamaki lenye urefu wa jumla ya kilomita 1.5.....?
- (h) Kuweka taa za kuongoza magari kwenye makutano ya barabara:-
- Mlandege;
  - Mtoni;
  - Biziredi (Unguja);
  - Chake Chake;
  - Wete.
- (i) Kununua vifaa vipya vya ujenzi na matengenezo ya barabara pamoja na mtambo mpya wa kupikia lami (Unguja). Kuimarisha karakana kuu ya Serikali kwa kupatiwa vitendea kazi vipya ili kufanyia matengenezo ya magari ya taasisi mbalimbali za Serikali na watu binafsi.
- (j) Kujenga madaraja makubwa tisa katika maeneo yafuatayo:-
- Zingwezingwe;
  - Mkaratini;
  - Mto mchanga;
  - Kinyasini;
  - Mtopweza
  - Kinuni (Chaani);
  - Kicheche;
  - Fuoni.
- (k) Kujenga madaraja madogo 19 katika maeneo yafuatayo: *Fidel Castro*, Mijinjeni, Changaweni, Mfikiwa jeshini, kwa mwari, Mto wa mawe, kwa vongo, Shangani, Kwa kichwa, Mivumoni, Kwa utao, Kicha, Konde, Hamsini, Mlima saad, Mto Mkuu, Kiwani, Pujini, Tasini na Bungala.

165. **Maendeleo ya uchumi yanahitaji miundombinu ya barabara za kisasa, zilizo imara, salama, zinazounganisha miji na vijiji, na zinazorahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii na masoko. Katika Ilani hii, CCM itaelekeza SMZ kuongeza masafa ya barabara zenye ubora na za kisasa, miundombinu shirikishi na zinazopitika katika hali na nyakati zote kwa kufanya yafuatayo:-**



- (a) Kufanyia mapitio ya Sera ya Taifa ya Usafiri na Mpango Mkuu wa Usafiri (*Transport Master Plan*) ili uendane na mahitaji ya sasa na baadae, hususan kwa miundombinu ya usafiri wa nchi kavu kwa lengo la kujenga na kuimarisha barabara za mijini na vijijini;
- (b) Kufanya utafiti wa kubaini na kuchora ramani ya miundombinu yote iliyopita chini ya ardhi na karibu na barabara ili kuimarisha uimara wa barabara;
- (c) Kuendeleza utunzaji na matengenezo ya barabara zilizokwisha kujengwa na kuendelea kununua vifaa vya kisasa vya kufanya marekebisho katika maeneo mbalimbali;
- (d) Kuzifanyia matengenezo makubwa (*overlaying*) barabara zote za miji (Unguja na Pemba) pamoja na kuijenga misingi ya maji ya mvua yanayotuwama na kuathiri ubora wa barabara hizo ili ziweze kutumika kwa usalama zaidi;
- (e) Kuwekwa taa za barabarani kwenye njia kuu za miji zilizobakia kwa urefu wa kilomita 50;
- (f) Kuweka taa za kuongozea magari kwenye makutano 10 ya barabara ambayo yamekuwa na msongamano wa magari;
- (g) Kujenga kilomita 30 za misingi ya kuondoshea maji ya mvua kwa barabara kuu;
- (h) Kuzijenga barabara kwa kiwango cha lami Unguja na Pemba zenye urefu wa kilomita 197.6 kwa mpango ufuatao:-
  - Tunguu – Jumbi (km 9.3);
  - Jozani – Charawe – Ukongoroni – Bwejuu (km 23.3);
  - Kizimbani – Kiboje (km 7.2);
  - Kichwele – Pangenji (km 4.8);
  - Kinduni – Kichungwani – Kitope (km 3.5);
  - Umbuji – Uroa (km 6.9);
  - Mkwajuni – Kijini (km 9.4);
  - Sharifumsa – Mwanyanya - Bububu Skuli (km 3.6);
  - Finya – Kicha (km 8.8);
  - Chake – Wete (km 22.1);
  - Fumba - Kisauni (km 12);
  - Tunguu - Makunduchi (km 48);
  - Mkoani Chake Chake/Chaanjani (Airport) (km 43.5).
- (i) Kuziimarisha barabara za miji zenye urefu wa kilomita 36 ambazo ni:
  - Bandari ya Malindi – Kinazini – Mtoni – Bububu (km 11.2);
  - Creek road – Mkunazini – Mnazimoja (km 1.3);
  - Welezo – Amani - Ng’ambo (km 2.9);
  - Mtoni – Amani – Kiembesamaki (km 8.5);
  - Uwanja wa Ndege – Kiembesamaki – Kilimani - Mnazimmoja



- (km 6.6);
- Mji wa Wete (km 2);
- Mji wa Chake Chake (km 3.5).

- (j) Kuzifanyia upembuzi yakinifu na usanifu kwa barabara zenye urefu wa kilomita 96.5 kama zifuatazo:
- Kitogani – Paje (km 11);
  - Kizimkazi – Makunduchi (km 13);
  - Dunga – Chwaka – Pongwe (km 30);
  - Kinyasini – Kiwengwa (km 10);
  - Mahonda – Donge – Mkokotoni (km 13);
  - Mshelishelini – Pwani Mchangani (km 7.5);
  - Muyuni (Matemwe) – Nungwi (km 12);
  - Chwale – Kilindini – Konde Sokoni (km 25);
  - Konde Sokoni – Ngezi – Makangale – Kigomasha (km 12);
  - Kilindini – Micheweni (km 6);
  - Micheweni – Kiuyu Bandarini – Maziwa Ng’ombe (km 10.5);
- (k) Kujenga daraja la Uzi Ng’ambwa lenye urefu wa kilomita 2.5.

### **Bandari**

166. Juhudi kubwa zimechukuliwa katika kuimarisha bandari za Unguja na Pemba ili ziweze kusaidia kukuza uchumi na shughuli za kijamii. Mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 ni kama ifuatavyo:

- (a) Kutengeneza gati ya mkoani Pemba na kiungo chake ambacho kiliathirika kutokana na nguvu za mawimbi;
- (b) Kufanya mapitio ya mpango wa uendelezaji wa bandari ya Mpigaduri pamoja na kufanya upya upembuzi yakinifu kwa kujenga bandari hiyo kulingana na mahitaji ya sasa;
- (c) Kutangazwa rasmi eneo la Mangapwani kuwa eneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa bandari mpya ya kuhudumia meli za mafuta na gesi;
- (d) Kuongeza vifaa vya kuhudumia mizigo katika bandari za Zanzibar kulingana na mahitaji ya sasa; na
- (e) Kuimarisha bandari ya Mkokotoni kwa kujenga jengo jipya la ofisi pamoja na kuanza ujenzi wa gati dogo.

167. **Bandari ni njia kuu inayounganisha visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na Tanzania Bara na sehemu nyengine duniani. Kwa kutambua umuhimu wake, katika Ilani hii, CCM itaelekeza SMZ kujenga na kuongeza uwezo na ufanisi wa bandari zetu katika upakuzi na upakuzi wa mizigo na kuhudumia abiria ili kuendelea kutoa huduma bora zaidi katika mwambao wa Afrika Mashariki kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-**



- (a) Kuendeleza miundombinu na kujenga bandari za kisasa zitakazotenganisha shughuli za abiria (Malindi), mizigo ya makontena (Mpigaduri) na mafuta na gesi (Mangapwani);
- (b) Kuimarisha huduma za bandari kwa kutumia vifaa na teknolojia za kisasa ili kuongeza idadi ya makontena (TEUs) kutoka 82,312 mwaka 2018 hadi makontena 105,000 ifikapo 2025; kupunguza idadi ya siku za kuegesha kutoka siku saba mwaka 2018 hadi siku tano mwaka 2025; kuongeza idadi ya abiria kutoka 2,780,299 mwaka 2018 hadi 3,800,000 mwaka 2025;
- (c) Kujenga miundombinu ya kuhudumia meli zinazopita mwambao wa Afrika Mashariki, kupata huduma za kuongeza mafuta, maji safi na kufanya matengenezo;
- (d) Kujengwa kwa Chelezo kikubwa cha kufanyia matengenezo vyombo vya ndani pamoja na vinavyopita katika bahari ya Zanzibar;
- (e) Kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari kubwa Pemba; na
- (f) Kufanya upembuzi yakinifu na kuanza ujenzi wa bandari kubwa ya uvuvi.

### Usafiri wa Baharini

168.

Juhudi kubwa zimechukuliwa katika kuimarisha usafiri wa baharini ili kusaidia kukuza uchumi na shughuli za kijamii. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kuimarisha huduma za usafiri kwa wananchi, hususan kati ya kisiwa cha Unguja na Pemba kwa kununua meli mpya ya abiria na mizigo (MV Mapinduzi II) yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 200 za mizigo na kufanya matengenezo makubwa ya MV. Maendeleo na MT. Ukombozi;
- (b) Kununua meli mpya ya mafuta (MT Ukombozi II) yenye uwezo wa kupakia tani 3,500 za mafuta;
- (c) Kununua boti ndogo tano kwa ajili ya kuvusha wananchi wanaoishi kwenye visiwa vidogo vidogo;
- (d) Kufanya mapitio ya sheria ya kusimamia usafiri wa baharini (*Zanzibar Maritime Transport Act*) na kuandaa kanuni 23 za kuimarisha usafiri wa baharini na Ofisi ya Mrajisi wa Meli ya Mamlaka ya Usafiri wa Baharini ("*Zanzibar Maritime Authority*" - ZMA); na
- (e) Kuimarika kwa usafiri wa baharini kutokana na uwekezaji wa sekta binafsi ambapo jumla ya kampuni 49 tayari zimewekeza katika sekta ya usafiri wa baharini na zinazoendelea kutoa huduma ni 33.



169. **CCM inatambua haja ya kuwepo kwa usafiri wa baharini ulio salama, wenye uhakika na wa haraka kwa raia na wageni na usafirishaji wa mali zao. Katika Ilani hii Chama kitaelekeza SMZ kuendelea kusimamia shughuli za usafiri wa baharini katika ubora na viwango vinavyokubalika kimataifa kwa kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuimarisha usalama wa usafiri baharini kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ya usafiri baharini kama inavyotolewa na Shirika la Usafiri wa Bahari Duniani (IMO);
- (b) Kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni za usafiri wa baharini ili kupunguza ajali za vyombo vya baharini kwa kuimarisha utendaji wa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini (ZMA); na
- (c) Kuendeleza usafiri wa baharini kwa kuliimarisha shirika la meli na kushajihisha uwekezaji zaidi wa sekta binafsi.

### **Usafiri wa Anga**

170. Juhudi kubwa zimechukuliwa katika kuimarisha usafiri wa anga (Unguja na Pemba) ili ziweze kusaidia kukuza uchumi na shughuli za kijamii. Mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kumalizika ujenzi wa jengo jipya la abiria (*Terminal III*) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (*Abeid Amani Karume International Airport - AAKIA*);
- (b) Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa Kiwanja cha Ndege cha Pemba kwa lengo la kukitanua na kuimarisha miundombinu na huduma za abiria, ndege na mizigo;
- (c) Kukamilika kwa mapitio ya Mpango Mkuu wa Usafiri wa Anga Zanzibar pamoja na Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Kiwanja cha Ndege cha AAKIA;
- (d) Kuimarisha ubora wa jengo la abiria (T2) kwa kufunga mashine tano za ukaguzi na mkanda wa kuhudumia mizigo ya abiria na kuweka vipooza hewa katika eneo la kufikia na kuondokea abiria;
- (e) Kuimarisha usalama katika kiwanja cha ndege cha AAKIA kwa kununua gari nne za zimamoto na kufikisha kiwango cha “*Category 9*”; na
- (f) Kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja cha ndege kidogo cha Kigunda (Nungwi) chenye urefu wa kilomita 2 ili kukuza sekta ya utalii.

171. **CCM inatambua kuwa usafiri wa anga ni njia muhimu na ya haraka inayounganisha visiwa vya Zanzibar na sehemu nyengine duniani. Katika Ilani hii, Chama kitaelekeza SMZ kuingeza uwezo na ufanisi wa viwanja**





**vya ndege kwa kuzingatia viwango vya kimataifa ili kuendana na kasi ya ongezeko la abiria hususan watalii na kuvutia mashirika ya ndege mengi zaidi kufanya safari zake nchini kwa kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuendeleza ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Pemba ikiwemo kuongeza urefu wa njia ya kurukia ndege (*runway*) kufikia mita 2,500, kujenga jengo jipya la abiria na kuimarisha huduma zote za mahitaji ya kiwanja hicho;
- (b) Kumalizia ujenzi wa uwanja mdogo wa ndege wa Kigunda na kujenga viwanja viwili vya kurukia na kutua helikopta, kimoja Unguja na kimoja Pemba; na
- (c) Kuimarisha ubora wa vifaa na huduma kwenye uwanja wa ndege wa AAKIA.

### **Mawasiliano**

172.

Juhudi kubwa zimechukuliwa katika kuimarisha sekta ya mawasiliano Zanzibar ili iweze kusaidia kukuza uchumi na shughuli za kijamii. Mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kuanzisha Wakala wa Mkongo wa Mawasiliano Zanzibar ambao unasimamia uendeshaji wa Mkongo wa Taifa kibiashara pamoja na kituo cha kutunzia kumbukumbu za kimtandao (*Data Center*) kwa Zanzibar;
- (b) Kuendeleza uunganishaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye majengo 84 ya Serikali;
- (c) Kuimarisha mawasiliano kwa kuuza uwezo wa ziada wa matumizi ya mkongo kwa sekta binafsi;
- (d) Kufanya mapitio na kuuimarisha Mkongo wa Mawasiliano; na
- (e) Kukamilika kwa ujenzi wa vituo 10 vya huduma za mawasiliano ya mtandao kwenye wilaya zote za Zanzibar kwa matumizi ya jamii.

173.

**Katika kuimarisha sekta ya mawasiliano CCM itaelekeza SMZ kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kujenga kituo mbadala cha kuhifadhia taarifa (*Disaster Recovery Centre*);
- (b) Kujenga miundombinu ya TEHAMA pamoja na kushajiisha matumizi ya TEHAMA kwa jamii;
- (c) Kutanua matumizi ya mkongo wa Taifa wa mawasiliano kuwa wa kibiashara; na
- (d) Kuboresha na kuimarisha kituo cha sasa cha “*data center*” kwa kuondoa vifaa chakavu na kuweka mifumo mipya.



## Nishati

174. Sekta ya nishati ni muhimu sana kwa wananchi na maendeleo ya nchi kiujumla hususan kuelekea katika uchumi wa viwanda na huduma. Maeneo yaliyopewa kipaumbele katika sekta ya nishati ni kufanya tafiti za kubaini nishati mbadala kama vile umeme wa jua na upepo, utafutaji wa mafuta na gesi asilia na kuimarisha usafirishaji na kuongeza kasi ya usambazaji umeme nchini. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita 2015 -2020 sekta ya nishati imepata mafanikio yafuatayo:-
- (a) Kufanya utafiti wa nishati mbadala wa jua na upepo na kuthibitika kuwepo kwa fursa ya kutumia umeme wa jua. Utafiti unaendelea kwa kubaini uwezekano wa kuzalisha umeme kwa kutumia upepo;
  - (b) Kuendelea kuimarisha huduma za umeme kwa kufikisha huduma hiyo kwa vijiji 389 sawa na asilimia 128 ya lengo lililowekwa la vijiji 305. Aidha, jumla ya visiwa vidogo vidogo vitano vimeunganishwa na huduma ya umeme;
  - (c) Kuimarisha miundombinu ya umeme Pemba kutoka 11KV kuwa 33KV;
  - (d) Kuimarisha Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) na kulitoa kutoka kuendeshwa kwa hasara hadi kupata faida ambapo mwaka 2019 shirika lilitoa gawio la shilingi bilioni moja;
  - (e) Kutayarisha Sera na Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia, kuunda Mamlaka ya Usimamizi wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) na Kampuni ya Zanzibar ya Mafuta (ZPDC);
  - (f) Kuandaa Mkataba wa Modeli ya Kugawana Mafuta na Gesi Asilia (*Model Production Sharing Agreement - MPSA*);
  - (g) Kuingia mkataba wa mgawanyo wa mafuta na Gesi Asilia itakayozalishwa na Kampuni ya RAKGas kwa ajili ya Kitalu cha Pemba – Zanzibar; na
  - (h) Kujenga uwezo kwa Wazanzibari 58 katika fani za mafuta na gesi asilia.
175. **Ili kuimarisha sekta ya nishati ambayo inajumuisha umeme, nishati mbadala, mafuta na gesi asilia, CCM itaelekeza SMZ kutekeleza yafuatayo:-**
- Umeme na Nishati Mbadala***
- (a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Mwaka 2020 na kuendeleza juhudi za upatikanaji wa umeme na nishati mbadala;
  - (b) Kuimarisha shughuli za usimamizi wa huduma za umeme na usambazaji wa nishati katika vijiji 305 (Unguja 180 na Pemba 125);



- (c) Kujenga njia kubwa ya umeme ya msongo wa 132KV kwa kuelekea kusini na kaskazini mwa kisiwa cha Unguja yenye urefu wa kilomita 100 pamoja na kujenga vituo vikubwa viwili vya kupoza umeme kwa lengo la kuimarisha huduma bora ya umeme;
  - (d) Kuimarisha miundombinu ya usambazaji umeme wa 11 KV kwa Unguja;
  - (e) Kufanya utafiti wa vyanzo vya umeme pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa jua ili kupata umeme wa Megawati 30 kwa Unguja na Megawati 8 kwa upande wa Pemba;
  - (f) Kuimarisha Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kwa lengo la kuliwezesha kujiendesha kibiashara;
  - (g) Kuwapunguzia wananchi gharama za uungaji umeme kwa watu wenye kipato cha chini;
  - (h) Kufanya utafiti wa kina wa mlinganisho (*Comparative Study*) wa kuwezesha kupata chanzo kipya cha nishati ya umeme ili kukidhi mahitaji ya ziada yanayojitokeza;
  - (i) Kuanza ujenzi wa bohari yenye uwezo wa kuweka tani 30,000 za mafuta ya petroli katika bandari mpya ya Mangapwani kwa ajili biashara ya mafuta na gesi;
  - (j) Kuhamasisha matumizi ya majiko banifu na kushajiisha matumizi ya gesi majumbani, viwandani na vyombo vya usafiri ili kupunguza matumizi ya makaa na kuni kwa ajili ya kulinda mazingira;
  - (k) Kushajiisha sekta binafsi kuwekeza katika usambazaji wa nishati ya mafuta na gesi; na
  - (l) Kuhamasisha uwekezaji wa huduma za vyombo vya usafirishaji wa mafuta na gesi (*supply vessels*).
- Mafuta na Gesi Asilia**
- (a) Kuendeleza utafiti wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vilivyopo chini ya usimamizi wa SMZ na kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa kazi za utafutaji, uchimbaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia kwa kitalu cha Pemba – Zanzibar;
  - (b) Kuendelea kuboresha na kuimarisha utendaji wa Kampuni ya Taifa ya Mafuta Zanzibar (ZPDC) na Mamlaka ya Usimamizi wa Mafuta na Gesi (ZPRA) ili yaweze kutoa mchango stahiki katika kutafuta, kuendeleza na kudhibiti sekta za mafuta na gesi
  - (c) Kushirikiana na kampuni za mafuta katika utafutaji, uchimbaji na uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia;



- (d) Kukuza uwezo wa watendaji na jamii katika sekta ya mafuta na gesi asilia na kuhamasisha wananchi kushiriki na kufaidika na sekta hiyo; na
- (e) Kujenga kituo cha kuhifadhi taarifa na sampuli za mafuta na gesi asilia (*Data Repository Centre*).

### **Ardhi**

176.

Ardhi ni rasilimali muhimu katika uwepo, uhai na ustawi wa Taifa. Moja ya lengo la Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Mwaka 1964 ni kuweka ardhi yote ya Zanzibar mikononi mwa wananchi wenyewe. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, CCM ilielekeza SMZ kuendelea kupanga, kupima, kusajili na kutoa hati ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- (a) Kusajili maeneo 3,067 Unguja 1,646 na Pemba 1,421;
- (b) Kutayarisha jumla ya ramani mpya 619, kati ya hizo 546 ni ramani msingi na 73 ni ramani picha (*orthophotographics*);
- (c) Kupima viwanja 990 na kutoa hati 1,469 kwa matumizi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii. Jumla ya miji midogo minne imepangwa kwa Unguja ambayo ni Chwaka, Mkokotoni, Nungwi na Makunduchi ikiwa ni miongoni mwa miji midogo 14 ya Zanzibar iliyokusudiwa kupangwa na maeneo mengine saba ikiwemo Dunga, Kiwengwa na Pongwe kwa Unguja na Shumba Mjini, Finya, Pagali na Mkanyageni kwa Pemba. Aidha, maeneo matano ya wazi (*open space*) yamepangwa ambayo ni Kibanda Maiti, Daraja Bovu, Chumbuni na Kiembesamaki kwa Unguja na Mwanamashungi kwa Pemba; na
- (d) Kupatiwa ufumbuzi migogoro ya ardhi 250 kupitia Mahakama ya Ardhi na elimu kwa jamii imetolewa kuhusu Sheria za Ardhi. Aidha, huduma za utatuzi wa migogoro ya ardhi zimesogezwa karibu na wananchi kwa kufungua Mahakama ya Ardhi katika Mikoa yote ya Unguja na Pemba.

177.

**CCM inatambua kuwa ardhi ndio utambulisho na mhimili mkuu wa maisha na maendeleo ya binadamu. Katika miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kusimamia matumizi endelevu ya ardhi pamoja na kuhakikisha wananchi wote wanapata fursa ya kutumia ardhi kwa shughuli za uzalishaji na makaazi kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-**

- (a) Kufanya utambuzi na usajili wa ardhi katika maeneo 15 ikiwemo Shakani, Mbweni, Mombasa kwa Mchina, Meya, Kidoti, Mahonda, Jambiani, Uroa, Fuoni, na Amani kwa upande wa Unguja na Bopwe, Utaani, Gombani, Konde na Micheweni kwa upande wa Pemba;
- (b) Kufanya mapitio na marekebisho ya ramani za visiwa vya Unguja na Pemba kwa mujibu wa mahitaji na mabadiliko yatakayojitokeza;



- (c) Kufanya mapitio ya Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi na kupanga ardhi kwa mujibu wa matumizi ya sasa na akiba kwa matumizi ya baadae;
- (d) Kuendeleza kazi ya upimaji wa viwanja na utoaji wa hati kwa matumizi ya kiuchumi na kijamii kwa kuzingatia mipango ya matumizi bora ya ardhi (kitaifa na ya miji) pamoja na ramani za miji kwa kutekeleza yafuatayo:-
  - (i) Kupanga na kupima maeneo ya miji midogo (townships) kumi na nne ikiwemo Nungwi, Mkokotoni, Chwaka, Dunga, Mahonda, Makunduchi, Kivunge, Kivinje, Kitogani na Gamba kwa Unguja na Wete, Mkoani, Konde, Micheweni na Kengeja kwa Pemba;
  - (ii) Kupanga maeneo mengine sita (*upgrading*) ili kupunguza ujenzi kiholela ikiwemo Sebuleni, Amani, Meya, Magomeni, Jang'ombe na Ziwa Maboga;
  - (iii) Kuimarisha Kamisheni ya Ardhi kwa kuipatia rasilimaliwatu na vifaa vya kutosha ili iweze kutimiza majukumu yake ipasavyo; na
  - (iv) Kuongeza mapato ya Serikali kwa kuimarisha ukusanyaji wa kodi za ardhi.
- (e) Kuendeleza jitihada za kupunguza mrundikano wa kesi za ardhi kwa kuongeza kasi ya utoaji wa maamuzi ya mashauri yanayowasilishwa katika Mahakama ya Ardhi na kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa usajili wa ardhi katika kupunguza migogoro;
- (f) Kuainisha na kuyatangaza katika Gazeti rasmi la Serikali maeneo ya akiba ya ardhi (*land bank*) kwa ajili ya matumizi ya baadae ya shughuli za kiserikali, kiuchumi na kijamii;
- (g) Kuandaa mpango wa matumizi wa visiwa vidogo vidogo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii; na
- (h) Kupata eneo jipya la ardhi kwa kufukia bahari katika eneo la Kinazini Pwani Mbovu kwa ajili ya ujenzi wa mji mpya wa kisasa kwa kushirikiana na sekta binafsi.

### **Makaazi**

178. Juhudi kubwa zimechukuliwa katika kuimarisha makaazi kwa wananchi wa Zanzibar na miongoni mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:

- (a) Kuanzishwa kwa Shirika la Nyumba mwaka 2015 ambalo limekuwa na dhamana ya kusimamia nyumba za Serikali zinazokaliwa na wananchi na kuanzisha miradi mipya ya ujenzi wa nyumba za makaazi kwa ajili ya wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba;



- (b) Kuanzisha Wakala wa Majengo mwaka 2017 kwa malengo ya kuimarisha ujenzi wa ofisi za Serikali na Nyumba za viongozi;
- (c) Kuimarishwa Bodi ya Kondominio mwaka 2018 kwa ajili kusimamia majengo yenye umiliki wa pamoja;
- (d) Kuanzisha kampuni ya ujenzi ya Serikali kupitia idara maalum za SMZ;
- (e) Kukamilika kwa majengo 15 yenye fleti 210 katika eneo ya Mweni na kuanza utekelezaji wa mradi wa Kwahani wenye majengo matano yenye fleti 70; na
- (f) Kuendelezwa kwa nyumba 70 za makaazi kupitia wawekezaji binafsi katika maeneo ya Fumba na Nyamanzi.

179. **Makazi bora ni moja kati ya mambo makuu na ya msingi yaliyopewa kipaumbele katika Manifesto ya Chama cha ASP na kuanza kutekelezwa mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu na kuendelezwa na CCM. Hivyo, katika miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kuhakikisha upatikanaji wa makaazi bora kwa wananchi wengi zaidi wa mijini na vijijini kwa kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuendeleza ujenzi wa nyumba kupitia taasisi za Serikali, sekta binafsi na kwa njia ya ubia (PPP) ili kuhakikisha wananchi wanapata makaazi bora, ikiwemo kuendelea na ujenzi wa nyumba za kisasa za ghorofa;
- (b) Kuimarisha Shirika la Nyumba, kujenga jumla ya nyumba mpya 120 (block 8 Unguja na 6 Pemba);
- (c) Kufanya utafiti maalum wa kubaini teknolojia bora ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu;
- (d) Kufanya matengenezo ya nyumba za maendeleo 300 na nyengine 164 zisizokuwa za maendeleo; na
- (e) Kuimarisha maeneo na mazingira ya majengo yanayokaliwa na wakaazi wengi (yaani kondominio) kwenye nyumba za maendeleo, Unguja na Pemba.

### **Sekta za Huduma za Jamii**

180. Huduma za elimu, afya, makaazi na maji ni muhimu sana kwa ustawi wa jamii. Katika miaka mitano iliyopita CCM kupitia SMZ imeimarisha na kuendeleza zaidi huduma hizo kwa wananchi wote. Mafanikio mahsusi kwa kila huduma ni kama ifuatavyo:-





## Elimu

181. SMZ imeendelea kutoa elimu bure katika ngazi ya maandalizi, msingi na sekondari na imeimarisha mafunzo ya amali na elimu ya juu.

### **Elimu ya Maandalizi**

- (a) Kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi kutoka 41,687 mwaka 2015 hadi wanafunzi 85,974 mwaka 2019;
- (b) Kuongezeka kwa idadi ya skuli za maandalizi kutoka 277 mwaka 2015 na kufikia skuli 382 mwaka 2019;
- (c) Kuanzisha vituo 152 vya TuTu katika Wilaya ya Kaskazini “A” (05), Kaskazini “B” (51), Magharibi “B” (05), Mkoani (69), Wete (05) na Chakechake (17) na kupatiwa vifaa mbalimbali vya kusaidia elimu ya mtoto;
- (d) Kuanzisha programu ya lishe kwa kuwapatia chakula wanafunzi katika skuli 167 za maandalizi na msingi; na
- (e) Kukaribia kufikia uwiano wa mwalimu kwa idadi ya wanafunzi ambayo mwalimu mmoja kwa wanafunzi 33 ikilinganishwa na kiwango cha kimataifa cha mwalimu mmoja kwa wanafunzi 25.

### **Elimu ya Msingi**

- (a) Kuongezeka kwa idadi ya skuli katika ngazi ya elimu ya msingi kutoka 260 mwaka 2015 na kufikia skuli 381 mwaka 2019;
- (b) Kuongezeka kwa uandikishaji wanafunzi kutoka 261,216 mwaka 2015 hadi kufikia 290,510 mwaka 2019;
- (c) Kusambaza chakula katika skuli za msingi 27 ambapo jumla ya wanafunzi 13,022 wamefaidika na huduma hiyo;
- (d) Kuwapatia wanafunzi wote wa maandalizi na msingi mabuku ya kuandikia 43,650,881, kununua boksi 14, 687 za chaki na madaftari ya mahudhurio 6,234;
- (e) Kuvuka kiwango cha kimataifa cha uwiano wa mwalimu kwa idadi ya wanafunzi na kufikia Mwl. moja kwa wanafunzi 40 (1:40) ikilinganishwa na kiwango cha kimataifa cha mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45 (1:45). na
- (f) Kujenga nyumba za walimu katika skuli ya Mbuyutende (02), Kidagoni (01) na Kiongwe (01) Mnarani (01) na Mahuduthi (01).

### **Elimu ya Sekondari**

- (a) Kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi elimu ya sekondari (kidato cha kwanza hadi cha nne) kutoka wanafunzi 84,211 mwaka 2015, sawa na asilimia 62.9, hadi kufikia wanafunzi 130,713 mwaka 2019, sawa na asilimia 87.2;



- (b) Kuongezeka kwa idadi ya skuli zinazotoa elimu ya sekondari ya juu za Serikali na binafsi kutoka skuli 29 mwaka 2015 hadi kufikia skuli 32 mwaka 2019. Aidha, skuli zote 205 za Serikali za sekondari zimepatiwa fedha za ruzuku kwa kiwango cha dola 15 kwa mwanafunzi kwa mwaka ili skuli zijiendeshe zenyewe kwa mujibu wa mipangokazi yao;
- (c) Kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi kutoka 2,647 mwaka 2015 na kufikia wanafunzi 4,808 mwaka 2019;
- (d) Kukamilika kwa ujenzi wa skuli tisa za ghorofa zilizojengwa katika maeneo ya Mwembeshauri, Bububu, Kinuni, Fuoni na Chumbuni kwa Unguja na Wara, Micheweni, Kizimbani kwa Pemba. Aidha, jumla ya madarasa 1,099 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi yamekamilishwa na kutumika;
- (e) Kuendelea kununua na kugawa mabuku ya kuandikia 450,004 na katuni 5,000 za chaki katika skuli za sekondari za Serikali Unguja na Pemba;
- (f) Kuzipatia vifaa vya sayansi skuli zote zenye kidato cha nne na sita ili kuongeza ufaulu wa masomo ya sayansi;
- (g) Kuongezeka kwa asilimia ya ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha pili kutoka asilimia 69.6 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 76.8 mwaka 2019, kidato cha nne kutoka asilimia 72.8 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 71.7 mwaka 2019 na kidato cha sita kutoka asilimia 92.3 mwaka 2015/2016 hadi kufikia asilimia 96.85 mwaka 2018/2019;
- (h) Kukamilika kwa ujenzi wa skuli kubwa yenye dakhalia ya Mkanyageni Pemba na ujenzi wa skuli kama hiyo ya Sekondari Kibuteni unaendelea na umefikia asilimia 89. Aidha, ujenzi wa skuli mbili za Bwefum na Kwarara na jengo la ghorofa la madarasa tisa, maabara, maktaba na chumba cha kompyuta katika skuli ya biashara Mombasa umekamilika;
- (i) Kuimarisha miundombinu ya skuli ya Donge msingi na sekondari ambapo ujenzi umefikia asilimia 95 na kuendelea na ujenzi wa skuli tatu (Mwanakwerekwe na Kibuteni kwa Unguja na Wingwi iliyopo Pemba), ujenzi wa madarasa 48, maabara na maktaba katika skuli 22 za Unguja na Pemba unaendelea na umefikia asilimia 90;
- (j) Kuvuka kiwango cha kimataifa cha uwiano wa mwalimu kwa idadi ya wanafunzi ambapo mwalimu mmoja kwa wanafunzi 25 ikilinganishwa na kiwango cha kimataifa cha mwalimu mmoja kwa wanafunzi 40; na
- (k) Kusambaza jumla ya kompyuta 185 katika skuli za sekondari, msingi, Kituo cha Taifa cha Walimu na vituo vya walimu Unguja na Pemba.



Aidha, kituo cha kuandaa vipindi vya elimu kwa kutumia redio na televisheni kimeanzishwa.

***Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Amali***

- (a) Kuendelea na ujenzi wa vituo viwili vya mafunzo ya amali katika eneo la Makunduchi kwa Unguja na eneo la Daya kwa Pemba ambao umefikia asilimia 65 kwa Makunduchi na asilimia 85 kwa Daya;
- (b) Kuendelea kutoa mafunzo ya elimu ya amali katika vituo vitatu vya Mkokotoni na Mwanakwerekwe kwa Unguja na Vitongoji kwa Pemba. Uandikishaji katika vituo hivyo umeongezeka kutoka wanafunzi 418 mwaka 2015 hadi wanafunzi 1,291 mwaka 2019. Jumla ya vijana 232 wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali na kuwajengea uwezo wa kuweza kuajirika;
- (c) Kukamilika kwa ujenzi wa uzio wa kituo cha Mwanakwerekwe na kituo cha vitongoji umekamilika na ujenzi wa jengo jipya katika Taasisi ya Utalii Maruhubi unaendelea na umefikia asilimia 90;
- (d) Kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la ghorofa mbili katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia pamoja na kununua samani zake. Uandikishaji katika taasisi hiyo umeongezeka kutoka wanafunzi 315 mwaka 2015 na kufikia wanafunzi 649 mwaka 2019. Aidha, taasisi hiyo imeanza kutoa mafunzo ya shahada ya kwanza ya urubani na uhandisi wa ndege na jumla ya wanafunzi 53 wanaendelea na mafunzo; na
- (e) Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wa ualimu katika SUZA, Alsumait na chuo cha kiislami kampasi za Mazizini na Kiuyu, kutoka 1,123 mwaka 2015 na kufikia wanafunzi 1,313 mwaka 2019.

***Elimu ya Juu***

- (a) Chuo Kikuu cha Taifa cha SUZA kimetanuka kwa kuunganishwa na vyuo vingine vinne vikiwemo Chuo cha Uongozi wa Fedha, Chuo cha Maendeleo ya Utalii, Chuo cha Afya na Chuo cha Kilimo na kufanya taasisi zinazoendeshwa katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kuongezeka kutoka Taasisi tano mwaka 2015 hadi kufikia taasisi 10 mwaka 2019;
- (b) Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaosoma katika elimu ya juu katika vyuo vikuu vya Zanzibar kutoka wanafunzi 6,370 mwaka 2015 na kufikia wanafunzi 7,067 mwaka 2019;
- (c) Kuongezeka kwa wanafunzi wanaodhaminiwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi kutoka 2,254 mwaka 2015/16 na kufikia wanafunzi 3,519 kwa mwaka 2018/19;
- (d) Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wa kike wanaojiunga na masomo ya elimu ya juu katika vyuo vikuu na fani mbalimbali ndani na nje

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA



ya Zanzibar kutoka wanafunzi 4,364 kwa mwaka 2015 hadi kufikia wanafunzi 8,571 mwaka 2019; na

- (e) Chuo Kikuu cha Taifa SUZA kimeimarisha mashirikiano na vyo 53 vya ndani na nje katika ufanyaji wa Tafiti, kubadilishana wataalam na fursa za masomo. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa ukumbi mkubwa wenye uwezo wa kuchukua watu 3,200 wa SUZA na kuanza kutumika. Aidha, chuo cha madaktari kimeanzishwa ambapo tayari kimetoa madaktari 58 pamoja na kuanzisha skuli ya madaktari wa meno SUZA.

***Elimu Mbadala na Elimu ya Watu Wazima***

- (a) Elimu Mbadala inatolewa katika madarasa 29 (19 Unguja na 10 Pemba) yaliyomo katika skuli za msingi. Jumla ya wanafunzi 791 wenye umri kati ya miaka 10 hadi 15 waliokuwa nje ya mfumo rasmi wa skuli wameandikishwa katika madarasa ya elimu mbadala;
- (b) Jumla ya wanafunzi 351 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 22 wameandikishwa katika Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo (Unguja) na Kituo cha Wingwi Mtemani (Pemba). Vijana hawa pamoja na masomo ya kawaida ya kuwajengea uwezo wa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu, pia wanasomea fani mbalimbali za mafunzo ya amali;
- (c) Madarasa mapya ya kisomo yamefunguliwa Unguja na Pemba na kufanya idadi ya madarasa kufikia 521 mwaka 2019 kutoka 440 mwaka 2015. Uandikishaji wa wanakisomo umeongezeka kutoka wanakisomo 8,884 mwaka 2015 na kufikia wanakisomo 8,899 mwaka 2019. Jumla ya wanakisomo 8,470 wamefanyiwa upimaji mkuu na wanakisomo 520 wamekombolewa. Vikundi 128 vyenye wanachama 2,863 vimeendelezwa kwa kupatiwa mafunzo ya uongozi, ujasiriamali na utunzaji wa fedha. Aidha, asilimia ya wanaojua kusoma, kuandika na kuhesabu imefikia 84.2.

***Elimu Mjumuisho***

- (a) Jumla ya walimu washauri nasaha 1,050 wa elimu ya msingi na sekondari wamepatiwa mafunzo ya usawa wa kijinsia katika elimu, walimu 4 wamepatiwa mafunzo ya kutengeneza mashine za kuandikia nukta nundu na walimu 40 wa elimu mjumuisho wamepatiwa mafunzo katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA);
- (b) Skuli nane zimepatiwa mafunzo ya kuwatambuwa watoto wenye matatizo ya usikivu, uoni na ulemavu kwa hatua ya awali. Vilevile, Kamusi ya Lugha ya Alama limechapishwa na jumla ya nakala 1,000 kusambazwa katika skuli; na
- (c) Walimu 77, wanafunzi viziwi 84 na marafiki wa wanafunzi viziwi 90 wamepatiwa mafunzo ya lugha ya alama.

**Michezo na Utamaduni Katika Skuli**

- (a) Kupitia Mpango Maalum wa Miaka Mitano wa Kuibua Na Kuendeleza Vipaji vya Michezo (2016 – 2020), wanafunzi wa skuli zote za Zanzibar wamepata fursa za kushiriki katika michezo kuanzia ngazi ya skuli, Wilaya, Mkoa hadi Taifa kwa kupitia maadhimisho ya Tamasha la Elimu Bila Malipo;
- (b) Jumla ya wanafuzi 1,210 na timu za michezo ya mpira wa miguu, mikono, wavu, kikapu, pete, meza, na riadha wameshiriki katika mashindano ya michezo na sanaa ya UMISSETA, Aidha, jumla ya wanafunzi 182 wameshiriki katika mashindano ya michezo kwa skuli za sekondari Afrika Mashariki - FEASSSA;
- (c) Kuandaa mpango maalum wa miaka miwili (2017 - 2019) - (SPORT 55) kwa lengo la kutatua changamoto zinazokabili maendeleo ya michezo katika skuli. Kupitia mpango huu zaidi ya skuli 110 zimewezeshwa kwa kupatiwa vifaa vya michezo mitano na walimu 475 wa michezo wamepatiwa mafunzo;
- (d) Kurudisha hamasa na vuguvugu la Tamasha la Elimu Bila Malipo kupitia michezo katika mfumo wa kubadilishana baina ya Unguja na Pemba. Wastani wa wanafunzi 12,800 wameshiriki maadhimisho hayo katika ngazi ya Taifa, kwa lengo la kuwashajiisha wanafunzi kujua historia ya nchi yao na kufahamu faida za Mapinduzi Matukufu ya Mwaka 1964;
- (e) Kuimarisha michezo katika elimu ya juu kupitia mashindano ya vyuo vikuu yanayoratibiwa na shirikisho la vyuo vikuu Zanzibar (ZAHILFE); na
- (f) Kujengwa kumbi maalum za michezo ya ndani katika skuli tisa mpya za ghorofa zilizojengwa katika kila wilaya.

**Huduma za Maktaba**

- (a) Kukamilisha ujenzi wa Maktaba Kuu Pemba na kufanya ukarabati wa Maktaba Kuu Unguja na Maktaba ya Wete Pemba. Mafunzo ya kuanzisha maktaba za sanduku katika skuli kumi za msingi za Wilaya ya Kati yametolewa. Jumla ya vitabu 8,325 na masanduku 25, mabusati 40 na madaftari ya kuwekea kumbukumbu na kompyuta 16 zimenunuliwa. Programu 1,632 za kusoma kwa watoto zimefanyika. Jumla ya wanajamii 1,650 wameshiriki katika matamasha ya usomaji wa vitabu;
- (b) Jumla ya walimu 596, wasimamizi na wasaidizi wasimamizi wa maktaba 364, walimu 20, walimu wakuu 210 na maafisa elimu wilaya 02 wamepatiwa mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa maktaba za skuli. Vitabu 48,636 vya masomo mbalimbali vimegaiwa maktaba



kuu za Unguja na Pemba, Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo na vituo vya walimu;

- (c) Jumla ya vitabu 68,168 vya fani mbalimbali vimegawiwa katika skuli za msingi, sekondari, vyuo vikuu na vyuo vya walimu na vitabu 119,808 vya wanafunzi, viongozi vya walimu 2,752 vya darasa la kwanza hadi la nne vya somo la Kiingereza na jumla ya vitabu 14,560 kwa ajili ya mafunzo ya Elimu Masafa vimechapishwa. Jumla ya vitini 600 vya masomo ya Jiografia na TEHEMA vimechapishwa kwa ajili ya walimu wa madarasa ya tano na sita. Vitini vya masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza kwa madarasa ya tano na sita na sekondari ya awali vimeandaliwa. Moduli 3,012 za masomo ya Hisabati, Jiografia na TEHEMA zimechapishwa na kusambazwa; na
- (d) Kuongezeka kwa watumiaji wa maktaba kufikia 48,043 mwaka 2019 kutoka watumiaji 31,441 mwaka 2015.

#### ***Ukaguzi wa Elimu***

- (a) Kuanzisha mfumo mpya wa ukaguzi ambao umeongeza idadi ya skuli zinazokaguliwa kutoka skuli 376 mwaka 2015 kufikia 730 mwaka 2019; na
- (b) Asilimia 81 ya skuli za sekondari zilikaguliwa katika mwaka 2019 kati ya hizo asilimia 45 zimekaguliwa zaidi ya mara moja.

**182. CCM inatambua umuhimu wa sekta ya elimu katika maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla, hivyo itaendelea kusimamia Sera ya ASP iliyoasisiwa na Sheikh Abeid Amani Karume ya kutoa elimu bure. Mkazo utawekwa katika kuongeza udahili wa wanafunzi katika ngazi zote, kuimarisha mafunzo ya amali kwa mujibu mahitaji ya soko la ajira na kupandisha kiwango cha kufaulu katika ngazi zote. Aidha, CCM itaendelea kutanua na kuimarisha ubora wa elimu hususan ya sayansi, hisabati, teknolojia, ufundi na mafunzo ya amali kwa kushirikiana na sekta binafsi na asasi za kiraia. Ili kutimiza malengo haya, CCM itaelekeza SMZ kuchukua hatua zifuatazo:-**

#### ***Elimu ya Maandalizi***

- (a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Makuzi na Malezi kwa Mtoto kwa kuongeza kiwango cha uandikishaji kutoka asilimia 81.4 Mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 100 mwaka 2025;
- (b) Kuhamasisha wananchi na washirika wa maendeleo ya elimu wa ndani na nje katika kujenga skuli za maandalizi 25 (skuli 5 katika kila mkoa) zenye madarasa 250 hususan katika maeneo ya vijijini;
- (c) Kuimarisha mazingira rafiki ya kujifunza katika skuli za maandalizi kwa kutekeleza programu ya lishe kwa wanafunzi wote wa skuli za maandalizi za Serikali; na
- (d) Kupitia na kuimarisha mtaala wa elimu ya maandalizi na kutoa vifaa na nyenzo za kufundishia ili viendane na mahitaji ya Taifa.





***Elimu ya Msingi***

- (a) Kuongeza kiwango halisi cha uandikishaji wanafunzi kutoka asilimia 83.9 mwaka 2019 hadi kufikia asilimia 100 mwaka 2025;
- (b) Kujenga skuli 10 za msingi (Unguja 6 na Pemba 4) katika maeneo yenye upungufu na msongamano mkubwa wa wanafunzi;
- (c) Kuimarisha programu ya lishe katika skuli za msingi zilizo katika mazingira magumu kutoka skuli 27 mwaka 2019 hadi skuli 50 mwaka 2025;
- (d) Kukamilisha ujenzi wa madarasa 1000 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi;
- (e) Kuimarisha ubora wa elimu kwa kuifanyia mageuzi mitaala ya elimu ya msingi na kuitekeleza; na
- (f) Kuhakikisha wanafunzi wote wa ngazi ya elimu ya msingi wanapatiwa madawati.

***Elimu ya Sekondari***

- (a) Kuongeza kiwango halisi cha uandikishaji kutoka asilimia 51.1 mwaka 2019 hadi asilimia 90 mwaka 2025;
- (b) Kusambaza vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa skuli zote za sekondari;
- (c) Kujenga skuli tatu za sekondari za kisasa zenye dakhalia katika mikoa ya Kaskazini Unguja, Mjini Magharibi na Kaskazini Pemba;
- (d) Kujenga dakhalia katika skuli mbili za Paje Mtule na Chwaka Tumbe;
- (e) Kujenga skuli mbili za sekondari za ufundi;
- (f) Kujenga maabara na maktaba katika skuli 20 za sekondari kwa lengo la kuimarisha elimu ya sayansi kwa wanafunzi wa sekondari Unguja na Pemba;
- (g) Kukamilisha ujenzi wa madarasa 500 ya sekondari yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi;
- (h) Kushajiisha ushiriki wa sekta sekta binafsi katika kutoa huduma bora za elimu kwenye ngazi zote; na
- (i) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kujifunza na kusomeshea.

***Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Amali***

- (a) Kujenga Ofisi ya Makao Makuu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, Ofisi ya Taasisi ya Elimu, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Bodi ya Mikopo na Baraza la Mitihani;



- (b) Kuviimarisha vituo vya mafunzo ya amali kwa kuvipatia vifaa vya kisasa ili viweze kutoa mafunzo kwa njia ya vitendo na nadharia;
- (c) Kuwapatia mikopo nafuu wanafunzi wanaomaliza mafunzo yao kwa kuanzisha vikundi vya ushirika kwa lengo la kujijiri wenyewe;
- (d) Kuimarisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia kwa kuipatia vifaa vya kisasa ili iweze kutoa mafunzo kwa ufanisi zaidi na kuanzisha mafunzo ya Shahada ya kwanza ya uhandisi katika fani za matengenezo ya ndege, Shahada ya ujenzi na usafirishaji pamoja na Shahada ya umeme;
- (e) Kujenga vituo vya amali na kuhakikisha kila wilaya ina kituo kikubwa cha mafunzo ya amali;
- (f) Kupitia upya mfumo wa elimu ya ufundi amali ili uweze kusajili vijana wengi zaidi na kuzalisha wataalam mahiri wa ngazi ya msingi na ya kati wenye ujuzi katika fani zao na uwezo wa kujijiri na kuajirika mahali popote duniani; na
- (g) Kuimarisha programu za mafunzo ya amali zinazoendana na mahitaji ya soko la ajira ili kupunguza tatizo la ajira na umasikini kwa ujumla.

#### ***Mafunzo ya Ualimu***

- (a) Kuongeza uandikishaji wa mafunzo ya ualimu katika vyuo vya ualimu na vyuo vikuu katika ngazi ya Stashahada na Shahada kutoka wahitimu 2,419 mwaka 2019 na kufikia 3,500 mwaka 2025;
- (b) Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya ualimu kazini kwa kuvipatia Vituo vya Walimu (TCs) vifaa vya kujifunzia, kufundishia na TEHAMA; na
- (c) Kuinua ubora wa elimu kwa kuwapatia walimu mafunzo ya mbinu za kufundishia hasa katika masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza.

#### ***Elimu ya Juu***

- (a) Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa kujenga awamu ya pili ya chuo hicho na kuanzisha programu mbalimbali za kuwawezesha wahitimu kuweza kujitegemea na zitakazolenga mahitaji ya Taifa;
- (b) Kuongeza nafasi za masomo katika elimu ya juu na kuimarisha Mfuko wa Bodi ya Mikopo ili kuongeza idadi ya wanafunzi watakaonufaika kutoka 4,045 mwaka 2019 hadi kufikia 7000 mwaka 2025;
- (c) Kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike wanaojiunga na elimu ya juu hususan katika fani za sayansi, ufundi, udaktari na teknolojia;
- (d) Kuanzisha chuo cha mafunzo ya Ubaharia;na



- (e) Kuimarisha skuli ya madaktari wa meno chini ya SUZA.

***Elimu Mbadala na Elimu ya Watu Wazima***

- (a) Kuendeleza jitihada za kuhamasisha vijana waliokosa fursa ya elimu rasmi na waliotoroka skuli kujiunga na madarasa ya elimu mbadala na kurejea katika mfumo wa elimu rasmi;
- (b) Kuimarisha utoaji wa elimu endelevu kwa watu wazima kupitia madarasa ya kisomo na kuongeza uandikishaji wa wanakisomo kutoka 8,896 mwaka 2019 na kufikia 10,000 mwaka 2025; na
- (c) Kuongeza asilimia ya wanaojua kusoma, kuandika na kuhesabu kutoka asilimia 84.2 mwaka 2019 na kufikia asilimia 95 mwaka 2025.

***Elimu Mjumuisho***

- (a) Kuimarisha miundombinu na mazingira ya skuli ili kukidhi mahitaji ya utoaji wa elimu mjumuisho na stadi za maisha pamoja na kuwapatia vifaa vya kujifunzia na kufundishia wanafunzi wenye mahitaji maalum; na
- (b) Kuimarisha uwezo wa walimu wa elimu mjumuisho kwa kuwapatia mafunzo kazini.

***Michezo na Utamaduni Katika Skuli***

Kufufua na kuendeleza michezo na utamaduni kwa wanafunzi wa skuli za msingi, sekondari na vyuo na kuzipatia skuli vifaa vya michezo.

***Huduma za Maktaba***

- (a) Kuimarisha huduma za maktaba kwa kujenga maktaba kuu ya kisasa;
- (b) Kujenga utamaduni wa kujisomea kwa kuhamasisha wananchi kuhusu matumizi ya maktaba na kujenga maktaba tatu za wilaya Unguja na Pemba; na
- (c) Kuendeleza mafunzo ya Ukutubi na kuongeza idadi ya vitabu katika maktaba zote zikiwemo za skuli za msingi na sekondari.

***Ukaguzi wa Elimu***

- (a) Kujenga ofisi tatu za ukaguzi katika mikoa ya Kaskazini Unguja, Kusini Unguja na Kusini Pemba;
- (b) Kuimarisha ukaguzi wa elimu kwa kuzikagua skuli zote zilizosajiliwa;
- (c) Kuimarisha utendaji wa skuli na walimu kwa ujumla hadi kufikia asilimia 75 kwa kutumia viwango vya ukaguzi vilivyopo; na
- (d) Kukagua skuli zote za sekondari mara mbili kwa mwaka.



### **Sekta ya Afya**

183. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), SMZ imeendeleza juhudi za kuwapatia wananchi huduma bora za afya na kupata mafanikio yafuatayo:-
- (a) Kuendeleza Misingi iliyoasisiwa na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kwa kutoa huduma za afya bure kwa wananchi wote;
  - (b) Kuunda kamati 98 za afya vijijini na kuhamasisha akina mama wajawazito kutumia huduma za afya ya uzazi na kujifungulia katika vituo vya afya; jamii kupeleka watoto chini ya miaka mitano kupatiwa chanjo dhidi ya maradhi; ugawaji wa vyandarua na kupuliza dawa majumbani kudhibiti mbu wanaoeneza malaria na kutoa elimu ya lishe na usafi wa mazingira;
  - (c) Kuendelea na ukaguzi wa hospitali binafsi na kuziruhusu hospitali 8 kati ya hizo kupatiwa dawa kwa ajili ya kutoa huduma za chanjo na huduma za UKIMWI kwa jamii bila malipo;
  - (d) Kuimarisha huduma za uchunguzi katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja ikiwemo kupandisha hadhi (*certificate of accreditation med 015*) maabara kuu ya hospitali hiyo katika kiwango cha kimataifa;
  - (e) Kuanzisha kituo cha mawasiliano cha matibabu masafa (*telemedicine*) katika hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuwezesha matibabu ya masafa ndani na nje ya nchi. Aidha, mfumo wa huduma ya matibabu kwa njia ya mtandao (*e-health*) umeanza;
  - (f) Kuendeleza huduma za matibabu ya saratani kupitia madaktari bingwa wanne ambapo wagonjwa 924 wametibiwa hadi mwaka 2019;
  - (g) Kufunga mashine sita za kusafishia figo (*haemodialysis*) ambapo wagonjwa 39 kwa siku hupatiwa huduma hiyo na hivyo kuokoa zaidi ya shilingi milioni 800.0 kwa mwaka;
  - (h) Kununua na kufunga mashine ya DNA na kuandaa kanuni za huduma zake;
  - (i) Kuongeza idadi ya wataalam wazalendo ikiwemo:
    - (i) Madaktari bingwa kutoka 28 mwaka 2015 hadi 33 mwaka 2019;
    - (ii) Kuendelea kusomesha madaktari bingwa 40 katika fani mbalimbali ikiwemo wataalam wa maradhi ya saratani, maradhi ya figo, mkojo, usingizi, ngozi, maradhi ya wanawake, watoto, wataalam wa mionzi na maradhi ya akili; na



- (iii) Kuongeza idadi ya wauguzi kutoka 1,199 mwaka 2015 hadi 1,347 mwaka 2020, wafamasia kutoka 158 mwaka 2015 hadi 315 mwaka 2020 na wataalam wa usingizi (*anaesthesiology*) kutoka mmoja (1) mwaka 2015 hadi 29 mwaka 2020;
- (j) Kuimarisha uwiano kati ya daktari na wagonjwa kutoka daktari mmoja kwa wagonjwa 9,708 mwaka 2015 hadi 6,276 mwaka 2020;
- (k) Kuimarisha miundombinu ya sekta ya afya kwa:
  - (i) Kukamilisha ujenzi wa wodi mpya za wazazi na watoto. Aidha, sehemu ya kuchomea taka (incenerator) na uzio katika Hospitali ya Mnazi Mmoja zimejengwa;
  - (ii) Kujenga upya Hospitali ya Abdalla Mzee - Pemba sambamba na uwekaji wa vifaa vya kisasa vya tiba na uchunguzi wa maradhi;
  - (iii) Kuanza ujenzi wa wodi ya wazazi, wanawake na watoto katika Hospitali ya Chakechake; na
  - (iv) Kuimarisha Hospitali za Wilaya za Makunduchi, Kivunge na Micheweni kwa ukarabati wa wodi, maabara pamoja na huduma za upasuaji.
- (l) Kukamilisha ujenzi wa vituo 17 vya afya katika vijiji mbalimbali Unguja na Pemba;
- (m) Kuanza matayarisho ya ujenzi wa hospitali ya Binguni kwa kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa michoro ya majengo;
- (n) Kufanya utafiti wa makundi maalum na kubaini kupungua maambukizi ya UKIMWI ambapo maambukizi kwa wanaotumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga sindano yameshuka kutoka asilimia 11 mwaka 2015 hadi asilimia 5.0 mwaka 2018/19;
- (o) Kutoa elimu ya afya kupitia vyombo vya habari na majarida kwa lengo la kujikinga na maradhi mbali mbali sambamba na kutayarisha mwongozo mpya wa kutibu maradhi ya kisukari na shinikizo la damu;
- (p) Kupandisha hadhi Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa – Zanzibar na kutoa wahitimu 771 hadi kufikia mwaka 2019;
- (q) Kusajili dawa za tiba asili na waganga (waganga 429, wasaidizi waganga 175) waliotimiza masharti kupitia Baraza la Tiba Asili. Maduka 113 na Kliniki 35 za dawa asili zimesajiliwa;
- (r) Kutekeleza mpango shirikishi wa kitaasisi uliohusisha kuelimisha jamii kuhusu lishe bora na kupelekea kushuka kwa hali ya utapiamlo



uliokithiri kwa watoto hadi kufikia asilimia 7 na hivyo kuvuka lengo lililowekwa la asilimia 12. Matone ya vitamin "A" yametolewa kwa watoto 231,939 wenye umri wa miezi 6 hadi 59 sambamba na utoaji dawa za minyoo;

- (s) Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Masuala ya Afya na kutoa mafunzo mbalimbali kwa wataalamu. Miongoni mwa tafiti zilizofanyika ni:-
- (i) *Annual Parasitological Survey* ulioangalia kiwango na mwenendo wa maradhi ya kichocho katika jamii;
  - (ii) Tafiti za kuangalia uelewa, tabia pamoja na mienendo ya jamii juu ya maradhi ya malaria na kifua kikuu katika jamii ya watu wa Zanzibar; na
  - (iii) Utafiti wa kuangalia maradhi ya moyo '*rheumatic heart disease*' kwa watoto wa skuli kwa upande wa ngazi ya msingi (darasa la kwanza hadi la darasa la sita).
- (t) Kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa walioathirika na dawa ya kulevya kupitia kituo maalum kilichoanzishwa ambapo jumla ya waathirika 670 (wanawake 51 na wanaume 619) wamehudumiwa;
- (u) Kuongeza bajeti ya ununuzi wa dawa, vitendanishi, vifaa vya tiba na vya uchunguzi kutoka shilingi bilioni 7.0 mwaka 2017/2018 hadi kufikia bilioni 15.2 mwaka 2019/2020 na kununua malori matatu kwa ajili ya kuimarisha Bohari ya Dawa (CMS); na
- (v) Kuimarisha takwimu za afya kwa kukusanya na kuhakiki taarifa kutoka vituo 50 kati ya 77 vilivyoanzishwa sambamba na kutumia mfumo wa *Electronic Medical Record*.

**184. Maendeleo ya kiuchumi nchini yatategemea sana kuwepo kwa jamii yenye nguvu na siha. Hivyo, kuimarika kwa huduma za afya kwa wote ni jambo la msingi na lazima kwa maendeleo ya Taifa. Katika utekelezaji wa Ilani hii, CCM itaelekeza SMZ kuendelea kutoa huduma za matibabu yaliyo bora na ya bure kwa wananchi wote kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-**

- (a) Kuendeleza sera za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar za kutoa huduma za afya bure kwa wananchi wote;
- (b) Kuimarisha afya ya msingi ili kutoa huduma bora kwa wote (*Universal Health Coverage – UHC*), kuimarisha vituo vya afya ya msingi 34 (PHCU+) ili viweze kutoa huduma za uzazi kwa masaa 24;
- (c) Kuanzisha Taasisi ya Matibabu ya Huduma za Mifupa na huduma za matibabu ya moyo na kuimarisha huduma za uchunguzi na utibabu wa maradhi ya saratani ya shingo ya kizazi, matiti na aina nyengine;





- (d) Kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Hospitali ya Binguni, kujenga upya Hospitali ya Wete na kuimarisha Hospitali ya Kivunge ili ziweze kutoa huduma katika ngazi ya mkoa, kukamilisha ujenzi wa nyumba za madaktari katika Hospitali ya Abdalla Mzee Pemba pamoja na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi Hospitali ya Kivunge;
- (e) Kujenga maabara ya kitaifa ya maradhi ya mripuko na kuwajengea uwezo wataalam wa maabara;
- (f) Kuimarisha hospitali za vitongoji na Micheweni Pemba kufikia ngazi ya hospitali za wilaya sambamba na kuimarisha huduma katika hospitali ya wilaya Makunduchi;
- (g) Kudhibiti maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI ikwemo maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto, Kifua Kikuu, Ukoma na Homa ya Ini na kuongeza kasi ya uibuaji huduma stahiki za tiba;
- (h) Kuendelea kutekeleza mpango shirikishi wa kutokomeza maradhi ya Kipindupindu Zanzibar. Aidha, juhudi za kutokomeza ugonjwa wa Malaria kwa wilaya zote za Pemba na wilaya za Kaskazini "A" na Kusini Unguja pamoja na kudhibiti uingiaji wa vimelea ya malaria;
- (i) Kuanzisha sehemu maalum ya kuhudumia wagonjwa wa maradhi ya mlipuko na waliopata maafa Unguja na Pemba, pamoja na kuimarisha uwezo na utayari wa kupambana na maradhi ya mlipuko na majanga ya kiafya;
- (j) Kutoa elimu ya afya ili kupelekea mabadiliko ya tabia miongoni mwa jamii yatakayowezesha kujikinga na maradhi yasiyo ya kuambukiza ikiwemo shinikizo la damu na kisukari pamoja na kudhibiti matumizi ya tumbaku;
- (k) Kufundisha madaktari bingwa na wauguzi bingwa ndani na nje ya nchi na kuongeza idadi ya madaktari na wauguzi ili kufikia uwiano wa daktari mmoja kuhudumia wagonjwa 3,612;
- (l) Kusimamia utoaji wa tiba asili na tiba mbadala na kuendelea kuimarisha udhibiti wa ubora na usalama wa chakula, dawa na vipodozi pamoja na kuendelea kushikilia ithibati na hati ya viwango vya ubora kimataifa;
- (m) Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa vya utibabu na uchunguzi kwa asilimia 95 au zaidi;
- (n) Kuweka mfumo endelevu wa kugharamia huduma za afya utakaowezesha wananchi kupata huduma za afya bila malipo;
- (o) Kuimarisha miundombinu na kuweka nyenzo za maabara za Taasisi ya Utafiti wa Afya ili kufanya tafiti mbalimbali za afya kwa kuzingatia agenda za utafiti za kitaifa na kisekta;



- (p) Kuendeleza utekelezaji wa mfumo wa utoaji wa huduma kwa kuzingatia kitita cha huduma za afya (*essential health care package*) kwa kuendeleza juhudi za Serikali katika kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto;
- (q) Kuongeza kiwango cha chanjo kwa watoto walio chini ya miaka mitano kufikia asilimia 100 na kuongeza kiwango cha chanjo ya kukinga saratani ya shingo ya kizazi kwa watoto wa umri wa miaka 9 – 14 kufikia asilimia 100 pamoja na kuimarisha huduma za kinga ya afya katika maeneo ya waingiaji wageni (bandarini na viwanja vya ndege); na
- (r) Kubuni na kutekeleza mkakati wa afya ya jamii ikiwemo kuendeleza kampeni ya kuondoa utapiamlo mkali na kutoa matone ya vitamin “A” kwa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano.

### Sekta ya Maji

185.

Huduma ya maji ni muhimu kwa maendeleo ya wanadamu kiuchumi na kijamii, maji ni rasilimali inayohitaji kulindwa, kuhifadhiwa na kuendelezwa kwa kuzingatia mahitaji na mwelekeo wa maisha ya viumbe wote wakiwemo wanadamu. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita sekta maji imepiga hatua kubwa ya mafanikio kama ifuatavyo:-

- (a) Kuchimba visima 150 Unguja na Pemba ili viweze kutoa huduma kwa wananchi ambapo visima 57 (Unguja 29 na Pemba 28) vimeunganishwa mfumo mkuu wa usambazaji maji na vinatoa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi;
- (b) Kukamilisha ulazaji wa mabomba yenye urefu ya kilomita 161.037 Unguja na Pemba;
- (c) Kuvifanyia matengenezo visima vikongwe 23 na vinaendelea kutoa huduma kwa jamii;
- (d) Kukamilisha kazi za uchimbaji wa visima 6 vya uzalishaji maji, kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji katika eneo la Mjini Magharibi;
- (e) Kujenga matangi mawili ya juu yenye ujazo wa lita 3,000,000, ambapo tangi moja lenye ujazo wa lita 2,000,000 limejengwa katika eneo la Saateni na moja lenye ujazo wa lita 1,000,000 limejengwa katika eneo la Mnara wa Mbao, matangi hayo yanaendelea kutoa huduma kwa wananchi;
- (f) Kukamilisha kazi ya ulazaji wa mabomba makubwa na madogo yenye urefu wa kilomita 68 kwa ajili ya uimarishaji wa huduma ya maji Mjini Magharibi kutoka visimani hadi matangini na kutoka matangini hadi kwa watumiaji;



- (g) Kukamilika kwa ujenzi wa vyoo, usafi wa mazingira na ukarabati uliohusisha skuli 24 za Mkoa wa Mjini Magharibi za msingi na sekondari;
- (h) Kukamilisha ujenzi wa uzio katika maeneo ya vyanzo vya maji Chaani, Donge, FFU Machui, Kianga, Mwembe-Mchomeke, Mtende, Melinne-Magirisi na Bumbwini -Misufini) kwa Unguja na Kengeja, Wingwi Mjananza, Ngwachani na Matuleni kwa upande wa Pemba;
- (i) Kuimarisha ukuzaji wa mapato na kupunguza upotevu wa maji ambapo jumla ya mita 2,980 zimefungwa kwa watumiaji wa maji katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba.

186. **CCM inatambua kuwa majisafi na salama ni huduma ya msingi ya kila mkaazi wa Zanzibar. Katika miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kuendelea kutimiza azma ya ASP na CCM ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi wote, mijini na vijijini kwa kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuendeleza juhudi za upatikanaji wa majisafi na salama katika shehia zote za Unguja na Pemba ikiwemo visiwa vidogo vidogo;
- (b) Kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na kuimarisha usalama wa fedha kwa kufunga mita kwa watumiaji wa maji pamoja na kutumia huduma za kielektroniki katika kulipia huduma hizo;
- (c) Kutoa elimu ya kuwashajiisha wananchi namna bora ya utumiaji na uchangiaji wa huduma ya maji ili kuiwezesha huduma hiyo kuwa imara zaidi na endelevu;
- (d) Kuyalinda, kuyatambua na kuyapima maeneo ya vyanzo vya maji ili kuhakikisha maeneo hayo hayavamiwi na kuharibiwa;
- (e) Kufanya utafiti juu ya hali halisi ya rasilimali maji iliyopo ardhini, matumizi ya sasa na baadae;
- (f) Kutafuta namna bora za kupunguza kiwango cha maji ya mvua kupotelea baharini badala ya kubakia ardhini na kusaidia urutubishaji wa ardhi na kupata kiwango kikubwa cha rasilimali maji ya ardhi;
- (g) Kuandaa na kutekeleza mkakati wa uvunaji wa maji ya mvua (*water harvest*) katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba;
- (h) Kuendeleza zoezi la utafiti wa kutumia umeme mbadala katika visima vya maji ili kupata namna bora ya kupunguza gharama za matumizi ya umeme katika huduma za majisafi na salama; na



- (i) Kujenga jengo la kisasa ili kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi kwa lengo la kuleta ufanisi wa kiutendaji kwa watendaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar.

### **MAENEO MENGINE YA KIPAUMBELE** **Sekta ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

187. Katika miaka mitano iliyopita mafanikio makubwa yalipatikana katika sekta ya utamaduni, sanaa na michezo kama ifuatavyo:-

#### ***Utamaduni***

- (a) Kuandaa na kurusha hewani vipindi 178 kupitia televisheni na redio kwa lengo la kutoa taaluma juu ya matumizi sahihi na fasaha ya lugha ya Kiswahili. Makongamano mawili ya kimataifa yalifanyika kwa lengo kukiendeleza Kiswahili. Aidha, machapisho mawili (Jahazi Toleo la kwanza na Toleo la Pili) yamechapishwa na nakala zake zimesambazwa;
- (b) Kukamilisha mchakato wa maandalizi ya sera ya lugha ya Kiswahili ili kudhibiti matumizi mabaya ya lugha. Kamusi la viumbe vya baharini limehaririwa kwa kunyoosha, kuweka sawa na kuviwekea fasili vidahizo ambavyo vilikuwa havina fasili pamoja na kuhakiki visawe vilivyomo;
- (c) Miswada mitano ya vitabu ikiwemo mswada wa kamusi la Kiingereza na Kiswahili, kitabu cha mawasiliano ya msingi ya kiswahili kwa wageni (Kiswahili na Kifaransa), kitabu cha utamaduni wa Mzanzibari kwa lugha ya Kiingereza, kitabu cha hadithi fupi na mswada wa jarida namba nne la Jahazi imetayarishwa;
- (d) Kufanya matamasha matano ya Utamaduni wa Mzanzibari kwa kushirikisha vikundi vya ngoma za kiasili, vikundi vya wajasiriamali wa kazi na bidhaa za kiutamaduni, vyakula vya kiasili, taraabu asilia, Maulidi ya homu, usiku wa sanaa, michezo na nyimbo za watoto, mchezo wa ng'ombe pamoja na muziki wa kizazi kipya. Aidha, makongamano kuhusu nafasi na fursa za kiutamaduni kwa vijana yalifanyika;
- (e) Kuratibu na kushiriki katika maandalizi ya matamasha 29 ya utamaduni yakiwemo Tamasha la vyakula vya asili ya Kimakunduchi, Tamasha la Utamaduni la Rafiki network, Tamasha la Elimu bila ya malipo, Tamasha la Nchi za Jahazi (ZIFF), Tamasha la Watu wa Mangapwani, Tamasha la Muziki wa JAZZ, Tamasha la Sauti za Busara, Tamasha la Mwakakogwa na Tamasha la Urithi wa Mtanzania; na
- (f) Kuwapatia mafunzo ya utamaduni na filamu kwa walimu 543, maofisa utamaduni wa wilaya 11 na wanafunzi wa skuli za msingi 87 na wasanii 752 wa filamu na maigizo na wasanii 33 wa fani ya uchoraji, ushonaji, uchapishaji, na urithi juu ya tamaduni zetu.



### **Sanaa**

- (a) Kuzipatia mafunzo jumuiya nne za sanaa;
- (b) Kuwapatia mafunzo wasanii 752 wa filamu na maigizo ya fani za filamu, muziki;
- (c) Kuwajengea uwezo wazalishaji na waongoza filamu kwa kuwapatia mafunzo katika fani za ubunifu, uandaaji na uzalishaji wa filamu fupi fupi, uongozaji na uigizaji wa filamu;
- (d) Kufanya utambuzi wa sheria na haki za wasanii kwa kuweka mikataba na kusajili kazi zao; na
- (e) Kuendelea kuzilinda kazi za ubunifu wa wasanii.

### **Michezo**

- (a) Kufanya matengenezo makubwa kiwanja cha michezo cha Mao-Zedong kwa kujenga viwanja viwili vya mpira sambamba na uwekaji wa nyasi bandia, ujenzi wa kiwanja mchanganyiko na kiwanja cha michezo ya ndani (*indoors game*) na kiwanja cha mazoezi ya viungo. Vilevile, viwanja vya michezo cha Amaani na Gombani Pemba vimefanyiwa matengenezo;
- (b) Kujenga viwanja vitatu vya michezo vya wilaya ambavyo ni Kiwanja cha Kitogani Wilaya ya Kusini – Unguja, Kiwanja cha Kishindeni Wilaya ya Micheweni na Kangani Wilaya ya Mkoani – Pemba na kuendelea na taratibu za ujenzi wa viwanja viwili vilivyopo katika kijiji cha Mkokotoni Wilaya ya Kaskazini “A” na Kama Wilaya ya Magharibi “A”. Ujenzi huo umesaidia kupunguza uhaba wa viwanja;
- (c) Kuhamasisha jamii kushiriki katika michezo kwa lengo la kuimarisha afya ambapo vikundi vya mazoezi vimeongezeka kutoka 36 mwaka 2015 hadi kufikia vikundi 81 mwaka 2020 pamoja na kuandaa Tamasha la Kitaifa la Mazoezi ya Viungo ambalo hufanyika kila mwaka ifikapo tarehe 1 Januari;
- (d) Kuendeleza, kukuza na kuimarisha michezo ya asili kwa ajili ya kuhifadhi utamaduni wa Zanzibar;
- (e) Kukiimarisha Kituo cha Michezo cha Dole (*Dole Academy*) ili kuendeleza michezo ya aina mbalimbali kwa vijana pamoja na kufanya tathmini ya kukiendeleza kituo hicho kwa lengo la kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya wanamichezo nchini kwa kushirikiana na taasisi za michezo za kitaifa na kimataifa;
- (f) Kuandaa sera ya michezo ambayo imeweka msingi wa kuendeleza michezo kwa ajili ya kukuza uchumi, kujenga afya na burudani;



- (g) Kuziwezesha timu za michezo kushiriki mashindano 76 ya kimataifa ili kuonyesha vipaji vyao kimataifa na hatimae kupata nafasi za kujiunga na timu za nje;
- (h) Kuziwezesha timu za Zanzibar (Timu ya Taifa ya Zanzibar Heroes, Timu ya soka la ufukweni, Timu ya soka ya Wanawake, Timu ya Taifa ya Riadha) kushiriki mashindano ya kimataifa ikiwemo mashindano ya CECAFA, klabu Bingwa Barani Afrika na Mashindano ya “Copa beach Soccer”, Mashindano ya Jumuiya ya Madola, mashindano ya “All Africa Games” na Mashindano ya Kimataifa ya Kilimanjaro Marathon;
- (i) Kushiriki katika mashindano ya Afrika Mashariki kwa timu ya mpira wa pete na watu wenye ulemavu kushiriki Mashindano ya Kimatifa ya michezo ya watu wenye ulemavu wa akili Abu-Dhabi, UAE;
- (j) Kutoa vifaa vya michezo kwa vyama saba, Chama cha Mchezo wa Riadha, Chama cha Mchezo wa Mpira wa Wavu, Chama cha Mpira wa Miguu, Chama cha Mpira wa Kikapu, Chama cha Viziwi, Chama cha Karata na Chama cha Bao. Vilevile, imewapatia mafunzo makocha na waamuzi 102 Unguja na Pemba, ambapo 56 wanatoka Unguja na 46 Pemba. Vilevile, kuwapatia mafunzo makocha 22 juu ya michezo ya watu wenye ulemavu; na
- (k) Kuongeza usajili wa vyama na vilabu vya michezo ambapo hadi kufikia mwaka 2019 jumla ya vyama vya michezo 38 na vilabu 1,873 vimesajiliwa kwa Unguja na Pemba. Aidha, uhamasishaji wa uanzishaji wa matamasha na michezo mbalimbali nchini ikiwemo michezo maarufu wa Yamleyamle Cup ambayo hushirikisha timu kutoka wilayani, Mapinduzi Toto Cup ambayo husaidia kuibua vipaji vya vijana kuanzia ngazi ya shehia, wilaya hadi mkoa.

188. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, shughuli za utamaduni, sanaa, michezo na ubunifu zitaimarishwa ili kuendelea kuburudisha, kujenga afya na kuifanya Zanzibar kuwa kituo cha mfano katika ukanda wa Afrika Mashariki kwa kuimarisha miundombinu na vituo vya taaluma za utamaduni, sanaa na michezo, na kukuza vipaji vya wasanii ili kuchukua nafasi maalum katika kujenga uchumi na kuzalisha ajira hasa kwa vijana. Katika kufikia dhamira hii, CCM itaelekeza SMZ kuendelea kutoa kipaumbele kwa kufanya yafuatayo:-**

#### ***Utamaduni***

- (a) Kuanzisha kituo cha utamaduni cha kitaifa kitakachotumika katika kutunza, kuenzi, kukuza na kuendesha shughuli za kiutamaduni;
- (b) Kuendeleza, kukuza na kueneza Kiswahili na kuwa bidhaa katika matumizi ya shughuli za taaluma zikiwemo za uandishi, uchapishaji, ukalimani na kuwa moja ya lugha iliyo rasmi inayozungumzwa na kutambulika katika mashirika na mikutano ya kikanda na kimataifa;





- (c) Kuhamasisha sekta binafsi kutambua na kulinda mila na utamaduni;
- (d) Kuanzisha maktaba ya vitabu vya lugha ya Kiswahili Zanzibar;
- (e) Kuandaa sera ya lugha ya Kiswahili itakayotoa vipaumbele vya lugha ili kuwa bidhaa na kuwa chanzo cha ajira;
- (f) Kujenga uwezo wa wataalam wa ndani wa kutafsiri lugha mbalimbali za kigeni pamoja na kuongeza wataalam wa Kiswahili katika ngazi ya uzamivu;
- (g) Kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa matumizi ya mavazi, vifaa, vyakula na vitu vya kiasili ili kulinda, kuendeleza na kurithisha amali za kitamaduni kwa manufaa ya kizazi kilichopo na kijacho;
- (h) Kuandaa utaratibu wa kuzitambua, kuziendeleza na kuzisajili kazi za kiutamaduni zitakazozalishwa nchini na kuziongeza thamani pamoja na kulinda hakimiliki za ubunifu kisheria; na
- (i) Kuboresha utekelezaji wa mipango ya maandalizi na ushiriki wa wananchi katika sherehe za kitaifa, kidini, kiserikali na kijamii.

### **Sanaa**

- (a) Kuimarisha nyumba ya sanaa kwa lengo la kuibua, kukuza na kuhuisha vipaji kwa vijana katika sanaa na tasnia ya ubunifu ili kukuza uchumi na kuleta ajira na kipato chao;
- (b) Kuanzisha chuo cha sanaa kitakachotoa elimu na utalam wa sanaa katika tasnia mbalimbali;
- (c) Kuhakikisha kunakuwa na miundombinu ya sanaa katika maeneo mbalimbali pamoja na kuendeshwa kwa vikundi vya sanaa kwa misingi ya uwazi na uwajibikaji na kwa kufuata sheria na kanuni;
- (d) Kuendelea kusimamia na kulinda haki na masilahi ya wasanii;
- (e) Kuendelea kuimarisha mfumo wa kuibua vipaji vya wasanii na kuwatunza na kuwaenzi wasanii wakongwe waliohai na waliofariki.

### **Michezo**

- (a) Kuimarisha na kulinda miundombinu ya michezo ya wilaya, mkoa na Taifa;
- (b) Kuanzisha vituo viwili vya michezo (*sports academy*) vya Serikali pamoja na kuendelea kuviimarisha vituo vya Dole na JKU na vingine kwa kushirikiana na taasisi binafsi ili kuendeleza uibuaji wa vipaji;
- (c) Kuhifadhi miundombinu ya michezo katika skuli, mitaani na maeneo ya fukweni;



- (d) Kuwatambua na kuwawezesha wanamichezo wenye ulemavu kupata fursa na haki ya kushiriki katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya nchi;
- (e) Kuhamasisha vyama vya michezo kufanya jitihada za kupata uwanachama wa kudumu katika mashirikisho ya michezo kikanda, kitaifa na kimataifa na kusimaimia vyema vilabu kushiriki kikamilifu katika mashindano ya kitaifa, kikanda na kimataifa;
- (f) Kuhamasisha jamii kushiriki katika mazoezi ya viungo na michezo mtu mmoja mmoja au vikundi na kuendeleza Tamasha la Mazoezi ya Viungo la tarehe 1 Januari kila mwaka;
- (g) Kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa michezo katika skuli, vikosi, wizara, mitaa na jamii kwa ujumla kwa kushirikiana na vyama husika; na
- (h) Kuhamasisha jamii kushiriki katika michezo yote ya kisasa na asili ikiwemo michezo ya bao, karata na resi za ngalawa.

### **Sekta ya Habari**

189. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, SMZ ilitekeleza Ilani ya CCM kwa ufanisi katika tasnia ya habari na kupata mafanikio yafuatayo:-

- (a) Kuweka mazingira wezeshi ya kuimarisha uhuru wa habari na kuvutia uanzishwaji wa vyombo vya habari na kupelekea:-
  - (i) Kuongezeka vituo vya redio kutoka 19 mwaka 2015 hadi 25 mwaka 2020;
  - (ii) Kuongezeka vituo vya televisheni kutoka saba mwaka 2015 hadi kufikia 24 mwaka 2020 zikiwemo televisheni 12 za mtandaoni;
  - (iii) Kuongezeka idadi ya magazeti na majarida yaliyoajiliwa kutoka 53 mwaka 2015 hadi kufikia 70 mwaka 2020.
- (b) Kuimarisha Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) kwa kujenga studio mpya za redio na televisheni Unguja na Pemba pamoja na kulipatia vifaa vya kisasa. Kufanikisha kuonekana kwa matangazo ZBC TV ulimwenguni kupitia *Satellite*, mitandao ya kijamii na ving'amuzi mbalimbali ikiwemo DSTV;
- (c) Kuimarisha Shirika la Magazeti ya Serikali la Zanzibar kwa kuwapatia jengo jipya la ofisi na kuwezesha kuchapishwa magazeti ya shirika hilo kupitia Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na kuanzisha magazeti mapya ya Zanzibar *Mail* na *ZaSport* ;
- (d) Kuimarisha Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar kwa kuwapatia jengo jipya la kuwekea mitambo na bohari la vifaa, pamoja na kupatiwa



mashine na vifaa vya kisasa vya uchapishaji na kuongezewa mtaji wa kuliwezesha kutoa huduma za vifaa vya uchapishaji na kujiendesha;

- (e) Kuiwezesha Idara ya Habari Maelezo kuanzisha televisheni ya mtandaoni 'Habari online TV', mitandao ya kijamii na 'Portal' ya *Zanzibar daily* ambayo imewezesha Serikali kutoa taarifa za utekelezaji wa sera, mipango, Ilani na ahadi za Chama kwa wananchi;
- (f) Kuimarisha Chuo cha Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma cha Zanzibar kwa kuwezesha kujenga studio mpya ya redio, pamoja na kupatiwa vifaa na mtambo wa redio ulioiwezesha kufungua Redio FM inayotumika kitaaluma na kutoa habari kwa wananchi. Idadi ya wahitimu wa fani ya uandishi wa habari imefikia 483 mwaka 2019 na walimu wanne wamepatiwa mafunzo ya Shahada ya Uzamivu, walimu wanne Shahada ya Uzamili na mafunzo mengine kwa wanataaluma na wafanyakazi wa kada mbalimbali za chuo hicho;
- (g) Kuwapatia mafunzo watendaji wa vyombo vya habari vya Serikali katika fani tafauti ikiwemo kutengeneza kurasa za magazeti, kutengeneza na kutumia mtandao kwa kurusha habari, kutengeneza vipindi na kupiga picha, pamoja na matumizi ya teknolojia ya habari katika ufanyaji kazi zao za kila siku;
- (h) Kuimarika kwa upatikanaji wa habari ambapo huduma za vyombo vya habari vinapatikana mijini na vijijini bila ya matatizo; na
- (i) Kuunganisha huduma za Kampuni ya Usambazaji Maudhui (*Zanzibar Multiplex Company - Z-Mux*) na mkongo wa Taifa Unguja na Pemba, hivyo kuongeza uwezo wa upatikanaji wa huduma zake. Aidha, idadi ya watumiaji imeongezeka kutoka 15,000 mwaka 2015 hadi 18,500 mwaka 2020 na kupelekea kuongeza makusanyo kutoka shilingi milioni 74 mwaka 2016/17 hadi shilingi milioni 720 mwaka 2020.

190. **Sekta ya Habari itaendelea kuwa nguzo muhimu ya kushajiisha wananchi kushiriki katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mkazo mahsusi utawekwa kwa kuzingatia mabadiliko ya teknolojia ya sekta ya habari na kuhakikisha jamii yote inapata taarifa sahihi na kwa wakati. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kufanya mageuzi ya kisera na kisheria katika kusimamia masuala ya habari na kujengea uwezo Idara ya Habari Maelezo na Tume ya Utangazaji kwa kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ya kisasa;
- (b) Kuimarisha Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) na Z-MUX kwa kuzipatia vifaa ikiwemo gari maalum za kurushia matangazo (*OB Van*), na wataalam ili kuweza kutayarisha na kurusha hewani vipindi vyenye ubora na kuimarisha wigo wa upatikanaji na matangazo yake;



- (c) Kukiunganisha Chuo cha Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ili kuongeza hadhi ya taaluma inayotolewa na chuo hicho, ambapo kitatoa mafunzo ya uandishi wa habari, uhusiano na matangazo na mawasiliano ya umma katika ngazi za Shahada na Shahada ya Uzamili;
- (d) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika vyombo vya habari ili kutanua wigo wa upatikanaji wa habari kwa wananchi mijini na vijijini;
- (e) Kuimarisha uwezo wa Wakala wa Uchapaji na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuwapatia wataalam na mitambo bora na vifaa vya kisasa vya uchapaji na kuimarisha huduma za bohari kuu ya Serikali; na
- (f) Kuimarisha uwezo wa Shirika la Magazeti ya Serikali kwa kuongeza nakala za magazeti yanayochapishwa na kuhakikisha yanasambazwa kwa wakati nchi nzima.

### **Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

191.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita SMZ ilichukua juhudi mbalimbali katika kukabiliana na athari zinazotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kutekeleza yafuatayo:-

- (a) Kufanya mapitio ya Sera ya Mazingira ya Mwaka 1992 na kuzindua Sera ya Mazingira ya Mwaka 2013 ambayo inatoa mwongozo wa usimamizi wa mazingira nchini. Sheria ya Mazingira ya Mwaka 1996 ilifutwa kwa kuanzisha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar Na. 3 ya Mwaka 2015 ambayo imeweka mfumo bora wa kisheria na kitaasisi wa usimamizi wa mazingira Zanzibar;
- (b) Kutayarisha kanuni na miongozo ya usimamizi wa mazingira ikiwemo: Kanuni ya Mifuko ya Plastiki Mwaka 2011 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2018 na 2020; kanuni pamoja na Mwongozo wa Tathmini ya Athari za Kimazingira ya Mwaka 2019; Kanuni ya Uangamizaji wa Vitu Visivyofaa kwa Matumizi ya Mwaka 2019; Kanuni ya Usimamizi wa Taka kwa Manispaa ya Mjini Zanzibar ya Mwaka 2019; na mpango wa kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki Zanzibar;
- (c) Kukagua, kushauri na kutoa miongozo ya kimazingira kwa miradi 510 ya vitega uchumi na maeneo 204 ya kimazingira. Vilevile, jumla ya miradi 200 imefanyiwa tathmini za mazingira na kupewa vyeti vya kimazingira kwa ajili utekelezaji wa miradi ya kiuchumi na maendeleo;
- (d) Kuandaa mkakati wa usimamizi wa taka na mkakati wa tathmini ya kimazingira (*strategic environmental assessment*) kwa ajili ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia;



- (e) Kujenga jaa la Kitaalam (*sanitary landfill*) katika eneo la Kibele linahifadhi taka zinazotolewa katika maeneo mbalimbali ya Unguja. Kujenga kituo kidogo cha majaribio Shaurimoyo na Kituo cha Maruhubi kwa ajili ya kutenganisha taka;
- (f) Kujenga misingi ya maji ya mvua kilomita 22.3 katika maeneo ya Magomeni - Mpendae - Kwabitihamrani - Kilimani - Kiungani, Darajabovu - Kwamtipura - Chumbuni - Saateni, Mnazimmoja - Kizingo, Chumbuni - Mtopepo - Karakana, Kijangwani - Kibandamaiti na Kiembesamaki - Mbweni - Mazizini;
- (g) Kupanda Mikandaa (Mikoko) katika hekta 230 kuzuia maji ya chumvi kuingia katika maeneo pamoja na kuzuia mmongonyoko wa fukwe katika maeneo ya Kilimani, Kisakasaka, Tovuni, Ukele, Kisiwa Panza na Tumbe. Aidha, mikoko 220,000 na mivinje 14,000 imepandwa katika eneo la Jozani kwa ajili ya kutunza mazingira;
- (h) Kujenga kuta na matuta ya kuzuia maji ya bahari kupanda juu katika vijiji vya Tumbe West (250m), Ukele (700m), Sizini (200m), Gando Nduuni (150m), Chokaani (20m), Kengeja (120m), Kisiwa Panza (50m) Pemba na "groynes" (420m) Kilimani Unguja. Pia, ukuta wenye urefu wa mita 300 umejengwa katika eneo la bahari ya Mizingani Forodhani; na
- (i) Kutoa elimu kwa umma juu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira kupitia mikutano 45 ya wananchi, vipindi 102 vya redio na televisheni, vilabu 53 vya mazingira vya skuli, kamati 16 za uvuvi za shehia na wanafunzi 192.

**192. Zanzibar ipo katika hatari za kimazingira na inakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi na mazingira. Kwa hivyo, kuna umuhimu wa kutunza na kuhifadhi mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa mantiki hiyo, msisitizo utawekwa katika kulinda fukwe, matumizi ya bahari na misitu; utunzaji na uhifadhi wa mazingira; kudhibiti hewa ya ukaa; pamoja na ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi wa mazingira. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuboresha na kusimamia sera na sheria ya mazingira ili kupunguza na hatimaye kuondoa uharibifu na uchafuzi wa mazingira;
- (b) Kusimamia tathmini za athari za kimazingira, ukaguzi wa kimazingira na ufuatiliaji wa kimazingira katika maeneo mbalimbali ya nchi;
- (c) Kutoa elimu na kukuza mwamko wa jamii juu ya umuhimu wa utunzaji na usimamizi bora wa mazingira pamoja na ushiriki wa jamii katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwenye maeneo yao;



- (d) Kupunguza athari ya mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya Msuka na Tovuni Pemba pamoja na Mafufuni Unguja;
- (e) Kutekeleza mkakati wa kitaifa wa usimamizi wa taka wenye lengo la kuimarisha usafi wa mazingira kwa kuanzisha majaa mawili madogo ya kitaalam kwa ajili ya kutupa na kusarifu taka (Kaskazini Unguja moja na Pemba moja);
- (f) Kuhamasisha na kuanzisha sehemu ya kumwaga maji machafu (*sludge disposal*) Pemba;
- (g) Kufanya utafiti wa kina wa maeneo yanayodidimia Zanzibar kama vile Jang'ombe, Mwanakwerewe na mengine ili kujua sababu za kutokea hali hiyo;
- (h) Kujenga kuta (*groynes*) za kuzuia mmomonyoko wa fukwe katika maeneo ya Kizingo na Jambiani ambayo yameathirika na mabadiliko ya tabianchi;
- (i) Kudhibiti ukataji wa miti kiholela ili kuhifadhi mazingira; na
- (j) Kujenga miundombinu itakayozuia uingiaji wa maji ya bahari kwenye maeneo ya kilimo, kufanya tafiti na kutumia mbegu zenye kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na utoaji wa tahadhari ya mapema juu ya mabadiliko ya hali ya hewa na milipuko ya wadudu na maradhi.

### **Kukabiliana na Maafa**

193. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita SMZ ilitekeleza Ilani ya CCM kuhusiana na kukabiliana na maafa na kutoa huduma za uokoaji na kupata mafanikio yafuatayo:-
- (a) Kuanzisha Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa na kufanya tathmini ya miaka mitano ya utekelezaji wa sera ya kukabiliana na maafa Zanzibar. Kuandaa mwongozo wa ugawaji na upokeaji wa misaada ya kibinadamu kwa waathirika wa maafa na mwongozo wa tathmini baada ya maafa;
  - (b) Kutoa misaada ya kibinaadamu yenye thamani ya shilingi milioni 87 kwa wananchi 167 na shilingi milioni 235 kwa wananchi 3,658 baada ya nyumba zao kuathirika kwa mvua;
  - (c) Kutoa mafunzo ya kukabiliana na maafa kwa wananchi 3,030 wakiwemo watu wenye mahitaji maalum, viongozi wa dini, wazee, walimu na wanafunzi wa skuli za maandalizi, msingi na sekondari kutoka wilaya za Chake Chake na Micheweni. Kutoa elimu kupitia vipindi 44 vya televisheni na 100 vya redio; na
  - (d) Kujenga nyumba za wananchi walioathiriwa na mvua za masika za mwaka 2017 na upepo mkali katika kijiji cha Nungwi Unguja na Tumbe Pemba.





194. **Maafa ni moja ya changamoto zinazoikabili dunia kwa wakati huu. Hivyo, msisitizo maalum utaendelea kuwekwa kuhakikisha kunakuwepo huduma bora za uokozi na misaada na zinawafikia wananchi wote kwa wakati. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuimarisha utekelezaji wa mipango na mikakati ya kukabiliana na maafa ikiwemo kutoa elimu ya kukabiliana na maafa katika shehia zote za Unguja na Pemba;
- (b) Kuhamasisha jamii kutoa taarifa sahihi na kwa wakati pindi yanapotokea maafa;
- (c) Kuandaa mfumo wa kisasa wa mawasilino utarahisisha kutoa taarifa za maafa katika ngazi za shehia, wilaya na Taifa pamoja na kuandaa miongozo mbalimbali ya kukabiliana na maafa katika ngazi za shehia, wilaya na Taifa;
- (d) Kuimarisha vituo vya operesheni na mawasiliano ya dharura vilivyopo Maruhubi, Gamba na Makunduchi kwa Unguja na Mkoani, Chake Chake na Micheweni kwa Pemba;
- (e) Kuimarisha mfumo wa utoaji wa tahadhari za mapema na kinga dhidi ya maafa;
- (f) Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa utafutaji na uokozi kwa matukio ya maafa makubwa; na
- (g) Kuainisha na kuandaa ramani ya maeneo hatarishi (*Disaster zones*).

### **Dawa za Kulevya**

195. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita SMZ ilitekeleza Ilani ya CCM ya kudhibiti uingiaji na matumizi ya dawa za kulevya na kupata mafanikio yafuatayo:-

- (a) Kufanya marekebisho ya sheria ya dawa za kulevya kwa kuzidisha adhabu kwa waingizaji, wasafirishaji, wasambazaji wa dawa za kulevya;
- (b) Kutoa mafunzo ya kina ya utambuzi pamoja na uchunguzi wa dawa za kulevya kwa watendaji wa viwanja vya ndege pamoja na bandari na wasimamizi wa madiko katika shehia 78 kwa Unguja na 35 kwa Pemba;
- (c) Kuimarisha ukaguzi wa bidhaa na mizigo bandarini na viwanja vya ndege;
- (d) Kuweka vifaa vya ukaguzi wa mizigo na abiria ikiwemo mashine za x-ray pamoja na choo katika maeneo ya bandari na viwanja vya ndege pamoja na magari mawili maalum yenye uwezo wa kuchunguza dawa za kulevya;



- (e) Kufanya vikao vya mara kwa mara na wadau wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya ili kuwajengea uwezo;
- (f) Kutoa elimu juu ya athari za dawa za kulevya katika shehia 388, mabaraza ya vijana ngazi ya wilaya 11, skuli 336 na wafanyakazi 1,050. Aidha, jumla ya vipindi 225 vimerikodiwa na kurushwa hewani pamoja na vipeperushi 21,000 kutolewa kwa lengo la kuisaidia jamii kuondokana na janga la dawa za kulevya; na
- (g) Kujenga Kituo Maalum cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa waathirika wa dawa za kulevya (*rehabilitation center*) katika kijiji cha Kidimini Wilaya ya Kati Unguja.

**196. Biashara na utumiaji wa dawa za kulevya ni janga kwa jamii ya jinsia na rika zote hivyo udhibiti wake ni jambo muhimu kwa ustawi wa Taifa. Katika miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kutekeleza mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kudhibiti uingizaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya kwa kuendelea kuchukua hatua za kisheria;
- (b) Kutoa taaluma za kinga ya msingi pamoja na familia imara itakayosaidia kuwalea watoto ikiwemo kuziweka familia katika malezi yenye maadili mema yanayokubalika na yatakayowakinga na janga la dawa za kulevya;
- (c) Kujenga Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Pemba pamoja na kuongeza juhudi katika utoaji wa tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya na kuwapatia mafunzo ya stadi za maisha;
- (d) Kuhakikisha kesi za uhalifu wa dawa za kulevya zinasikilizwa na kukamilishwa kwa muda mfupi kwa kuanzisha vipindi maalum vya usikilizaji wa kesi hizo mahakamani sambamba na kuhakikisha kuwa mali na mapato ya wahalifu hao vinataifishwa;
- (e) Kuanzisha kituo maalum cha pamoja cha mashirikiano (*One Stop Center*) kwa vyombo vinavyosimamia mapambano dhidi ya dawa za kulevya ndani ya taasisi inayoshughulikia masuala ya dawa za kulevya kwa ajili ya kupokea taarifa zote za dawa za kulevya ili kufanyiwa kazi kwa haraka;
- (f) Kuimarisha ukaguzi wa abiria pamoja na mizigo bandarini na viwanja vya ndege kwa kuhakikisha dawa za kulevya haziingii nchini; na
- (g) Kuimarisha ushirikiano na jumuiya za kimataifa katika kupambana na makosa yanayohusiana na biashara haramu ya dawa za kulevya.

**Demokrasia na Utawala Bora**

197. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita CCM iliilekeza SMZ kuendelea kuzingatia misingi ya Demokrasia na Utawala Bora kama ilivyoainishwa katika Katiba za nchi, sheria, kanuni na miongozo iliyopo ya demokrasia na utawala bora na mafanikio makubwa yamepatikana kama ifuatavyo:-
- (a) Kutoa elimu ya utawala bora, kuandaa jarida la utawala bora la kila mwaka na mwongozo wa utawala bora Zanzibar pamoja na kufanya mapitio ya sera ya utawala bora. Pia, Serikali imefanya tathmini na kuandaa ripoti za utekelezaji wa misingi ya utawala bora;
  - (b) Kutunga Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Namba 4 ya Mwaka 2015 na kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
  - (c) Kuimarisha Kamisheni ya Utumishi wa Umma na Tume za Utumishi (Tume ya Utumishi Serikalini, Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi, Tume ya Utumishi ya Mahakama, na Tume ya Utumishi Idara Maalum za SMZ);
  - (d) Kutoa elimu ya uraia kupitia vipindi 72 vya redio na televisheni na kufanya mikutano 41 ya viongozi wa taasisi za umma na binafsi pamoja na wananchi. Jumla ya viongozi 351 wamehakikiwa taarifa zao za mali na madeni pamoja na tamko la mali za viongozi 2020 zimepokelewa na kusajiliwa pamoja na kuandaa na kuchapisha vipeperushi 3,000;
  - (e) Kuajiri watumishi wapya 20 katika Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi 65, mafunzo ya muda mfupi watumishi 73;
  - (f) Kuelimisha jamii athari ya vitendo vya rushwa kupitia vipindi vya redio na televisheni, mijadala ya wazi na maandishi wa habari, wafanyabiashara, maonesho na kutoa ushauri;
  - (g) Kuchukua hatua za uhibititi na uchunguzi wa makosa ya rushwa pamoja na kuratibu utekelezaji wa mpango mkakati shirikishi wa kupambana na rushwa. Jumla ya kesi 178 za rushwa na 279 za ubadhirifu na rushwa zimeripotiwa na kuchukuliwa hatua;
  - (h) Kufanya ukaguzi wa mahesabu kila mwaka na kuweza kutoa ripoti na kuziwasilisha Baraza la Wawakilishi. Aidha, ukaguzi maalum umefanyika kwa mashirika, miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo na ukaguzi wa fedha za mifuko ya majimbo. Jumla ya wakaguzi 130 wamepatiwa mafunzo katika fani mbalimbali;
  - (i) Kufanya ukaguzi wa kiutumishi katika wizara na taasisi zote za Serikali kwa lengo la kuangalia masuala ya mishahara, posho, uajiri na upandishaji vyeo;



- (j) Kuimarisha mhimili wa mahakama kwa kutunga sheria ya utawala wa mahakama, kuongezeka kwa idadi ya majaji wakiwemo watatu wanawake na mahakimu wa mikoa na wilaya. Jumla ya kesi mpya za madai 9,785 zimefunguliwa na kufanya kesi zote za madai kufikia 12,776. Vile vile, jumla ya kesi za Jinai 6,250 zilifunguliwa, kati ya hizo kesi 3,364 sawa na asilimia 54 zilitolewa uamuzi. Divisheni za mahakama ikiwemo mahakama za biashara na mahakama ya ardhi zimeimarishwa;
- (k) Kuimarisha usimamizi wa mashtaka juu ya kesi za jinai zilizofunguliwa katika mahakama mbalimbali za Unguja na Pemba;
- (l) Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwaachia huru wanafunzi 72 kutoka kwenye vyuo vya mafunzo;
- (m) Kujenga jengo jipya la Mahakama Kuu katika eneo la Tunguu, jengo jipya la Mahakama ya Watoto Mahonda na kufanya matengenezo ya majengo ya mahakama yakiwemo mahakama ya Wilaya ya Mkoani, Mahakama ya Kadhi ya Mwanakwerekwe, Mahakama ya Chake - Chake na Mahakama ya Mwanakwerekwe;
- (n) Kuandaa Sera na Sheria za Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2018, Sheria ya Chama cha Wanasheria ya Mwaka 2019, Sheria ya Skuli ya Sheria ya Mwaka 2019, na Sheria ya Mawakili ya Mwaka 2020; na
- (o) Kufanya vikao kumi na saba vya kawaida na kupitia vikao hivyo ripoti na taarifa mbalimbali ziliwasilishwa na sheria 62 kutungwa.

198. **Demokrasia na Utawala Bora ni sehemu ya misingi ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Juhudi kubwa zimechukuliwa kwa Zanzibar katika kuimarisha taasisi na mifumo ya upatikanaji wa haki. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kuendeleza demokrasia kwa kuzingatia umoja na mshikamano, usawa, upatikanaji wa haki na uwajibikaji kwa kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kutekeleza shughuli za Serikali kwa kuzingatia misingi ya demokrasia na utawala bora kama ilivyoainishwa katika Katiba za nchi na kuimarisha uwazi na uwajibikaji kwa wananchi;
- (b) Kuimarisha usimamizi wa maadili ya viongozi wa umma kwa kutoa elimu kwa viongozi na wananchi kuhusu umuhimu wa kukuza maadili na kuimarisha mfumo wa kukusanya, kuhifadhi na kuhakiki taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma;
- (c) Kujenga jengo jipya la Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi na kuipatia wataalam na vifaa vya kisasa vya uchunguzi na kukamilisha uandaaji wa kanuni mbali mbali za udhibiti wa rushwa. Elimu kuhusiana na madhara ya rushwa itaendelea kutolewa kwa jamii na kuandaa mitaala ya elimu katika skuli na vyuo vikuu;



- (d) Kuanzisha skuli ya sheria kwa lengo la kuongeza weledi na kuwathibitisha wanasheria;
- (e) Kutekeleza Sheria za Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2018 na Sheria ya Mawakili ya Mwaka 2020 ili kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wananchi wote;
- (f) Kuimarisha mihimili ya Mahakama na Baraza la Wawakilishi kwa kuwapatia rasilimali watu, maeneo ya kazi na vitendea kazi;
- (g) Kuhakikisha sekta binafsi inasimamia na kuendesha biashara bila ya ubaguzi wa kidini, jinsia, maumbile na hali ya mtu na sehemu anayotoka. Aidha, sekta binafsi itawajibika kuzingatia misingi ya utawala bora na kufuata sheria za nchi hususan kutoa kipaumbele kwa wazawa kwa kuajiri wananchi wenye ujuzi na uwezo waliofikia umri wa kuajiriwa, kutimiza wajibu wake katika kulipa kodi kwa usahihi, ukamilifu na kwa wakati; na
- (h) Kupitia na kuzifanyia marekebisho sheria zote zinazokwaza maendeleo ya kijamii na kiuchumi hususan sheria zinazozuia fursa za ajira kwa wananchi.

### **Kuwaunganisha Wananchi wa Zanzibar**

199. Katika miaka mitano iliyopita CCM ilielekeza SMZ kuhakikisha kuwa Wazanzibar wanaendelea kuwa wamoja kwa kuishi bila ya kubaguana kwa rangi, kabila na sehemu wanayotoka ambapo mafanikio makubwa yamepatikana kama ifuatavyo:-

- (a) Kulinda na kuimarisha misingi ya umoja wa kitaifa, amani na utulivu nchini;
- (b) Kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea kuishi kwa umoja, mshikamano na kwa upendo; na
- (c) Kulinda na kuimarisha mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

200. **Kwa kutambua umuhimu wa kuwaunganisha wananchi wote kuwa wamoja na kuishi kwa amani na utulivu. CCM itaendelea kuisimamia SMZ kuhakikisha kuwa Wazanzibar wanaendelea kuishi kwa udugu, umoja, mshikamano na ustahamilivu kwa kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuendeleza kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa amani, umoja na mshikamano ili kujenga mazingira ya kuaminiana, kuvumiliana na kushirikiana katika masuala mbalimbali ya kijamii;
- (b) Kupiga vita na kudhibiti vitendo vyote vya ubaguzi utoaji wa huduma za kiuchumi, kijamii, kisiasa, kimaeneo, kijinsia na kidini;



- (c) Kuimarisha mifumo ya taasisi za uratibu na kushughulikia malalamiko na kero za wananchi kwa wakati, haki na uadilifu; na
- (d) Kuwasisitiza viongozi kusikiliza kero na malalamiko ya wananchi kwa hekima, unyenyekevu na busara.

### **Serikali za Mitaa**

201.

Katika kipindi cha miaka mitano CCM iliielekeza SMZ kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya halmashauri za wilaya, mabaraza ya miji na manispaa, kuimarisha usafi wa mazingira mijini na vijijini ambapo mafanikio makubwa yamepatikana kama ifuatavyo:-

- (a) Kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato na kutoa mafunzo kwa watendaji katika vituo vya ukusanyaji wa mapato. Mapato katika serikali za mitaa yameongezeka kutoka shilingi bilioni 2.8 mwaka 2015/2016 hadi bilioni 12.8 mwaka 2018/2019;
- (b) Kufanya ugatuzi kwa sekta ya elimu (elimu ya msingi na maandalizi), afya (afya ya msingi) na kilimo (huduma za ugani) na kuimarisha ubora wa huduma za elimu, afya na kilimo kwa wananchi;
- (c) Kuimarisha usafi wa mazingira katika maeneo ya mijini kwa kusambaza vifaa vya usafi katika shehia 27 za majaribio, kuingia mikataba na vikundi 49 vya usafi kwa ajili ya kusafisha barabara, masoko, misingi ya maji ya mvua pamoja na kuondosha taka katika makaazi ya watu. Aidha, bustani zimeanzishwa na kuendelezwa katika maeneo mbalimbali;
- (d) Kamati za maendeleo 499 zimeundwa kwa mujibu wa mwongozo uliotayarishwa, kati yake 388 ni kamati za mashauriano za shehia ni 388 na 111 mabaraza ya wadi. Kamati hizi zina jukumu la kuibua na kupanga mipango ya maendeleo katika ngazi ya wadi na shehia. Kamati zote zimeshapatiwa mafunzo ya kutekeleza majukumu yao;
- (e) Kufuatilia matukio ya uvunjifu wa amani kwa kufanya operesheni na kuunda kamati za usalama, kamati za kupinga udhalilishaji kwa kina mama na watoto, kamati za maadili na vikundi vya ulinzi shirikishi katika ngazi za shehia 388;
- (f) Kuwezesha utekelezaji wa miradi ya wananchi 172 iliyohusu upatikanaji wa majisafi na salama, ujenzi na ukarabati wa vyumba vya madarasa, vyoo, vituo vya afya na matengenezo ya barabara za ndani kwa kiwango cha kifusi pamoja na ujenzi wa madaraja madogo;
- (g) Kutoa fedha zinazotokana na mapato ya ndani ili kusaidia vikundi vya wajasiriamali vijana, wanawake na watu wenye ulemavu katika maeneo ya miji na vijijini;





- (h) Kuanzisha jiji la Zanzibar linalosimamia mabaraza matatu ya manisipaa; na
- (i) Kuweka taa za barabarani zinazotumia nguvu za jua katika maeneo ya mji wa Zanzibar, unyanyuaji wa barabara ya Mwanakwerekwe, na ununuzi wa vifaa vya kuzolea taka zikiwemo gari na hifadhi ya eneo la urithi wa Mji Mkongwe.

202.

**Serikali za Mitaa ni chombo muhimu kinachoshirikisha wananchi katika kupanga na kutekeleza shughuli za maendeleo na utoaji wa huduma katika sehemu zao. Kutokana na umuhimu wa chombo hicho, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuimarisha serikali za mitaa ili ziweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu kuendana na dhana ya ugatuzi wa madaraka;
- (b) Kuimarisha huduma za jamii ikiwemo afya ya msingi, elimu ya maandalizi na msingi, na kilimo ili wananchi hasa vijijini waweze kupata huduma hizo kwa wakati na ubora;
- (c) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ambapo asilimia 25 ya fedha hizo zitaelekezwa kutekeleza miradi ya maendeleo katika ngazi za wadi kwa kuzingatia vipaumbele vya wananchi wanavyoviibua kupitia mabaraza ya wadi na kamati za halmashauri za shehia;
- (d) Kuongeza uwezo wa Manisipaa ya Mjini katika kusafirisha taka ngumu kutoka asilimia 67 za taka zinazokusanywa kwa siku (tani 280) mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 95 mwaka 2025 na kuimarisha serikali za mitaa nyengine Unguja na Pemba katika uwezo wa kukusanya na kutupa taka;
- (e) Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kusarifu taka ngumu na kuongeza ajira kwa vijana;
- (f) Kuandaa miongozo bora ya utendaji kazi kwa dhamira ya kupanga mipango ya maendeleo yenye lengo la kupunguza umasikini na kudumisha amani, ulinzi na usalama wa maisha ya wananchi na mali zao katika maeneo mbalimbali;
- (g) Kuanzisha idara ya huduma za jamii kwa kila manisipaa, mabaraza ya miji na halmashauri na kuzijengea uwezo wa kubuni miradi bora ya maendeleo kwa jamii ili thamani ya fedha iendane na miradi husika;
- (h) Kupanua wigo wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi hususan makundi maalum ya wajasiriamali, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kutoa fedha katika makusanyo ya serikali za mitaa na kuandaa mwongozo wa usimamizi wa misaada inayotolewa ili kuhakikisha fedha zinatumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa;

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA



- (i) Kujenga uwezo wa Halmashauri ya Jiji la Zanzibar ili kutekeleza wajibu wake ipasavyo;
- (j) Kuboresha miundombinu katika Manispaa ya Zanzibar kwa kuhakikisha kwamba mvua hazileti athari kwa makaazi ya wananchi, ikiwemo kujenga misingi ya kupitisha maji ya mvua katika barabara zote za Manispaa ya Zanzibar.

### **Idara Maalum za SMZ**

203. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ya utekelezaji wa Ilani ya CCM, Idara Maalum za SMZ zilipata mafanikio makubwa ikiwemo kuimarisha ulinzi na usalama mijini na vijijini kwa kutelekeza yafuatayo:-

- (a) Kuandaa mpango mkuu wa mafunzo kwa idara maalum za SMZ na jumla ya maafisa 2,053 wamepatiwa mafunzo ya kijeshi katika ngazi mbalimbali na askari 723 wamepatiwa mafunzo ya kitaaluma;
- (b) Kutoa vifaa na vitendea kazi vya kisasa kwa vikosi vya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM), Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Chuo cha Mafunzo na Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ) na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU) kwa kununua magari 59, boti 11 za doria na vifaa vya mawasiliano na uzamiaji na mashine 36 za kazi za amali; na
- (c) Kuongeza masilahi ya vikosi vya idara maalum kwa kuongeza mshahara kwa asilimia 100 kwa kima cha chini na kupandisha vyeo watumishi 896.

#### ***Kikosi Maalum Cha Kuzuia Magendo (KMKM)***

- (a) Kujenga Kambiya Makombeni, Kisiwa Panza, Fundo, Kojani, Tungamaa na Kengeja;
- (b) Kujenga vituo vitatu vya uokozi Kibweni, Nungwi na Mkoani; na
- (c) Kuimarisha hospitali ya KMKM Kibweni kwa kujenga jengo la kisasa la ghorofa mbili.

#### ***Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)***

- (a) Kujenga Mabweni mawili na bwalo moja katika Kambi ya Msaani;
- (b) Kukamilika kwa jengo la skuli ya sekondari ya JKU lenye ghorofa tatu na kuanza ujenzi wa Kituo cha Amali cha JKU;
- (c) Kuanzisha Wakala wa Ulinzi wa Serikali kwa ajili ya kutoa huduma za ulinzi katika maeneo mbalimbali; na
- (d) Kuwapatia jumla ya vijana 2,561 mafunzo ya ufundi katika fani 13 katika kituo cha Amali Mtoni ambazo zinaenda sambamba na mahitaji ya soko la ajira. Kati yao vijana 1,332 wamemaliza mafunzo hayo na vijana 1,229 wanaendelea.



**Chuo Cha Mafunzo**

- (a) Kuendelea kurekebisha tabia na mienendo ya wanafunzi ili kuwa raia wema; na
- (b) Kujenga jengo la chuo cha urekebishaji tabia kwa wanafunzi watoto.

**Kikosi Cha Valantia Zanzibar (KVZ)**

- (a) Kujenga kambi mpya ya Kijichame kwa kuinua jengo la ghorofa moja; na
- (b) Kujenga hanga na kukamilisha kwa asilimia 50 ujenzi wa jengo la ofisi ghorofa moja katika kambi ya Ndogukitu na jengo la ofisi katika Kambi ya Micheweni.

**Kikosi Cha Zimamoto na Uokozi**

- (a) Kuendelea kutoa huduma ya kupambana na majanga ya moto na kufanya uokozi wa mali na binadamu; na
- (b) Kutoa elimu kwa jamii kuhusu kupambana na majanga ya moto.

204. **Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni vyombo muhimu katika kutekeleza dhana ya uzalendo kwa vitendo, kudumisha na kutoa huduma bora za uokoaji, ulinzi na usalama kwa jamii. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kuendelea na kuziimarisha Idara Maalum za SMZ kwa kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazowaongoza;
- (b) Kuendeleza mradi wa majengo ya ofisi, Mahanga na nyumba za maofisa wa idara maalum za SMZ kwa lengo la kuweka mazingira bora ya kazi na makambi na kuimarisha shughuli za ulinzi na usalama;
- (c) Kuendeleza Wakala wa Ulinzi wa Serikali na kuanzisha Kampuni ya Ujenzi ya Serikali;
- (d) Kuwajengea uwezo maofisa na askari wake kwa kuwapatia mafunzo ya kisasa katika vyo vya ndani na nje ya nchi;
- (e) Kutoa mafunzo ya ulinzi kwa vijana 150 na kuanzisha ulinzi wa Jeshi Usu kwa kuimarisha usimamizi wa misitu na wanyamapori katika hifadhi;
- (f) Kuanza ujenzi wa chuo cha kisasa Hanyegwa Mchana na ujenzi wa chuo cha kisasa cha Zimamoto na Uokozi huko Kitogani Mkoa wa Kusini Unguja;



- (g) Kuimarisha utendaji kazi wa Idara Maalum ili kutekeleza majukumu yao ipasavyo;
- (h) Kumaliza ujenzi wa chuo cha kisasa cha ufundi JKU Mtoni kitakachokuwa na uwezo wa kutoa mafunzo ya ufundi kwa vijana wasiopungua 3,000 kwa mwaka; na
- (i) Kujenga nyumba za maafisa na askari katika kambi za Micheweni na Pujini kwa Pemba na Kambi ya Kikungwi kwa Unguja.

### Utafiti na Takwimu

205.

CCM inaamini kwamba utafiti na takwimu ni sekta mtambuka ambayo ni chanzo kikubwa cha upatikanaji wa taarifa mpya na za kina zitakazotumika kuiarifu na kuishauri jamii juu ya masuala mbalimbali ya kiuchumi, kijamii na mazingira inayoizunguka. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 – 2020), Chama kiliendelea kuisimamia vyema SMZ katika sekta mtambuka ya utafiti na takwimu na kupata mafanikio yafuatayo:-

- (a) Kuendelea kusimamia udhibiti wa usalama na maadili katika uendeshaji wa tafiti zinazofanyika nchini;
- (b) Kuendeleza uratibu wa shughuli za utafiti za kisekta kupitia idara za sera, mipango na utafiti katika wizara zote. Mfumo wa uratibu kupitia idara hizo umesaidia katika ukusanyaji na utoaji wa taarifa za ufuatiliaji na tathmini Serikalini;
- (c) Kuandaa na kuchapisha Agenda ya Utafiti ya Zanzibar (*Zanzibar Research Agenda, 2015*) iliyoibua maeneo makuu ya kipaumbele;
- (d) Kuanzisha taasisi tatu za utafiti ikiwemo Taasisi ya Utafiti ya Mifugo (ZALIRI), Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi na Mazao ya Baharini (ZAFIRI) na Taasisi ya Utafiti ya Sayansi za Afya Binguni;
- (e) Kufanya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya ya Mwaka 2019 (*Household Budget Survey of 2019*);
- (f) Kufanya mapitio ya takwimu za Pato la Taifa kwa kizio cha mwaka 2015 kutoka bei za kudumu za mwaka 2007 kwa lengo la kupata matokeo halisi ya ukuaji uchumi;
- (g) Kuendeleza utekelezaji wa mpango wa uimarishaji wa takwimu Tanzania ambao ulifikia ukomo mwaka 2018. Aidha, mkakati wa maendeleo ya takwimu wa Zanzibar unaendelea kuandaliwa;
- (h) Kumarisha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu za kiuchumi na kijamii kama vile utalii, kilimo na afya; na



- (i) Kufanya tafiti za kutoa matoleo katika nyanja mbalimbali pamoja na kuendeleza tafiti za kimafunzo kwa kutoa matoleo sahihi kupitia Chuo Kikuu cha Taifa SUZA.

206.

**CCM inatambua umuhimu wa tafiti na takwimu katika kusaidia kutoa uamuzi sahihi katika mipango ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hivyo, katika miaka mitano ijayo, Chama kitaelekeza SMZ kuendelea kutoa kipaumbele katika kukusanya, kuchambua na kutumia takwimu na tathmini pamoja na kufanya tafiti zenye tija kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kukusanya tafiti zote zilizofanyika nchini kabla na baada ya kuanzishwa taasisi mpya za utafiti wa kisekta na kufanya mikutano ya uwasilishaji na uchapishaji wa matoleo;
- (b) Kuendeleza tafiti katika sekta za uzalishaji, maendeleo ya jamii, masoko na maeneo mtambuka kwa mujibu wa vipaumbele vilivyoainishwa;
- (c) Kuandaa na kuchapisha Agenda ya Utafiti ya Zanzibar (*Zanzibar Research Agenda, 2020*) itakayoibua maeneo makuu ya kipaumbele;
- (d) Kuendeleza kazi za utafiti, kuibua matokeo na kutoa ushauri wa kitaaluma katika maeneo maalum ya kiuchumi ikiwemo zoezi la utafutaji wa mafuta na gesi asilia;
- (e) Kutoa elimu kwa watafiti katika ngazi za Uzamili na Uzamivu kupitia taasisi za utafiti za kisekta na Chuo Kikuu cha Taifa - SUZA, sambamba na kuimarisha miundombinu na vitendea kazi katika taasisi hizo;
- (f) Kufanya utafiti wa kutambua maeneo muhimu na aina ya miradi ya uwekezaji ili kuwekeza kwa ufanisi;
- (g) Kuendeleza tafiti nane za mazao ya kilimo ikiwemo mpunga, karafuu na mazao mengine ya kimkakati;
- (h) Kukamilisha tafiti zinazoendelea na kufanya tafiti mpya kwa mujibu wa mahitaji, kuwajengea uwezo watafiti pamoja na kuimarisha miundombinu ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini na Maruhubi kuwa kituo bora cha utafiti wa baharini (*ocean focused heritage research*) katika Ukanda wa Mwambao Magharibi wa Bahari ya Hindi (*WIO Region*);
- (i) Kufanya sensa zifuatazo:-
  - (i) Sensa ya watu na makazi; Sensa ya kilimo na mifugo;

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA



- (ii) Sensa ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi; na
- (iii) Sensa ya viwanda na biashara.
- (j) Kufanya utafiti wa sekta sizizo rasmi pamoja na mapitio ya faharisi za bei (CPI) kwa kutumia mkoba mpya; na
- (k) Kukamilisha na kutekeleza mkakati wa maendeleo ya takwimu pamoja na kuandaa mipango midogo midogo ya takwimu za kissekta.

### **Kuyaendeleza Makundi Mbalimbali**

#### **Watoto**

207. Katika miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), CCM imendelea kuisimamia SMZ kuimarisha haki za watoto ambapo mafanikio makubwa yamepatikana kama ifuatavyo:-

- (a) Kutoa uelewa juu ya biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu kwa taasisi za Serikali na taasisi binafsi ili kudhibiti biashara hiyo;
- (b) Kuendelea kuwatunza na kuwahudumia watoto waliopo katika nyumba ya Serikali ya kulelea watoto Mazizini kwa kuwapatia elimu, michezo, lishe bora, huduma ya afya na mazingira yanayowajengea kimwili, kiakili na kimaadili;
- (c) Kuanzisha na kuendeleza kamati za wazazi katika shehia za Unguja na Pemba na kuzijengea uwezo juu ya malezi bora, kujikinga na vitendo vya ukatili na udhalilishaji pamoja na kuchukua hatua ya kuripoti matukio hayo; na
- (d) Kuandaa mwongozo wa mafunzo ya walimu wa ushauri nasaha katika maskuli. Jumla ya wilaya tatu (Magharibi "A" na "B" za Unguja na Wete kwa Pemba) na walimu 3,500 wamefikwa kwa kujengewa uwezo wa namna bora ya mawasiliano na watoto katika kuwakinga na matukio ya ukatili.

208. **CCM inatambua kuwa watoto wanayo haki ya kuishi, kutoa mawazo, kupata lishe bora, malezi, ulinzi, elimu na kutobaguliwa kwa namna yoyote. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuzipatia familia 1,500 mafunzo ya kujikinga, kuripoti na mawasiliano kwa watoto na stadi mbalimbali za maisha na kujitathamini;
- (b) Kuhamasisha na kuelimisha jamii, familia na watoto juu ya kuimarisha malezi bora kutoa elimu kuhusu upigaji vita udhalilishaji wa watoto kupitia vyombo vya habari;
- (c) Kuendeleza na kuunda mabaraza mapya ya watoto pamoja na kuratibu vikao vya mabaraza hayo. Aidha, mabaraza yote ya vijana yataimarishwa kwa kujengewa uwezo juu ya kujikinga na kuripoti matukio ya ukatili na udhalilishaji wa watoto;





- (d) Kutoa huduma katika kituo cha kurekebisha tabia watoto wanaokinzana na sheria kilichopo Madema;
- (e) Kutoa huduma kwa watoto wanaolelewa Mazizini na kutayarisha na kuendesha nyumba salama kwa wahanga wa udhalilishaji wenye kuhitaji hifadhi; na
- (f) Kusimamia uendeshaji wa vituo binafsi vya kulelea watoto ili kutoa malezi bora kwa mujibu wa sheria.

### **Vijana**

209.

**Katika miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), CCM iliielekeza SMZ kutatua changamoto zinazowakabili vijana hasa ukosefu wa ajira, kukosa ujuzi na maarifa ya kisasa na mitaji na hivyo kushindwa kushiriki vyema katika kujenga uchumi. Kwa kutambua azma ya CCM ya kukabiliana na matatizo ya vijana SMZ ilichukua juhudi kubwa kuwawezesha vijana kuwajengea uwezo na kuwapa hamasa ya kujituma kwa kutukeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuwawezesha vijana 3,050 kwa kuwapatia vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 5 kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji, ushonaji, uchongaji, michezo, sanaa na mafunzo mbalimbali ya stadi za kazi;
- (b) Kuliimarisha baraza la vijana na jumuiya za vijana za shehia, wilaya na Taifa kwa kuwapatia mafunzo, vifaa na vitendea kazi;
- (c) Kutoa elimu ya stadi za maisha kwa vijana 220,738 kuhusu madhara ya mimba na ndoa za umri mdogo, mafunzo ya afya ya uzazi, elimu ya UKIMWI, madawa ya kulevya, mimba za utotoni mafunzo haya yalitolewa Unguja na Pemba;
- (d) Kuwajengea uwezo viongozi 2,689 wa Baraza la Taifa la Vijana ili kuongeza ufanisi na ushiriki wa vijana katika shughuli za uchumi na kijamii;
- (e) Kuwaunganisha vijana katika Mfuko wa Uwezeshaji na Programu za Ajira za wadau mbali mbali, ambapo jumla ya vijana 730 wamewezeshwa katika maeneo ya ufugaji wa kuku, nyuki na samaki. Vile vile, vijana 40 wamepatiwa ujuzi wa kutumia kilimo cha kisasa kupitia programu ya kilimo endelevu “Fursa Kijani”;
- (f) Kutoa mafunzo kazi kwa vijana 660 katika vyuo vya Amali Mwanakwereke, Mkokotoni, Vitongoji pamoja na Chuo cha Polisi Ziwani mafunzo hayo yanahusisha uchongaji, uchomaji na ushonaji. Aidha, vijana 140 kutoka baraza la vijana wamepatiwa mafunzo katika nyanja tofauti ili waweze kujitegemea kiuchumi;
- (g) Kushajiisha vijana kushiriki katika shughuli mbalimbali za kitaifa na kimataifa na kuwajengea moyo wa uzalendo kwa kushiriki katika matukio mbalimbali yakiwemo mbio za Mwenge, kumbukizi za Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume pamoja na kuandaa Makongamano matano na bonanza moja, na vijana 15,596 kushiriki katika shughuli hizo;



- (h) Kuyajengea uwezo mabaraza ya vijana ili yaendeele kufanya majukumu yao ipasavyo katika ngazi zote kitaifa na kimataifa; na
- (i) Kushajiisha vijana 1,120 kujiunga na programu ya *U report* (Jukwaa la vijana kutoa maoni kupitia mtandao) katika wiki ya vijana na kumbukumbu ya Baba wa Taifa na Vijana 1,300 walijiunga na jukwaa hilo.

**210. CCM inatambua kuwa vijana wanaunda kundi kubwa la nguvu kazi na lenye msukumo katika maendeleo ya nchi. Hata hivyo, kundi hili linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa ajira na kukosa elimu na huduma muhimu za afya. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kuendelea kulitilia maanani suala la vijana katika mipango yake ya maendeleo kwa kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuwa na sera rafiki kwa masuala ya vijana na sheria kuhusu ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa;
- (b) Kupeleka vijana 47,000 katika vituo vya mafunzo vya amali kupata elimu ya ufundi, kazi za mikono, ujasiriamali na sanaa;
- (c) Kuwapatia vijana 5,000 mafunzo ya uongozi na usimamizi wa fedha, utalii, uandishi wa miradi, usimamizi na uendelezaji wa miradi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali;
- (d) Kuwahamasisha vijana 20,000 waliomaliza vyuo kuanzisha vikundi vya uzalishaji mali na utoaji huduma, kuvipatia mafunzo na mikopo ili waweze kujijajiri;
- (e) Kuandaa mazingira bora ya kisera, kisheria na mipango katika kuwajenga, kuwahamasisha na kuwabadilisha vijana kifikra ili kujihusisha katika uzalishaji mali na utoaji wa huduma kwa ajili ya kuongeza pato binafsi na Taifa;
- (f) Kutoa taaluma kwa vijana kuhusu matumizi sahihi ya sayansi na teknolojia na kuanzisha vituo vya ubunifu wa teknolojia ya habari, uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo na utengenezaji wa vifaa mbalimbali vya kuleta maendeleo; na
- (g) Kuandaa na kutekeleza programu za elimu na malezi kwa vijana 100,000 pamoja na mikakati ya kujenga moyo wa uzalendo, ari ya kujitolea na kuipenda nchi yao.

**Wanawake**

**211. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 – 2020), CCM iliisimamia SMZ kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu katika kusukuma kasi ya maendeleo na kuleta mageuzi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa ambapo mafanikio makubwa yamepatika kama ifuatavyo:-**



- (a) Kusimamia upatikanaji wa haki ya kulindwa dhidi ya ubaguzi, udhalilishaji, dhulma, unyanyasaji, ukatili wa kijinsia na mila potofu;
- (b) Kutoa elimu ya uelewa juu ya dhana ya udhalilishaji, athari zake na jinsi ya kujikinga na vitendo hivyo hasa kwa wanawake na watoto;
- (c) Kuandaa na kutekeleza mpango kazi wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto; na
- (d) Kuendelea kuchukua hatua za kufikia lengo la uwiano wa asilimia 50:50 katika nafasi za uongozi.

**212. CCM inatambua uwezo mkubwa wa wanawake wa kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi, hivyo Chama kitaendelea kuielekeza SMZ kuweka mkazo katika kushirikisha wanawake katika shughuli za kimaendeleo kwa kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake katika masuala ya maendeleo;
- (b) Kuanzisha mfuko maalum wa uwezeshaji wanawake utakaowawezesha kupata mikopo ya gharama nafuu;
- (c) Kusimamia upatikanaji wa haki za wanawake na kupiga vita mila na desturi zinazowabagua au kudhalilisha wanawake na kusimamia utekelezaji wa sheria na mikataba ya kimataifa inayohusu ustawi wa mwanamke; na
- (d) Kutekeleza mkakati wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhini ya wanawake na watoto.

**Wazee**

**213. Katika miaka mitano iliyopita, CCM, kupitia SMZ, iliendelea kuwatunza wazee wote kwa kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuanzisha mpango wa pensheni jamii kwa wazee wenye umri wa miaka 70 na kuendelea na kuwalipa wazee shilingi 20,000 kwa kila mwezi ili kusaidia huduma zao za kila siku. Jumla ya wazee 22,273 (Unguja 12,722 na Pemba 8,541) wamesajiliwa. Aidha, mfumo wa kuweka kumbukumbu za wazee (*database*) umeimarishwa;
- (b) Kuchapisha vitambulisho 2,314 (1,284 Kusini, 497 Magharibi A na 533 Magharibi B) vya wazee wanaopatiwa Pensheni ili kurahisisha kupata huduma za kijamii ikiwemo matibabu na usafiri;
- (c) Kuimarisha huduma za wazee wanaoishi katika Makao ya Wazee Sebleni, Welezo na Limbani kwa kupatiwa chakula pamoja na matibabu; na



- (d) Kuendelea kutekeleza sera ya hifadhi ya jamii, kutunga na kuanza kutekeleza Sheria ya Kuwalinda na Kuwatunza Wazee ya Mwaka 2019.

214.

**CCM inatambua umuhimu wa wazee katika Taifa letu na itaendelea kuwapatia huduma za kijamii na kisheria. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuimarisha huduma za jamii na mahitaji muhimu kwa wazee wanaotunzwa katika nyumba za wazee;
- (b) Kufanya matengenezo ya nyumba ya wazee iliyo Sebleni na kujenga uzio wa Makao ya Wazee Welezo;
- (c) Kutekeleza mpango wa pencheni jamii kwa wazee wenye umri wa miaka 70 na kuendelea kwa kuongeza bajeti ya mpango kutoka shilingi bilioni 6.5 hadi shilingi bilioni 7 kwa ajili ya malipo ya wazee walioongezeka Unguja na Pemba;
- (d) Kuweka mifumo ya kutoa kipaumbele maalum kwa wazee katika kupata huduma za jamii; na
- (e) Kuratibu zoezi la kusajili wazee na kutoa mafunzo kwa watendaji juu ya utoaji bora wa huduma na malipo kwa wazee.

**Watu Wenye Ulemavu**

215.

**Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 – 2020), CCM kupitia SMZ iliweka kipaumbele kuweka mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu na kupata mafanikio makubwa yafuatayo:-**

- (a) Kuzipatia ruzuku jumuiya 40 za watu wenye ulemavu Zanzibar. Vikao 16 vya Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu na vikao 16 vya maafisa waratibu wa masuala ya watu wenye ulemavu vimefanyika;
- (b) Kuanzisha mfumo wa takwimu (JUMUISHI DBASE) za watu wenye ulemavu kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa za watu wenye ulemavu na kufanya maboresho katika mfumo wa ukusanyaji taarifa zao kupitia mfumo wa simu (*mobile application*);
- (c) Kuanzisha kituo cha kuhifadhi taarifa za watu wenye ulemavu (*Zanzibar Disability Data Centre*) kwa lengo la kuhifadhi taarifa na kuunganisha mfumo wa TEHAMA wa JUMUISHI DBASE na kujiweka katika kituo ili kukuza urahisi wa kutumia taarifa hizo kwa kuwapatia haki zao zikiwemo visaidizi, elimu, afya, ajira na ujasiriamali;
- (d) Kuandaa Mpango Mkakati wa Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu pamoja na Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Watu Wenye Ulemavu na kutafsiri sera hiyo kwa lugha ya Kiswahili ili kurahisisha uratibu wa masuala ya watu wenye ulemavu na kufikia Dira ya 2020 ya Zanzibar; na

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMCOA



- (e) Kufanya upembuzi yakinifu juu ya vijana wenye ulemavu katika masuala ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango ili kujua kwa kiasi gani vijana wenye ulemavu wanapata haki hiyo.

216. **Chama kinaamini kwamba watu wenye ulemavu ni kundi maalum linalohitaji kupewa kipaumbele katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, CCM itaelekeza SMZ kuendelea kulinda haki za watu wenye ulemavu kwa kutekeleza yafuatao:-**

- (a) Kutatua changamoto za watu wenye ulemavu nchini kwa kuhakikisha inaratibu kikamilifu masuala ya watu wenye ulemavu;
- (b) Kutekeleza sheria na kanuni zinazowalinda na kuelekeza namna ya kuwahudumia watu wenye mahitaji maalum; na
- (c) Kuwawezesha kwa kuwapa mtaji na maarifa watu wenye ulemavu bila kubagua jinsia na aina ya ulemavu walionao.

### **Wafanyakazi**

217. **Katika miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), CCM kupitia SMZ ilifanya mageuzi makubwa katika nyanja ya utumishi wa umma na binafsi na kupelekea wafanyakazi kuwa ari na moyo wa kufanya kazi, hivyo kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo:-**

- (a) Kuimarisha mashirikiano ya UTATU kupitia vyombo vya UTATU - yaani Serikali, Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi na Jumuiya ya Waajiri;
- (b) Kuratibu shughuli za Wakala Binafsi wa Ajira ili kuhakikisha kuwa sheria za kazi zinafuatwa;
- (c) Kurusha kupitia redio na televisheni vipindi 26 vinavyohusiana na mambo ya usalama na afya kazini vilirushwa hewani kupitia redio tofauti;
- (d) Kuajiri vijana 16,675 katika taasisi za umma. Aidha, watumishi 938 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi (868) na muda mrefu (70) nje ya nchi;
- (e) Kufanya marekebisho ya mishahara na posho kwa watendaji wakuu na watumishi wa kawaida katika wizara, mashirika na taasisi zinazojitegemea kwa kuongeza kima cha chini cha mishahara kutoka shilingi 150,000 hadi shilingi 300,000;
- (f) Kuongeza kiwango cha pensheni kwa wastaafu wa kawaida kutoka shilingi 40,000 hadi shilingi 90,000 sawa na ongezeko la asilimia 125; na
- (g) Kuimarisha taasisi za usuluhishi migogoro kazini pamoja na kupanua shughuli za usalama na afya kazini ili kuzifikia sekta zote za kiuchumi.



218. **Maendeleo ya Zanzibar yanategemea sana juhudi na nidhamu za wafanyakazi katika sekta ya Umma na Binafsi. Kuendeleza kundi la wafanyakazi ni chachu ya uwajibikaji kwao na ufanisi sehemu za kazi. Kwa kutambua umuhimu wa wafanyakazi CCM itaelekeza SMZ kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuboresha ushirikiano na jumuiya za wafanyakazi na waajiri na kuweka mfumo imara kwa kupanga biashara katika sekta binafsi ili kuyaimarisha masilahi ya wafanyakazi kwa kuhakikisha kwamba mfanyakazi atalipwa kima cha chini cha mshahara kinachokidhi mahitaji muhimu ya maisha kwa kuzingatia uwezo wa Taifa kiuchumi;
- (b) Kuhakikisha kunakuweko jumuiya imara za waajiri na wafanyakazi ili kukuza utatu, majadiliano ya pamoja na kuleta tija na mustakabali mzuri katika kutetea haki na masilahi ya wafanyakazi na waajiri;
- (c) Kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi juu ya haki na wajibu wanapokuwa katika sehemu zao za kazi;
- (d) Kuwaendeleza watumishi wa umma wapatao 2,700 katika fani na ngazi mbalimbali kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na maarifa ya utendaji kazi ili waweze kutoa huduma bora na zenye tija kwa umma;
- (e) Kupanua shughuli za usalama na afya kazini ili kuzifikia sekta zote za kiuchumi; na
- (f) Kuboresha mazingira na masilahi ya watumishi wa umma kadri hali ya uchumi inavyoruhusu.

### **Hifadhi ya Jamii**

219. **Ili kuhakikisha kwamba huduma za hifadhi ya jamii zinaimarika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), mafanikio yafuatayo yamepatikana:-**

- (a) Mfuko umeimarisha mafao ya wanachama wake kwa kuimarisha huduma na kuongeza kiwango cha malipo cha kiinua mgongo;
- (b) Kuongezeka kwa idadi ya wanachama waajiri kutoka 1,282 kwa mwaka 2015 hadi 1,963 mwaka 2020. Kwa upande wa wanachama waajiriwa, idadi imeongezeka kutoka 73,137 kwa mwaka 2015 hadi kufikia 96,844 mwaka 2020;
- (c) Kuongeza kwa michango ya wanachama kutoka shilingi bilioni 30.3 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 76 mwaka 2020;
- (d) Kulipa kwa wakati mafao ya pensheni kutoka shilingi 2.7 bilioni mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 17.6 mwaka 2020. Aidha, malipo





ya kiinua mgongo yameongezeka kutoka shilingi bilioni 9.6 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 17.6 mwaka 2020;

- (e) Kuanzisha mfuko wa fao la uzazi kwa wanachama wake ambapo fedha za mafao ya uzazi zimeongezeka kutoka shilingi milioni 95.9 mwaka 2015 hadi shilingi milioni 213.5 mwaka 2020;
- (f) Kuazisha mfuko wa uchangiaji wa hiari unaojulikana kwa jina la Mfuko wa Hiari (VSSS) unaojumuisha wafanyakazi katika sekta isiyo rasmi;
- (g) Kuanzisha utaratibu wa kutoa mikopo kwa wastaafu wake kwa kushirikiana na benki za TPB na NMB;
- (h) Kurahisisha utoaji huduma ili kupunguza na kuondoa usumbufu kwa wateja kwa kuanzisha dirisha maalum la kuhudumia wateja na hivyo kupunguza muda wa kusubiri huduma na kuanzisha “*mobile application*” ambapo mwanachama anaweza kuangalia michango yake kwa kutumia simu yake ya mkononi;
- (i) Kuongeza mapato ya uwekezaji kutoka shilingi bilioni 21.3 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 39.3 mwaka 2020. Aidha, thamani ya Mfuko imeongezeka kutoka shilingi bilioni 206.8 hadi shilingi bilioni 451 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 118;
- (j) Kuwekeza katika miradi ya maendeleo na kijamii ikiwemo ujenzi ya *Michenzani Mall, Sheikh Thabit Kombo Building*, matengenezo ya hoteli ya Mkoani Pemba, jengo la maegesho Michenzani, ujenzi wa majengo 15 yenye ghorofa saba kila moja, jumba la Treni “*Chawl Building*” Darajani na kununua nyumba iliyokuwa “*High Hill Hotel*” iliyopo Kilimani Mnara wa Mbao na kiwanja katika eneo la Kigamboni Dar-es-Salaam.

**220. Kutokana na umuhimu wa hifadhi ya jamii kwa wananchi CCM katika miaka mitano ijayo itaelekeza SMZ kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kusimamia utekelezaji wa sera na sheria ya hifadhi ya jamii kwa manufaa ya wanachama wote na Taifa kwa ujumla;
- (b) Kujenga majengo ya makaazi na biashara katika eneo la Mombasa Unguja;
- (c) Kuongeza kiwango cha usajili wa wanachama hadi kufikia asilimia 50 ya wanachama wanaoweza kufanya kazi;
- (d) Kufungua ofisi za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii katika mikoa ya Zanzibar; na
- (e) Kuanzisha mafao mapya kama vile mafao ya matibabu na kupunguza muda wa kulipa mafao kufikia wiki mbili.



## SURA YA TISA

### MAENEO MENGINE YA KIPAUMBELE

#### Uamuzi wa Kuhamia Dodoma

221.

**Chama Cha Mapinduzi kimefanikiwa kuyaenzi maono ya Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya kuhamishia Makao Makuu ya nchi katika mji wa Dodoma. Maono hayo yametekelezwa kwa ufanisi mkubwa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kutekeleza azma hiyo, mafanikio yafuatayo yamepatikana:-**

- (a) Kuweka jiwe la msingi na kuanza ujenzi wa miundombinu ya barabara, ukuta, majengo ya ofisi na nyumba za makazi kwenye eneo la Ikulu ya Chamwino;
- (b) Kuwezesha Makao Makuu ya Nchi kuwa ya kisasa kwa kuandaliwa na kutekelezwa kwa Mpango Kabambe wa kuendeleza jiji la Dodoma;
- (c) Kuhamishwa kwa taasisi za umma kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma. Taasisi hizo ni: Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC); Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAO); Tume ya Kurekebisha Sheria; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP); Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa; Mamlaka ya Udhhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA); Wakala wa Huduma za Ajira (TAESA); Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS); Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF); Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF); Wakala ya Serikali Mtandao (eGA); Idara ya Kumbukumbu za Taifa; Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB); na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF);
- (d) Kukamilishwa kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa ofisi za Serikali jijini Dodoma katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba ambapo ujenzi wa majengo 23 ya wizara na taasisi mbili umekamilika;
- (e) Kuanza ujenzi wa barabara za kiwango cha lami katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba zenye urefu wa kilomita 39.9 ili kuboresha mazingira na kurahisisha usafiri katika eneo hilo;
- (f) Kuhamisha watumishi 15,361 kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma wanaojumuisha watumishi kutoka wizara zote, Bunge, Ofisi ya Rais, Ikulu na taasisi zake, vyombo vya ulinzi na usalama na baadhi ya taasisi za Serikali;



- (g) Kuhamishwa kwa ofisi za vyombo vya ulinzi na usalama kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma;
- (h) Kuipatia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Hati Miliki ya kiwanja chenye ukubwa wa hekta 33 ili kuhamishia ofisi zake za uratibu kwenye jiji la Dodoma; na
- (i) Kuwezesha ofisi za ubalozi na mashirika ya kimataifa kuhamia Dodoma kwa kuzipatia hati miliki 62 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za kibalozu na tano kwa ajili ya taasisi za kimataifa zenye hadhi ya kidiplomasia.

**222. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuhakikisha kwamba Makao Makuu Dodoma yanaboreshwa zaidi ikiwa ni pamoja na kuwezesha kujengwa kwa miundombinu mbalimbali ya utoaji huduma za kijamii na kiuchumi. Miundombinu hiyo ni pamoja na barabara, nyumba za makazi, majengo ya ofisi za serikali na balozu za nchi mbalimbali na huduma za jamii. Ili kufikia azma hiyo, Chama kitaelekeza Serikali kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya barabara, majengo ya ofisi na nyumba za makazi kwenye eneo la Ikulu ya Chamwino;
- (b) Kuanza na kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa ofisi za Serikali katika Mji wa Serikali Dodoma;
- (c) Kujenga nyumba nyingi zaidi za viongozi na watumishi katika makao makuu ya nchi Dodoma;
- (d) Kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama katika jiji la Dodoma kwa kutekeleza mikakati ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ikiwa ni pamoja na kujenga Bwawa la Farkwa;
- (e) Kuboresha upatikanaji wa huduma za majitaka katika jiji la Dodoma;
- (f) Kuboresha huduma za umeme kwa kuongeza na kuimarisha miundombinu kwa ajili ya mahitaji ya sasa na baadae;
- (g) Kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa lengo la kurahisisha usafiri ndani ya jiji la Dodoma ikiwa ni pamoja na:-
  - (i) Ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje (outer ring road) yenye urefu wa Km 110 ambapo itapita katika maeneo ya Mtumba - Barabara ya Morogoro, Veyula - Barabara ya Arusha, Nala - Barabara ya Singida na Matumbulu - Barabara ya Iringa;
  - (ii) Ujenzi wa barabara za mzunguko wa ndani (*inner ring roads*) zenye urefu wa Km 39 kutoka barabara ya mzunguko wa



Airport (Barabara ya Arusha) - Mzunguko wa Shabiby (Barabara ya Morogoro) - barabara mpya kutoka Ihumwa (Barabara ya Morogoro) - Chinyoya- Kikuyu (Barabara ya Iringa) - Barabara ya Nanenane (Barabara ya Morogoro) - Miyuji (Barabara ya Arusha) - Mkonze (Barabara ya Iringa) na barabara ya Emmaus (Barabara ya Morogoro) - Mlimwa (Makazi ya Waziri Mkuu) Wajenzi (Barabara ya Arusha); na

- (iii) Kukamilisha ujenzi wa barabara za kiwango cha lami katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba ili kuboresha mazingira na kurahisisha usafiri katika eneo hilo.
- (h) Kutekeleza ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano ili kuboresha huduma ya mawasiliano katika Mji wa Serikali kwa kujenga mkongo wa mawasiliano (*optic fiber distribution network*) na kuboresha huduma ya mawasiliano jijini Dodoma;
- (i) Kuanza ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Msalato kwa ajili ya kuboresha usafiri wa anga katika jiji la Dodoma;
- (j) Kuendelea kuimarisha huduma za afya katika jiji la Dodoma kwa:-
  - (i) Kuongeza vituo vipya vitano ambavyo ni Zepisa, Chididino, Mpamaa, Makutupora na Tambukareli;
  - (ii) Kuanza ujenzi wa vituo vipya vya afya viwili vya Chang'ombe na Nala pamoja na Zahanati itakayojengwa katika Kata ya Zuzu;
  - (iii) Kuanza ujenzi wa Hospitali ya Uhuru Dodoma; na
  - (iv) Kutekeleza Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma (2019 – 2039) ambao katika sekta ya afya unalenga kuongeza zahanati 456, vituo vya afya 114 na hospitali 29.
- (k) Kuendeleza ujenzi wa taasisi za elimu zikiwemo shule za sekondari, vyo vya elimu ya kati na juu kwa ajili ya kuboresha huduma za elimu katika jiji la Dodoma.
- (l) Kutekeleza mpango kwa kujenga nyumba za makazi na biashara ili kutatua changamoto ya makazi;
- (m) Kutekeleza mpango wa kukopesha nyumba kwa mikopo ya riba nafuu na kuweka miundombinu muhimu katika eneo la mradi;
- (n) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya nyumba usiopitia Benki (*Tenant Purchase*) Mkopo wa aina hii mnunuzi wa nyumba analipa malipo yanayofanana na kodi ya nyumba na hatimaye anamiliki nyumba anayokaa;



- (o) Kutekeleza mradi ujulikanao kama (*smart village*) kwa ajili ya makazi ya kisasa;
- (p) Kuhamasisha taasisi za ndani, taasisi za kimataifa na mabalozi wa nchi mbalimbali kuhamishia makao makuu yake katika jiji la Dodoma; na
- (q) Kujenga nyumba za Makazi ya *villa type* na maghorofa kwa kutumia teknolojia ya kujenga haraka (*tunnel form technology*).

### **Ulinzi na Uendelezaji wa Rasilimali za Taifa**

223.

Nafasi ya nchi yetu kijiografia ni mojawapo ya fursa ya kipekee kwa maendeleo ya nchi yetu. Nafasi hiyo imeiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa na rasilimali nyingi ambazo ni msingi mkuu wa maendeleo na tegemeo kwa Taifa letu. Rasilimali hizo ni pamoja na mbuga za wanyama, maziwa makuu, Bahari ya Hindi, ardhi kubwa yenye rutuba, rasilimaliwatu ya kutosha na madini. Jukumu la kulinda rasilimali hizo ni la kila Mtanzania ili kuhakikisha zinatumiwa kwa vizazi vya sasa na vijavyo. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 – 2020), Chama Cha Mapinduzi kupitia Serikali kilichukua hatua mbalimbali katika kuzilinda rasilimali hizo. Kufuatia hatua hiyo, nchi yetu imepata mafanikio yafuatayo:-

- (a) Kuongezeka kwa wanyamapori na ushiriki wa wananchi katika umiliki wa madini;
- (b) Kuboreshwa kwa mifumo na miundo ya taasisi katika kusimamia rasilimali za Taifa;
- (c) Kuzijengea uwezo taasisi mbalimbali na rasilimaliwatu katika kusimamia rasilimali za Taifa;
- (d) Kubuni na kutekelezwa kwa mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa rasilimali hizo katika maeneo mbalimbali;
- (e) Kuimarishwa kwa usimamizi wa utajiri na maliasili za nchi kwa kutungwa Sheria ya *The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act 2017 (Permanent Sovereignty Act)* na kuwezesha majadiliano kwenye mikataba ya uwekezaji yenye masharti hasi ili yaondolewe na mikataba hiyo iwe kwa manuafaa ya pande zote kwa kutungwa Sheria ya *The Natural Wealth and Resources (Review and Re-Negotiations of Unconscionable Terms) Act 2017 (Contract Review Act)*; na
- (f) Kuongezeka kwa utashi wa kisiasa katika kulinda rasilimali za Taifa.

224.

**Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuhakikisha kuwa rasilimali za Taifa zinalindwa kwa masilahi mapana ya Taifa letu. Ili kutimiza lengo hilo, Chama kitaelekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:-**



- (a) Kusimamia utekelezaji wa sheria ya kulinda rasilimali za Taifa (*The Natural Wealth and Resources – Permanent Sovereignty - Act 2017*) na kuboresha sera na sheria zinazohusu ulinzi, uendelezaji na uwekezaji katika rasilimali za Taifa;
- (b) Kusimamia utekelezaji wa sheria ya kuwezesha majadiliano kwenye mikataba ya uwekezaji na maliasili za nchi *The Natural Wealth and Resources (Review and Re-negotiation of Unconscionable Term Act, 2017)* yenye masharti hasi ili yaondolewe;
- (c) Kuboresha sera, sheria na miongozo mbalimbali inayohusu ulinzi, uendelezaji na uwekezaji katika rasilimali za Taifa;
- (d) Kuhakikisha kuwa maeneo yenye rasilimali za Taifa yanabainishwa, yanalindwa na yanaendelezwa ili kuleta manufaa stahiki kwa Taifa;
- (e) Kujenga uwezo wa taasisi na rasilimaliwatu katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za Taifa;
- (f) Kubuni na kutekeleza mikakati madhubiti katika kulinda na kuendeleza rasilimali za Taifa; na
- (g) Kuhakikisha kuwa mikataba ya uendelezaji wa rasilimali ina manufaa kwa Taifa na wananchi ikiwa ni pamoja na uongezaji thamani ya rasilimali hizo.

### **Kudumisha Muungano**

225. Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kuthamini na kudumisha Muungano wetu ambao ni wa kipekee na kihistoria, uliunganisha nchi mbili zilizokuwa huru za Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Muungano huu ni nguzo ya umoja, mshikamano, amani na utulivu wa wananchi wa pande zote mbili. Kutokana na umuhimu huo, Chama kimeendelea kuzielekeza serikali zake kuchukua hatua za kuulinda na kuenzi Muungano wetu ambao ni adhimu na adimu kwa lengo la kuwawezesha wananchi kufurahia matunda yake.

226. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015-2020), mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongeza fursa za majadiliano ili kuimarisha ushirikiano wa pande zote mbili kwa manufaa ya Watanzania wote. Aidha, hatua hizo zimeongeza wigo wa mashirikiano kwa kuongeza nafasi kubwa ya kubadilishana ujuzi, utaalum na uzoefu kupitia mafunzo, masuala ya sera na ushiriki katika masuala ya kimataifa. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na:-

- (a) Kuwepo kwa vikao vya mara kwa mara vya kisekta katika ushirikiano na kujadili masuala mbalimbali yenye manufaa kwa Muungano kama vile nishati, maji, madini, uchukuzi, utumishi na utawala bora, viwanda na biashara, maliasili na utalii, afya, maendeleo ya jamii, serikali za mitaa, kilimo, habari, utamaduni, sanaa na michezo, ardhi, elimu, fedha na mipango na mazingira;





- (b) Kufanya ziara za kikazi katika taasisi za Muungano na zisizo za Muungano kwa lengo la kujifunza utendaji kazi wa taasisi hizo kwa manufaa ya pande zote mbili;
- (c) Kuandaliwa kwa utaratibu maalum wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ mwaka 2019 vya kushughulikia masuala ya Muungano. Kutokana na utaratibu huu zimeundwa kamati ndogo mbili ambazo ni Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara; na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ili kushughulikia masuala mbalimbali katika maeneo hayo;
- (d) Kufanyika marekebisho ya gharama za umeme kutoka TANESCO kwenda ZECO kwa kufuta kodi ya ongezeko la thamani na malimbikizo ya deni la kodi hiyo lenye thamani ya shilingi bilioni 22.9;
- (e) Kupitishwa kwa Mwongozo Kuhusu Ushiriki wa SMZ katika masuala mbalimbali ya kimataifa na kikanda kwa lengo la kuongeza nafasi za masomo ya elimu ya juu na mafunzo mengine nje ya nchi na utafutaji wa fedha za misaada na mikopo ya kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo;
- (f) Kufikia maridhiano ya masuala mbalimbali yakiwemo utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asili; gharama za kushusha mizigo (*landing fees*); upatikanaji wa fursa za ushiriki katika miradi ya maendeleo ya viwango na ubora wa bidhaa; na maendeleo ya wajasiriamali;
- (g) Kuibua, kutekeleza na kufuatilia utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ya Muungano kama vile Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA); Mpango wa Kupanua Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania; Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*Tanzania Social Action Fund -TASAF*); na Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi Kanda ya Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (*South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth - SWIOFISH*); na
- (h) SMZ imeendelea kupata gawio la asilimia 4.5 ya fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, PAYE, gawio la faida ya Benki Kuu ya Tanzania na fedha za Misaada ya Kibajeti.

227. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, lengo la Chama Cha Mapinduzi ni kuendelea kuimarisha na kudumisha Muungano wa Serikali mbili kwa ajili ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo. Ili kufikia lengo hilo, Chama kitazielekeza serikali zake kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kuhakikisha ushirikiano wa wizara/idara na taasisi zisizo za muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika mambo yasiyo ya muungano unaendelea kuimarishwa;



- (b) Kuimarisha uratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ vya kushughulikia masuala ya muungano kwa lengo la kutatua changamoto kwa kasi zaidi;
- (c) Kuhakikisha masuala muhimu ya muungano yanaratibiwa kwa faida ya pande mbili; na
- (d) Kuimarisha utoaji elimu ya muungano kwa umma wa Watanzania ili kuendelea kujenga ari ya kuulinda, kuutetea, kuuenzi na kuuimarisha.

### **Maendeleo ya Jamii**

228.

Chama Cha Mapinduzi kinatambua umuhimu wa sekta ya maendeleo ya Jamii kama chachu ya fikra za kimaendeleo zinazohitajika kuwezesha wananchi kutumia fursa zilizopo kujiletea maendeleo yao na kushiriki katika shughuli za ujenzi wa Taifa. Aidha, sekta hii ni nyenzo muhimu katika kuiandaa jamii kukabiliana na mabadiliko na changamoto mbalimbali zinazojitokeza nchini na duniani. Katika kipindi cha (2015 – 2020), miongoni mafanikio yaliyopatika katika sekta hii ni pamoja na yafuatayo:-

- (a) Kuongeza ushiriki wa jamii katika shughuli za maendeleo katika sekta mbalimbali;
- (b) Kuwezesha jamii kushiriki na kufanikisha miradi ya maendeleo ikiwemo kaya 617,100 kuboresha vyoo, kaya 305,724 kuboresha maeneo ya kunawa mikono, kujengwa madarasa shule za msingi 6,521 na sekondari 2,499, hospitali 67 za halmashauri na miradi mingine vijijini na mijini;
- (c) Kutoa mafunzo ya kada ya maendeleo ya jamii kwa vyuo nane vya maendeleo ya jamii na taasisi ya maendeleo ya jamii Tengeru ambapo wanafunzi 14,327 wamedahiliwa. Aidha, wanafunzi 9,489 walihitimu masomo yao kwa kipindi hicho;
- (d) Kuboresha mazingira ya kujifunzia katika vyuo vya maendeleo ya jamii kwa kujenga na kukarabati kumbi za mihadhara, hosteli, majengo ya utawala, nyumba za watumishi, madarasa, maktaba, uzio, miundombinu ya majisafi, majitaka na mifumo ya umeme;
- (e) Kuanzisha na kutekeleza mpango wa kuhamasisha maendeleo ya jamii katika maeneo mbalimbali nchini hasa jamii zinazozunguka vyuo hivyo. Hatua hii imechochea ufanisi katika miradi ikiwemo ufugaji na kilimo cha kisasa, usindikaji wa mazao, utunzaji wa mazingira, lishe bora, miradi ya ujenzi wa zahanati na ofisi ya kijiji pamoja na kutoa elimu ya kupambana na changamoto mbalimbali ikiwemo kukabiliana na watoto walio katika ajira;

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA



- (f) Kuanzisha vituo vya kitaifa vya kidijitali vya ubunifu na maarifa vitakavyopokea na kulea wabunifu kutoka kwenye vituo vya kidijitali vya ubunifu na maarifa viliopo kwenye Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na vyo nane vya maendeleo ya jamii kwa lengo la kukuza vipaji vya kibunifu katika jamii ili kuwaendeleza vijana waweze kuchangia maendeleo ya Taifa kwa kuzalisha teknolojia zinazohitajika katika maendeleo ya viwanda, usindikaji wa mazao na bidhaa mbalimbali;
- (g) Kuanzisha mpango wa wahitimu wa vyo kufanya kazi kwa kujitolea kwa lengo la kuwapatia uzoefu na maadili ili waweze kuajiriwa na kujiajiri wenyewe kwa kutumia fursa zilizopo; na
- (h) Kuwezesha vitendea kazi kwa wataalam wa maendeleo ya jamii ili waweze kutimiza wajibu wao vizuri.

**229. Katika miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha Serikali inajenga jamii iliyoelimika, kujiamini na inayomudu kupata mahitaji ya msingi na kuchangia ipasavyo katika ajenda ya maendeleo, ili kufikia azma ya kuwa na jamii na Taifa linalojitegemea. Chama kitaelekeza Serikali kuongeza tija kwenye sekta ya maendeleo ya jamii kwa kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuimarisha jitihada za kukuza ari ya jamii, uzalendo na kujenga moyo wa kujitolea na kufanya kazi kwa bidii ili kujitelea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kutumia nguvukazi na rasilimali zinazowazunguka;
- (b) Kuwezesha Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na vyo vya maendeleo ya jamii kutekeleza mpango wa mafunzo kwa vitendo (uanagenzi) ili wahitimu wa taaluma ya maendeleo ya jamii wawe na ujuzi utakaowawezesha kuwa na sifa na uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa;
- (c) Kuanzisha kituo cha Kitaifa cha Kidigitali cha Ubunifu na Maarifa kitakachopokea na kulea wabunifu kutoka kwenye vituo vya kidigitali vya ubunifu na maarifa viliopo kwenye Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na vyo nane vya maendeleo ya jamii kwa lengo la kukuza vipaji vya ubunifu katika jamii na kuwajengea uwezo wa kujiamini, kuajiriwa na kujiajiri ili kuchangia maendeleo ya Taifa kwa kuzalisha teknolojia zinazohitajika katika maendeleo ya viwanda, usindikaji wa mazao na bidhaa mbalimbali;
- (d) Kushirikisha jamii kutoa suluhisho kwa changamoto zinazoikabili na kutumia fursa zilizopo kwa maendeleo yao;
- (e) Kukarabati na kujenga miundombinu ya Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na vyo nane vya maendeleo ya jamii ili kuongeza udahili wa wanafunzi;



- (f) Kuanzisha mpango wa wahitimu wa vyuo kufanya kazi kwa kujitolea kwa lengo la kuwapatia uzoefu na maadili ili waweze kuajiriwa na kujiajiri wenyewe kwa kutumia fursa zilizopo;
- (g) Kuratibu na kuweka mazingira wezeshi ya kuendeleza huduma atamizi na uwezeshaji kiuchumi kwa makundi ya jamii yakiwemo ya vijana, wanawake na wazee; na
- (h) Kuhamasisha jamii kuwa na makazi bora na yanayotumia teknolojia rahisi na gharama nafuu katika maeneo yote nchini.

### **Usawa wa Jinsia**

230.

Chama Cha Mapinduzi kinatambua umuhimu wa kuwa na usawa wa kijinsia kama sehemu ya utekelezaji wa imani yake kuwa binadamu wote ni sawa na wanastahili heshima na fursa sawa. Serikali imeendelea kuongeza jitihada katika kujenga jamii inayozingatia usawa wa jinsia. Katika kipindi cha (2015 – 2020), miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na yafuatayo:-

- (a) Kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa wanawake kupitia vyanzo mbalimbali ikiwemo mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 39.7 imetolewa kwa wanawake wajasiriamali 877,071 kupitia asilimia 4 ya mapato ya ndani ya halmashauri. Aidha, shilingi bilioni 2.1 zimetolewa kwa wanawake wajasiriamali 3,035 kupitia dirisha la wanawake katika Benki ya Posta Tanzania;
- (b) Kuondoa kero kwa wajasiriamali wakiwemo mama lische na wauza mbogamboga kwa kupatiwa maeneo rasmi ya kufanyia biashara yenye ukubwa wa hekta 15,822.64 katika halmashauri 150 nchini. Aidha, jumla ya kodi, ada na tozo 108 kati ya 139 zimefutwa ili kupunguza kero kwa wajasiriamali wakiwemo wanawake;
- (c) Kuhamasisha wanawake kujiunga na SACCOS na VICOBA ambapo zaidi ya SACCOS 130 za wanawake zimeanzishwa;
- (d) Kutoa fursa kwa wanawake kuongeza ubora wa bidhaa zao na masoko kwa bidhaa hizo kwa kutoa mafunzo kuhusu urasimishaji na uboreshaji wa bidhaa kwa wanawake wajasiriamali 7,713. Aidha wanawake 13,566 wamewezeshwa kushiriki katika maonesho ya biashara ya kitaifa na kimataifa yakiwemo maonesho ya Sabasaba, Juakali, Nanenane na VICOBA;
- (e) Kuweka na kuimarisha mifumo ya kulinda haki za wanawake kwa kufanya yafuatayo;
  - (i) Kuanzisha madawati ya jinsia na watoto 420 katika vituo vya polisi;
  - (ii) Kuanzisha madawati ya jinsia vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu;

TUMETEKELEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA



- (iii) Madawati ya jinsia 162 yameanzishwa katika jeshi la magereza;
- (iv) Vituo 13 vya huduma ya mkono kwa mkono (*One stop centres*) katika mikoa sita ya Dar es Salaam, Pwani, Mbeya, Mwanza, Iringa na Shinyanga vimeanzishwa;
- (v) Kuwezesha wafanyakazi wanawake kufurahia haki ya kunyonyesha mtoto wakati wa muda wa kazi kwa kipindi cha masaa mawili kila siku kwa kipindi cha miezi 6 baada ya muda wa likizo ya uzazi kwa kufanya Marekebisho ya Sheria ya Mahusiano Kazini Na.6 ya Mwaka 2004;
- (vi) Kuwezesha wanawake kushiriki katika ngazi mbalimbali za maamuzi. Kutokana na jitihada hizo nchi yetu imeweza kuwa na wanawake katika ngazi mbalimbali ikiwemo kwa mara ya kwanza kuwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, idadi ya Wabunge wanawake imeongezeka kutoka wabunge 127 sawa na asilimia 36 mwaka 2015 hadi kufikia wabunge 145 sawa na asilimia 37 mwaka 2019. Vilevile, idadi ya majaji wanawake imeongezeka kutoka 24 mwaka 2015 sawa na asilimia 18 hadi kufikia majaji 40 mwaka 2019 sawa na asilimia 39;
- (vii) Kuongezeka kwa huduma za msaada wa sheria kutokana na kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria Na. 1 ya Mwaka 2017. Sheria imewezesha makundi maalum ikiwemo wanawake na watoto kupata haki zao katika vyombo vya usimamizi wa sheria. Aidha, taasisi za kutoa huduma za msaada wa kisheria 125 zimetambuliwa na wasaidizi wa kisheria 494 wamesajiliwa kote nchini. Wanufaika wakubwa wa huduma hizo ni wanawake na watoto; na
- (viii) Kupambana na vitendo vya rushwa ya ngono kupitia kampeni mbalimbali ikiwemo kampeni ya “Vunja Ukimya” inayoratibwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

**231. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama kitahakikisha kinasimamia Serikali katika kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi. Ili kufikia azma hii Chama kitaelekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:-**

- (a) Kuhakikisha sekta zote zinazingatia masuala ya jinsia katika shughuli zao;
- (b) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu;
- (c) Kuanzisha vituo atamizi vya uwezeshaji wanawake kiuchumi;
- (d) Kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika shughuli za kujiletea maendeleo kwa kubadili mtazamo hasi na kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi;



- (e) Kuwezesha upatikanaji wa teknolojia sahihi na rahisi kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji, masoko na ufungashaji wa bidhaa na huduma mbalimbali zinazotolewa na wanawake;
- (f) Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma zinazotolewa na wanawake wajasiriamali kupitia maonesho ya biashara ya ndani na nje ya nchi;
- (g) Kuimarisha vituo vya taarifa na maarifa kwa wanawake ili kuwawesha kupata taarifa sahihi zitakazowawesha kujiendeleza kiuchumi;
- (h) Kuwezesha ushiriki wa wanawake katika kupata zabuni kama inavyoelekezwa katika sheria ya manunuzi;
- (i) Kuimarisha utendaji wa madawati ya jinsia ili kuzuia ukatili wa kijinsia;
- (j) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika maamuzi na uongozi kwenye nyanja za kisiasa na kiuchumi hadi kufikia 50:50;
- (k) Kuimarisha huduma za msaada wa kisheria kwa wanawake na watoto katika maeneo yote nchini; na
- (l) Kuongeza kasi ya kupambana na kutokomeza aina zote za ukatili na unyanyasaji wa kijinsia ikiwemo rushwa ya ngono dhidi ya wanawake na watoto katika jamii, katika maeneo yote nchini.

### ***Maendeleo ya Watoto na Familia***

232.

Chama Cha Mapinduzi kinatambua umuhimu wa kuwa na familia imara kama kiini cha ujenzi wa jamii bora. Serikali imeendelea kukuza haki za watoto za kuishi, kulindwa, kutobaguliwa, kushirikishwa na kuendelezwa. Katika kipindi cha (2015 – 2020), miongoni mafanikio yaliyopatika katika sekta hii ni pamoja na yafuatayo:-

- (a) Kuimarisha ulinzi na ustawi wa mtoto kupitia hatua mbalimbali zikiwemo; kuanzisha kamati za ulinzi wa wanawake na watoto 11,520, katika mamlaka za serikali za mitaa;
- (b) Kuweka na kuratibu mtandao wa mawasiliano ya simu ya bure namba 116 ili kuwezesha jamii kutoa taarifa za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto;
- (c) Kuanzisha vikundi 1,186 vya malezi chanya katika maeneo mbalimbali nchini ili kuimarisha malezi na kukuza uwajibikaji kwa wazazi na walezi wa watoto; na
- (d) Kuanzisha na kuendesha jumla ya mabaraza ya watoto 1,669 na klabu za watoto 2,475 katika kipindi cha mwaka 2015/16 hadi 2018/19 ili kuwezesha watoto kushiriki katika ajenda ya masuala yanayowahusu na jukwaa la kujadili haki na ukatili dhidi yao.





233. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kihakikisha kuwa maendeleo ya mtoto na familia yanazingatiwa. Ili kutimiza azma hii Chama kitaelekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:**

- (a) Kuanzisha na kuimarisha kamati za ulinzi na usalama wa wanawake na watoto katika maeneo yote nchini;
- (b) Kuongeza kasi ya kuhamasisha jamii kubadili fikra na mitazamo hasi inayochochea vitendo vya ukatili dhidi ya watoto katika maeneo yote nchini;
- (c) Kuimarisha mabaraza ya watoto ili watoto wajaadili masuala yanayowahusu na kujenga uwezo wa watoto kuwa jamii imara yenye mtazamo wa kizalendo kwa Taifa lao;
- (d) Kuanzisha na kutekeleza afua zinazolenga kuboresha na kuimarisha familia;
- (e) Kuanzisha madawati ya watoto katika shule za msingi na sekondari ili kuwapa nafasi na mbinu mbadala za kujilinda dhidi ya ukatili; na
- (f) Kuimarisha na kuendelea kuanzisha vikundi vya malezi chanya ili kupunguza vitendo vya ukatili na unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto.

#### **Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

234. Utunzaji na uhifadhi wa mazingira ni suala muhimu kwa kuwa mazingira ni mtambuka na uhusiano wake na maendeleo ya sekta nyingine ni mkubwa. Athari za kutokutunza na kuhifadhi mazingira husababisha sekta nyingine kushindwa kuzalisha kikamilifu na hivyo kuongeza umasikini. Aidha, ni muhimu kuyarejesha mazingira yaliyoharibiwa kwa majanga ya asili na shughuli za kibinadamu. Chama Cha Mapinduzi kwa kutambua umuhimu huo, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), kiliweka mkakati na kuchukua hatua za kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya Tabianchi na kupata mafanikio yafuatayo:-

- (a) Kutokomeza matumizi ya mifuko ya plastiki katika nchi;
- (b) Kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu mabadiliko ya Tabianchi na umuhimu wa kutunza mazingira na kuweza kushiriki katika jitihada mbalimbali za kulinda na kuhifadhi mazingira ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kupanda miti na kutumia mbinu za uzalishaji zenye athari ndogo katika mazingira;
- (c) Kuhamasika kwa mamlaka za serikali za mitaa katika upandaji wa miti ambapo hadi kufikia mwaka 2020 jumla ya miti 608,494,464 ilipandwa katika mikoa yote pamoja na halmashauri zote;
- (d) Kuandaliwa kwa mwongozo wa sheria ndogo ya mazingira ambao utatumika kuandaa sheria ndogo za mazingira katika mamlaka



za serikali za mitaa. Vile vile, mwongozo kwa maafisa mazingira wa mamlaka za serikali za mitaa kuhusu majukumu yao katika kusimamia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 na kanuni zake umeandaliwa;

- (e) Kuboresha utekelezaji wa mikakati ya kusimamia na kuhifadhi maeneo ya fukwe ikiwa pamoja na kujenga uwezo wa jamii za pwani kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kufanya yafuatayo:-
- (i) Kupandwa kwa mikoko katika wilaya za Kibiti/Rufiji Delta (hekta 792), Pangani (hekta 10), Kisiwa Panza (hekta 200), Kilimani (hekta 4), Kinondoni-Mbweni (hekta 3.2) na Kisakasaka (hekta 8);
  - (ii) Kutolewa kwa elimu ya uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za ukanda wa Pwani kupitia vipindi vya redio, televisheni na magazeti pamoja na njia nyingine kwa lengo la kuhamasisha na kukuza uelewa wa wananchi;
  - (iii) Kujengwa kwa ukuta Mto Pangani Tanga mita 795 kati ya mita 950 zilizopangwa;
  - (iv) Kukamilika kwa ujenzi wa ukuta wenye urefu wa mita 40 katika Kisiwa Panza;
  - (v) Kukamilika kwa ujenzi wa ukuta katika Barabara ya Obama wenye urefu wa mita 920; na
  - (vi) Kukamilika kwa ujenzi wa ukuta wenye urefu wa mita 500 katika Chuo cha Mwalimu Nyerere.
- (f) Kuendeleza ulinzi wa ikolojia ya bonde la Mto Ruaha Mkuu kwa kutambua vyanzo vya maji 5,373 katika mikoa saba na kati ya hivyo, vyanzo 652 vililwekewa mipaka ya kudumu;
- (g) Kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 78 ili kuhakikisha usimamizi bora wa vyanzo vya maji;
- (h) Kuwekeza katika kuhifadhi vyanzo vya maji chini ya mradi wa mazingira wa Bonde la Kihansi;
- (i) Kuweka na kutekeleza mikakati na mipango ya kitaifa na kimataifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na
- (j) Kupunguza athari hasi kwa mazingira, hususan zitokanazo na utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ili kulinda mazingira kwa faida ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho kwa kufanya tathmini ya mipango saba ya kimkakati ambayo ni:- Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere katika Mto Rufiji; uboreshaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji; Mpango Kabambe wa Usafiri Katika Jiji la Dar es Salaam; Sera, mikakati, sheria na kanuni za uvuvi wa bahari kuu.



235. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa kuwashirikisha wananchi na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi. Ili kufikia malengo hayo, katika kipindi hicho, Chama kitaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kuboresha utekelezaji wa mikakati ya kampeni za kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na upandaji, utunzaji na ukuzaji miti milioni 1.5 kila mwaka katika halmashauri ili kuondokana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame;
- (b) Kuratibu, kusimamia na kuhakikisha mamlaka za serikali za mitaa zinazingatia mwongozo wa sheria ndogo katika kuandaa sheria ndogo za mazingira na kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004;
- (c) Kuboresha mifumo ya uratibu wa utekelezaji wa mkakati wa kuhifadhi mazingira ya bahari, ukanda wa pwani, maziwa, mito na mabwawa kwa kushirikisha wadau wengine;
- (d) Kufanya tathmini ya vyanzo vya maji vilivyohifadhiwa, kuongeza vyanzo vipya na kufufua vilivyopotea ama kuharibika katika maeneo ambayo hayajafanyiwa tathmini kwa lengo la kuwa na uhakika wa upatikanaji wa majisafi na salama;
- (e) Kubuni na kuweka mikakati ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa lengo la kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira kwa kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ikiwemo gesi na umeme;
- (f) Kuongeza kasi ya tathmini za uanzishwaji wa viwanda na shughuli za kiuchumi, ili kutoa vyeti vya Tathmini ya Athari za Mazingira (TAM) kwa muda mfupi na vilevile, kuhakikisha kuwa miradi hiyo inazingatia uhifadhi wa mazingira;
- (g) Kufanya ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria ya mazingira hususan katika viwanda na migodi;
- (h) Kuanzisha maeneo lindwa ya mazingira (*Environmental Protected Areas*) ili kuongoa na kuhifadhi maeneo muhimu ya kimazingira;
- (i) Kuongeza kasi ya kutoa elimu juu ya kulinda na kuhifadhi mazingira ikiwemo madhara ya uchomaji moto holela;
- (j) Kuendeleza ushirikiano na wadau wa kikanda na kimataifa katika jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na



- (k) Kuimarisha utekelezaji wa mikataba ya kimataifa na ya kikanda kuhusu hifadhi ya mazingira.

### **Utamaduni, Sanaa na Michezo**

236. Utamaduni, sanaa na michezo ni miongoni mwa sekta muhimu nchini ambazo zinachangia moja kwa moja katika maendeleo na ustawi wa jamii kwa kuwa zinagusa sehemu kubwa ya maisha ya wananchi walio wengi mijini na vijijini. Sekta hizi zinawawezesha wananchi kuboresha afya zao ikiwa ni pamoja na kuimarisha umoja, udugu, uzalendo na mshikamano wa kitaifa. Chama Cha Mapinduzi kwa kutambua umuhimu huo, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), kimeendelea kuisimamia Serikali kuchukua hatua mbalimbali katika kuboresha sekta hizi kwa lengo la kuongeza mchango wa utamaduni, sanaa na michezo kwa jamii na Taifa kwa ujumla. Aidha, kulinda, kusimamia na kuendeleza lugha ya Kiswahili imekuwa eneo muhimu katika kuitangaza nchi yetu kikanda na kimataifa.

### **Utamaduni**

237. Chama Cha Mapinduzi kimeendelea kutambua umuhimu wa utamaduni kama utambulisho wa Taifa, chanzo cha ajira, burudani na chombo cha kuziunganisha jamii za Watanzania. Utamaduni umekuwa ni nyezo ya kuwawezesha wananchi kukabiliana na maisha kulingana na mazingira wanayoishi kwa kutumia maarifa, maadili, mila nzuri na desturi za mahali husika. Utamaduni pamoja na masuala mengine unajumuisha lugha, fasihi, sanaa, sayansi na teknolojia.

238. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), Chama Cha Mapinduzi kiliendelea kuchukua hatua katika kuhakikisha sekta ya utamaduni inaimarishwa kwa lengo kuiwezesha kuchangia kikamilifu katika kudumisha utamaduni wa Mtanzania, hususan matumizi ya lugha ya Kiswahili. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

- (a) Kuwawezesha wananchi kujipatia kuimarisha utambulisho wetu kama Taifa;
- (b) Kuongeza ajira kutokana na kazi za kiutamaduni, sanaa na ubunifu;
- (c) Kuimarisha mahusiano ya wananchi na mataifa mengine kupitia kazi za utamaduni;
- (d) Kuimarishwa kwa mila na desturi na tamaduni nzuri zinazojenga utaifa;
- (e) Kuongeza wigo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuanzishwa kwa Tume ya Lugha ya Kiswahili ya Afrika Mashariki. Kiswahili kimeendelea kuenea, kutumika na kutambulika zaidi kikanda na kimataifa, sasa ni mojawapo ya lugha mahsusi kwenye SADC;



- (f) Kuandaliwa kwa mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kusajili na kutunza kanzidata ya wataalam wa Kiswahili kama hatua ya kupanua wigo wa fursa zitokanazo na matumizi ya lugha hiyo ndani na nje ya nchi ambapo hadi kufikia mwaka 2020 wataalam 1,224 wamesajiliwa katika mfumo huo;
- (g) Kuwezesha nchi yetu kutumia vyema fursa ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kitaifa na kimataifa kwa kujenga uwezo wa wataalam 10 wa ukalimani wa ndani wenye uwezo wa lugha za kigeni za Kiingereza, Kifaransa na Kireno;
- (h) Kurahisisha na kuimarisha usimamizi na maendeleo ya lugha ya Kiswahili kwa kutungwa kwa kanuni za Sheria ya Baraza la Kiswahili la Taifa Na. 27 ya Mwaka 1967;
- (i) Kupanuliwa kwa wigo wa msamiati na Istilahi za lugha ya Kiswahili kupitia Kongoo la Kiswahili lililoandaliwa kuwa na maneno 50,000,000 ambapo tayari lina maneno 1,500,000;
- (j) Taftiti mbalimbali zimefanyika kuhusu mila nzuri na desturi katika mikoa ya Morogoro, Iringa, Singida, Lindi na Mtwara kwa lengo la kuhifadhi mila na desturi za mikoa hiyo;
- (k) Kuhuishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa mitaji kwa njia ya mikopo nafuu kwa watendaji wa kazi za kitamaduni, sanaa na ubunifu;
- (l) Kubainishwa kwa maeneo 255 yaliyotumika wakati wa harakati za ukombozi wa Bara la Afrika kwa ajili ya kuhifadhiwa na kutangazwa kuwa vivutio vya utalii; na
- (m) Kubainishwa, kukusanywa na kuhifadhiwa kidijitali kwa vifaa na nyaraka mbalimbali 6,782 kuhusu historia ya ukombozi wa Bara la Afrika. Vilevile, mahojiano na wazee 227 walioshiriki au kushuhudia harakati za ukombozi wa Bara la Afrika katika mikoa mbalimbali yamefanyika.

239. **Katika kulinda, kuendeleza, kuhifadhi na kurithisha amali za kiutamaduni, Chama kina lengo la kuchochea na kuhamasisha jamii kuhusu dhana chanya ya utamaduni ili wananchi wote waweze kufahamu umuhimu wake katika kutambulisha Utanzania, kuburudisha, na kuongeza fursa za ajira. Ili kufikia malengo hayo, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama kitaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kuimarisha Tume ya Lugha ya Kiswahili ya Afrika Mashariki na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kama fursa ya kueneza Kiswahili sanifu katika kanda ya Afrika Mashariki, Afrika na Duniani;



- (b) Kuongeza wigo wa misamiati ya lugha ya Kiswahili kwa kurasimisha maneno na Istilahi za lugha hiyo ambazo matumizi yake yamezoeleka katika jamii;
- (c) Kusimamia matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi na kubidhaisha lugha hiyo kama chanzo cha ajira na mapato;
- (d) Kufanya tafiti za lugha, historia, mila nzuri na desturi za jamii za Tanzania kwa ajili ya kulinda, kuenzi, kuhifadhi na kuendeleza kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho;
- (e) Kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kutoa matokeo ya utafiti kisayansi na machapisho ya kitaaluma;
- (f) Kuboresha utekelezaji wa mikakati ya kuelimisha umma kuhusu wajibu wao wa kuimarisha misingi ya utafu, kulinda na kuenzi maadili ya kitanzania ili kukabiliana na mmomonyoko wa maadili unaochangiwa na athari za utandawazi na kutozingatiwa kwa malezi na makuzi bora ya vijana;
- (g) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuhamasisha umma wa Watanzania kushiriki katika sherehe za kitaifa pamoja na kuenzi falsafa ya Mwenge wa Uhuru na malengo yake ya kustawisha maendeleo, kudumisha umoja na utafu;
- (h) Kuendelea kuhifadhi kumbukumbu ya ushiriki na mchango wa Tanzania katika harakati za ukombozi wa Umoja wa Afrika, hususan ukombozi wa Kusini mwa Afrika kwa kushirikisha idara inayohusika na Malikale na Makumbusho ya Taifa;
- (i) Kutoa elimu kwa umma kuhusu historia ya urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika ili jamii, hususan vijana waweze kufahamu historia kwa kushirikisha idara inayohusika na Malikale na Makumbusho ya Taifa;
- (j) Kuhakikisha kuwa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika inajumuishwa katika sera na mipango ya kitaifa na kulindwa kisheria kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho;
- (k) Kuwajengea uwezo wataalam wa kitanzania wa kutafsiri lugha mbalimbali za kigeni ili waweze kunufaika na fursa za kukua kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili duniani;
- (l) Kuweka kumbukumbu na kuhimiza matumizi ya mila na desturi dhidi ya utandawazi kwa kufanya utafiti wa mila na desturi za jamii ya kitanzania; na
- (m) Kutekeleza programu maalum ya kukitangaza Kiswahili duniani.



**Sanaa**

240. Tasnia ya sanaa ni muhimu katika kutambulisha utaifa, utamaduni wa nchi husika, kuleta burudani na kuchangia katika fursa za ajira. Kutokana na umuhimu huo, kwa miaka mitano iliyopita, Chama kimeendelea kuunga mkono juhudi za kuendeleza sanaa nchini kama sehemu ya kutoa ajira, hususan miongoni mwa vijana kupitia kazi za sanaa kama vile filamu, muziki na michezo ya kuigiza. Katika hatua hizo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- (a) Kuimarisha maendeleo na usimamizi wa tasnia ya sanaa nchini kwa kuijengea uwezo Bodi ya Filamu Tanzania ili kuendeleza mila nzuri, desturi na utamaduni wa Mtanzania kwa kuhakikisha sanaa ya filamu na michezo ya kuigiza inazingatia maadili ya Taifa;
- (b) Kuimarisha maendeleo na usimamizi wa tasnia ya filamu nchini kwa kufanya mapitio ya sheria ya filamu na michezo ya kuigiza nchini;
- (c) Kuboresha mazingira ya tasnia ya sanaa kwa kununua eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 46,080 katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kwa ajili ya ujenzi wa Jumba Changamani la Uzalishaji wa Filamu na shughuli nyingine;
- (d) Kuimarisha ubora wa kazi za sanaa nchini kwa kuwapatia mafunzo na ushauri wa kitaalam wadau wa sanaa wapatao 10,437 kuhusu uendeshaji wa matukio na utafutaji wa masoko;
- (e) Kutambua shughuli za wasanii kwa kusajili na kutoa vibali vya kuendesha shughuli za sanaa kwa wasanii na wadau 1,084;
- (f) Kuimarishwa kwa tasnia ya sanaa kwa kuipatia vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika maeneo ya teknolojia ya sauti, muziki, ubunifu pamoja na uzalishaji wa picha jongevu Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa). Aidha, taasisi hiyo imedahili wanafunzi 893 wa kozi za muda mrefu na 388 wa kozi fupi hadi mwaka 2020;
- (g) Kuongeza weledi katika kazi za filamu kwa kutoa mafunzo kwa wanatasnia ya filamu 1,777 kuhusu hakimiliki na hakishiriki, uzalishaji wa filamu bora, uingiaji wa mikataba yenye tija;
- (h) Kukabiliana na wizi wa kazi za wasanii kwa kuanzisha utaratibu wa kuweka stempu za ushuru wa bidhaa kwa kazi zote za filamu na muziki;
- (i) Kulinda kazi na masilahi ya wasanii kwa kuendesha operesheni mbalimbali kwa ajili kukagua kazi zinazolingia sokoni bila kufuata utaratibu pamoja na mitambo ya kuzalisha kazi za filamu kinyume na sheria. Aidha, jumla ya kazi za filamu 5,547 zilizojumuisha filamu za kitanzania 4,837 na 710 kutoka nje ya nchi zilihakikiwa na kupatiwa vibali (*certificate of approval*);



- (j) Kutolewa kwa jumla ya vibali 685 vya utayarishaji wa picha jongevu ambapo 140 vilitolewa kwa waombaji kutoka ndani na 545 kutoka nje ya nchi kwa lengo la kuendeleza tasnia ya filamu;
- (k) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika tasnia ya sanaa ambapo, majumba ya sinema yamejengwa kupitia sekta hiyo na kufunguliwa. Aidha, jumba la utayarishaji wa kazi za filamu lenye studio mbili za kurekodi kwa kutumia vyombo vya kisasa litwalo *Wanene Entertainment Limited* lililopo jijini Dar es Salaam limejengwa na kufunguliwa. Vilevile, maeneo yasiyokuwa rasmi yapatayo 5,210 ya kuoneshea kazi za filamu, studio na maktaba za filamu yamebainishwa ili yarasimishwe;
- (l) Kulinda haki na masilahi ya wasanii na kanuni za usajili, muonekano, na uendeshaji wa vibanda vya kuonyeshea filamu wa maeneo yasiyo rasmi kwa kukamilisha kanuni mpya zinazowataka wadau watakaofanya kazi na wasanii kuwasilisha mikataba ya makubaliano baina ya msanii na mdau husika;
- (m) Kuanzishwa kwa Dawati la Msaada wa Kisheria linalotoa elimu ya mikataba kwa wasanii ili kuwajengea uelewa na hatimaye kuwawezesha kupata tafsiri sahihi za mikataba ya wasanii na kampuni zinazowasimamia;
- (n) Kuandaliwa kwa mfumo wa urasimishaji wa kazi za filamu na muziki utakaowezesha kutambuliwa rasmi kwa wasanii na kazi zao; na
- (o) Kuitangaza nchi yetu kupitia Tamasha la Utamaduni na Sanaa la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) lililofanyika jijini Dar es Salaam mwaka 2019 na kufuatiliwa na watu zaidi ya milioni 94 duniani. Pamoja na manufaa mengine, tamasha hilo liliwezesha kufahamika kwa kazi za kitamaduni, sanaa na ubunifu ndani na nje ya nchi.

**241. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha tasnia ya sanaa nchini. Lengo ni kuendesha tasnia ya sanaa kibiashara na kuongeza tija ikiwa ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa fursa zaidi za ajira kwa makundi yote ya jamii. Vilevile, tasnia ya sanaa itaendelea kutumika kama nyenzo ya kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Ili kufikia malengo hayo, Chama kitaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kuweka mazingira wezeshi kwa makampuni ya ndani na nje ya nchi kupiga picha za filamu ili kutangaza utalii ndani na nje ya nchi;
- (b) Kujenga mazingira wezeshi ya kukuza sanaa zetu zikiwemo ngoma na bongo *movie* ili kufikia viwango vya kimataifa;



- (c) Kuboresha mbinu na mikakati ya utekelezaji wa sera na sheria za kurasimisha kazi za sanaa nchini kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa sanaa hususan wasanii;
- (d) Kuanzisha na kuimarisha miundombinu mbalimbali ya sekta ya sanaa ili kutoa fursa kwa wadau kujiajiri katika tasnia ya ubunifu;
- (e) Kuanzisha Kituo cha Taifa cha Sanaa cha Watoto na Vijana wenye vipaji ambao hawapo katika mfumo rasmi wa elimu ili kuhakikisha kunakuwa na vikundi bora vya sanaa na utamaduni;
- (f) Kubuni mbinu na mikakati ya kulinda wasanii dhidi ya vitendo vya unyonyaji, wizi na kughushiwa kwa kazi zao;
- (g) Kubuni mikakati na mbinu madhubuti za kuwavutia wawekezaji katika tasnia ya filamu ili iweze kuzalisha mazao bora na yenye ushindani katika soko la ndani na nje ya nchi;
- (h) Kuhakikisha kunakuwa na matamasha na tuzo mbalimbali pamoja na kuanzisha tamasha maalum kitaifa kwa lengo la kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza;
- (i) Kuanza ujenzi wa Jumba Changamani la Uzalishaji wa Filamu pamoja na kubaini vyanzo vipya vya mapato; na
- (j) Kuimarisha mfumo wa kisheria na kitaasisi wa kusimamia kazi za sanaa ili kuwezesha wanatasnia kupata masilahi stahiki kutokana na kazi zao.

### **Michezo**

242. Sekta ya michezo ina umuhimu mkubwa katika kutoa burudani, kuimarisha afya, na kuongeza furaha kwa wananchi wote. Michezo pia inachangia katika kuziunganisha jamii zetu ndani na nje ya mipaka ya nchi. Aidha, michezo ni moja kati ya sekta inayotoa fursa za ajira kwa wananchi hususan vijana na kuwawezesha kuongeza vipato vyao na kuboresha maisha ya wanamichezo na wadau wote katika sekta hiyo. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015 - 2020), Chama kililenga kuimarisha sekta ya michezo ili kuinua kiwango cha michezo nchini ikiwa ni pamoja na kuifanya sekta ya michezo kutoa fursa za ajira hususan kwa vijana. Katika jitihada za kufikia lengo hilo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- (a) Kuboreshwa kwa Uwanja wa Taifa ikiwa ni pamoja na kupanda nyasi katika eneo la kuchezea na kukarabati vyumba vya kubadilisha nguo za wachezaji katika uwanja huo. Aidha, Uwanja wa Uhuru umefanyiwa ukarabati kwa kuwekwa nyasi mpya bandia. Vilevile, viwanja vya Kaitaba mkoani Kagera na Nyamagana mkoani Mwanza vilikarabatiwa kwa kuwekwa nyasi bandia;



- (b) Kuanzishwa kwa mikakati mbalimbali ya kuinua michezo nchini iliyofanikisha yafuatayo:-
- (i) Tanzania kushiriki fainali za Mpira wa Miguu za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) mwaka 2019 nchini Misri baada ya miaka 39;
  - (ii) Kuwa wenyeji wa fainali za mpira wa miguu kwa vijana wenye umri chini ya Miaka 17 (AFCON U-17) mwaka 2019, jijini Dar es Salaam. fainali hizo zimesaidia kuitangaza nchi yetu kimataifa;
  - (iii) Timu ya Riadha kushinda medali nane (dhahabu saba na fedha moja) katika mashindano ya Nagai City Marathon (Japan) mwaka 2018; Timu ya Olimpiki Maalum (*Special Olympics*) kushinda medali 15 (dhahabu 12, fedha moja na shaba mbili) katika mashindano ya Riadha na Mpira wa Wavu yaliyofanyika Abu Dhabi, Falme za Kiarabu mwaka 2019;
  - (iv) Timu ya wanawake ya mpira wa miguu (*Kilimanjaro Queens*, chini ya miaka 20) kushinda mashindano ya CECAFA yaliyofanyika mwaka 2018 Kigali, Rwanda kwa mara ya pili mfululizo, (Tanzanite, chini ya miaka 17) kutwaa Kombe la COSAFA kwa timu ya wanawake ya mpira wa miguu chini ya umri wa miaka 20 mwaka 2019 nchini Afrika Kusini; na
  - (v) Kushiriki na kutwaa kombe la Afrika Mashariki la mpira wa miguu kwa timu ya Taifa ya vijana wa kiume chini ya umri wa miaka 20.
- (c) Kuundwa kwa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania ambayo imeratibu na kusimamia mabondia wa Tanzania kupata mafanikio katika michezo mbalimbali ya ngumi za kulipwa;
- (d) Kuimarishwa kwa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na shughuli za michezo kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ya viingilio katika Uwanja wa Taifa na Uwanja wa Uhuru;
- (e) Kusajiliwa kwa vikundi 269 vya “jogging”, vyama 76, vilabu 1,055, wakuzaji na mawakala wa michezo 43 na vituo vya michezo 58;
- (f) Kuimarishwa kwa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kwa kujenga na kukarabati mabweni, kuchimba kisima cha maji safi na kujenga na kukarabati viwanja vya michezo kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Aidha, jumla ya wanachuo 364 wamedahiliwa katika chuo hicho na washiriki 1,104 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi;
- (g) Kumarishwa kwa michezo ya shule za msingi na sekondari (UMITASHUMTA na UMISSETA) ili kuibua na kukuza vipaji vya michezo. Aidha, shule 56 zimeteuliwa kuwa shule rasmi za michezo;



- (h) Vibali 45 vimetolewa kwa timu za Taifa, vilabu, vituo vya michezo na mabondia kwenda nje ya nchi kushiriki mashindano mbalimbali;
- (i) Michezo ya jadi iliendelea kuratibiwa ikiwa ni pamoja na kuvuta kamba, bao, kukuna nazi, mdako, kirumbizi, kulenga shabaha, kusuka ukili na mieleka iliyoratibiwa wakati wa TAMASHA la Sanaa na Utamaduni (JAMAFEST) lililofanyika Dar es Salaam, mwaka 2019; na
- (j) Kuundwa kwa kamati maalum kupendekeza njia bora ya kuhusisha sekta binafsi katika kujenga Uwanja Changamani wa Ndani wa Michezo na Sanaa (*Arts & Sports Arena*) kwa kuanzia jijini Dar es salaam.

**243. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha michezo nchini. Lengo ni kuongeza fursa zaidi za ajira kwa makundi yote ya jamii hususan vijana. Vilevile, sekta ya michezo itaendelea kuimarisha udugu na mshikamano wa Taifa na mahusiano kati ya Taifa letu na mataifa mengine. Ili kufikia azma hiyo, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama kitaelekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-**

- (a) Kujenga uwanja wa kisasa wa michezo makao makuu ya nchi jijini Dodoma;
- (b) Kuweka mazingira wezeshi kwa wanamichezo kushiriki katika mashindano ya kimataifa, kuwatambua na kuwaenzi wanamichezo wanaofanya vizuri katika nyanja hizo ili kuwawezesha kunufaika na vipaji vyao na vilevile kuitangaza nchi yetu kimataifa;
- (c) Kuhamasisha wananchi kufanya mazoezi na kuanzisha vilabu vya michezo na matamasha ya mazoezi ili kuboresha afya zao na kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza;
- (d) Kuwa na mipango na mikakati maalum ya kuendeleza michezo ya kulipwa ikiwemo uanzishaji wa shule maalum za kukuza vipaji vya wanamichezo (*sports academy*) ili waweze kushindana katika soko la kimataifa;
- (e) Kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa shule za michezo na kuboresha utoaji wa mafunzo ya tasnia ya michezo;
- (f) Kuimarisha usimamizi wa shughuli za michezo katika mamlaka ya serikali za mitaa na mikoa ili kuhamasisha na kusimamia maendeleo ya michezo katika ngazi zote kuanzia ngazi za vijiji, kata, wilaya, mikoa hadi Taifa;
- (g) Kuanzisha mfumo thabiti wa michezo ya kulipwa ili kulinda na kuendeleza vipaji vilivyopo kwa manufaa ya Taifa;



- (h) Kuimarisha mikakati ya uboreshaji wa vyanzo vya fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za michezo;
- (i) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuwezesha vijana kushiriki katika michezo ili kuimarisha afya zao, kudumisha amani, umoja, upendo, uzalendo na maadili ya Taifa;
- (j) Kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine pamoja na kuvutia uwekezaji katika upatikanaji wa vifaa vya michezo; na
- (k) Kuwahamasisha wanamichezo kujiunga na kunufaika na fursa zitolewazo na mifuko ya hifadhi ya jamii kwa ustawi na maisha yao ya baadaye.

### **Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya**

244.

Matumizi ya dawa za kulevya yana madhara makubwa katika maisha ya binadamu, uwezo wa rasilimaliwatu na maendeleo endelevu ya nchi. Chama kwa kutambua athari zitokanazo na matumizi ya dawa za kulevya kimeendelea kuisisitiza Serikali kuweka mikakati ya kupambana na uzalishaji, usambazaji, uuzaji na utumiaji wa dawa hizo. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

- (a) Kupunguza uingizaji wa dawa za kulevya nchini kwa asilimia 90 na hivyo kuiwezesha nchi yetu kutambuliwa na Shirika la Kimataifa linaloshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu wa Kupanga (UNODC). Kutokana na kutambulika huko, Tanzania ilipewa heshima ya kuwa mwenyeji wa mkutano wa 28 wa wakuu wa vyombo vinavyopambana na dawa za kulevya Afrika (HONLEA AFRICA 2018);
- (b) Kupungua kwa biashara na matumizi ya dawa za kulevya kutokana na juhudi za makusudi zilizochukuliwa katika kupambana na biashara hiyo. Hatua hii imesaidia ustawi wa jamii, hususan kwa vijana ambao ndiyo nguvukazi ya Taifa;
- (c) Kuimarisha udhibiti wa uzalishaji, usambazaji, uuzaji na utumiaji wa dawa za kulevya kwa kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (*Drug Control and Enforcement Authority - DCEA*) iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha 3 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015;
- (d) Kudhibiti biashara ya dawa za kulevya kwa kushirikiana na mataifa mengine na taasisi mbalimbali kimataifa ambapo iliwezesha:-
  - (i) Kuzuia zaidi ya tani 1.55 za heroin kuingia nchini kwetu na hivyo kuokoa maelfu ya Watanzania ambao wangeathirika kwa kutumia dawa hizo; na
  - (ii) Kuzuia uingizaji wa zaidi ya tani 700 za kemikali bashirifu na hivyo kuondoa uwezekano wa kemikali hizo kuchepushwa na kutumika kutengenezea dawa za kulevya.





- (e) Kuongeza utoaji wa dawa na matibabu pamoja na kuanzisha vituo vya kuhudumia wananchi walioathirika na matumizi ya dawa za kulevywa kwa kuanzisha kliniki sita na kutoa huduma kwa waathirika zaidi ya 7,500 ambao wanapata huduma za *Methodone* na magonjwa mengine yanayoambatana na athari za matumizi ya dawa za kulevywa katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Dodoma;
- (f) Kuandaliwa na kutekelezwa kwa Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Nyumba za Upataji Nafuu (*Sober Houses*). Jumla ya nyumba za upataji nafuu 40 nchini zimetambuliwa na kuendelea kusimamiwa ili kuhakikisha zinatoa huduma kulingana na mwongozo;
- (g) Kuzijengea uwezo Asasi za Kiraia 40 kwa kuziwezesha kifedha na kuzipatia vitendea kazi kama pikipiki na kompyuta;
- (h) Kudhibitiwa kwa kilimo cha bangi na mirungi ambapo mashamba 279 yenye jumla ya hekta 708.5, katika mikoa mbalimbali hapa nchini ikiwemo ya Mara (Tarime/Rorya), Morogoro, Arusha, Tanga, Kagera na Ruvuma yaliteketezwa;
- (i) Kufanikisha ukamataji wa watuhumiwa na dawa za kulevywa kama ifuatavyo:-
- (i) Bangi tani 97.99 zikiwahusisha watuhumiwa 21,594;
  - (ii) Mirungi tani 85.84 zikiwahusisha watuhumiwa 2,992;
  - (iii) *Heroin* kilo 567.97 zikiwahusisha watuhumiwa 1,730; na
  - (iv) *Cocaine* kilo 23.383 zikiwahusisha watuhumiwa 399.
- (j) Kushughulikia kesi kuhusu dawa za kulevywa ambapo jumla ya kesi 16,863 zilifikishwa mahakamani zikiwahusisha watuhumiwa 26,717. Kati ya kesi 748 zilizotolewa maamuzi mwaka 2018, Jamhuri ilishinda kesi 610 ambayo ni asilimia 81.6;
- (k) Kuteketezwa kwa dawa za kulevywa ambapo jumla ya tani 6.7 za dawa za kulevywa aina ya bangi ziliteteketezwa. Aidha, dawa nyingine za kulevywa zilizoteteketezwa ni kilo 127.8 za *heroin* na kilo 71.5 za *cocaine*. Dawa hizo zilihusisha kesi 35 zilizomalizika katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rushwa na Uhujumu Uchumi; na
- (l) Kushughulikia kimkakati mtandao mkubwa wa dawa za kulevywa hususan wafanyabiashara wakubwa na maarufu wanaojihusisha na biashara hiyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya *Interpol*. Hali hiyo imedhoofisha mitandao wa wanaojihusisha na dawa za kulevywa.



245. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuelekeza Serikali kuchukua hatua za kupambana na uzalishaji, usambazaji, uuzaji na utumiaji wa dawa za kulevya kwa kufanya yafuatayo:-**

- (a) Kulinda mafanikio yaliyopatikana katika vita dhidi ya dawa za kulevya kwa kuendelea kuibua na kutekeleza mikakati ya kupambana na kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya;
- (b) Kuimarisha ushirikiano na mataifa mengine na asasi za kimataifa katika kupambana na makosa yanayovuka mipaka ikiwemo biashara haramu ya madawa ya kulevya;
- (c) Kuongeza juhudi katika utoaji wa tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya pamoja na kuanzisha vituo vya kuhudumia wananchi walioathirika na matumizi ya dawa za kulevya katika mikoa ambayo imeathirika zaidi na matumizi ya dawa za kulevya ili kuwafikia waathirika wengi zaidi;
- (d) Kuongeza nguvu katika kushirikiana na asasi za kijamii na kuziwezesha ili kuinua uwezo wa kushiriki katika kutoa elimu juu ya athari ya matumizi ya dawa za kulevya katika jamii zinazowazunguka; na
- (e) Kuiboresha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015 na Kanuni zake ili kuendana na wakati kwa kuwa tatizo la dawa za kulevya hubadilika mara kwa mara.



## SURA YA KUMI

### CHAMA CHA MAPINDUZI

TUJITEKELEZEZA KWA KISHINDO; TUNASONGA MBELE PAMOJA

246. Lengo kuu la Chama Cha Mapinduzi ni kujenga Taifa la kijamaa, linalojitegemea na lililoendelea katika nyanja zote za ustawi wa watu. Kwa kutambua hili, wajibu wa Chama hauishii tu katika kutoa ahadi kwa wananchi, kupitia Ilani ya Uchaguzi Mkuu na kuzikabidhi Serikali zake kwa utekelezaji, bali pia Chama kinao wajibu wa kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo. Katika Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 - 2020, Chama Cha Mapinduzi, kilibeba wajibu na majukumu yafuatayo:-
- Kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM;
  - Utekelezaji wa maazimio ya Mkutano Mkuu wa Nane wa Taifa, ambayo ni:-
    - Kudumisha Muungano;
    - Kuimarisha Chama Kitaasisi;
    - Kudumisha maadili na miiko ya uongozi; na
    - Kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi.
  - Kukabiliana na athari za kukua kwa tofauti kubwa ya kimapato katika jamii;
  - Chama kujitegemea kimapato; na
  - Mafunzo kwa makada na viongozi wa Chama.
247. Ili kufanikisha utekelezaji wa wajibu na majukumu hayo, Mkutano Mkuu Maalum wa CCM wa Taifa uliofanyika tarehe 12 Machi, 2017, pamoja na mambo mengine, ulifanya marekebisho ya Katiba ya CCM ya mwaka 1977, Toleo la 2012. Lengo la marekebisho hayo ni kuboresha mfumo na muundo wa Chama na Jumuiya zake, kuongeza ufanisi na kuimarisha utendaji kazi wa Chama, kukipeleka Chama kwa wananchi na kukifanya Chama na Jumuiya zake kujitegemea kiuchumi.
248. Taarifa ya Chama Cha Mapinduzi, juu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, katika kipindi cha miaka miwili (2015 - 2019), iliyowasilishwa mbele ya Mkutano Mkuu wa Tisa wa CCM wa Taifa uliofanyika tarehe 18 - 19 Disemba, 2017 ilibainisha na kufafanua kwa kina hatua za utekelezaji wa majukumu hayo katika kila eneo.
249. Aidha, Mkutano Mkuu huo wa Tisa wa CCM wa Taifa, mbali na kupokea na kupitisha taarifa hiyo ya Chama Cha Mapinduzi, pia uliridhia na kupitisha mambo makubwa manne yaliyopendekezwa na Mwenyekiti wa CCM na Rais



wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, wakati akitoa hotuba yake ya ufunguzi wa Mkutano huo. Ilikubalika kuwa mambo hayo manne ndiyo malengo makuu ya Mradi wa Awamu ya Nne ya Kujenga na Kuimarisha Chama, katika kipindi cha mwaka 2017 - 2022. Malengo hayo ni kama yafuatayo:-

- (a) Kukiimarisha Chama kwa kuongeza idadi ya wanachama;
- (b) Kuhakikisha kuwa Chama kinajitegemea kiuchumi;
- (c) Kuhakikisha kuwa Chama kinakua kiungo kati ya Serikali na wananchi; na
- (d) Kusimamia uadilifu kwa viongozi na kuwa mfano wa kuigwa kwa wanachama na wananchi kwa jumla.

250. **Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kutekeleza jukumu la kihistoria na la kimapinduzi, la kuongoza mapambano ya kutetea na kulinda utu, usawa na haki chini ya misingi ya Ujamaa na Kujitegemea. Katika kutimiza wajibu huu wa kujenga na kuimarisha Chama, CCM kitaendelea kusimamia mambo yafuatayo:-**

- (a) Kuimarisha misingi ya uchumi wa kitaifa;
- (b) Kuimarisha misingi ya maadili na uongozi bora;
- (c) Kudumisha tunu za Taifa;
- (d) Kuimarisha demokrasia nchini; na
- (e) Kuendeleza harakati za mapinduzi dhidi ya unyonge, uonevu na udhalimu duniani.

251. Ilani hii ambayo CCM itaikabidhi kwa wagombea wake wa ngazi zote kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, ndiyo mkataba kati ya Chama na wananchi, ili kukichagua na kukipa tena ridhaa ya kuongoza nchi yetu. Baada ya kushinda uchaguzi, CCM itakuwa na wajibu wa kusimamia utekelezaji wa Ilani hii kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kupata mafanikio yaliyokusudiwa na kuendelea kujenga imani kwa wananchi waliotoa ridhaa kwa wagombea wa CCM. Usimamizi wa utekelezaji wa Ilani hiyo utafanyika kwa utaratibu ufuatao:-

- (a) Katika ngazi ya Taifa, usimamizi wa utekelezaji wa Ilani ya CCM, utafanywa na wabunge pamoja na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kupitia kamati zao za kudumu. Aidha, Mwenyekiti wa kamati ya wabunge wote wa CCM (Waziri Mkuu) na Mwenyekiti wa kamati ya wawakilishi wote wa CCM (Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar)



wanao wajibu wa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani, mbele ya vikao vya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa;

- (b) Vikao vya Halmashauri Kuu za CCM vya ngazi ya mkoa, wilaya, majimbo, kata/wadi na matawi, vinapaswa kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika maeneo yao, kupitia taarifa kutoka kwa wabunge, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na madiwani wao;
- (c) Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Mwaka 2020 – 2025, utaratibu wa vikao vya CCM kupokea taarifa za utekelezaji wa Ilani kutoka kwa wahusika, utakiwezesha Chama kufanya tathmini ya kesi ya utekelezaji wa Ilani katika ngazi mbalimbali kwa kuzingatia Katiba pamoja na kalenda ya vikao vya CCM;
- (d) Njia nyingine ya kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ni kwa viongozi wa CCM kutembelea na kukagua miradi inayotekelezwa na Serikali katika maeneo yao ili kujiridhisha juu ya maendeleo ya utekelezaji wa miradi hiyo. Hivyo, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya mwaka 2020 – 2025, Viongozi wa CCM wa ngazi zote watajiwekea ratiba za kutembelea na kukagua miradi inayotekelezwa katika maeneo yao, na iwapo watabaini dosari au hitilafu zozote, watatoa taarifa kwa viongozi wa Serikali wa ngazi ya juu yao mara moja; na
- (e) Hatua nyingine muhimu kwa Chama katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ni kuhakikisha kuwa, Chama kinatenga siku maalum kila wiki ili kusikiliza kero za wananchi na kuzifikisha serikalini kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

252. Kuendelea kusimamia kwa ufanisi zaidi malengo makuu ya Mradi wa Awamu ya Nne ya Kujenga na Kuimarisha Chama, kama yalivyopitishwa na kuridhiwa na Mkutano Mkuu wa Tisa wa CCM wa Taifa. Malengo hayo ni:-

- (a) Kuongeza idadi ya wanachama na kuwahamasisha kulipa ada zao kwa wakati na kulifanya zoezi la usajili wa wanachama wa CCM na Jumuiya zake kwa kutumia mfumo wa TEHAMA na utoaji wa kadi za kielektroniki kuwa ni endelevu;
- (b) Kusimamia kwa ufanisi kazi ya utambuzi, usajili, uhifadhi na udhibiti wa taarifa za mali na rasilimali za Chama na Jumuiya zake kwa kutumia mfumo wa TEHAMA ili kukiwezesha Chama na Jumuiya zake kujitegemea kimapato na kiuchumi;
- (c) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya CCM ya Kujitegemea Kimapato na Kiuchumi ya Mwaka 2014, kwa kuendeleza miradi ya kiuchumi na kuanzisha mingine mipya. Chama kitaendelea kukuza moyo wa kujitolea na kuhamasisha utoaji wa michango ya hiari kwa Chama na Jumuiya zake chini ya usimamizi wa Kanuni za Fedha na Mali za Chama na Jumuiya zake;



- (d) Kwa kutambua kuwa, uimara wa CCM ni Mashina na Matawi yake, Chama kitaendeleza jitihada za kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kukomaza Demokrasia Mashinani na Matawini ili kuimarisha uhai wa CCM na Jumuiya zake na kuepuka uongozi wa mazoea;
- (e) Kuhakikisha kuwa, CCM inakua kiungo imara na daraja madhubuti linalo waunganisha wananchi na Serikali na kuyatangaza mafanikio ya Serikali zetu mbili, ambazo ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kupambana na kuondoa umasikini, ujinga, maradhi na dhuluma;
- (f) Kusimamia nidhamu, viapo vya wanachama na viongozi, maadili na uwajibikaji wa viongozi na watendaji wa CCM na Jumuiya zake;
- (g) Kuendeleza na kukuza demokrasia na haki ndani ya Chama na Jumuiya zake;
- (h) Kuendeleza na kuimarisha uhusiano mwema kati ya CCM na Taasisi mbalimbali za ndani ya nchi na vyama rafiki na vya kindugu;
- (i) Kuendeleza mafunzo ya siasa na itikadi ya Chama kwa viongozi na watendaji wa Chama na jumuiya zake pamoja na maandalizi ya makada;
- (j) Kuendeleza utafiti, kuimarisha utendaji wa vyombo vya habari vya CCM ili kubuni mbinu mpya za kuenza hamasa, kuenzi utamaduni wa kitaifa na kuboresha njia za mawasiliano kwa umma;
- (k) Kuboresha utendaji kazi na mafunzo ya watumishi wa Chama na Jumuiya zake na kuboresha masilahi yao;
- (l) Kudumisha na kuendeleza Muungano wa Serikali mbili; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Tunu za Taifa;
- (m) Kuyalinda na kuyaendeleza Mapinduzi Matukufu ya tarehe 12 Januari, 1964;
- (n) Kuendelea kuwa kiungo kati ya wanamapinduzi wa Tanzania na wanamapinduzi wengine kokote kule duniani; na
- (o) Kuendelea kuwa kiungo imara kati ya wananchi na serikali zao.





## JUMUIYA ZA CCM

253. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo ya utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 - 2025, Jumuiya za CCM zitatekeleza malengo yafuatayo;-

**(a) Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT)**

- (i) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi na ya kihistoria ya UVCCM kama yaliyoainishwa katika Kanuni za Umoja wa Vijana wa CCM;
- (ii) Kuandaa na kutekeleza programu na mipango mbalimbali ya mafunzo kwa viongozi wa UWT, ili kuwajengea uwezo na kuwaandaa katika kuwahamasisha wanawake kushiriki kwa vitendo katika mapambano dhidi ya mfumo dume na kupiga vita aina zote za uonevu na ukandamizaji wa haki za wanawake;
- (iii) Kuendelea kushirikiana na vyombo vya sheria pamoja na taasisi mbalimbali za kijamii katika kupiga vita mila potofu na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto;
- (iv) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mipango mbalimbali ya mafunzo ili kuwaendeleza wanawake kielimu na kuwajengea uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni;
- (v) Kuandaa na kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali ya kuimarisha UWT kimuundo, kiutendaji na kiuchumi ili kuiwezesha kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa malengo na madhumuni ya CCM; na
- (vi) Kubuni na kutekeleza mkakati wa kuhamasisha wananchi kujiunga na CCM.

**(b) Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM)**

- (i) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi na ya kihistoria ya UVCCM kama yaliyoainishwa katika Kanuni za Umoja wa Vijana wa CCM;
- (ii) Kubuni, kuandaa na kutekeleza mipango na programu za mafunzo kwa viongozi wa ngazi mbalimbali za UVCCM, ili kuwaandaa na kuwajengea uwezo wa kuwahamasisha vijana, kuzitambua fursa zilizopo katika maeneo yao na kuzitumia kikamilifu katika kujiendeleza kielimu, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni;
- (iii) Kubuni, kuandaa na kutekeleza miradi mbalimbali ya kiuchumi, ikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi na shughuli



nyinginezo za uzalishaji. Vilevile, kutumia miradi hiyo kama mashamba darasa kwa ajili ya mafunzo kwa vijana, hasa wasomi ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri wenyewe na kujitegemea;

- (iv) Kubuni, kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mipango ya maandalizi na malezi ya Chipukizi, ili kuwajenga kuwa raia wema na wazalendo;
- (v) Kuandaa na kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali ya kuimarisha UVCCM kimuundo, kiutendaji na kiuchumi, ili kuiwezesha kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa malengo na madhumuni ya CCM; na
- (vi) Kubuni na kutekeleza mkakati wa kuhamasisha wananchi kujiunga na CCM.

(c) **Jumuiya ya Umoja wa Wazazi (WAZAZI)**

- (i) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yake ya msingi ya kuanzishwa kwake, kama yalivyoainishwa katika Kanuni za Jumuiya ya WAZAZI;
- (ii) Kuendeleza juhudi za kuimarisha nguvu na uhai wa Jumuiya ya WAZAZI, kimuundo, kiutendaji na kiuchumi pamoja na kuongeza idadi ya wanachama wake. Vilevile, kutoa mafunzo mahsusi kwa watendaji na viongozi wa ngazi zote sambamba na kuratibu na kufanya ziara nchi nzima ili kusajili wanachama wapya pamoja na kupanua uwekezaji katika sekta za kiuchumi;
- (iii) Kufanya tathmini na tafakuri ya kina ili kuimarisha uwezo wa Jumuiya ya WAZAZI, katika kuendesha na kusimamia shule zake za Sekondari kwa kuzingatia mazingira ya wakati wa sasa na changamoto zake;
- (iv) Kuandaa mikakati ya malezi, elimu na mazingira ili kusaidia kutoa mwongozo wa malezi bora kwa watoto/familia, elimu pamoja na utunzaji wa mazingira kwa maendeleo endelevu; na
- (v) Kuandaa na kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali ya kuimarisha Jumuiya ya WAZAZI kimuundo, kiutendaji na kiuchumi, ili kuiwezesha kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa malengo na madhumuni ya CCM; na
- (vi) Kubuni na kutekeleza mkakati wa kuhamasisha wananchi kujiunga na CCM.



**(d) Mabaraza ya Wazee wa CCM**

- (i) Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuwaenzi na kutumia busara na uzoefu wa wazee katika ujenzi wa Chama na nchi. Hivyo:-
  - (i) Kitawatumia wazee katika kurithisha kwa Taifa busara, hekima na ujasiri wao ndani ya Jamii;
  - (ii) Kitawashirikisha wazee kuona kwamba nchi yetu inaendeshwa kwa misingi ya kudumisha amani, utulivu, demokrasia na uongozi bora;
  - (iii) Chama kitahakikisha kuwa, wazee wanaendelea kutoa michango yao katika:-
    - Kuhifadhi, kukuza na kudumisha umoja na uzalendo wa kitaifa;
    - Kuwashauri viongozi wa Chama kwa hekima kuhusu njia bora za ujenzi wa Chama na Taifa; na
    - Kuhakikisha kuwa, kupitia mabaraza yao, wazee wanaendelea kuwa mfano bora wa tabia njema kwa Taifa na hivyo kuongoza mafanikio ya imani, malengo na madhumuni ya CCM.
  - (iv) Kubuni na kutekeleza mkakati wa kuhamasisha wananchi kujiunga na CCM.

**Wajibu wa CCM**

254. Akihutubia Mkutano Mkuu wa Chama Cha Uganda People's Congress, tarehe 7 Juni, 1968, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alitukumbusha kwamba, **"Kazi ya Chama kilicho imara ni kuwa daraja linalowaunganisha wananchi na Serikali yao. Ni wajibu wa Chama kuwasaidia wananchi, kuelewa Serikali yao inafanya nini na kwanini; na kuwashawishi wananchi kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Serikali yao, ikiwemo kuondoa umasikini wao. Zaidi ya hapo, Chama kinalo jukumu au wajibu wa kuwasemea wananchi"** mwisho wa kunukuu.

255. Ni ukweli usio na shaka kuwa, ili CCM iendelee kukubalika na kuaminiwa na wananchi na kupewa ridhaa ya kuongoza nchi yetu, upo muhimu mkubwa kwa viongozi wa Chama Cha Mapinduzi, kuwa karibu na wananchi kwa kuwatembelea, kusikiliza kero zao na kushirikiana nao katika kuzipatia majawabu. Ni muhimu pia kwa CCM wakati wote kuwa kimbilio, msemaji na mtetezi wa wananchi wote na hasa wanyonge. Hii ni muhimu kwa kuwa, kwa asili yake, CCM ni Chama cha wakulima na wafanyakazi kinachowatetea wale ambao sauti zao sio rahisi kusikika.

